**12 JUNI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Arobaini na Tano – Tarehe 12 Juni, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. BARAKA LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:**

Maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:**

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 *(Monetary Policy Statement for the Year 2025/2026)*.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. BARAKA LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali. Tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake, hakuna! Haya, sasa ninaona mmesimama watatu. Kwanza nimemwona Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile.

Na. 576

### Hitaji la Stendi ya Kisasa – Namanyere

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE K.n.y. MHE. AIDA J. KHENANI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Stendi ya Kisasa na kuweka Taa za Barabarani Namanyere – Nkasi?

**SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi tayari imebainisha eneo rasmi kwa ajili ya ujenzi wa stendi ya kisasa katika Mji wa Namanyere. Eneo hilo limepimwa na lina ukubwa wa takribani mita za mraba 14,678.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu na mahitaji ya wananchi wa Namanyere, Halmashauri imejenga jengo dogo la kupumzikia abiria katika eneo hilo, sambamba na kuingia mikataba na wafanyabiashara waliowekeza kwa kujenga

vibanda vya biashara vinavyozunguka eneo la stendi. Hadi sasa, vibanda 88 vimejengwa na vinatoa huduma kwa wananchi, wakati jitihada za kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa stendi ya kisasa zikiendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa halmashauri inaendelea na ukamilishaji wa andiko la mradi ambalo litatumika kuwasilisha maombi ya fedha kwa ajili ya ujenzi wa stendi hiyo ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, suala la taa za barabarani katika Mji wa Namanyere, *TARURA* Wilaya ya Nkasi imewasilisha tathmini ya shilingi milioni 630, kwa ajili ya uwekaji wa taa za barabarani 196 kwenye barabara zote za lami mjini Namanyere.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya ujenzi wa stendi pamoja na kufunga taa kwenye maeneo yaliyokidhi vigezo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini, ikiwemo barabara za Mji wa Namanyere.

**SPIKA:** Mheshimiwa Simon Songe, swali la nyongeza.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu ya Serikali. Ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Kwa kuwa sasa watu wa *TARURA* kule Nkasi wameshaleta maombi ya shilingi milioni 680 kwa ajili ya kuweka taa za barabarani, je, Serikali iko tayari sasa Julai kupeleka sehemu ya fedha ili waanze kuweka hizi taa za barabarani kama ilivyoombwa na *TARURA*?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Tuliahidiwa ujenzi wa stendi pale Lamadi. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi huu ili wananchi waweze kutumia stendi ambayo imeahidiwa na Serikali? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika,

ahsante sana. Ni kweli kwamba, Mji wa Namanyere wameleta maombi ya kuweka taa barabarani na tayari Meneja wa *TARURA* Wilaya ya Nkasi na Mkoa wa Rukwa wamefanya tathmini na shilingi milioni 630 zinahitajika.

Mheshimiwa Spika, hatua ambayo inaendelea hivi sasa ni Serikali kufanya *process* za kupata fedha hizo kwa ajili ya kwenda kuanza kufunga taa katika Mji wa Namanyere kwa awamu. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Songe kwa niaba ya Mheshimiwa Aida Khenani kwamba, Serikali tayari imeshaanza mkakati wa kutafuta fedha kwa ajili ya kufunga taa hizo za barabarani na zoezi hilo litafanyika kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na uhitaji wa stendi katika Mji wa Lamadi, ni kweli na tayari maombi hayo ya Halmashauri ya Busega yamewasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI na tumeshaingiza kwenye mpango wa maeneo yanayohitaji kujengwa stendi za kimkakati. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Songe kwamba, Serikali itakwenda kutekeleza ahadi hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Changamoto iliyopo Namanyere ni sawasawa na changamoto iliyopo katika Jimbo la Buhigwe Makao Makuu ya Wilaya ya Buhigwe. Lini Serikali itatujengea stendi ya kisasa katika Mji wetu wa Buhigwe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali ilishaweka mpango mkakati wa utekelezaji kwa awamu kwa ajili ya kuhakikisha maeneo yote ambayo yanahitaji huduma za stendi kwa ajili ya kuboresha mapato ya ndani ya halmashauri na huduma za kijamii katika eneo la usafiri katika kila halmashauri zetu, yanaainishwa na yanaanza kutengewa fedha kupitia vyanzo vya ndani vya halmashauri kwa kadri ya uwezo wa

halmashauri. Pia, lile pengo la bajeti liwasilishwe Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa stendi hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba nichukue nafasi hii nimwelekeze Mkurugenzi wa Halmashauri ya Buhigwe, kuanza kufanya tathmini ya mahitaji ya fedha katika eneo hilo la ujenzi wa stendi ili kuwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya hatua zaidi za utekelezaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI italeta fedha katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ili kukamilisha ujenzi wa stendi pale Nangurukuru, ambayo halmashauri kupitia mapato yake ya ndani imeuanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kilwa na Menejimenti nzima, Baraza la Madiwani na Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo yote mawili kwa kuanza kutoa fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya kuanza ujenzi wa stendi ya mabasi pale Nangurukuru.

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo maelekezo ya Serikali, kwamba halmashauri zianze kutenga fedha za mapato ya ndani badala ya kusubiri fedha zote kutoka Serikali Kuu na pale ambapo kunakuwa na pengo la ukamilishaji wawasilishe maombi hayo Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili Serikali Kuu iweze kuona namna ya kuwaunga mkono na kukamilisha ujenzi huo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Kassinge kwamba, hoja hiyo tumeichukua na tutaifanyia kazi kuona namna ambavyo tutatenga bajeti kwa ajili ya kwenda kumalizia ujenzi wa stendi pale Nangurukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Kyela ni lini mtakuja kutuwekea taa katika stendi kuu pale?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninaomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tutawasiliana na uongozi wa Wilaya na Halmashauri ya Wilaya ya Kyela. Pia, nitumie nafasi hii kumwelekeza Meneja wa *TARURA* Mkoa wa Mbeya pamoja na Meneja wa *TARURA* Wilaya ya Kyela, wafanye tathmini ya mahitaji ya taa za pale stendi ili tuweze kuona namna ya kuanza kutenga bajeti kwa ajili ya utekelezaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Je, ni lini Serikali itatujengea stendi ya kisasa Ngara Mjini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Ngara imeshawasilisha pia maombi ya kujengewa stendi ya kisasa. Hata hivyo, tunafahamu kwamba, pamoja na kipaumbele cha stendi, kulikuwa na kipaumbele cha barabara, na tayari tumeanza utekelezaji wa barabara za pale Ngara Mjini.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Oliver Semuguruka kwamba, ombi hilo limefika Serikalini na Serikali inaendelea kufanya utaratibu kwa ajili ya kuanza kutenga fedha kwa mapato ya ndani ya halmashauri, lakini pia kutoka Serikali Kuu kwa awamu kwa ajili ya kuanza ujenzi wa stendi katika eneo la Ngara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Mji wa Kibara unakua kwa kasi sana. Je, ni lini Serikali itajenga stendi ya kisasa ili kusaidia wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Bunda na Baraza la Madiwani kuanza kufanya tathmini ya kupata eneo kwa ajili ya ujenzi wa stendi katika Mji wa Mwibara. Pia, waone gharama zinazohitajika kwa ajili ya ujenzi na kuanza kutenga fedha za mapato ya ndani kwa awamu; na baadaye kuwasilisha maombi kwa ajili ya Serikali Kuu kuchangia nguvu hizo na kujenga stendi katika eneo la Mwibara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mwandabila, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, Stendi ya Wilaya ya Mbozi pale Vwawa Mjini ni chakavu sana. Ni upi mkakati wa Wizara kuhakikisha inaboresha stendi ile? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ninafahamu kwamba stendi ile ni ya siku nyingi na ni chakavu, lakini Mheshimiwa Neema Mwandabila na Mbunge wa Jimbo hilo mara kadhaa wameulizia kuhusiana na ujenzi wa stendi hiyo na tayari tulishawasiliana na Mkurugenzi wa Mbozi na wameshawasilisha maombi ya fedha.

Mheshimiwa Spika, kinachofuata sasa ni kuona namna ambavyo tutaanza kutenga bajeti kwa awamu kupitia mapato ya ndani, lakini pia kupitia Serikali Kuu kwa ajili ya kuanza ujenzi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Neema Mwandabila na wananchi wa Vwawa pale Mbozi kwamba, Serikali imechukua hoja hiyo na inaendelea kuifanyia kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shamsia Mtamba, swali la nyongeza.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itatujengea stendi ya kisasa katika Halmashauri yetu ya Wilaya ya Mkunwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, tunafahamu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara Vijijini eneo la Mkunwa, kuna uhitaji wa ujenzi wa stendi na Mheshimiwa Shamsia amewasilisha mara kadhaa.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Mtwara Vijijini kwamba, Serikali hii sikivu ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imepokea hoja hiyo na itakwenda kuifanyia kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo Mbunge wa Mbagala, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Janejelly James Ntate.

Na. 577

**Ukarabati Mkubwa Soko la Mbagala Kizuiyani**

**MHE. JANEJELLY J. NTATE K.n.y. MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya ukarabati mkubwa Soko la Mbagala Kizuiani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Halmashauri ya Manispaa ya Temeke imetenga shilingi milioni 800 kwa ajili ya kufanya ukarabati mkubwa wa masoko yake likiwemo soko la Mbagala Kizuiani.

Mheshimiwa Spika, usanifu na upembuzi yakinifu wa mahitaji ya ukarabati wa soko la Mbagala Kizuiani umeshakamilika na utekelezaji wake utaanza mapema katika mwaka wa fedha 2025/2026.

**SPIKA:** Mheshimiwa Janejelly Ntate, swali la nyongeza.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Chamazi ni eneo lenye wakazi wengi, je, kwenye masoko yanayotegemewa kujengwa, itakuwemo na yenyewe kujengewa soko kubwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Soko la Karata na Mbande nalo limo kwenye mpango huo kufanyiwa ukarabati? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwamba Soko la Chamazi, Mbande na ambalo Mheshimiwa Mbunge amelitaja ni miongoni mwa masoko katika Manispaa ya Temeke ambayo nayo yanahitaji ukarabati na mengine ujenzi na kuongeza miundombinu muhimu.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa bajeti ya Manispaa ya Temeke kwa mwaka 2025/2026 masoko yaliyotengewa shilingi milioni 800 ni masoko matano ambayo ni Soko la Temeke Sterio, Tandika Kuu, Mbagala Kizuiani, Lumu, na Toangoma.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa awamu hiyo tutakwenda kukarabati masoko hayo Matano, lakini Serikali inatambua umuhimu wa kukarabati masoko hayo mengine pia, hivyo

itaendelea kutenga bajeti kwa awamu ili tuyafikie na kuyakarabati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Je, Wizara ya TAMISEMI inashirikianaje na Wizara ya Kilimo ili kuharakisha uboreshaji wa miundombinu kwenye masoko ya Kisambo, Himo, Mwika, na Marangu Mtoni? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inashirikiana kwa karibu sana na Wizara ya Kilimo katika masoko, hususan masoko yaliyoko mipakani katika Jimbo la Vunjo, Mwika, na mengine. Pia, yako masoko ambayo tayari hatua za ujenzi zinaendelea, lakini yako masoko ambayo tunaendelea kufanya tathmini na yatajengwa kwa Mfumo wa *PPP*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Kimei hoja zake amezileta mara kadhaa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Wizara ya Kilimo tayari tumeanza utekelezaji na tunaamini wakati wowote tutaanza utekelezaji wa ujenzi wa masoko hayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Priscus Tarimo, swali la nyongeza.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya kuweka paa pamoja na sakafu kwenye Soko la Manyema, Moshi Mjini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue hoja ya Mheshimiwa Priscus Tarimo, Mbunge

wa Moshi Mjini, kuhusiana na uhitaji wa sakafu na paa katika soko hilo.

Mheshimiwa Spika, pia, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI nimwelekeze Mkurugenzi wa Manispaa ya Moshi kuanza kufanya tathmini haraka iwezekanavyo kujua gharama ya matengenezo ya soko hilo na kuona uwezekano wa kuanza kutenga fedha kwa ajili ya mapato ya ndani kufanya kazi hiyo, na pia, kuwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI eneo la *gap* ambalo litapatikana ili Serikali pia iweze kuona namna ya kupeleka fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Benardeta Mushashu, swali la nyongeza.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha biashara ya mpakani, ni lini sasa Serikali itajenga na kukamilisha soko kwenye mpaka kati ya Uganda na Tanzania pale Mutukula?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali ilishafanya tathmini ya masoko yote ya mpakani likiwemo soko lile la Mutukula mpakani mwa Tanzania na Uganda.

Mheshimiwa Spika, tayari tumeanza kuandaa mpango mkakati wa utekelezaji wa ujenzi, upanuzi, na ukarabati wa masoko hayo. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mushashu kwamba, Soko la Mutukula ni moja ya masoko ambayo yameshaainishwa na ninakumbuka mwaka juzi 2023 tulipita pale kwenye ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na alitoa maelekezo hayo na Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumeanza taratibu za utekelezaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah Mbunge wa Donge, sasa aulize swali lake.

Na. 578

**Uhifadhi wa Mazingira Bwawa la Nyerere**

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH** aliuliza: -

Je, kuna mkakati gani kuimarisha uhifadhi wa mazingira ya Mradi wa Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere ili kuhakikisha uendelevu wa Mradi huo?

**SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Hamza, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha uhifadhi wa mazingira ikiwemo uhifadhi wa Mazingira ya Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kuendelea kupanda na kutunza miti kwenye vyanzo vya maji, kuendelea kutoa elimu ya mazingira, kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Taifa wa Matumizi endelevu ya Ardhi Eneo la Hifadhi ya Mita 60 kutoka kwenye vyanzo vya maji, pamoja na kuunda kamati za mazingira kwa ajili ya kudhibiti uharibifu wa mazingira kwenye vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, swali la nyongeza.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini ninayo maswali mawili kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Kwa kuzingatia umuhimu wa Bwawa la Mwalimu Nyerere na uhifadhi wake; je, Serikali ina mkakati gani wa kuwashirikisha wananchi wanaoishi pembezoni mwa Bwala la Mwalimu Nyerere ili kusaidia uhifadhi wa mazingira yake?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Je, uwepo wa Bwawa la Mwalimu Nyerere umesaidia kwa kiasi gani kuhamasisha matumizi ya nishati safi na salama na kuweza kuepuka au kupunguza uharibifu wa misitu kutokana na matumizi ya kuni na mkaa? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Soud, amekuwa mdau mzuri sana wa mazingira na jambo kubwa la athari ya mabadiliko ya tabia ya nchi. Ushirikishwaji wa wananchi waliozunguka maeneo haya ya Bwawa la Mwalimu Nyerere ni wa kiasi kikubwa sana; na kwa sababu, tunafahamu wao ndio wapo karibu na bwawa hili, na kama ni wanufaika, basi wa mwanzo wanakuwa ni wao. Kwa hiyo, tumewapa jukumu la kuwashirikisha kusaidia katika kutunza na kuhifadhi mazingira ya maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la kwanza ambalo tumelifanya ni kuwahimiza kupanda miti ambayo haikaushi vyanzo vya maji pembezoni mwa bwawa hili. Kwa kushirikiana na Maafisa wetu wa Mazingira, Mabolozi wetu wa Mazingira na wenzetu wa Halmashauri tumekuwa tukiwahimiza wenzetu hawa kwa kuwapa elimu ya mara kwa mara juu ya suala zima la usimamizi wa Sheria za Mazingira, lakini kubwa zaidi tumekuwa tunawaambia wawe wanafanya usafi. Lengo ni bwawa lile liendelee kuwa salama kwa sababu, tunachoamini ni kwamba maji ni mazingira, na mazingira ni maji.

Mheshimiwa Spika, kingine ni bwawa hili limesaidia ama linakwenda kusaidia kwa kiasi kikubwa matumizi ya nishati safi, hasa ya kupikia, na kuwaambia wananchi watoke katika

matumizi ya nishati chafu. Kwanza, bwawa hili linakwenda kupeleka upatikanaji wa umeme wa uhakika, maana yake ni kwamba, watu ama wananchi wanakwenda kuacha kutumia kuni na mkaa na kutumia umeme, kama sehemu ya nishati.

Mheshimiwa Spika, sasa, kupitia bwawa hili, umeshafikishwa umeme mijini na vijijini, kitu ambacho wananchi wetu wanakwenda kuacha matumizi ya kuni na mkaa na kutumia nishati safi ya kupikia ambayo ni umeme. Nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Prof. Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na juhudi za Serikali kuhifadhi Mlima Kilimanjaro, bado kuna changamoto kubwa ya kukata miti kwa kutumia *chainsaw* na kuranda mbao. Je, Serikali ina mikakati gani kukabiliana na hali hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Ndakidemi, kama ifuatavyo: Nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge, wananchi na Watanzania wote kwamba, suala la ukataji wa miti ni kosa kisheria, na suala la upandaji wa miti lipo kisheria.

Mheshimiwa Spika, nimwambie tu Mheshimiwa kwamba, Serikali ipo katika mkakati wa kuhakikisha tunawachukulia hatua wale wote ambao wanakata miti na misitu, ambayo ni sehemu ya mazingira, hasa maeneo yaliyozunguka katika vivutio na maeneo yaliyozunguka katika miradi mikubwa.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kuchukua hatua, lakini kubwa zaidi ni kuwaelimisha wananchi wasikate miti na badala yake wapande miti, hasa katika maeneo haya ya Kilimanjaro. Nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdul Maalim, swali la nyongeza.

**MHE. ABDUL YUSSUF MAALIM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nini mpango wa Serikali katika kutunza vyanzo vya maji, hasa vinavyopeleka maji katika Bwawa la Mwalimu Nyerere? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, upo mpango kabambe wa kutunza vyanzo vya maji vyote ambavyo vinapeleka maji katika Bwawa la Mwalimu Nyerere na vile ambavyo vinapeleka maji katika mabwawa, mito na maeneo mengine. Mpango wa kwanza ni kuhakikisha kwamba, tunawaambia wananchi wasimamie Mwongozo ule wa Mita 60 maana pale ndiyo kuna msingi wa uchafuzi na uharibifu wa vyanzo vya maji. Pale kuna wananchi wanalima, wanafanya shughuli za kilimo katika vyanzo vya maji, wengine wanafanya shughuli za viwanda katika vyanzo vya maji, wengine wanafuga katika vyanzo vya maji. Kwa hiyo, kwa kupitia mwongozo ule wa kusimamia sheria ya mita 60, tumekuwa tunaendelea kuwaelimisha wananchi sambamba na kuchukua hatua za kisheria kwa kuzingatia Sheria ya Mazingira. Nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali inadhibiti vipi taasisi za mazingira zilizojitokeza kuchangisha wadau fedha na *T-Shirt* kwa madai ya kutunza mazingira ya bwawa, ili kuhakikisha taasisi hizo hazitumii michango hiyo kwa maslahi binafsi?

**SPIKA:** Hebu rudia swali.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali inadhibiti vipi taasisi zetu hizi za mazingira ambazo zimejitokeza kule kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere, maana Jimbo la Kilombero lina sehemu ya Bwawa la Mwalimu Nyerere, kuchangisha fedha na vitu mbalimbali kwa madai ya kutunza

mazingira kuhakikisha kweli zinatumika kwa kile wanachokichangisha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abubakari Asenga. Ni kwamba, hili jambo tulikuwa hatuna taarifa nalo. Sasa nimwambie tu, tutalichukua, tutashirikiana na wenzetu wa nishati, halmashauri na mkuu wa wilaya tuone namna ambavyo tunalichulia hatua hili na kuwaambia Watanzania wote upandaji wa miti na suala la utunzaji wa mazingira lipo kisheria.

Mheshimiwa Spika, taasisi au mtu yeyote, ya/wa kitaifa au Kimataifa, ikiwa wanataka kupanda miti ni lazima wafuate sheria na utaratibu. Kwanza, waende Ofisi ya Mkuu wa Wilaya wakutane na maafisa wetu wa mazingira, waridhiwe, ndipo waje wafanye shughuli hiyo, siyo labda kupita kuchangisha kwa kisingizio cha jambo fulani, lakini hata hivyo tutalichukua twende tukalifanyie kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tena, hauruhusiwi kuzungumza na simu ukiwa Bungeni. Milango iko mingi, toka nje, nenda kazungumze huko. Usitafute majira haya ukaanza kuambiwa toka nje kaongee na simu, halafu wapigakura wanakupigia simu, hupokei, unasema niko Bungeni. Mbona nyingine unapokea? *(Makofi)*

Sasa hivi nitaanza kuwataja. Nenda nje ukaongee na hao Wajumbe wanaokupigia simu. *(Makofi)*

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini. Sasa aulize swali lake.

Na. 579

**Ujenzi wa Bwawa la Lambo la Kunyweshea Mifugo, Nkasi Kusini**

**MHE. VINCENT P. MBOGO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itamaliza ujenzi wa Bwawa la Lambo la kunyweshea mifugo Kijiji cha Kacheche na ujenzi wa Josho Nyikankulu, Kata ya Chala, Nkasi Kusini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Nkasi Kusini, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, imejenga Bwawa la Kacheche kupitia Mpango wa Kuendeleza Kilimo *(ASDP I)* kati ya Mwaka 2008 na 2009. Hata hivyo kwa kuwa, bwawa hilo limejengwa muda mrefu, kwa sasa limejaa tope, na hivyo kupunguza uwezo wake wa kuhifadhi maji. Kutokana na hali hiyo, Serikali itatuma timu ya wataalam kufanya tathmini ya hali halisi ya bwawa hilo, ili hatua stahiki za kukamilisha ujenzi huo ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na ujenzi wa majosho katika maeneo mbalimbali hapa nchini, likiwemo Josho la Nyikankulu lililopo Kata ya Chala, Nkasi Kusini, kadiri ya upatikanaji wa fedha. Aidha, Naomba kutoa rai kwa Halmashauri ya Nkasi kutenga fedha kutoka kwenye mapato yake ya ndani, kwa ajili ya kujenga majosho katika maeneo yenye uhitaji wa huduma hiyo Wilayani Nkasi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vincent Mbogo, swali la nyongeza.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Ningeweza kuuliza swali la nyongeza, lakini wananchi wa Jimbo la Nkasi Kusini wanaishukuru sana Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, ndani ya miaka mitano mmejenga majosho sita. Sina swali la nyongeza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Naamini Mheshimiwa Naibu Waziri amezipokea pongezi hizo.

Hakukuwa na Mbunge mwingine aliyesimama. Kwa hiyo, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Festo Sanga.

Na. 580

**Kumpata Mkandarasi wa Barabara ya Mlowo – Kamsamba**

**MHE. FESTO R. SANGA K.n.y. MHE. JULIANA D. SHONZA** aliuliza: -

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Mlowo – Kamsamba utaanza?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Mhandisi Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, taratibu za manunuzi ya mkandarasi, kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kiwango cha lami wa kilometa tano kuanzia Mlowo kuelekea Kamsamba na nyingine tano kuanzia Kamsamba kuelekea Mlowo zipo katika hatua za mwisho *(Negotiations)*. Taratibu za manunuzi zikikamilika na Mkandarasi wa ujenzi kupatikana, kazi ya ujenzi wa barabara hiyo utaanza. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naishukuru Serikali kwamba, imeanza kuonesha nia ya kuijenga barabara hii ambayo kwa kweli, ina matumizi makubwa sana ya wananchi. Nachukua nafasi hii pia, kuiomba Serikali, kwanza

kuwauliza ni lini utaratibu huu utakamilika, ili mkataba uweze kusainiwa na barabara ianze kujengwa kwa sababu, wananchi wamekuwa wakisubiri kwa muda mrefu sana na, Mbunge, Mheshimiwa Juliana Shonza amekuwa akiipigania sana barabara hii?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili kwa ajili ya Jimbo la Makete. Tuna barabara ya kutoka Chimala kuelekea Matamba kuja Kitulo, kilometa 51; ni lini upembuzi yakinifu utakamilika ili barabara hii ianze kujengwa kwa kiwango cha lami kwa sababu, kwenye bajeti imeoneshwa kwamba, mna nia ya kuijenga barabara hii? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumjulisha tu Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wa Majimbo hayo, Mheshimiwa Shonza, Mheshimiwa George Mwenisongole na Mheshimiwa Condester Sichalwe, ambao barabara hizo zinawahusu kwamba, mkataba umekamilika. Sasa tunachofanya tu ni siku ya kusaini huo mkataba kwa sababu, mkandarasi ameshapatikana na *documents* zote ziko tayari, kwa ajili ya kusaini kuanza huo ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, kwanza n Mheshimiwa Mbunge, atakubaliana nami kwamba, hii barabara ilikuwa chini ya *TARURA,* imeshapanda hadhi na sasa hivi tunaiingiza kuanza kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, ili iweze kuendana na *standard* za *TANROADS* na pia, ikiwa ni maandilizi ya kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Omari Kigua, swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, barabara inayotoka Handeni kupitia Kata ya Negero hadi Mziha, kwa kipindi hiki kuna mashimo mengi sana baada ya mvua kunyesha. Je, nini mpango wa Serikali, ili kufukia mashimo hayo kabla ya kufanya ukarabati mkubwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba tu nitumie nafasi hii kumwelekeza Meneja wa Mkoa wa Tanga kwamba, baada ya kipindi cha mvua kwisha, aweze kuhakikisha kwamba, hii barabara inakwenda kukarabatiwa kwa sababu bajeti imeshatengwa, lakini kwa kuwa, mvua imekatika, basi ni muda sahihi sana wa kwenda kuikarabati, ikiwa ni pamoja na kuziba hayo mashimo, ili wananchi waweze kufanya shughuli zao za usafiri na usafirishaji kwa uhakika. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Magige. Swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Barabara inayotokea Babati kuelekea Makuyuni imeharibika sana na imekuwa inaleta usumbufu mkubwa kwa watumiaji. Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha barabara hii inakarabatiwa haraka sana? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, hata katika bajeti yetu tuliyoipitisha, fedha nyingi sana tumezielekeza kwenye ukarabati wa barabara na barabara aliyoitaja, hii ni barabara kuu ambayo inaanzia Dodoma – Kondoa – Babati – Makuyuni kwenda Arusha. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Wizara tayari imeshaainisha barabara hizo, ikiwa ni pamoja na kipande hiki cha Babati – Makuyuni kuhakikisha kwamba, zinafanyiwa ukarabati. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati. Swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itajenga barabara inayotoka Makao Makuu ya Kilolo kwenda Kising'a – Ukwega – Wotalisoli – Mlafu mpaka Ilula, ili wananchi wasipate adha ya kuzunguka mpaka mjini kwenda Makao Makuu yao ya Kilolo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, barabara hii kimsingi bado haijafanyiwa upembuzi yakinifu. Tumeshapata maombi, kwa maana ya mapendekezo ya Mkoa wa Iringa kupitia kwa Meneja wa *TANROAD* kwamba, barabara hii tuweze kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ikiwa ni maandilizi kwa baadaye kuijenga kwa kiwango cha lami, lakini kwa sasa ni kuifanyia usanifu kuikarabati, ili ipitike mwaka mzima. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Barabara ya Mlowo – Kamsamba, mkataba upo tayari. Sasa ni lini mkataba huo utaisaniwa kati ya Serikali na mkandarasi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa, kama nilivyosema, upo tayari. Tukubaliane na Mheshimiwa Mbunge, tungetamani pia, yeye mwenyewe ashuhudie wakati tunasaini. Tukubaliane lini tuusaini huo mkataba, lakini upo tayari. Ahsante.

**SPIKA:** Sasa hapo, kwa lugha nyingine ni mtasaini kabla ya Bunge halijavunjwa ili Mbunge aweze kushiriki.

Haya, Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza. *(Kicheko)*

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, Barabara ya kutoka Buhigwe – Msalala – Kahama kwenda Mwakitolyo, Shinyanga ni barabara muhimu sana. Je, ni lini itajengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI**: Mheshimiwa Spika, ahsante. Barabara hii tumekuwa tukiijenga kwa awamu na hasa tumeanza kwenye vipande vya mji, lakini tumeshakamilisha usanifu. Tunachofanya sasa hivi ni kutafuta fedha ili kuijenga yote kwa kiwango cha lami. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, haya Mwenyekiti, Mheshimiwa Deo Mwanyika.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Barabara ya Makambako – Songea muda mrefu tumeambiwa kwamba, Serikali inaendelea kutafuta fedha na imefanya majadiliano. Je, imefikia wapi kupata hizo fedha? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara ya Makambako – Songea, kwanza kipande cha kutoka Songea mpaka Lutukira, kama kilometa 92, tulishapata fedha kupitia *World Bank* mpango ambao una *TANTIP* na tayari tuko kwenye maandilizi ya kuanza kuijenga kwa sababu na mkandarasi ameshapatikana.

Mheshimiwa Spika, kutoka Lutukira – Njombe kuja Makambako, Serikali inaendelea kutafuta chanzo kikubwa cha uhakika cha fedha kwa sababu, ni moja ya barabara kubwa ambayo inatakiwa ikarabatiwe. Kweli tunakiri ni barabara ya zamani na ni kati ya barabara ambazo zimechoka sana, Serikali inaendelea kutafuta fedha, ili tuweze kuikarabati yote kama tutakavyofanya Songea hadi Lutukira. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya maji. Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, sasa aulize swali lake.

Na. 581

**Ujenzi wa Mradi wa Maji Kata ya Songambele, Kyerwa**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Mradi wa Maji Kata ya Songambele, Kyerwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Bilakwate, umetaja namba ya swali?

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, naomba Swali Namba 581 lipewe majibu.

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Maji. Mheshimiwa Mhandisi Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha huduma ya majisafi na salama inapatikana kwa wananchi wote waishio vijijini, wakiwemo wananchi wa Kata ya Songambele iliyopo Wilayani Kyerwa, Mkoa wa Kagera. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali kupitia mpango wa muda mfupi wa Programu Maalum ya Uchimbaji wa Visima 900, imekamilisha uchimbaji wa kisima kirefu pamoja na ujenzi wa miundombinu rahisi ya kutolea huduma kwa wananchi *(point source)* katika Kijiji na Kata ya Songambele na wananchi wanapata huduma. Aidha, katika mpango wa muda mrefu, Serikali katika mwaka wa fedha 2025/2026 itaanza kutekeleza awamu ya kwanza ya mradi wa usambazaji maji katika Vijiji vya Kata ya Songambele.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa kazi zinazotarajiwa kutekelezwa ni pamoja na ujenzi wa tanki lenye ujazo wa lita 300,000, ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 21 sanjari na ujenzi wa vituo 23 vya kuchotea maji. Mradi huo unatarajiwa kutekelezwa ndani ya miezi nane, ambapo utanufaisha zaidi ya wananchi 18,404 waishio kwenye Vijiji vya Kata ya Songambele. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, naishukuru Serikali kwa hatua mbalimbali ambazo wamekuwa wakichukua kuwapatia wananchi wa Wilaya ya Kyerwa maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Mradi wa Lunyinya, Rwabwere mpaka Chanya umesimama kwa sababu ya mkandarasi anadai zaidi ya bilioni mbili. Ni lini mkandarasi atalipwa ili mradi huu uweze kukamilika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Mradi wa Isingirio, Rutunguru na Kilela, awamu ya kwanza imekamilika. Ni lini awamu ya pili itaanza ili wananchi waweze kupata maji safi na salama? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Namshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Innocent Bilakwate kwa kuendelea kuwapigania wananchi wake na kwa kazi nzuri ya kushirikiana na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Ni dhamira ya Serikali kuhakikisha miradi yote inakamilika na wakandarasi wote wanalipwa hati zao za madai, ili miradi iendelee kutekelezwa na ikamilike kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mradi wa Lunyinya na Rwabwere pamoja na Chanya, ambao mpaka sasa mkandarasi alikuwa na hati ya madai ya bilioni 2.2 tayari tumeshawasilisha Hazina, kwa ajili ya malipo ya mkandarasi huyu.

Mheshimiwa Spika, vilevile Mradi wa Kilela, Isingiro pamoja na Rutunguru, ni kweli kabisa tumeshakamilisha awamu ya kwanza na sasa Serikali imeshauweka katika Bajeti ya Fedha ya 2025/2026, kwa ajili ya kuhakikisha tunaingia sasa kwenye awamu ya pili. Nimtoe hofu, Serikali inaendelea kutafuta fedha na

zitakapopatikana tu, tayari tutaanza awamu ya pili katika mradi huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali sasa itakamilisha mradi wa Jeti-Buza na Kigamboni KK ili kuimarisha kupatikana kwa maji safi na salama katika Jimbo la Temeke?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana na ninamshukuru sana dada yangu kwa kuendelea kuwapigania Wanatemeke na kwa kazi nzuri ambayo anaendelea kuifanya. Ninakumbuka wiki iliyopita pia aliongelea kuhusu mradi huu.

Mheshimiwa Spika, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, Serikali dhamira yake ni kuhakikisha kwamba Jimbo la Temeke ikiwemo Jeti pamoja na Buza, mradi huu ni kipaumbele chetu sisi kama Serikali kwa sababu upo katika utekelezaji wa Ilani. Tutahakikisha kwamba mradi huu unakamilika ndani ya mkataba ambavyo tulisaini na mkandarasi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Fiyao, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Wananchi wa Kata ya Chitete iliyopo ndani ya Wilaya ya Ileje wamekuwa wakikumbana na changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa maji. Ninataka kujua, je, ni lini Serikali watakamilisha mradi wa maji wa Mtembo Msia ili kurahisisha huduma kwa wananchi wetu wa Kata ya Chitete?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru, na ninamshukuru sana dada yangu Stella. Hakika Wanaileje wanahitaji huduma ya majisafi na salama, na mradi huu

ninafahamu pia kuwa ni kipaumbele, hasa katika hii Kata ya Chitete. Mimi ninafahamu kabisa kwamba huu mradi upo katika *progress* nzuri.

Mheshimiwa Spika, na tuna mkataba, na ndani ya mkataba bado hatujaenda nje ya mkataba, kwa hiyo, tunaamini kabisa kwamba mradi huu utakamilika kulingana na mkataba ambao tulisaini na mkandarasi. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Issa Mchungahela.

Na. 582

**Hitaji la Pampu Kata za Mlingura, Mkwapa na Namatutwe**

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA K.n.y. MHE. AGNES E. HOKORORO** aliuliza: -

Je, lini Visima vilivyochimbwa katika Kata za Mlingula, Mkwapa na Namatutwe – Masasi vitawekwa pampu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Nia ya Serikali ni kuhakikisha huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza inapatikana kwa wananchi wote nchini ikiwemo wananchi wa Kata za Mlingula na Namatutwe zilizopo Wilayani Masasi Mkoa wa Mtwara. Katika kutimiza azma hiyo Serikali imekamilisha zoezi la ufungaji wa pampu kwenye visima vyote tisa vilivyochimbwa kwenye kata hizo na vimeanza kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Mchungahela, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na maswali mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini yeye

mwenyewe aliahidi maji katika Kata ya Lipumburu, Kijiji cha Lipumburu wakati tulipokuwa tumefanya naye mkutano kwenye Kijiji cha Lupaso, je, anatekeleza lini ahadi hii ya uchimbaji wa kisima katika kata hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kati ya mikoa ambayo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amewekeza fedha nyingi sana, ni katika huu Mkoa wa Mtwara ikiwemo mradi wa Makonde, mradi wa kutoka Ruvuma kwenda Mangaka Nanyumbu, mradi wa kuboresha miundombinu; na pia eneo lile ambalo Mheshimiwa Mbunge ametaja. Ni kweli kabisa nilifika mimi mwenyewe Lupaso na ni ahadi ya Serikali kwamba ni lazima kisima kichimbwe kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inaendelea kuhakikisha kwamba fedha zipatikane ili tukatekeleze ahadi hiyo ya Serikali, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, Mbunge wa Mbarali swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Suma Ikyenda Fyandomo.

Na. 583

**Mkakati wa Upatikanaji Maji Mbarali**

**MHE. SUMA I. FYANDOMO K.n.y. MHE. BAHATI K. NDINGO** aliuliza: -

Je, nini mkakati wa Serikali kusaidia upatikanaji wa majisafi na salama Mbarali kutoka 58% kufikia lengo la Serikali la 85%?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama Wilayani Mbarali imepanda kutoka wastani wa 58% mwaka 2022 na kufikia 73% mwezi Desemba, 2024. Hali hii imechagizwa kutokana na kukamilika jumla ya miradi nane ya Mkunywa Awamu ya I & II, Igurusi Awamu ya I, Luduga – Mawindi Awamu ya 4&5, Magigiwe, Utengule usangu, Miyombweni, Mhwela – Mapogoro sanjari na mradi wa maji Matebetena ambapo kwa pamoja imewezesha vijiji 22 vya wilaya hiyo kufikiwa na huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali inaendelea na utekelezaji wa jumla ya miradi tisa kwenye Wilaya hiyo ambayo ni Ilongo – Group Awamu ya I, Isunura – Ikanutwa, Itamboleo Awamu ya II, Mbuyuni Awamu ya I, Warumba, Nyakazombe sanjari na upanuzi wa Skimu ya Maji Igava kwenda Vijiji vya Igunda, Muungano, Vikaye na Igava.

Mheshimiwa Spika, aidha, miradi mingine inayoendelea ni pamoja na ukarabati wa mradi wa maji Ruiwa Awamu ya I, ujenzi wa mradi wa maji Chimala pamoja na uchimbaji wa visima vitano na ujenzi wa miundombinu rahisi ya kutolea huduma kwa wananchi *(point source)*.

Mheshimiwa Spika, miradi hiyo ipo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji ambapo inatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2025/2026 na kunufaisha zaidi ya watu 147,151 waishio kwenye vijiji 40 vya Wilaya ya Mbarali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma Ikyenda Fyandomo, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa maswali mawili madogo ya nyongeza. Mbarali kuna vijiji 14 ambavyo havina maji kabisa: -

(a) Je, nini mkakati wa Serikali?

(b) Je, ni lini vijiji vya Matwebe, Maskuru, Lufingo, Masovo na Suma vitaondokana na shida ya maji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana na ninamshukuru sana dada yangu Mheshimiwa Suma. Serikali inaendelea kuchukuwa hatua mbalimbali kuendelea kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto ya maji. Vilevile nchi yetu yenye vijiji 12,318 na hatua iliyofanyika ndani ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa kipindi cha miaka hii minne ni hatua kubwa sana kutoka kwenye 75% mpaka sasa tumefikia 80% na kitu.

Mheshimiwa Spika, sasa tunatambua kwamba bado kuna vijiji ambavyo vitakuwa havijafikiwa; na huduma na ndiyo maana tunashukuru sana Bunge lako Tukufu kwa kupitisha bajeti ya kishindo ya Wizara ya Maji ya trilioni 1.016. Lengo lake ni kwenda kuhakikisha kwamba Watanzania wote wenye uhitaji wa maji wafikishiwe huduma ya majisafi na salama. Nina hakika vijiji 14 hivi vitakuwa ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya Serikali kwenda kuhakikisha kwamba wanapata huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Spika, kwa swali la pili, ni kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi. Katika miradi hii ambayo itakwenda kukamilika na hayo maeneo ambayo ameyataja Mheshimiwa Mbunge na yenyewe yatakuwa sehemu ya utekelezaji wa mradi huo ambao utakuwa na suluhisho kwa wananchi katika maeneo haya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Afya Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 584

**Kudhibiti Ongezeko la Ugonjwa wa Kansa Nchini**

**MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti ongezeko la Wagonjwa wa Kansa nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali katika kukabiliana na ongezeko la wagonjwa wa Kansa kwa kufanya yafuatayo: -

(a) Kutoa elimu kwa umma kuhusu kujikinga na ugonjwa wa saratani kupitia vipindi vya redio, televisheni, machapisho, magazeti na mitandao ya kijamii;

(b) Serikali inatoa chanjo ya *Human Papilloma Virus* kwa wasichana ili kuwakinga na kirusi kinachosababisha saratani ya mlango wa kizazi;

(c) Kuanzisha huduma za awali za uchunguzi na matibabu ya saratani kuanzia ngazi ya zahanati hadi hospitali za Taifa;

(d) Serikali imeimarisha huduma za kibingwa za uchunguzi na matibabu kwa kuhakikisha uwepo wa wataalamu na vifaa tiba kwa ajili ya kukabiliana na Saratani.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako kwanza ninapenda niipongeze Serikali kwa jinsi ilivyowekeza katika afya, ni suala ambalo hatuwezi, ni lazima tuongee. Tulikuwa na Kituo cha Kansa *cha Ocean Road,* lakini sasa Tanzania nzima katika hospitali za rufaa za kanda kuna matibabu ya kansa; na hata kwenye hospitali binafsi nazo zimepewa vibali navyo vinatoa matibabu ya kansa. Tunaipongeza sana Serikali kwa jambo hilo

kubwa. Kwa kweli elimu wanayoitoa ni kubwa sana, kansa watu wameanza kuielewa na wanapona wanaoenda mapema.

Mheshimiwa Spika, mimi kwangu ni ushauri, Serikali sasa ina mpango gani wa kufanya tafiti wa hizo kansa nyingine kama vile walivyoweza kudhibiti kansa ya mlango wa kizazi kwa akina mama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kweli kwa kutambua uwekezaji mkubwa uliowekezwa na Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye Taasisi yetu ya *Ocean Road;* lakini sio taasisi yetu tu ya *Ocean Road,* hata kwenye hospitali zetu za kata.

Mheshimiwa Spika, unajua kule Mbeya kwako umepigania sana, kuna kazi inakwenda kuanza na kazi ya ujenzi imeanza kwa ajili ya kuhakikisha kwamba watu wa Mbeya hawatahitaji kwenda *Ocean Road,* lakini wakati huo huo kule Kanda ya Kaskazini na sehemu nyingine; kwa kweli na kutuweka katika nchi tisa Afrika bora kabisa ambazo zinatoa huduma za kansa.

Mheshimiwa Spika, nimwambie, siyo tu kwa hili suala la kansa ya kizazi, kuna suala la kansa nyingine zote, Serikali inaendelea kuongeza. Ukiona wananunua vifaa hivi, siyo tu kwa ajili ya kutibu, pia vinasaidia kutambua magonjwa mapema na pia kusaidia utafiti ili ukijua vyanzo vingine vinavyosababisha kansa ili viweze kuzuiliwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa kansa ni ugonjwa ambao ni gharama sana kwa matibabu yake. Kwa kuwa tumekuwa tukishuhudia Watanzania wengi ambao wameathirika na ugonjwa huu, wakichangisha ili kuweza kwenda kutibiwa bila mafanikio, je, Serikali haioni kwamba kuna haja sasa

walao kwenye ile *package* ya bima ya kawaida kabisa, ile ya chini, waweze kuweka matibabu haya ili huko mbeleni muweze kuyafanya yawe ya bure kwa Watanzania?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kweli dada yangu Mheshimiwa Matiko ameuliza swali zuri sana, na maana ya bima ya afya kwa wote ni hicho anachokisema. Mimi kama Mbunge, na sisi kama Jamii ya Watanzania, sisi jamii ya Watanzania ukioa ni rahisi watu kuchangia shilingi milioni 100 uoe, lakini ukizaa mtoto akapata tatizo la kansa watu hawakupi hata shilingi 10 kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, moja, kuna suala la mila zetu na jinsi sisi wenyewe tunavyoishi. Ni rahisi watu kufanya sherehe, lakini kwenda kwenye tiba yake na kukata bima anaona ni tatizo, lakini sherehe anaona ni kitu cha maana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni kweli ni muhimu kufanya hivyo, lakini kwa sasa kuna *room* ile ambayo tumesema kama mtu hawezi kulipia matibabu, basi kupitia mtendaji wa kata anaandikiwa barua na anapata tiba zote bure; na ndiyo kikubwa anachofanya na ndiyo maana tunatenga fedha hapa hizi za *MSD* na nyingine ndiyo maana mara nyingi hatuulizani tumetenga shilingi bilioni 200 kwa ajili ya dawa na vitendanishi na vifaatiba mbona hazijarudi, hazionekani kwenye mzunguko? Ni kwa sababu kuna fedha nyingi zinaenda kwenye eneo hilo. Pia, ni kweli kwamba siyo wote wanaweza kuhudumiwa kwa kutumia bilioni 200.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, tatizo la tezi dume limeendelea kuongezeka hasa kwa watu wazima. Je, Serikali imejipanga vipi kutoa elimu ya dalili na kinga ili watu waelewe na kujikinga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli Serikali imejipanga kueleza dalili za magojwa yote na kutoa elimu ya uelewa kwa magonjwa yote ikiwepo tezi dume. Kwa kweli kwa sisi wanaume tunahitaji kuhamasishana kwa nguvu zaidi, sio suala tu la kujua ugonjwa lakini kwenda kwa wakati wote hospitalini kila baada ya miezi sita au mara mbili kwa mwaka kuhakikisha unapima afya yako kwa ujumla ili kuhakikisha wakati wote unaijua, na kama kuna ugonjwa wowote unaotokea uweze kugundulika mapema na kutibiwa mapema.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Lishe bora ni njia mojawapo pia ya kudhibiti kansa. Je, Serikali ipo tayari sasa kutoa elimu kwa vyakula ambavyo vinaweza vikatumika mara nyingi ili kuzuia tatizo hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, Serikali ipo tayari kutoa elimu. Mojawapo ya elimu ni namna ya kula, kwa sababu kuna baadhi ya vyakula ambavyo vina vitamin nyingine kama Vitamin E na nyingine ambazo zina tabia ya kukamata zile vitu ambazo vinazunguka ndani ya mwili wa binadamu vinavyoweza kugonga seli na kusababisha seli nyingine ziache sasa kuwa *controlled* na ubongo mwisho wa siku vinasababisha kansa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuna vyakula ambavyo ukila unapata hivyo ambavyo vinaondoa vitu vinavyosababisha suala hilo. Kwa hiyo, tunaendelea kuelimishana.

Mheshimiwa Spika, kama unakumbuka tulikuwa tunazungumzia watu wanaokufa kwa kukosa chakula huko miaka ya nyuma, lakini sasa hivi tunazungumzia watu wanaokufa kwa kula kupita kiasi. Kwa hiyo, pia kwenye suala la ulaji kwa maana ya kiasi na kufanya mazoezi na mambo mengine, hayo ndiyo mambo ya msingi ya kuhakikisha tunazingatia wakati wowote na kufuatilia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nikupongeze wewe kwa kazi kubwa na nzuri ambayo unaifanya. Vilevile nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya katika Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kansa ni maradhi makubwa, kansa ni maradhi magumu. Sambamba na hilo, Serikali imefanya kazi kubwa kuhakikisha kwamba wanapeleka mashine kwa ajili ya kutambua au kwa ajili ya kufanya matibabu kwenye hospitali zote za rufaa. Swali langu ni kwamba, je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka mashine hizi kwenye hospitali za wilaya kwa sababu watu wengi hawana uwezo wa kufikia hizo hospitali za rufaa na wengi wapo vijijini na wanakufa kwa ajili ya maradhi haya makubwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze mama yetu kwa swali zuri lenye umakini wa hali ya juu. Mimi niseme tu kwamba Serikali inafanya hivyo. Ndiyo maana sasa hivi siyo tu kwamba tunajitahidi kuhakikisha kwamba ule upimaji wa awali na kutambua kuanzia ngazi ya zahanati mpaka Taifa unafanyika, lakini pia umeona kuna madaktari wanaoitwa Madaktari wa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambao wanazunguka nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, wanazunguka kwa kazi, kwa maana wakienda kule wanajenga uwezo kwa wataalam waliopo pale kwa magojwa husika kulingana na ubigwa wao, lakini pia wanatibu na kuacha ujuzi ili watu waweze kutambuliwa mapema.

Mheshimiwa Spika, ni kweli, kwa maana ya teknolojia, teknolojia hizi kubwa za utambuzi zimeishia kwenye *level* ya Hospitali ya Mkoa. Sasa Serikali inajipanga kutengeneza wataalam baada ya hapo ili kupeleka sasa teknolojia hizo kubwa kwenye ngazi ya wilaya, na ikiwezekana vituo vya afya kwa vile

teknolojia ambazo zinaweza kuwa *handled* ni kwenye eneo la kituo cha afya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Lugangira, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, hivi punde Mheshimiwa Naibu Waziri ameelezea kwamba kuna vyakula ambavyo vinachangia kwenye ongezeko la magojwa ya saratani. Sasa ningependa kufahamu, je, ni lini sasa Serikali itaamua kulinda haki na afya za Watanzania kwa kurejesha suala la usalama wa chakula kwa maana ya *food safety* kuwa chini ya Wizara ya Afya kwa sababu kimsingi ni Wizara ya Afya ndiyo ambayo ina dhamana ya kuhakikisha kwamba walaji wanalindwa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge Lugangira, kwani kwenye eneo hili la lishe amekuwa kama balozi mzuri sana kwenye kulipigania. Nimwambie tu, sijasema kwamba kuna vyakula ambavyo vinasababisha, lakini nadhani kuna baadhi ya mambo yakifanyika ya kwenye vyakula yanasababisha patokee matatizo kama hayo unayozungumza.

Mheshimiwa Spika, ni kweli pia kwamba kuna hili suala la lishe, kwa maana ya usimamizi wa chakula na vitu vingine ipo kwenye eneo gani badala ya Wizara ya Afya kama ambavyo tumekwishakusema hapa? Mjadala huu unaendelea ndani ya Serikali. Mimi naamini tutafikia muafaka mzuri kwa sababu kila mtu ni mwathirika kama hatutazingatia yale ambayo yatatufanya sisi wote tuwe salama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Angeline Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri, wamewekeza pesa nyingi sana za kujenga majengo kwa ajili ya kuweka mashine za saratani katika Hospitali ya Bugando lengo ikiwa ni kukifanya kitu

kile kuwa ni cha umahiri lakini mashine zilizopo ni pungufu. Je, ni lini wataweka mashine ili kutosheleza mahitaji ya pale, hasa mashine aina ya *liner accelerator?* Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, kwa kweli nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo wakati wote anapambania wananchi wake. Maana yake hata hili swali ambalo analiuliza hapa, pia ameandika barua kwa ajili ya kuikumbusha Wizara ya Afya suala hilo la hiyo *machine* kwenye hospitali hiyo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, wewe unajua Serikali imeshawekeza pale zaidi ya shilingi bilioni saba kwenye eneo hilo la *cancer* na maana yake majengo yanaenda na kuna baadhi ya *machine* zimenunuliwa, na kwa maana ya bajeti ya mwaka ujao tunajipanga kwa ajili ya kuona namna ya kuhakikisha na eneo hilo linajitosheleza, kwa sababu lengo ni kupunguza mkusanyiko wa watu kwenye hospitali yetu ya *Ocean Road*, watu wabaki kwenye kanda zao na ikiwezekana wabaki baadaye kwenye mikoa yao. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Sasa nitaleta matangazo tuliyonayo hapa Bungeni asubuhi hii. *(Makofi)*

Kwanza, ni tangazo la wageni. Nitaanza na wageni wangu watano waliokaa Jukwaa la Spika. Wapo Wanachama wa Taasisi ya Watu Wenye Ulemavu kutoka Mkoani Singida, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, hawa ni wageni 18 wa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa ambaye ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hawa ni wanafunzi

wa Chuo Kikuu cha Dodoma, wakiongozwa na Ndugu Mohamed Wajika, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wengine ambao wamekaa Jukwaa la Spika, tutaanza na wageni wanne wa Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, hawa ni Viongozi kutoka Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Yupo Dkt. Tausi Kida ambaye ni Katibu Mkuu. Yupo Dkt. Fred Msemwa, Katibu Mtendaji Tume ya Taifa ya Mipango; yupo Ndugu Omar Issa, Mjumbe wa Tume ya Taifa ya Mipango; yupo Dkt. Mursali Milanzi, Naibu Katibu Mtendaji Mipango ya Kitaifa; yupo Ndugu Gilead Teri, Mtendaji Mkuu Kituo cha Uwekezaji *(TIC)*. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine ni wageni wenu. Tutaanza na Wageni 30 wa Mheshimiwa Dkt. Selemani Said Jafo, Waziri wa Viwanda na Biashara. Hawa ni Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari kutoka Kisarawe Mkoa wa Pwani. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 16 wa Mheshimiwa Dorothy George Kilave, Maafisa Elimu Kata kutoka Temeke Mkoani Dar es Salaam. *(Makofi)*

Haya, Mgeni wa Mheshimiwa Tunza Issa Malapo ambaye ni mdogo wake kutoka Tandahimba Mkoani Mtwara. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko ambaye ni mama yake mdogo kutoka Tarime Mkoani Mara. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Robert Chacha Maboto ambaye ni ndugu yake kutoka Bunda Mkoani Mara. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli ambao ni wapiga kura wake kutoka Kipunguni Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Ally Mohamed Kasinge ambao ni watoto wake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile ambao ni marafiki zake kutoka nchini Canada. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo: Wanafunzi 147 na Walimu 10 wa Shule ya Sekondari Nyamata kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 63 na Walimu watano wa Shule ya Awali na Msingi kutoka Mallen Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni tulionao asubuhi hii, hapa Bungeni.

Ninalo tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge. Anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Ofisi ya Bunge imeendaa tamasha la michezo na burudani *(Grand Bunge Bonanza)* ambalo litafanyika siku ya Jumamosi tarehe 21 Juni, 2025 katika Viwanja vya Shule ya Sekondari ya John Merlini iliyoko Miyuji Jijini Dodoma. Tamasha hili ambalo litahusisha Timu za Bunge na wadau wengine litakuwa na michezo mbalimbali kama ifuatavyo: -

Mpira wa miguu, mpira wa kikapu, mpira wa pete, mpira wa wavu na kuvuta kamba. Michezo ya burudani ni kama ifuatayo: -

Riadha, kukimbia na gunia, mchezo wa bao, kufukuza kuku, kupenya kwenye mapipa, kuruka kamba na kuvaa soksi.

Waheshimiwa Wabunge wote, mnahamasishwa kushiriki kikamilifu bonanza hili na mnashauriwa kuanza maandalizi mapema kwa kufanya mazoezi kulingana na mchezo utakaokuwa umeuchagua. Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo, aje awasilishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii, ninawasilisha vitabu vya Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/2026. Taarifa hizi mbili ndiyo msingi wa Bajeti Kuu ya Serikali kwa Mwaka 2025/2026 ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha atawasilisha katika Bunge lako Tukufu baadaye (leo alasiri).

Mheshimiwa Spika, tumeaswa kuwa kila tunapopata fursa hatuna budi kumshukuru Mungu na kuwashukuru watu ambao wameleta tofauti katika maisha yetu na katika jamii zetu. Katika kushukuru, kuna baraka na furaha.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mungu kwa wingi wa rehema, baraka na fadhila zake kwangu ziliyoniwezesha kusimama hapa mbele kuwasilisha Taarifa ya Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/2026, ikiwa ni mara ya pili kama Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na mara ya mwisho katika Bunge hili la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mambo mengi, lakini uniruhusu niyataje matatu tu. Mosi, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais

kwa jinsi alivyoniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, na hivyo kunifanya kuwa sehemu ya timu yake muhimu ya kutafsiri na kutekeleza maono ya Serikali yake. Ni nafasi hii ambayo leo imenipa fursa ya kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu na kuwasilisha hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, niendelee kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jinsi anavyoendelea kuliongoza Taifa letu kwa weledi, umahiri na utulivu mkubwa. Katika kipindi chake cha miaka minne, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameonesha weledi, umahiri, uthabiti, uimara, uadilifu, na uzalendo wa hali ya juu kwa nchi yake. Kupitia falsafa yake ya *4R*, ameendelea kujenga maridhiano mapana ya kijamii na kisiasa na kuweka mazingira sawia ya kufanya siasa kwa vyama vyote nchini, ndiyo *Reconciliation* hiyo; ametoa uhuru wa kutoa maoni, huku akionesha ustahimilivu wa hali ya juu, ndiyo hiyo *Resilience*.

Mheshimiwa Spika, kiongozi wetu ameleta mageuzi makubwa katika kuweka mazingira bora ya biashara na uwekezaji ikiwa ni sehemu ya hiyo *Reform*. Ameimarisha sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na madini na kuwapa matumaini mapya mamilioni ya wakulima, wafugaji, wavuvi na wachimbaji wadogo wa madini. Hakika anaijenga upya nchi yetu ambayo ndiyo *Rebuilding* na kupitia uongozi wake, Serikali yetu na nchi yetu imeendelea kuimarisha amani, utulivu na usalama.

Mheshimiwa Spika, tatu, ninampongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kupata tuzo nyingi tangu awe Rais lakini kwa kipekee na kwa muktadha wa leo, ninaomba nimpongeze sana kwa kuweka historia ya kipekee ya kutunukiwa Tuzo Maalumu na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake mahiri na jitihada zake kubwa anazozifanya katika kuendelea kuijenga Zanzibar yenye maendeleo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwashukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge, na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge, na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, kwa maelekezo na miongozo yao kwetu, na kazi kubwa wanazofanya katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kuongoza nchi yetu vyema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kukushukuru na kukupongeza wewe kwa kuliongoza vizuri sana Bunge hili la Kumi na Mbili. Katika kipindi chako chote cha kuongoza Bunge hili, umejitahidi sana kutenda haki kwa Wabunge wote bila kujali hali na nafasi zao. Aidha, ulijitahidi kulitendea Bunge, Serikali na wananchi haki. Pale ambapo Serikali ilipaswa kuonywa, kuelekezwa na kuwajibishwa hukusita kufanya hivyo na pale ambapo Serikali ilistahili kupongezwa, ulifanya hivyo bila kusita. Kwa kifupi, ulitenda haki. Wewe ni mtenda haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umeweka historia ya kutukuka kwa Bunge hili la Kumi na Mbili ulililoliongoza kwa kutoa Tuzo Maalumu kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutambua mchango wake katika kusukuma mbele maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nirudie. Umeweka historia ya kipekee na ya kutukuka kwa Bunge hili la Kumi na Mbili, kwa Bunge lako kutoa Tuzo Maalumu kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa yote uliyoyafanya katika kipindi chako cha Uspika, hakuna shaka kwamba Bunge hili linakuhitaji, Wabunge hawa wanakuhitaji, Watanzania wanakuhitaji, dunia inakuhitaji, na muhimu zaidi wananchi wa Jimbo Jipya la Uyole wanakuhitaji uendelee kuwa kiongozi wao na kiongozi wao makini. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, tunakuombea na kukutakia kila la heri katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu, na mimi kama mwalimu mwenzako wa chuo kikuu, niwaombe sana wananchi wa Jimbo la Uyole waturudishie mama huyu hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza na kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, kwa kuiongoza Kamati hii muhimu kwa ustadi, hekima na utulivu mkubwa. Historia yake ya kufanya kazi katika sekta binafsi ilimpa fursa ya kujua mambo mengi na kuifanya sekta binafsi kuwa karibu sana na Kamati yake.

Mheshimiwa Spika, tunapokutana na viongozi wa sekta binafsi huwa wanamshukuru na kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. Kwa kweli Mawaziri wenzangu watakubaliana nami kwamba katika kuhudhuria Vikao vya Kamati ya Bajeti, tulijifunza na kuchota maarifa mengi sana kutoka kwa Mwenyekiti huyu na Wajumbe wenzake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi, Kamati ya Bajeti imesheheni maarifa na uzoefu mkubwa na vikao vyake vilikuwa darasa murua kwa kila aliyefika mbele yake. Aidha, ninawapongeza na kuwashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa ushirikiano waliotupa na michango yao makini katika maandalizi ya Taarifa ya Hali ya Uchumi na Mpango ya Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024 imeandaliwa kwa kuzingatia mwenendo wa viashiria vya uchumi jumla, ikijumuisha ukuaji wa pato la Taifa, mfumuko wa bei, thamani ya shilingi pamoja na ajira, tathmini ya maendeleo ya sekta mbalimbali kwa mwaka 2024/2025, hali ya biashara na uwekezaji, changamoto pamoja na vihatarishi vilivyojitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/2026 yamezingatia vipaumbele vya Serikali vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026), pamoja na miongozo mingine ya kisera ya Kitaifa na kikanda ikiwemo: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Dira ya Maendeleo ya Afrika Mashariki 2050; Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Kusini mwa Afrika *(SADC)*;

Ajenda 2063 ya Umoja wa Afrika; na Malengo Endelevu ya Maendeleo ya 2030 ya Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Spika, sasa nieleze Mwenendo wa Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2024. Kwa mujibu wa Taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF)* ya mwezi Aprili mwaka 2025, kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia imeendelea kupungua hadi kufikia 3.3% mwaka 2024 ikilinganishwa na 3.5% mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, upungufu huo ulitokana na sababu mbalimbali ikiwemo athari za utekelezaji wa sera za fedha za Mataifa mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kupunguza ukwasi na kuongeza riba ili kukabiliana na mfumuko wa bei, na migororo ya kisiasa hususan Ulaya Mashariki na Mashariki ya Kati. Aidha, Taarifa ya *IMF* inaonesha kuwa ukuaji wa uchumi wa dunia unatarajiwa kuendelea kupungua na kufikia 2.8% kwa mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya *IMF* ya Aprili, mwaka 2025 kiwango cha ukuaji wa pato la Taifa kwa nchi za ukanda wa Afrika Mashariki na Jumuiya ya *SADC* inaonesha kuwa kwa upande wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2024 uchumi ulikuwa kwa 1.5% na mwaka 2025 unatarajiwa kwa 2.7%. Kwa upande wa *SADC* uchumi ulikuwa mwaka 2024 kwa 3.1% ikilinganishwa na 3.9% kwa mwaka 2023 na unatarajiwa kukua kwa 3.5% kwa mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, kupungua kwa ukuaji wa uchumi kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika kulitokana na migogoro ya kisiasa ikiwemo migogoro inayoendelea nchini *DRC* na Sudani Kusini, ambapo kumekuwa na ukuaji hasi *(negative)* 27.6%.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa la Dunia la Kimataifa *(IMF)* ya Aprili 2025, mfumuko wa bei duniani ulipungua na kufikia wastani wa 5.8% mwaka 2024 kutoka 6.7% mwaka 2023 na mfumuko huu unatarajiwa kuendelea kupungua hadi kufikia 4.3% kwa mwaka 2025 na 2.2% mwaka 2026.

Mheshimiwa Spika, sasa nifanye Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Taifa. Mwaka 2024, pato halisi la Taifa lilifikia shilingi trilioni 156.6 kutoka shilingi trilioni 148.5 kwa mwaka 2023, sawa na ukuaji wa 5.5% na hivyo kuifanya nchi yetu kuwa ni miongoni mwa nchi ambazo zilikuwa na ukuaji mkubwa katika ukanda huu wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, ukuaji huo ulichangiwa na jitihada mbalimbali za Serikali, sekta binafsi na wadau wengine wa maendeleo ikiwa ni pamoja na: kuanza uzalishaji wa umeme katika Bwawa la Mwalimu Nyerere; kuendelea na utekelezaji endelevu wa miradi ya kimkakati na ya kielelezo ikihusisha kwa mfano miundombinu ya nishati, miundombinu ya usafiri na usafirishaji; kuongezeka kwa mikopo ya sekta binafsi; usimamizi madhubuti wa Sera za Fedha; kuimarika kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo; na uwekezaji wa Serikali katika huduma za jamii hususan katika huduma za afya, elimu, maji na hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2024, sekta tano ziliongoza kwa ukuaji wa uchumi ni pamoja na: sanaa na burudani iliyokua kwa 17.1%; uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme iliyokua kwa 14.4%; habari na mawasiliano kwa 14.3%; fedha na bima kwa 13.8%; na afya kwa 10.1%. Sekta tatu zilichangia zaidi takribani nusu ya pato la Taifa ni: kilimo, iliyochangia 26.3%; ujenzi 12.8%; na uchimbaji wa madini na mawe 10.1%.

Mheshimiwa Spika, katika siku za mbeleni, Serikali itaendelea kuongeza tija zaidi kwenye uzalishaji katika kilimo ili kilimo kiendelee kuwainua Watanzania wengi zaidi kimapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfumuko wa bei nchini ulipungua na kufikia 3.1% kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na 3.8% kwa mwaka 2028.

Mheshimiwa Spika, mikopo kwa sekta binafsi iliendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha ambapo mwaka 2024 ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulifikia wastani wa 12.4%. Sekta zilizoongoza kupokea mikopo hiyo ni kilimo kwa 41%, uzalishaji viwandani 16.3%, mikopo katika shughuli binafsi 14.7%, uchukuzi

na mawasiliano 13.2%, biashara 12.7% na ujenzi 4.4%. Matokeo hayo yanaonesha mwelekeo chanya katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya sekta mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi, hususan katika sekta za kilimo, viwanda, pamoja na shughuli binafsi na uchukuzi na mawasiliano, linaashiria uimarishaji wa mazingira ya biashara na ukuaji wa shughuli za kiuchumi. Hatua za kisera zilizolenga kupunguza viwango vya riba na kuongeza bajeti katika sekta muhimu hususan kilimo zimeonekana kuwa na matokeo chanya katika kuchochea ukuaji huo.

Mheshimiwa Spika, akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kuridhisha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi. Mwaka 2024, akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani bilioni 5,546.

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba nifanye Mapitio ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi kwa Taifa kwa mwaka 2025. Malengo ya uchumi wa Taifa kwa mwaka 2025 yapo sita yafuatayo: -

(i) Kuongeza kasi ya ukuaji wa pato halisi la Taifa kufikia asilimia sita mwaka 2025 kutoka asilimia tano nukta tano kwa mwaka 2024;

(ii) Kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja wa wastani wa asilimia kati ya tatu hadi asilimia tano katika muda wa kati;

(iii) Mapato ya ndani (mapato ya kodi na yasiyo ya kikodi) kufikia 16.4% ya pato la Taifa kufikia mwaka 2025/2026 ikilinganishwa na matarajio ya 15.8% kwa mwaka 2024/2025;

(iv) Mapato ya kodi kufikia 13.3% ya pato la Taifa kwa mwaka 2025/2026 ukilinganisha na 12.8% kwa mwaka 2024/2025;

(v) Nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa asilimia tatu nukta sifuri ya pato la Taifa kwa mwaka 2025/2026 kutoka matarajio ya asilimia tatu nukta nne mwaka 2024/2025; na

(vi) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango kinachokidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina ya taarifa ya Hali ya Uchumi yanapatikana katika Kitabu cha Hali ya Uchumi ambacho tumekigawa kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, sasa nifanye tathmini ya utekelezaji ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Mwaka 2024/2025. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Bunge liliidhinisha jumla ya shilingi trilioni 15.944, sawa na 32.3% ya Bajeti Kuu ya Serikali kwa ajili ya programu na miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla wake, katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026) kwa bajeti ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameisoma leo, Serikali ilitenga jumla shilingi trilioni 80.076 kwa ajili ya programu na miradi ya maendeleo, ikiwa ni sawa na wastani wa 35% ya Bajeti Kuu ya Serikali katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, kupitia bajeti za maendeleo, hizo zilizoidhiniwa na Bunge lako Tukufu katika kipindi cha Bunge hili na utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi na wadau wengine wa maendeleo, imeweza kuchochea ukuaji wa uchumi, uwezeshwaji wa wananchi kiuchumi, kuimarisha na kupanua huduma za jamii, na kuboresha ustawi wa wananchi kwa ujumla. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ni kama ifuatavyo: -

(i) Kuongeza uwezo wa kuzalisha umeme kutoka Megawati 2,138 mwaka 2024 hadi za sasa Megawati 4,031.71 ilipofika Aprili, 2025, sawa na ongezeko la 86.6%. Hii ni hatua

kubwa kwa sababu umeme ndiyo kichocheo kikubwa cha ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, tuliseme hili, ni kwamba, katika miaka 60 ya uhuru wetu, tuliweza kuzalisha umeme takribani Megawati 1,600, lakini katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2020/2021 kuja mpaka leo, tumeweza kuzalisha Megawati 2,115. Kwa hiyo, inawezekana kukimbia katika mbio za maendeleo.

(ii) Katika jitihada za kuendelea kuifungua nchi na kutumia jiografia yetu vizuri, tumeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha Kimataifa. Kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wanafahamu, tayari reli imeshaanza kufanya kazi na ujenzi katika vipande ambavyo vimebaki unaendelea kwa kasi;

(iii) Tumekamilisha ujenzi wa daraja la kisasa la Kigongo – Busisi, lenye urefu wa kilimeta 3.2 lililopo Mwanza. Utekelezaji wake umekamilika na daraja hili linatarajiwa kuzinduliwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, tarehe 19 Juni, 2025; *(Makofi)*

(iv) Tumekamilisha ujenzi wa madaraja ya juu ya Uhasibu na Chang'ombe katika Jiji la Dar es Salaam. Kukamilika kwa madaraja haya kunachochea ukuaji wa uchumi, kurahisisha usafiri ndani ya Jiji la Dar es Salaam;

(v) Kuongezeka kwa matumizi ya mbolea kutoka tani 580,623 mwaka 2022/2023 hadi tani 840,714 mwaka 2024, na hivyo, kuendelea kuchochea tija katika uzalishaji katika Sekta ya Kilimo kulikosababisha nchi yetu kuendelea kujitosheleza katika chakula kufikia 128% mwaka 2024/2025 ukilinganisha na 124% kwa mwaka 2023/2024;

(vi) Kuongezeka kwa mchango wa viwanda katika ajira zote kutoka asilimia nane nukta moja mwaka 2023 hadi 12.8% mwaka 2024; na kuongezeka kwa mchango wa bidhaa zilizozalishwa viwandani kwa teknolojia ya juu katika mauzo nje kutoka 25% mwaka 2023/2024 hadi 36% mwaka 2024/2025;

(vii) Kuongezeka kwa idadi ya watalii nchini kutoka watalii milioni 3.7 mwaka 2023/2024 hadi kufikia watalii milioni 4.244;

(viii) Kutokana na kuimarika kwa miundombinu ya uchumi na mazingira ya uwekezaji, kumeendelea kuongezeka kwa miradi ya uwekezaji ambapo katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi 2025, Kituo cha Uwekezaji Nchini, *(TIC)* kilisajili jumla ya miradi mipya 691 yenye thamani ya dola za Kimarekani bilioni 7.9 ikiwa ni ongezeko la 35.8% katika mwaka huu (2025);

(ix) Kuongezeka idadi ya wanafunzi wanaomaliza darasa la saba na kujiunga kidato cha kwanza kutoka 48% mwaka 2019/2020 hadi 70% mwaka 2024/2025;

(x) Kuendelea kuimarika kwa upatikanaji wa huduma za afya karibu na wananchi kwa kujenga zahanati 980, vituo vya afya 367, hospitali mpya za halmashauri 129, hospitali tano za rufaa za mikoa na Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini Mtwara pamoja na kukarabati hospitali kongwe 50 na kuboresha hospitali tisa za rufaa za mikoa; *(Makofi)*

Aidha, Serikali imekamilisha ujenzi wa majengo 116 ya huduma za tiba za dharura na ajali na kuweka vifaatiba vya kisasa na hivyo kuwezesha kuwa na mfumo wa huduma za dharura kuanzia ngazi ya Taifa hadi ngazi ya Hospitali za Wilaya; na

(xi) Kuimarika kwa upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama ambapo idadi ya wananchi vijijini wanaopata huduma ya maji ilifikia 79.7% mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, kama unavyofahamu, mwelekeo wa muda mrefu wa sera za kiuchumi za Chama cha Mapinduzi (Chama Tawala) ni kujenga uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea na kutekeleza sera ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kwa lengo la kutokomeza umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuwezesha wananchi kiuchumi kuna hatua mbili za msingi: -

(i) Ni kuweka mazingira ya wananchi kujitengenezea kipato kwa njia ya kuajiriwa, kujiajiri au biashara;

(ii) Ni Serikali kuwapunguzia wananchi gharama za maisha kwa kuwaondolea baadhi ya gharama za lazima.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka minne iliyopita ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan (2021 – 2024), Serikali ilichukua hatua mahsusi nne zifuatazo katika kuwapunguzia gharama wananchi kwa kuondolewa gharama za lazima ambazo wangezifanya.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi ziliwaokolea wananchi jumla ya shilingi trilioni 5.724 ambazo kama Serikali ingezibeba, ingebidi wananchi wazibebe na hivyo kuweza kuwanufaisha wananchi milioni 11.036. Hatua hizi ni kama ifuatavyo: -

(i) Katika kipindi cha 2020 hadi 2024, Serikali ya CCM ilitumia shilingi bilioni 961.5 kama ruzuku iliyotolewa kwa kaya masikini ili kuziwezesha kuongeza kipato cha kaya katika kuzisaidia kaya hizo kumudu gharama za mahitaji ya msingi kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini *(TASAF)* na kunufaisha wananchi milioni 5.2. Serikali ili-*pump* katika uchumi moja kwa moja kwa wananchi bilioni 900.5;

(ii) Katika kipindi cha 2020 – 2024, Serikali ya CCM ilitumia shilingi bilioni 693.6 kama ruzuku ya mbolea ili kupunguza makali ya bei kwa wakulima, na jumla ya wakulima milioni 2.2 waliweza kunufaika. Hizi ni fedha ambazo katika hali ya kawaida wakulima wetu wangezitumia kununua mbolea, lakini Serikali ilitoa ruzuku na hizi fedhea wananchi wali-*save* ziweze kubaki katika mifuko yao; *(Makofi)*

(iii) Katika kipindi cha 2020 – 2024, Serikali ya CCM ilitumia shilingi trilioni 1.31katika kuendelea kutoa elimu bila ada kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha sita ambapo jumla ya wanafunzi

milioni 3.314 walinufaika. Kama unavyofahamu, Serikali iliondoa ada, na kuondoa ada huku, tumeweza kuwaokolea wananchi shilingi trilioni 1.8; na *(Makofi)*

(iv) Serikali ya CCM ilitumia shilingi trilioni 2.760 kwa ajili ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, ambapo wanafunzi 321,215 walinufaika. Hizi shilingi trilioni 2.76 pia tuliweza kuokoa kutoka kwenye mifuko ya wananchi ambao wangeweza kuitumia.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina ya kuhusu tathmini ya utekelezaji kwa mwaka 2024 tumeyaainisha katika kitabu ambacho tumekigawa kwa Waheshimiwa Wabunge. Haya ni mafanikio makubwa ambayo tumeyaonyesha kwa tathmini ambayo imefanywa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, sambamba na matokeo ya tathmini ya utekelezaji wa mipango ya Serikali niliyoieleza hapo juu, tathmini ya kitafiti inaonyesha pia kwamba wananchi walio wengi katika nchi yetu, wanaridhishwa na utendaji wa Serikali katika kutekeleza programu na miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, utafiti uliofanywa na Taasisi ya *Afrobarometer* mwezi Juni – Julai, 2024 unaonyesha kuwa 71% ya wananchi waliohojiwa walisema wanaridhishwa na utendaji wa Serikali, na 70% walisema nchi ipo katika mwelekeo sahihi.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, wastani wa nchi za Afrika, wastani wa idadi ya wananchi wanaoridhishwa na utendaji wa Serikali zao, Afrika ni 40%, kwa Tanzania ni 71%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tathmini hizi ambazo tunazieleza hapa siyo tu kwa mtazamo wa Serikali, lakini pia pale ambapo wananchi wanahojiwa, walio wengi wanaona kwamba tunafanya kazi nzuri na tuendelee kuchapa kazi.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kueleza sasa malengo na vipaumbele katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka

2025/2026. Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/2026 unaongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inayolenga kuwezesha Tanzania kuingia katika kundi la nchi za uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025 ambapo tuliingia mwaka 2020, miaka minne kabla ya muda na kuwa na kiwango cha juu cha maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Spika, aidha, mpango unaopendekezwa ni wa mwisho katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Hivyo, mpango huu umejikita katika kuendeleza na kukamilisha utekelezaji wa afua zinazotoa matokeo katika maeneo matano ya kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, kwa Waheshimiwa Wabunge, miradi ambayo mwaka huu itapewa kipaumble ni ile miradi ambayo inaendelea na miradi ambayo tunaamini itachochea kukamilisha utekelezaji wa afua ambazo zitatoa matokeo chanya katika kukamilisha utekelezaji wa vipaumbele ambavyo tunavyo katika Mpango wetu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika, Mpango huu ni kiungo kati ya mipango inayokamilika na mipango mipya inayotarajiwa kutekelezwa chini ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Hivyo basi, Mpango huu utajielekeza katika kuainisha na kutekeleza programu na miradi muhimu ambayo haijakamilika ili kuandaa mazingira shirikishi na endelevu kwa mipango ijayo.

Mheshimiwa Spika, nguzo muhimu ya maandalizi ya Mpango ni ukuaji wa uchumi pamoja na maeneo matano ya vipaumbele yaliyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya vipaumbele vya Mpango yamezingatia vigezo vilivyoainishwa kwenye Mpango ambavyo ni ukuaji endelevu wa uchumi, kupunguza umaskini, kuzalisha ajira, kuimarishwa kwa ushindani katika masoko ya kikanda na Kimataifa, maendeleo endelevu, utawala bora na utawala wa sheria. Vilevile, Mpango huu unalenga kutekeleza na kukamilisha

programu na miradi ya maendeleo ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha ufanisi wakati wa utekelezaji, Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi itaweka mkazo katika maeneo ya miradi ya kielelezo yenye manufaa na matokeo makubwa na kujielekeza katika vipaumbele vitano vifuatavyo: -

(i) Kuchochea uchumi shindani na shirikishi;

(ii) Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji wa Bidhaa Viwandani na Utoaji Huduma;

(iii) Kukuza Uwekezaji na Biashara;

(iv) Kuchochea Maendeleo ya Watu; na

(v) Kuendeleza Rasilimali Watu.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia vipaumbele vilivyoainishwa, Serikali itaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kielelezo na kimkakati. Baadhi ya miradi itakayoendelea kutekelezwa ni pamoja na: -

(i) Miradi ya kuongeza uwezo wa uzalishaji katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi ikiwemo ya kuongeza matumizi ya mbegu bora na mbolea, kuongeza eneo la umwagiliaji na kukamilisha ujenzi wa bandari za uvuvi;

(ii) Miradi ya ujenzi wa miundombinu ya usafiri na uchukuzi, pamoja na miundombinu ya kidigitali kwa ajili ya kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii, ikiwemo kuendelea na ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha cha Kimataifa *(SGR)*, kuendelea na utekelezaji wa mradi wa uimarishaji wa Shirika la Ndege Tanzania, kuendelea kuboresha na kupanua mtandao wa barabara nchini, hususan zinazounganisha maeneo ya uzalishaji vijijini na masoko, kukamilisha ujenzi wa daraja la (hili nimeshalitaja), mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta, kuendelea na upanuzi wa miundombinu ya

digitali ili kupanua matumizi ya TEHAMA katika uzalishaji, biashara na utoaji wa huduma kwa wananchi;

(iii) Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme;

(iv) Kuendelea na utekelezaji wa miradi inayolenga kuleta maendeleo ya watu ikiwemo utekelezaji wa sera mpya ya elimu, miradi ya afya, maji na usafi wa mazingira; na

(v) Miradi ya kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuhamasisha wawekezaji kutoka nje na kuwezesha uwekezaji wa ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Mafanikio ya utekelezaji wa nilivyovitaja yanajengwa katika nguzo na misingi ifuatayo: -

(i) Kuendelea kuwepo kwa amani, utulivu na usalama wa ndani ya nchi, katika nchi jirani na duniani kwa ujumla;

(ii) Kuendelea kudumisha utawala bora na utawala wa sheria nchini;

(iii) Kuendelea kuimarika kwa utoshelevu wa chakula nchini;

(iv) Kuendelea kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli za uwekezaji na biashara;

(v) Kuendelea kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi na majanga ya asili na yasiyo ya asili (ukame, vita, magonjwa ya mlipuko na mafuriko);

(vi) Kuwa na rasilimali watu iliyo bora na inayokidhi matakwa ya sasa ambayo yanatawaliwa na teknolojia na ubunifu;

(vii) Nidhamu katika matumizi ya fedha za umma na udhibiti wa deni la Taifa;

(viii) Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, ikiwa ni pamoja na kuwasaidia wafanyabiashara na wawekezaji wadogo na wa kati ili waongeze tija, wakue na kujirasimisha; na

(ix) Kuwa na nidhamu ya utekelezaji wa vipaumbele kama tuliyopanga katika mipango na mikakati ya Kitaifa na ya kisekta.

Mheshimiwa Spika, nihitimishe kwa kulihakikisha Bunge lako Tukufu kuwa hali ya uchumi wa nchi yetu kwa sasa ni himilivu, ukiwa na mwelekeo chanya na ukuaji endelevu. Kama nilivyoeleza, uchumi karibu nchi zote, uchumi wa dunia kwa ujumla, mpaka Mataifa makubwa unashuka. Uchumi wetu unakua, hili ni jambo jema.

Mheshimiwa Spika, kuimarika kwa uchumi kunatokana na usimamizi makini wa sera za uchumi jumla, pamoja na ushiriki wa wananchi wote katika ujenzi wa Taifa lao. Ninawashukuru na kuwapongeza Watanzania wote kwa mshikamano huu wa kizalendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapohitimisha, ninaomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM kwa uamuzi wao sahihi wa kuwachagua, hapo tarehe 18 - 19 Januari, 2025, kuwachagua Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu kuwa Mgombea wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kuwa mgombea wake mwenza katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka huu, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuteuliwa kuwa mgombea wa nafasi ya Urais wa Zanzibar kupitia tiketi ya Chama cha Mapinduzi (CCM). Ni imani yangu na uhakika kwamba hii ni timu sahihi ya kuiongoza Tanzania kufikia maendeleo makubwa zaidi katika miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Spika, nina imani na wananchi wa Tanzania na Zanzibar kwamba watafanya uamuzi sahihi wa kuwachagua katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu, 2025. Hakika "Kazi Na Utu – Tunasonga Mbele." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwashukuru sana viongozi wenzangu katika Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, pamoja na Tume ya Taifa ya Mipango kwa ushirikiano wao katika kuandaa Taarifa ya Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, viongozi hawa ni pamoja na Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge wa Jimbo la Maswa Mashariki na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, ambaye anafanya kazi nzuri sana, mtu rahim sana, mtu mwema sana, ambaye nchi hii inamhitaji. Nina uhakika wananchi wa Jimbo la Maswa Mashariki watatturudishia ndugu yetu huyu katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Dkt. Tausi Mbaga Kida, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; na Dkt. Fred Matola Msemwa, Katibu Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Mipango. Aidha, ninawashukuru Menejimenti na watumishi wote wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Tume ya Taifa ya Mipango kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi ya kuandaa Taarifa ya Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo wa Taifa ni shirikishi, iliyofanywa na wataalam wa Tume ya Taifa ya Mipango na wenzao kutoka Wizara ya Fedha. Aidha, katika mchakato wa kuandaa taarifa hizi mbili, tumeshirikiana kwa karibu na mdogo wangu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge wa Iramba Magharibi. Tumefanya kazi kwa ushirikiano.

Mheshimiwa Spika, kama unavyofahamu Ofisi yangu ina miaka miwili tu, nilikuwa nimeipokea kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba aliyekuwa Waziri wa Fedha na Mipango.

Ninamshukuru sana kwa jinsi ambavyo amenisaidia kuhakikisha ofisi inasimama. Amenipa kila aina ya msaada, Mungu ambariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nimshukuru Dkt. Natu Mwamba Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali, pamoja na timu yake yote ya wataalam. Ninashukuru sana kwa ushirikiano ambao tumekuwa nao katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kusimamia uchumi wa nchi hii kuhakikisha kwamba unaendelea kukua na wananchi wetu wanafaidika na matunda yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa ushirikiano ambao wamenipa katika miaka hii miwili tangu niwe Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Ninawashukuru sana kwa michango yao, kwa pongezi zao, lakini kwa upendo wao mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wa kipekee, ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Ubungo kwa ushirikiano wao katika kipindi chote tangu niwe Mbunge wa jimbo hilo. Ninakishukuru Chama cha Mapinduzi kwa imani kubwa kilichonipatia ya kupeperusha bendera ya chama hiki katika uchaguzi wa mwaka 2020, na nina imani kubwa kwamba wananchi wa Jimbo la Ubungo na Chama cha Mapinduzi kitanirudisha nigombee na hatimaye kushinda tena Ubunge huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba hii pamoja na vitabu vya Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa inapatikana pia katika Tovuti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa ninaomba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hoja hii kwa sababu kwa kawaida huwa ni hoja ambayo ni pacha na hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Kwa utaratibu wetu wakati tunajadili wiki ijayo wakati tukiwa tunajadili Hotuba ya Bajeti, tutakuwa tukijadili hoja hii pia. Kwa hiyo, ili watu wasije wakachanganya mambo, mbona utaratibu mwingine haujaendelea? Kwa hiyo, huwa vinajadiliwa vyote kwa pamoja.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kusema hivyo, nimeletewa hapa ujumbe kwamba kuna wageni wawili ambao hawakuwa wametajwa, nao wanatoka Tume ya Mipango, nao ni Ndugu Angela Shayo Mkurugenzi wa Mipango ya Kitaifa Tume ya Mipango, karibu sana. Ndugu Aristides Mbwasi Mkurugenzi wa Idara ya Uwekezaji wa Sekta Binafsi, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo la mdahalo na tangazo linatoka kwa Katibu wa Bunge. Waheshimiwa Wabunge wote, mnatangaziwa kuwa kesho kutakuwa na Mdahalo wa masuala ya Kibajeti na Uchumi utakaofanyika Ukumbi wa Msekwa kuanzia saa 4.00 asubuhi. Mada mbalimbali zitawasilishwa na wataalamu wa uchumi kutoka Wizara ya Fedha, Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Benki Kuu ya Tanzania; na Wizara ya Mipango na Uwekezaji.

Waheshimiwa Wabunge wote mnashauriwa kuhudhuria mdahalo huu ambao ni muhimu sana ili kujifunza zaidi, lakini pia kuelewa zaidi masuala ikiwa ni pamoja na haya ambayo Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Uwekezaji ameyasema kwa ufupi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wataalam watapata nafasi ya kutudadavulia mambo mengi, na yale ambayo yatakuwa hayajaeleweka, basi kule mtakuwa mnaruhusiwa kuuliza maswali. Kwa hiyo, mpango huu umewekwa maalum kabisa kwa ajili yetu Waheshimiwa Wabunge, ili tuwe na uelewa mpana wa masuala haya yote ambayo tumeshamsikia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, lakini baadaye tutamsikia Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Sasa hayo yote pamoja tutaelezana vizuri kesho kwenye mdahalo. Kwa hiyo, naomba msikose.

Baada ya kusema hayo, ninasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 leo jioni.

*(Saa 4.47 Asubuhi Bunge Lilisitishwa hadi Saa Kumi Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, japo sijayaelewa hayo makofi, lakini ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Katiba yetu Ibara ya 63 Mheshimiwa Rais kama sehemu ya Bunge hili, leo atakuwa pamoja nasi na tutamwona kupitia *television.* Kwa hiyo, atakuwa akitufuatilia moja kwa moja akiungana nasi. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD - KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Fedha Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, aje awasilishe hoja kuhusu Bajeti ya Serikali. Mheshimiwa Waziri, karibu. *(Makofi/Vigelegele)*

*(Hapa Waziri wa Fedha Mhe. Dkt. Mwigulu L. N. Madelu aliingia Ukumbini akiongozwa na Mpambe wa Bunge, kuwasilisha Bajeti Kuu ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikari kwa Mwaka 2025/2026. Uwasilishaji wa bajeti hii umezingatia Ibara 137 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, ikisomwa pamoja na Kifungu cha 23 (3) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni ya 124 (4) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hotuba hii, vipo vitabu vinne sambamba na hotuba hii, vinavyoelezea kwa kina takwimu za Bajeti ya Serikali. Kitabu cha Kwanza kinahusu Makadirio ya Mapato yatakayowezesha utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, Kitabu cha Pili kinahusu Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala wa Serikali. Kitabu cha Tatu ni Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na Kitabu cha Nne kina Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Ofisi za Wakuu wa Mikoa pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, upo pia Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2025, Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa mwaka 2025 pamoja na Taarifa ya Vihatarishi vya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2025/2026 ambayo ni sehemu ya bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki vikao vya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hadi tunapoelekea kuhitimisha muda wa uwakilishi wa wananchi kwa awamu hii.

Mheshimiwa Spika, kwa moyo wa simanzi na huzuni kubwa niruhusu nitoe pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watanzania kwa ujumla kwa kuondokewa na wapendwa wetu. Mtakumbuka kuwa tumewapoteza viongozi mbalimbali wa Kitaifa, Wabunge wenzetu, watu wengine mashuhuri pamoja na wananchi wa Tanzania wenzetu. Bwana alitoa na Bwana ametwaa, jina la Bwana lihimidiwe.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, nitumie fursa hii kuwaomba wananchi waungane nami kumpongeza Mheshimiwa Prof. Mohamed Yakub Janabi, Mkurugenzi wa Hospitali yetu ya Taifa Muhimbili na Mshauri wa Rais wa Afya kwa kutuheshimisha tena na kushinda kwa kishindo uchaguzi wa Ukurugenzi wa Shirika la Afya Duniani *(WHO)* Kanda ya Afrika. Ushindi huu ni alama nyingine ya kazi nzuri anayoifanya pamoja na kutambuliwa kwa mchango wa nchi yetu Barani Afrika. Kwa ushindi huu wa Prof. Janabi, hakika naiona Afrika yenye watu wenye afya njema na wanaozingatia ulaji wenye afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2024/2025, Serikali ilipanga kukusanya jumla ya shilingi trilioni 50.29 kutoka katika vyanzo vya ndani na nje. Hadi Mei, 2025 kiasi cha shilingi trilioni 45.07 kimekusanywa, sawa na 89.6% ya lengo la mwaka. Mchanganuo wa mapato yaliyokusanywa katika kipindi hicho ikilinganishwa na lengo la mwaka ni kama ifuatavyo: -

a) Mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*, yalikuwa shilingi trilioni 26.86, sawa na 91.3% ya lengo;

b) Mapato yasiyo ya kodi yanayokusanywa na Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala za Serikali yalifikia shilingi trilioni 2.97, sawa na 77.4% ya lengo;

c) Mapato yaliyokusanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa yalifikia shilingi trilioni 1.26, sawa na 93.2% ya lengo;

d) Misaada na mikopo nafuu kutoka nje iliyopokelewa ilikuwa shilingi trilioni 5.32, sawa na 87.5% ya lengo;

e) Mikopo ya ndani ikijumuisha mikopo ya kulipia dhamana za Serikali zilizoiva ilifikia shilingi trilioni 6.23, sawa na 94.1% ya lengo; na

f) Mikopo ya masharti ya kibiashara ya nje ya nchi ilifikia shilingi trilioni 2.43, sawa na 81.3% ya lengo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita imefanya mageuzi makubwa ambayo yameongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani. Ifahamike kuwa, kuimarika kwa makusanyo ya mapato ya ndani ni msingi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, utoaji wa huduma bora kwa wananchi na ustawi wa Taifa kwa ujumla, Kodi Yetu Ndiyo Maendeleo Yetu. Kila Mtanzania anapaswa kuelewa kwamba maendeleo hayawezi kupatikana kwa kutegemea misaada, ni lazima tulipe kodi, ni lazima tulipe kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Makadirio ya Matumizi yaliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka 2024/2025 ni shilingi trilioni 50.29 ambapo shilingi trilioni 33.75 ni matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 16.54 ni matumizi ya maendeleo. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Mei, 2025 ridhaa ya matumizi iliyotolewa ilikuwa shilingi trilioni 42.90, sawa na 85.3% ya lengo la mwaka.

Mheshimiwa Spika, kati ya kiasi hicho, ridhaa ya matumizi ya shilingi trilioni 30.63, sawa na 90.8% ya lengo la mwaka ilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, ridhaa ya matumizi ya shilingi trilioni 15.74, sawa na 95.1% ya lengo la mwaka ilitolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo 95.1% ya lengo la mwaka. Ridhaa ya matumizi ya maendeleo ilijumuisha shilingi trilioni 3.47 kutoka kwa washirika wa maendeleo ambacho kilipelekwa moja kwa moja kwenye utekelezaji wa miradi *D-Fund*.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maeneo yaliyopelekewa fedha katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Mei, 2025 ni pamoja na ugharamiaji wa deni la Serikali, ugharamiaji wa mishahara ya watumishi wa umma, maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, aidha, mtakumbuka kuwa michango ya wakandarasi, wazabuni, watoa huduma kwa ajili ya kujenga Taifa, Serikali iliendelea kulipa madeni yaliyohakikiwa ambapo kiasi cha shilingi trilioni 1.01 kimelipwa kwa ajili ya ulipaji wa wakandarasi waliofanya kazi za maendeleo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uhimilivu wa deni la Serikali, hadi Aprili, 2025 deni la Serikali lilikuwa shilingi trilioni 107.70. Kati ya kiasi hicho, deni la nje ilikuwa ni shilingi trilioni 72.94, na deni la ndani ni shilingi trilioni 34.76. Tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Oktoba, 2024 imeonesha kuwa deni ni himilivu katika kipindi cha muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, katika tathmini hiyo, viashiria vinaonesha kuwa kwa mwaka 2024/2025, thamani ya sasa ya deni la Serikali kwa pato la Taifa ni 40.3% ikilinganishwa na ukomo wa 55%, hatupaswi kuwa na hofu kabisa kuhusu jambo hili. Kwa upande wa thamani ya sasa ya deni la nje kwa pato la Taifa ni 23.6% ikilinganishwa na ukomo wa 40% ambayo ni *standard* ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni 123.8% ikilinganishwa na ukomo wa 180%, hatupaswi kuwa na hofu na jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2025 kampuni ya *Moody's Investors Service* ilifanya zoezi la mapitio ya kwanza ya tathmini ya nchi kukopesheka katika masoko ya fedha ya Kimataifa kwa mwaka 2025, ambayo inaongelea pia uimara wa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa zoezi hilo, kampuni hiyo ilichapisha matokeo ambayo yameendelea kuiweka Tanzania katika daraja la B1 kama ilivyokuwa kwa matokeo ya mwisho ya mwaka 2024. Aidha, kampuni nyingine kubwa *Fitch Ratings* inaendelea na mapitio ya kwanza kwa mwaka 2025 na inatarajia kuchapisha matokeo hivi karibuni. Kampuni hiyo ilichapisha matokeo ya mapitio ya mwisho Desemba, 2024 ambapo iliiweka Tanzania katika daraja la B+.

Mheshimiwa Spika, katika matokeo ya tathmini ya nchi kukopesheka katika masoko ya mitaji na uhimilivu na uimara wa uchumi Kimataifa yanaendelea kuipa taswira chanya nchi yetu katika medani za Kimataifa. Matokeo hayo ni bora kuliko nchi nyingine za ukanda wa Afrika Mashariki na Kati na Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine, matokeo hayo yamechangiwa na jitihada za Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni katika kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji kwa sekta binafsi, kukuza uchumi, kusimamia kwa makini deni la Serikali na kuimarisha ushirikiano wa Kimataifa, yaani diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ili kuhakikisha deni linaendelea kuwa himilivu ikiwemo kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi wa mikopo katika ugharamiaji wa bajeti, kuelekeza fedha za mikopo katika miradi inayokuza mapato ya ndani na mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi, na kuendelea kuwahimiza Maafisa Masuuli kuzingatia maandalizi ya msingi ya miradi kabla ya kuingia mikataba kwa mujibu wa sheria, kanuni

na miongozo iliyopo ili kuepuka ongezeko la gharama za mradi unayokopewa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea zaidi, naomba nitoe maelezo ya jumla. Kwa ujumla, kwa kuwa bajeti hii ni ya mwisho kabla ya kuelekea kwenye Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2025 sina budi kubainisha masuala muhimu ili wananchi watakapokuwa wameshika kalamu zao za maamuzi, wasisite kuweka alama ya vema kwa mgombea Urais na mgombea mwenza na wagombea wa nafasi za Ubunge, Uwakilishi na Udiwani kupitia Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa mgombea wa Chama cha Mapinduzi katika nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye Uchaguzi Mkuu utakaofanyika Oktoba, 2025.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawapongeza Wajumbe wa Halmashauri Kuu na Mkutano Mkuu wa CCM kwa kumchagua kiongozi huyu makini kupeperusha Bendera ya Chama katika Uchaguzi Mkuu. Ni ukweli usiopingika kuwa kuchaguliwa kwake kugombea nafasi hiyo kumetokana na juhudi za kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM kikamilifu ili kuwaletea wananchi maendeleo. Ni dhahiri kuwa chombo madhubuti bila nahodha imara na hodari hakiwezi kumudu mawimbi. Hakika Tanzania ya Mama inameremeta.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Chama cha Mapinduzi kilimteua Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kuwa mgombea mwenza wa nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa tiketi ya CCM. Watanzania wanamfahamu Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa misimamo yake thabiti isiyoyumba kwenye masuala ya msingi yenye maslahi mapana kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa misimamo hiyo inaenda sambamba na falsafa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan

ya kutokutetereka wala kuyumba kwenye masuala yenye maslahi mapana kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kuwa mgombea wa CCM katika nafasi ya Urais wa Zanzibar kwenye Uchaguzi Mkuu utakaofanyika Oktoba, 2025. Hivyo, ninawasihi wananchi wa Zanzibar kumchagua tena Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kuwa Mheshimiwa Rais ili aweze kuendeleza mazuri yote aliyoanzisha.

Mheshimiwa Spika, uteuzi huu umeleta matumaini mapya kwa Watanzania kwa kuwa uchaguzi mkuu utakwenda kuwapa Watanzania viongozi wanaokidhi matarajio yao. Tunamfahamu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunamfahamu Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, tunamfahamu Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Hatubahatishi, hatubahatishi! Hakika kwa safu hii, Oktoba, 2025 ushindi ni mapema mno. Mapema! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa safu hiyo, tuna uhakika kuwa Serikali tutakayoichagua itasimamia uhuru wa Taifa letu, italinda Utaifa na Muungano wetu, itaendelea kupambana na wahujumu uchumi, wala rushwa, mafisadi, wakwepa kodi na wazembe katika ofisi za umma. Huu ndiyo umekuwa msimamo na maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kila wakati anapokutana nasi wasaidizi wake.

Mheshimiwa Spika, Chama cha Mapinduzi kimewaletea Watanzania safu hii ya wagombea kwa sababu bado kuna kazi ya kufanya. Tumemaliza baadhi ya miradi ya kimkakati, lakini bado tuna kazi ya kuendelea na miradi ya kimkakati kwenye vipengele vilivyosalia. Tumemaliza suala la upatikanaji wa huduma za afya, tunakwenda kwenye ubora wa huduma za afya, tumemaliza upatikanaji wa elimu, lakini sasa tunakwenda kwenye ubora wa elimu anayopewa mtoto wa Kitanzania, tumemaliza kufikisha umeme kila Kijiji, sasa tunakwenda kwenye ngazi ya kitongoji na kaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakwenda kwenye upatikanaji wa maji kwenye kila kaya, ubora wa miundombinu ya barabara mijini na vijijini, *modernization* kwenye shughuli za uzalishaji ikiwepo kilimo ambayo tayari kazi hiyo imeanza, mbegu bora, ufugaji wa kisasa na uvuvi wa kisasa, kuongeza thamani mazao ya ndani ya nchi na kuongeza ujenzi na upanuzi wa viwanda na kuweka mazingira yaliyo bora ya uwekezaji na kufanya mazingira bora ya kufanya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa undani mambo haya yameongelewa na Ilani bora kabisa ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi iliyowasilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine kama Mtanzania na kwa Watanzania wote, tuna kila sababu ya kujivunia umoja wetu na Utaifa wetu, Muungano wetu na hatua kubwa za kimaendeleo ambazo tumezipiga tangu tulipopata uhuru mwaka 1961. Tumevishinda vita vya ukabila (hatuulizani makabila), tumevishinda vita vya udini, tunasonga mbele pamoja na umoja wetu na Utaifa wetu na Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, pongezi nyingi ziende kwa kila Mtanzania kwa ushindi huo, kwa uzalendo huo na uhodari huo wa kulipenda Taifa letu. Tangu kuasisiwa kwake, Tanzania limekuwa Taifa kimbilio kuanzia majirani na hata Mataifa ya mbali. Jambo hilo tulilinde kwa wivu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, historia hii njema katu haiwezi kutengwa na kazi nzuri iliyofanywa na Chama chenye vinasaba vya ukombozi (Chama cha Mapinduzi) ambacho kilirithi harakati za ukombozi tangu kuanzishwa kwake kwa muungano wa vyama vya *TANU* na *ASP*. Chama cha Mapinduzi kimeendelea kuwa Chama pekee Tanzania, Afrika na duniani kote ambacho mchango wake katika historia ya ukombozi hapa nchini na Kusini mwa Afrika hauwezi kutenganishwa nacho.

Mheshimiwa Spika, Chama cha Mapinduzi ndiyo kimeongoza vita dhidi ya maadui wakuu watatu aliowatangaza Mwalimu Nyerere, yaani ujinga, maradhi na umaskini. Ni dhahiri

kuwa nchi yetu imepiga hatua kubwa sasa katika kukabiliana na maadui hao ambao walitangazwa na Rais wetu wa kwanza Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati tunapata uhuru, asilimia kubwa ya Watanzania walikuwa hawajui kusoma na kuandika. Tulianza na idadi ndogo sana ya shule za msingi na sekondari pamoja na vyuo pamoja na idadi ndogo ya wanafunzi. Kwa mfano, kwa mwaka 1961 tulikuwa na shule za msingi 3,270, walimu 9,000 na wanafunzi 486,000; shule za sekondari 41 tu, walimu 764 tu na wanafunzi 11,000; vyuo vya ualimu nane tu na walimu 164 tu na wanafunzi 1,723 tu; na Chuo Kikuu kikiwa kimoja tu na wahadhiri sita na wanafunzi 14 tu. Hapa ndipo nchi ilipoanzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii tunavyoongea, kwa takwimu za mwaka 2024 nchi yetu sasa imefikisha shule za msingi 20,533 kutoka shule 3,000, walimu 229,000 kutoka walimu 9,000 na wanafunzi 11,000 kutoka wanafunzi 400,000 na shule 6,269 za sekondari kutoka shule 41 tu, walimu 128,000 kutoka walimu 764 tu, na wanafunzi 300,300 kutoka wanafunzi 11,000, vyuo vya ualimu 65 kutoka nane, na walimu 1,633 kutoka walimu 164 na vyuo vikuu 79 kutoka chuo kikuu kimoja, na wahadhiri 8,625 kutoka wahadhiri sita huku wanafunzi wakiwa 334,000 kutoka wanafunzi 14. Hayo yote yalikuwa katika kumpiga vita adui ujinga na yamefanyika chini ya uongozi wa CCM. CCM na iheshimiwe, imefanya kazi kubwa mpaka hapa tulipofika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kumpiga vita adui maradhi, hatua kubwa imefikiwa katika nyanja zote ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya afya, wataalamu wa afya wa ngazi zote, upatikanaji wa vifaatiba, dawa na vitendanishi. Wakati tunapata uhuru, tulikuwa na madaktari watano tu, ambapo kwa sasa ukiongelea madaktari bingwa peke yake tunao 2,469 na zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati tunapata uhuru, huduma za afya kwa nchi nzima zilikuwa duni sana, sasa tuko hatua kubwa na tunaelekea kwenye Bima ya Afya kwa wote, tukiwa tumefanikiwa kupunguza vifo vya watoto, vifo vya wakina mama wajawazito,

kuimarisha huduma za kibingwa hapa nchini, na sasa Tanzania inakuwa nchi kimbilio kwa ajili ya huduma za kibingwa. Mafanikio hayo ni dhahiri kwamba harakati na jitihada za kumpiga vita adui maradhi na hayo yote yamefanikiwa ikiwa ni chini ya uongozi wa Chama cha Mapinduzi. CCM na iheshimiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kumpiga vita adui umaskini, Taifa limepiga hatua kubwa, ambapo takwimu rasmi zinaonesha kuwa kati ya mwaka 1991 na 2018, umasikini umepungua. Mathalani, katika kipindi hicho cha marejeo, asilimia ya watu waliokuwa wakiishi katika umasikini wa hali ya juu (umasikini wa chakula) ilipungua kutoka kiasi kikubwa kutoka 21.6% hadi 8.0%, huku kiwango cha umasikini wa mahitaji ya msingi kikitoka 38.6% kwenda 26.4%.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Serikali ya Awamu ya Sita imeonesha uhimilivu mkubwa wa kukabiliana na misukosuko ya kiuchumi ya ndani na nje ya nchi iliyosababishwa na majanga ya asili pamoja na mabadiliko ya tabianchi na yale ya kibinadamu yanayohusiana na mizozo ya Kimataifa pamoja na mabadiliko ya kisera.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kuwa msukosuko wa kiuchumi ulioikumba dunia kwa muda mrefu ulitokana na mzozo wa Ulaya Mashariki uliofuatia baada ya UVIKO 19 na umesababisha kupanda kwa gharama za maisha na madhara mengineyo ikiwemo kupanda kwa gharama za usafirishaji na uzalishaji. Hali hii ilisababisha nchi nyingi kuingia kwenye madeni makubwa. Hata hivyo, Serikali ilichukua hatua za haraka na madhubuti kukabiliana na madhara yaliyojitokeza na hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kutoa ruzuku kwa kaya maskini ili kuwapunguzia makali Watanzania ambapo zaidi ya shilingi bilioni 9,615 zilitumika, kuendelea na mpango wa kutoa elimu bila ada ambapo takribani shilingi trilioni 1.3 zimetumika, kuendelea kutoa mikopo kwa elimu ya juu ambapo zaidi ya shilingi trilioni 2.7 zimetumika, na kulipa nusu ya bei ya mbolea ambayo mkulima anatumia. Mkulima wa Tanzania amelipiwa nusu ya bei ya mbolea ili aweze

kumudu manunuzi ya mbolea ambapo zaidi ya shilingi bilioni 708 zilitumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika programu hii ya ruzuku, Serikali imekuwa ikiwalipia wakulima wa Tanzania nusu ya gharama ya bei ya mbolea ili kuweza kuwawezesha kumudu gharama.

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, katika hatua nyingine Serikali ilitoa shilingi bilioni 100 kila mwezi katika kipindi ambacho dunia ilikuwa imekumbwa na uhaba wa nishati ya mafuta *(petrol, diesel* na mafuta ya taa). Hii iliwezesha nishati hizo muhimu kuwa na bei inayohimilika kwa kila Mtanzania na kuwezesha upatikanaji wake wa kila wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi nyingine hadi sasa hawajarejea katika hali ya kawaida ya kuweza kupata mafuta. Mafuta yanapatikana kwa mgao na kwa kipimo na kwa siku za kuweza kuyapata mafuta hayo. Hali hii imelifanya Taifa la Tanzania kuwa na uimara katika mfumuko wa bei, ukuaji wa uchumi, na viashiria vingine vya uchumi jumla.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali ilichukua hatua hizi kupunguza ama kufuta kodi katika baadhi ya bidhaa muhimu kama vile mafuta ya kula ili kumfanya Mtanzania kumudu gharama za maisha. Siyo kila nchi ilifanya jambo hili na hii inaonesha ni kiasi gani Serikali ya CCM inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inawajali wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ambayo yalijitokeza na kuleta taharuki katika Mataifa mengi ni pamoja na kuadimika kwa fedha za kigeni katika nchi nyingi za Afrika. Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania, imetekeleza vyema Sera ya Fedha na hivyo kuimarisha viwango vya kubadilisha fedha na upatikanaji wa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tumeshuhudia mabadiliko ya sera za nje hususan katika baadhi ya Mataifa makubwa ikiwemo nchi mbalimbali na wabia mengine wanaoshirikiana na Tanzania

kwenye maendeleo. Sera hizo zinajumuisha kufuta ama kupunguza misaada kupitia taasisi ama mashirika ya Kimataifa ya nchi hizo ambazo kwa sehemu ilikuwa ikitekeleza kushirikiana na Sekta Binafsi na sehemu na Serikali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kufuatia hali hiyo, Serikali imefanya tathmini ya kina na kubaini sekta ambazo zimeathirika na imeanza kuchukua hatua. Maeneo ambayo yaliguswa ikiwemo Sekta ya Afya ambapo mengine ni maeneo ambayo yanahusisha sekta za huduma za jamii. Serikali hadi sasa imetoa zaidi ya shilingi bilioni 82 kuweza kuziba pengo hilo na uhitaji wa fedha ambazo zilikuwa zinahitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika muda wa kati, Serikali itatenga bajeti itakayolenga kuziba pengo la fedha zilizokuwa zinatarajiwa kutoka kwa wahisani hao, na katika hatua ya muda mrefu, Serikali imepanga kuwekeza kwenye viwanda vinavyozalisha bidhaa hizo ambazo zilikuwa zinapatikana kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa mkakati wa utakaoongeza uzalishaji wa bidhaa ndani ya nchi na kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje *(import substitution)* pamoja na mkakati wa kuongeza mauzo nje ili kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni na kuimarisha thamani ya shilingi ya yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunao uwezo wa kushirikiana na Sekta Binafsi tukazalisha dawa za Malaria, Kifua Kikuu na magonjwa mengineyo ndani ya nchi, na jambo hili litafanyika. Ninaomba niwahakikishie Watanzania kuwa hakuna maisha ya Mtanzania yatapotea kwa kuwa tu kumepungua fedha za misaada ama fedha kutoka kwa wahisani ambao tulikuwa tunashirikiana nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizi ni baadhi tu ya hatua ambazo zimeoneshwa na Serikali na zimechukuliwa na Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kukabiliana na hatua zinazojitokeza katika masuala ya kiuchumi. Nitoe rai kwa Watanzania wote tunaoipenda nchi yetu tusiruhusu

misingi na nguzo za Taifa letu zitikiswe wala tusiingie kwenye mtego wa adui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sote ni mashahidi kuwa Mataifa yaliyowahi kuingia kwenye mifarakano kwa kiasi kikubwa ilisababishwa na mizaha mizaha na kutokuheshimu misingi ya Mataifa hayo ikiwemo maneno ya rejareja yasiyo na ushahidi; ya mtu mmoja mmoja yasiyo na ushahidi; na maneno ya rejareja ya taasisi ama baadhi ya vikundi yasiyo na ushahidi ama ya vyombo vya habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine uhalifu wa mtu mmoja mmoja tu au wa kikundi hujitokeza kwa kuwa na tishio kwenye maisha ya kila siku ya mtu ama mwananchi mmoja. Ikumbukwe kuwa katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tatu viliwahi kujitokeza vitu vya aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, ulikuwepo uhalifu, watu walikuwa wanateka magari ya mizigo, tunayakumbuka haya. Wakati mwingine wanateka mabasi ya abiria katika maeneo mbalimbali. Jambo la aina hiyo lilileta vitisho kwa wananchi wa Tanzania. Hata hivyo, vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vilisimama imara na kukomesha uhalifu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Nne ulitokea uhalifu mwingine wenye sura tofauti ambao ulikuwa unaweza ukaufananisha na sura ya kigaidi uliohusisha urushwaji wa mabomu kwenye nyumba za ibada, mikusanyiko ya watu, mikutano ya hadhara, mashambulizi ya mtu mmoja mmoja wakiwemo watu wenye ulemavu wa ngozi. Watanzania tumeyasahau haya?

Mheshimiwa Spika, matukio hayo yalitokea kwenye nchi yetu na yalileta tishio kubwa la mikusanyiko, makanisa, misikiti, na mikutano kurushiwa mabomu. Hata hivyo, vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vilisimama imara na kukomesha uhalifu huo. Vilisimama imara vyombo vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano, ulitokea tena uhalifu watoto kutekwa na kuuwawa, tunakumbuka hiyo; mtu mmoja mmoja kupigwa risasi kwenye makazi yake, wengine kwenye kazi zao na utekelezaji wa majukumu yake, mtu mmoja mmoja aliathirika sana kutokana na sintofahamu hiyo iliyokuwa inahusisha mtu mmoja mmoja kulengwa na kuuawa.

Mheshimiwa Spika, mtakumbuka, waliuawa Wenyeviti wa Vijiji (kwa Wilaya za Pwani watakumbuka vizuri jambo hili), vitongoji, mitaa na mbaya zaidi wengine walikuwa wanalengwa kwa nafasi zao na kwa itikadi zao. Wenyeviti wa CCM wengi tulishuhudia. Pia tulishuhudia miili kwenye magunia, na mifuko ikiwa imetupwa baharini.

Mheshimiwa Spika, ninayasema haya na ni mabaya kuyataja kwa sababu familia zilipoteza watu wao; lakini ninayasema kwa sababu watu wakumbuke kwamba tumewahi kupita vipindi vya aina hii, na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vilikomesha uhalifu wa aina hiyo; havijawahi kushindwa. Vilikomesha uhalifu wa vikundi na wa mtu mmoja mmoja na makao yao walipokuwa wameyaweka ndani ya nchi ambapo walikimbia na wengine walikutana na mkono wa sheria. Vyombo vyetu havijawahi kushindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata sasa vimeanza kujitokeza viashiria vya uhalifu kama huo ambavyo kimsingi havipaswi kupiganwa kwa kupeleka vikosi wala kupiga kampeni wala kusemasema tunapigana vipi, kwa sababu hii ni tofauti na vita ya vikosi kwa vikosi.

Mheshimiwa Spika, tukiendelea kunyoosheana vidole, na kunyooshea vidole vyombo vyetu vya ulinzi na usalama, tutaacha adui aendelee na uhalifu huku sisi tukiendelea kushughulikiana sisi kwa sisi. Hili siyo jambo lenye afya kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, isichukuliwe kuwa Serikali imezuia watu kusema, wala isichukuliwe kuwa Serikali haichukui hatua dhidi ya uhalifu, ninachokisema ni kwamba, vita ya aina hii, nimetaja,

miaka yote na maeneo yote na muda wote ambavyo ilikuwa inatokea, vilipiganwa kwa intelijensia. Hivyo, niwasihi Watanzania wenzangu, tuviache vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vifanye kazi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine uchochezi wa adui huwa ni kwa lengo la kuzifikia rasilimali, Mataifa ambayo yana rasilimali za kipekee, mengi yameingia kwenye matatizo kama hayo. Tunayo mifano, yakiwemo Mataifa yaliyokuwa na migogoro mingine ilichochewa na waliokuwa wanatamani rasilimali katika Mataifa hayo. Migogoro hiyo iliisha tu pale rasilimali zilipoisha.

Mheshimiwa Spika, uchochezi mwingine katika Mataifa mengi huwa unapenyezwa tu nyakati za uchaguzi kupitia wananchi; kwa wananchi wao kwa wao wanapoelekea kwenye chaguzi. Niwasihi Watanzania, sote tuwe macho, hatuna Taifa lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuna Taifa lingine zaidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nchi yetu ni hii hii, na utulivu, amani na usalama hatuna mbadala wake. Lazima tuendelee kufuata misingi iliyotufanya tukaishi mpaka muda huu tukiwa Taifa moja, tuishikilie ili tusije tukajaribu njia nyingine ambazo Mataifa mengine walipofuata walifikia kubaya. Watanzania hatuna Taifa lingine, hatuna Taifa lingine; *we have to calm down* na tulilinde Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuhakikisha kuwa mipaka yote ya nchi yetu imekuwa salama, pamoja na kuwepo kwa umoja, amani, mshikamano na utulivu. Jeshi letu la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeendelea kutoa mchango mkubwa hata katika kushiriki operesheni mbalimbali za ulinzi wa amani katika misheni mbalimbali za Umoja wa Mataifa na jumuiya za kikanda. Ushiriki huo umeimarisha diplomasia ya kiulinzi, ushirikiano wa Kimataifa na kuiletea sifa kubwa Tanzania, ndani na nje ya mipaka yetu.

Mheshimiwa Spika, ninavipongeza vyombo vyetu vya ulinzi na usalama chini ya Amiri Jeshi Mkuu Mheshimiwa Dkt. Samia

Suluhu Hassan kwa jitihada kubwa zinazoendelea kuchukuliwa ili kuweza kuhakikisha hali ya ulinzi, usalama na amani vinaendelea kuimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya jumla, sasa niende kwenye mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita. Kama unavyofahamu, bajeti ya mwaka 2025/2026 inakamilisha kipindi cha kwanza cha Awamu ya Sita ya Utawala wa Mama yetu Mpendwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sote ni mashahidi kuwa tangu ashike hatamu ya uongozi mwaka 2021, amesimama kidete kuhakikisha shughuli za maendeleo zinasonga mbele. Hakika ni mengi yamefanyika katika kipindi cha uongozi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ya Awamu ya Sita inapokea uongozi, utekelezaji wa miradi wa kielelezo, mfano ujenzi wa Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ambao ni wa *Megawatts* takribani 2,115 ulikuwa unaendelea ambapo hadi sasa tumeshakamilisha. Tumeshaanza kuvuna na tumeshaanza kupata matunda yake ambapo tayari *Megawatts* zimeshaanza kuwafikia wananchi, na zinaendelea kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utekelezaji wa ujenzi wa Daraja la Kigongo – Busisi lenye urefu wa zaidi ya kilomita tatu ambao unaunganisha upande mmoja wa Mkoa wa Mwanza na upande wa Mkoa wa Geita. Tayari umeshakamilika kwa 100% na unatarajiwa kuzinduliwa tarehe 19 Juni, 2025 na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alipokea pia, Mradi wa Reli ya Kisasa kwa vipengele ambavyo vilikuwa vimeshatekelezwa, *lot one* na *lot two,* ikiwemo 57.57% kwa kipande cha Morogoro hadi Makutupora sasa imeshafunguliwa na imeshaanza kutumika. Hivi tunavyoongea imesafirisha zaidi ya abiria 2,000,000 na zaidi ya shilingi bilioni 60.25 zimekusanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa pia, kwa upande wa *lot* zingine zilizosalia, kama alivyosema, ataendeleza na kukamilisha

miradi iliyopo na kuleta mipya. Mradi wa Makutupora – Tabora kwa sasa umeshafika zaidi ya 14.53%, Mradi wa Tabora – Isaka zaidi ya asilimia 6.65, Mradi wa Tabora – Kigoma na *Lot seven* ambazo hazikuwepo, tayari zimeshapata mkandarasi na siku si nyingi ataanza kazi yake kwa upande wa *lot seven* kwa kuwa, fedha zake zimeshapatikana. Katika kutekeleza malengo haya, Serikali itaendelea kutafuta fedha, ili kuweza kukamilisha maeneo mengine, ambayo yanahitaji ujenzi wa reli za kisasa kwa kiwango hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, upatikanaji wa rasilimali fedha utawezesha ujenzi wa Reli ya *SGR* kwa maeneo yaliyobaki. Tunajua kuna maeneo ambayo yako kwenye mipango ya ujenzi wa reli ikiwemo Kaliua – Mpanda – Karema; Mtwara – *Mbamba Bay* na matawi yake ya Liganga na Mchuchuma; Tanga – Arusha – Musoma; Reli ya Jiji la Dar es Salaam na Jiji la Dodoma. Kwa upande wa Reli ya *TAZARA*, Serikali za Tanzania, Zambia pamoja na China tayari walishasaini makubaliano ili kuweza kuifufua na kuiboresha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Uchukuzi. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali imeendelea kuwekeza katika bandari zetu hapa nchini, ili ziweze kutoa huduma kwa tija na ufanisi. Mafanikio ambayo yamepatikana ni pamoja na kuongeza mapato ya kodi ya forodha, ambapo katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Februari, 2025 jumla ya shilingi trilioni 8.26 zimekusanywa, ikiwa ni sawa na ongezeko la shilingi trilioni 1.18 ikilinganishwa na shilingi trilioni 7.08 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho Mwaka wa Fedha 2023/2024. Shilingi trilioni 1.18 ni ongezeko, ni tofauti ikilinganishwa na fedha zilizokusanywa kwa kipindi kama hicho kabla ya uwekezaji huo. Takwimu zinaongea kuliko maneno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo pia na ufanisi wa kupungua kwa gharama za uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam kutoka shilingi bilioni 975.0 hadi shilingi bilioni 685.2 katika kipindi hicho. Hii imewezesha kuwa na fedha za ziada kuanza utekelezaji wa miradi mingine ya kuendeleza bandari, ikiwa ni

pamoja na Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Matenki ya Kupokea Mafuta kwa Pamoja katika Bandari ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni ujenzi na ukarabati wa Viwanja vya Ndege vya Songwe – Mbeya, Mtwara, Songea, Iringa, Geita, Msalato, Kigoma, Tabora, Sumbawanga, Shinyanga, pamoja na Musoma. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni kuendelea kuliimarisha Shirika la Ndege Tanzania *(ATCL),* kwa kununua ndege zingine saba, ambapo ndege sita ni za abiria na moja ni ya mizigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ujenzi. Katika kuimarisha miundombinu yetu, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuongezeka kwa mtandao wa barabara zinazounganisha wilaya na mikoa pamoja na nchi jirani ambazo zinasimamiwa na *TANROADS* kutoka kilometa 36,361.95 mwaka 2021 hadi kilometa 37,435.04 Aprili, 2025. Kukamilika kwa ujenzi wa madaraja makubwa, kama ambavyo nimetoka kutaja, kubwa zaidi, lakini pia, yapo Madaraja ya Tanzanite, Wami, Ruhuhu kule Ruvuma, Mpwapwa kule Dodoma, Msingi kule Mkalama, Singida na Kigongo – Busisi ambalo nimetoka kulitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara za mijini na vijijini zinazosimamiwa na *TARURA*. Serikali ya Awamu ya Sita imeongeza bajeti kwa zaidi ya mara sita, hii imewezesha kufungua barabara nyingi za mijini na vijijini. Aidha, ujenzi na ukarabati wa matengenezo ya miundombinu ya barabara, kupitia *TARURA,* umefanyika na kuongeza viwango vya ujenzi wa barabara za changarawe kutoka kilomita 24,493 hadi kilomita 44,372.21 Aprili, 2025.

Mheshimiwa Spika, kwa lugha nyingine tunaongelea barabara ambazo tangu uhuru kuna vijiji havikuwa na barabara zinazounganisha vijiji na makao makuu ya kata zao, ama vijiji na vijiji na hiyo ndiyo inayoleta hizo 81.16%, kama ongezeko la barabara zilizojengwa vijijini na mijini. Urefu wa barabara za vijijini na mijini zilizojengwa kwa kiwango cha lami umeongezeka kutoka kilomita 2,025 hadi kilomita 3,467.30, ikiwa ni ongezeko la 71.22%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Nishati. Serikali imefanya maboresho makubwa katika sekta ya nishati na hivyo kuwezesha upatikanaji wa uhakika kwa gharama nafuu. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kukamilika kwa 99.93% ya ujenzi wa miradi ambayo ilikuwa inaendelea na tayari mingine imeanza kutoa huduma kwa upande wa Tanzania bara, ujenzi wa bomba la mafuta ghafi ya *EACOP,* kukamilika kwa njia ya kusafirishia umeme msongo wa *kV* 400 kutoka Singida hadi Arusha, *kV* 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma na *kV* 132 kutoka Tabora hadi Urambo. Hizi ni hatua kubwa ambazo zilikuwa bado hazijafanyika na Serikali ya Awamu ya Sita imezifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine mafanikio yaliyopatikana katika sekta hiyo ni kuendelea na maandalizi ya kutekeleza mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia *(LNG)*. Hili ni jambo kubwa ambalo litaleta mapinduzi makubwa ya kiuchumi kweli.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia, imeendelea na kuimarisha upatikanaji wa matumizi ya nishati safi ya kupikia hapa nchini, ambapo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni *Champion* wa jambo hili. Serikali imeandaa na inatekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 – 2034) kwa lengo la kuhakikisha kuwa, 80% ya Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034. Hii ni hatua ambayo itapunguza utegemezi wa kuni na mkaa, ambao husababisha uharibifu mkubwa wa misitu na athari kubwa kiafya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma za jamii, nikianza na Afya. Sekta ya afya imeendelea kupata mafanikio makubwa, ikiwemo uboreshaji wa miundombinu ya kutolea huduma za afya, ambapo hapa nchini vituo vya afya vimeongezeka kutoka 8,458 kwa mwaka 2020 hadi 9,826 kwa mwaka 2024. Kukamilika kwa awamu ya kwanza ya ujenzi na kuanza kutoa huduma kwa hospitali mpya za rufaa, ikiwemo ya Mikoa ya Songwe, Geita, Simiyu na Katavi; ujenzi wa hospitali mpya za halmashauri 129, ikiwa ni ongezeko la 31.63% ya lengo la kujenga hospitali 98. Uboreshaji wa huduma za dharura, ambapo idadi ya hospitali zenye majengo ya kutolea huduma za dharura

zimeongezeka kutoka saba hadi 116 kwa mwaka 2024. Haya ni mabadiliko makubwa na mtu anayependa afya yako anakupenda kuliko vyote kwa sababu, afya ndiyo mtaji wa kwanza katika kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa  mwaka 2020 hadi 2024, mafanikio mengine yaliyopatikana ni kuongezeka kwa majengo ya *ICU* kutoka 14 hadi 73. Idadi ya magari ya kubeba wagonjwa imeongezeka kutoka 540 hadi 1,267, zaidi ya mara mbili. Pia, kumekuwepo na kuimarika kwa huduma za afya ya mama na mtoto, ambapo vituo vya afya vinavyotoa huduma za dharura na uzazi vimeongezeka kutoka 340 hadi 523. Hivyo hivyo kwenye huduma zingine za kiuchunguzi, ambapo tayari kumekuwepo na mitambo ya uchunguzi wa magonjwa, kama vile *MRI*, ambayo imeongezeka kutoka minne tuliyokuwa nayo toka uhuru hadi 13, *CT-Scans* kutoka 12 hadi 45 na *Digital X Rays* kutoka 73 hadi 491. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imetunga Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Namba 13 ya Mwaka 2023 na sasa inaendelea kuweka mazingira wezeshi ya utekelezaji wa Sheria hiyo. Jambo hili ni kubwa na linakwenda kuwapa uhakika wa matibabu Watanzania wote, hususan, wale wenye kipato cha chini. Watanzania wana kila sababu ya kuichagua CCM na kumchagua Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Uchaguzi wa Mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu. Serikali imeendelea kutekeleza vipaumbele vya elimu, kama ambavyo imeelezewa kwa kina na hotuba ya Wizara ya kisekta. Serikali pia, imeendelea kuongeza vyumba vya madarasa ya elimu ya msingi kutoka 128,000 hadi 155,000 kwa mwaka 2024 na vyumba vya madarasa ya elimu ya sekondari kutoka 46,000 hadi 81,000 kwa mwaka 2024.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza mpango wa elimu bila ada kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha sita kwa kuongeza fedha za kugharamia mpango huo kwa baadhi ya vyuo vya masomo maalum. Hadi sasa Serikali imetumia zaidi ya

shilingi trilioni 1.3, kwa ajili ya utekelezaji wa zoezi hilo. Maboresho hayo yamechangia ongezeko la wanafunzi kutoka 14,940,925 mwaka 2020 hadi 16,155,281 kwa mwaka 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha ujenzi wa vyuo 29 vya Mafunzo ya Ufundi Stadi ambavyo vimeanza kutoa elimu, kuendelea na ujenzi wa vingine 65 na ukarabati wa vyuo 29 vya elimu ya mafunzo ya ufundi stadi. Jitihada hizo zimewezesha ongezeko la udahili wa wanafunzi katika vyuo vya elimu ya ufundi kutoka wanafunzi 344,000 hadi 440,000 kwa mwaka 2024. Serikali imeendelea kuongeza bajeti ya mikopo ya elimu ya juu, ili kuhakikisha wanafunzi wananufaika na matunda ya uhuru wa Taifa lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Maji. Serikali ya Awamu ya Sita imekwamua miradi iliyokuwa imekwama kwa muda mrefu, kama Mradi wa Maji wa Same – Mwanga – Korogwe ulioanza kujengwa mwaka 2014 na kukamilika Machi, 2025; mradi huu umetumia, takribani, zaidi ya miaka 11. Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imeukwamua mradi huo na una uwezo wa kuhudumia wananchi zaidi ya 456,000. Aidha, Mradi wa Maji wa Bunda ulioanza kujengwa Mwaka 2012 umekamilika mwaka 2022, takribani miaka 10 na utahudumia wananchi wapatao 227,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadhalika, mradi wa ujenzi wa tekeo la maji, kwa ajili ya Mji wa Kigoma ulioanza kujengwa mwaka 2015 umekamilika mwaka 2022, takribani miaka saba na una uwezo wa kuhudumia wananchi wapatao 215,000. Vilevile, Mradi wa Maji wa Mugango – Kiabakari hadi Butiama ulioanza kujengwa mwaka 2020 na kukamilika mwaka 2025, takribani miaka mitano, una uwezo wa kuhudumia wananchi zaidi ya 100,000.

Mheshimiwa Spika, kukwamua miradi yote iliyokwama, iliyoshindikana na sasa ikawezekana, tungekuwa tunaongea kisukuma tungesema, Serikali hii inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan ni "*jidula mabammbasi*". Inaweza kutindua maeneo yaliyoshindikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanikisha ununuzi wa seti 25 za mitambo ya uchimbaji wa visima na kuwezesha uchimbaji wa visima 1,221 pamoja na seti tano za mitambo ya kuwezesha ujenzi wa mabwawa 16. Aidha, Serikali imeanza kutumia mifumo ya takwimu na usimamizi wa ankara za maji; mitambo hii ya maji tangu uhuru tulikuwanayo miwili tu.

Mheshimiwa Spika, ndani ya miaka minne imenunuliwa mitambo 25 ya kuchimba visima, mitambo mitano ya kuwezesha uchimbaji wa mabwawa na mitambo ya kila ukanda ya kuweza kupima upatikanaji wa maji. Hii ni hatua kubwa inayolenga kumfanya kila Mtanzania apate maji ya kutumia majumbani na pia, maji ya umwagiliaji, kwa ajili ya kujiletea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta za Uzalishaji. Mafanikio yaliyopatikana, nikianza na sekta ya kilimo, mazao, ni pamoja na kuongezeka kwa ukuaji wa sekta kutoka asilimia 2.7 kwa mwaka 2022 hadi asilimia 4.0 kwa mwaka 2024. Uzalishaji wa mazao ya chakula kutoka tani 17,000,000 hadi kufikia tani milioni 22.8 kwa mwaka 2023 na hivyo, kuongeza utoshelevu wa chakula hapa nchini. Sasa tuna akiba ya fedha za kigeni, tuna akiba ya dhahabu na tuna akiba ya chakula kwenye uhifadhi wetu wa chakula. Utumiaji wa mbolea umeongezeka kutoka tani 32,000 hadi tani 158,628 kwa mwaka 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha ujenzi wa maghala 46 na vihenge 20 vya kuhifadhia nafaka hivyo, kuongeza uwezo wa kuhifadhi mazao kutoka tani 200,000 hadi 700,000. Aidha, Serikali itaendelea na utekelezaji wa kuanzisha vituo 1,000 vya zana za kilimo "*Mechanization Program*" na kununua matrekta 10,000 inayolenga kuwezesha upatikanaji wake kwa wakulima. Vilevile, mtandao wa umwagiliaji umeongezeka kutoka hekta 560,000 kwa mwaka 2021/2022 ambazo ndiyo tulikuwa nazo tangu uhuru hadi kufikia hekta 960,000 kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na kazi hiyo inaendelea. Ongezeko hilo ni 80% ndani ya miaka minne, lengo ni kufikia hekta 1.2 na miradi 780 yenye zaidi ya hekta 500,000 inaendelea kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uvuvi, mafanikio yaliyopatikana katika sekta hii ni pamoja na ujenzi wa Bandari ya Uvuvi, Kilwa Masoko, ambao umeshakamilika kwa zaidi ya 81%. Serikali ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu, ikiongea inatekeleza na ujenzi unaoonekana unaongea kuliko maneno haya tunayoyasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali pia, imeongeza mauzo ya mazao ya uvuvi nje kutoka tani 167,000 hadi tani 199,000 na ununuzi wa maboti ya kisasa ya uvuvi 219 yenye thamani ya shilingi bilioni 19. Maboti hayo yamegawanywa Mkoa wa Pwani 144, Ziwa Victoria, Tanganyika, Nyasa, Rukwa pamoja na maeneo mengine. Aidha, jumla ya vizimba 248 vimetolewa kwa wanufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mifugo mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuongezeka kwa viwanda vya kuchakata nyama inayouzwa nje na ndani ya nchi kutoka tani 1,669 hadi tani 14,701 na maeneo ya malisho, hekta 2,788,000 kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi hekta 3,489,000 kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Aidha, Serikali imenunua na kusambaza mitamba 1,630 katika mashamba matano ya Serikali yanayozalisha mifugo pamoja na ujenzi wa mabwawa 19 yenye thamani ya shilingi bilioni 10.69. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha, kuendeleza ushirika na hatimaye kuinua sekta ya kilimo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amefanya uzinduzi wa Benki ya Ushirika Tanzania, tarehe 27 Aprili, 2025. Hili ni jambo jipya kwa wafugaji, wakulima pamoja na sekta zingine za uzalishaji. Benki hii imeanza na mtaji wa shilingi bilioni 58. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa viwanda, biashara na uwekezaji, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuchukua hatua mahsusi za kuimarisha na kuboresha mazingira ya biashara katika uwekezaji. Pamoja na hatua zinazochukuliwa, ikiwa ni kufanya maboresho ya Sheria Namba 12, ili kuboresha mazingira ya kufanyia biashara, matokeo yake ni tumejitosheleza katika uzalishaji wa baadhi ya bidhaa zinazopatikana ndani ya nchi. Nawasihi Watanzania tuzipende bidhaa zinazopatikana ndani ya

nchi yetu ili kuendeleza uwekezaji na uzalishaji wa ajira kwa watoto wa Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa madini. Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita mchango wa sekta ya madini umeongezeka kwenye pato la Taifa. Ninaipongeza Wizara ya Madini kwa mchango wanaochangia.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa madini, katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita mchango wa sekta ya madini umeongezeka kwenye pato la Taifa. Niwapongeze Wizara ya Madini kwa mchango wanaochangia katika ukusanyaji wa maduhuli hadi kufikia 10.1% kwa mwaka 2024 kutoka asilimia sita iliyokuwa inapatikana hapo awali.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni kupatikana na kuongezeka kwa maduhuli kutoka shilingi bilioni 587.3 katika mwaka 2021 hadi shilingi bilioni 875.6 Julai, 2024. Katika kipindi hicho Serikali imeendelea kuboresha sheria, kanuni na miundombinu mbalimbali ikiwemo nishati na maji migodini, hali ambayo inaweka mazingira wezeshi ya uwekezaji katika migodi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kila sekta mafanikio yameelezewa kwa kina na hotuba za Wizara za kisekta. Niombe taarifa yangu yote hii iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama ambavyo imebainishwa katika kitabu kikubwa.

Mheshimiwa Spika, lingine la mafanikio, Serikali imefanikiwa kuyaenzi maono ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, kuifanya Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi. Maono hayo yalianza kutekelezwa na Serikali ya Awamu ya Tano iliyokuwa inaongozwa na Dkt. John Pombe Magufuli. Maono hayo yalitekelezwa kwa kiasi na sasa kasi imeendelea ya utekelezaji wa ujenzi wa Makao Makuu mapya ya Dodoma ikihusisha kukamilishwa kwa Ikulu.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeendelea na ujenzi wa majengo 34 ya ofisi za Serikali katika Mji wa Serikali Mtumba

ambapo ukamilishwaji wake umeshakamilika kwa kiwango kikubwa. Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato kimekamilika barabara za mzunguko wa nje *(outer ring road)* zimeshakamilika kwa kiwango kikubwa na mzunguko wa ndani *(inner ring road)* zinaendelea kujengwa. Ukamilishwaji wa majengo ambayo miundombinu ya Jiji la Dodoma unategemewa na utawezesha wananchi kupata huduma hapa hapa. Haturudi nyuma. Haya ndiyo Makao Makuu ya Nchi yetu na kwa Kigogo wanasema *Langa Idodoma Kunojile; kunojile kudodoma.*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ya fedha Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa huduma jumuishi za fedha chini ya uwepo wa kujenga na kuanza kutumika kwa Mfumo wa Malipo ya Papo kwa Papo *(Tanzania Instant Payment System – TIPS)*. Aidha, katika kuhakikisha bei nafuu na rafiki kwa wananchi, Benki Kuu ya Tanzania ilitoa mwongozo wa kupunguza gharama kwa ajili ya kupunguza gharama za matumizi ya masuala ya kifedha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hizo Serikali inaendelea kushirikiana na watoa huduma wote wa sekta ya fedha katika kufanya mageuzi ya kupunguza matumizi ya fedha taslimu katika uchumi wetu. Serikali inapanga kuzindua Mkakati wa Kukuza Matumizi ya Huduma za Fedha kwa Malipo ya Njia ya Kidijiti kwa kipindi cha miaka mitatu. Katika mapendekezo ya kikodi tunayoleta leo yapo yanayoleta unafuu kwa wale watakaofanya malipo kwa njia za kidijiti.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuweka mazingira wezeshi katika kuhakikisha kuwa sekta binafsi inapata mikopo kwa wakati na gharama nafuu. Mikopo kwa sekta binafsi imeongezeka kutoka shilingi bilioni 20 kwa mwaka 2020 hadi kufikia shilingi bilioni 36 kwa mwaka 2024. Hii ni hatua kubwa na Serikali ya Awamu ya Sita inaendelea kuboresha maslahi kwa watumishi wa umma na wastaafu ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza hilo mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na upandishwaji wa vyeo watumishi wa

umma wapatao laki nne na 76 ambapo jumla ya shilingi bilioni 689 zimetumika. Hali hii imeongeza ari ya kazi kwa watumishi ikiwa ni pamoja na utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2022/2023 Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliongeza kima cha chini cha mshahara kutoka shilingi laki tatu hadi shilingi laki tatu na 70 ikiwa ni sawa na ongezeko la 23%.

Mheshimiwa Spika, Mei Mosi kwa mwaka 2025 katika Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani Mheshimiwa Rais ameongeza tena kima cha chini cha mshahara kutoka shilingi laki tatu na 70 hadi shilingi lakini tano ikiwa ni sawasawa na ongezeko la 35%. Haijawahi kutokea ongezeko la mara kwa mara kama alivyofanya Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi na yale ya mafanikio, huku nikisisitiza hotuba yote iingie ndani ya Kumbukumbu rasmi, sasa nihamie kwenye bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/2026 imeandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020, Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya 2020/2050, Ajenda Endelevu 2020/2030, pamoja na nyaraka na miongozo na makubaliano mengine ya kikanda pamoja na kimataifa ambayo Tanzania imeridhia.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Serikali ya Mwaka wa Fedha 2025/2026 ni ya tano na ya mwisho katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano wenye dhima ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Aidha, dhima kuu ya bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026, kama ilivyokubaliwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ni mageuzi jumuishi ya uchumi kupitia uimarishwaji wa ukusanyaji wa mapato ya ndani na uwekezaji wa kimkakati

wenye kuzalisha fursa za ajira na uboreshaji wa hali ya maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, shabaha kuu za uchumi wa jumla kwa mwaka wa fedha unaokuja, kwa kuzingatia mwenendo wa viashiria mbalimbali vya uchumi jumla pamoja na utekelezaji wa bajeti ya Serikali, shabaha na malengo ya kiuchumi jumla kwa mwaka huu huu itakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Kuongeza kasi ya ukuaji wa pato halisi la Taifa kufikia asilimia 6.0 kwa mwaka 2025 kutoka asilimia 5.5 kwa mwaka 2024;

(b) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa takwimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0 katika muda wa kati;

(c) Mapato ya ndani kufikia 16.7% ya Pato la Taifa mwaka 2025/2026 ikilinganishwa na 15.8% mwaka 2024/25;

(d) Mapato ya kodi kufikia 13.3% ya Pato la Taifa mwaka 2025/2026 kutoka 12.8% ya mwaka 2024/2025;

(e) Nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa asilimia 3.0 ya pato la Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ikilinganishwa na asilimia 3.4 ya Mwaka wa Fedha 2024/2025; na

(f) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya vipaumbele kwa mwaka 2025 ya bajeti hii inaendeleza na kukamilisha utekelezaji wa miradi, programu za maendeleo na afua zinazochangia maeneo makuu ya vipaumbele vya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambavyo ni kuchochea uchumi shindani na shirikishi, kuimarisha uzalishaji wa bidhaa viwandani na utoaji

huduma, kukuza uwekezaji na biashara, kuchochea maendeleo ya watu na kuendeleza rasilimali watu ili kuhakikisha kuwa ufikiwaji wa malengo ya dira 2025.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maeneo mahususi yatakayopewa kipaumbele katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2025 ni pamoja na kuendelea kutekeleza na kukamilisha miradi ya kielelezo ili kuweza kukamilisha miradi hiyo, kuimarisha sekta za uzalishaji, matokeo chanya katika kukuza uchumi, kuimarisha rasilimali watu hususan katika sekta za huduma za jamii, kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji nchini ili kuvutia ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine mahususi ya vipaumbele pamoja na ugharamiaji wa deni la Serikali, mishahara, stahiki za watumishi wa umma pamoja na ujenzi na ukarabati wa viwanja vya michezo kwa ajili ya *AFCON*. Aidha, ninapenda kuwafahamisha kuwa Tanzania kwa Uchaguzi Mkuu wa 2025 tutaugharamia kwa fedha zetu wenyewe na zoezi hilo limekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi mahsusi ya maendeleo katika maeneo ya vipaumbele itakayotekelezwa na Serikali katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026 imeainishwa kwa kina katika hotuba iliyowasilishwa leo asubuhi na Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, kaka yangu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji alipokuwa akiwasilisha Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba yake Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ameambatisha Taarifa ya Tathmini ya Baadhi ya Miradi iliyofanyiwa tathmini ya athari za mabadiliko ya tabianchi. Tathmini hii ilifanyika kwa lengo la kujiridhisha na uzingatiaji wa masuala ya mazingira katika utekelezaji wa miradi. Nitumie fursa hii kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imejipanga na

itahakikisha upatikanaji wa fedha zote zilizoidhinishwa ili kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ni ushahidi wa dhamira ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Chama Cha Mapinduzi chini ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuendeleza mafanikio yaliyopatikana kwenye Dira ya Maendeleo ya 2025, hususan katika kuboresha ustawi wa maisha ya Watanzania. Hivyo, niwashawishi na kuwaomba wananchi wa Tanzania waendelee kuiamini CCM na kukichagua Chama Cha Mapinduzi kwa kishindo katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika 2025.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maboresho ya mifumo ya kodi, ada, tozo na hatua nyingine za mapato; sasa ninaomba kuwasilisha kwako mapendekezo ya kufanya maboresho ya mfumo wa kodi, ikiwemo baadhi ya viwango vya kodi, tozo na ada zinazotozwa chini ya sheria mbalimbali pamoja na kuboresha taratibu za ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, maboresho haya yamezingatia migogoro na vita vya kibiashara baina ya mataifa mbalimbali yaliyoendelea kutokana na nchi ya Marekani kutangaza mabadiliko mbalimbali ya kisera pamoja na wadau wengine wa maendeleo. Lengo letu ni kuhakikisha miradi inaendelea kutekelezwa kama ambavyo ilikuwa imepangwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na dhamira ya kuwa na mfumo wa kodi ambao ni tulivu na wa kutabirika unaolenga kuchochea shughuli mbalimbali za uzalishaji mali ndani ya nchi na kuweka mkazo katika sekta za kimkakati ikiwemo viwanda, madini, kilimo, ufugaji na uvuvi, nishati, uchukuzi na usafirishaji, pamoja na sekta za huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, ninapendekeza kurekebisha mfumo wa kodi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 unaotarajiwa kuongezea Serikali jumla ya shilingi 4,260,023.77 na marekebisho yanayopendekezwa yanahusisha sheria zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, nimeorodhesha orodha ya sheria kwenye ukurasa wa 77 wa hotuba yangu na nitazipitia moja baada ya nyingine wakati ninasoma marekebisho ninayoyapendekeza.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148: ninapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148 kama ifuatavyo:-

(1) Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye viuatilifu vinavyotambulika kwa *HS Codes* 3808.61.00, 3808.62.00 na 3808.69.00. Lengo la hatua hii ni kuwapa unafuu wakulima wa kupata dawa za kuua wadudu mashambani na hivyo kuongeza uzalishaji wa mazao nchini. Hatua hii inaendana na kanuni za usawa wa utozaji kodi kwa kuwa viuatilifu vya aina nyingine vinasamehewa kodi hii.

(2) Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye miamala ya ununuzi wa bima mtawanyo *(reinsurance)* inayofanywa baina ya kampuni za bima na zile za bima mtawanyo. Lengo la hatua hii ni kuongeza ushindani wa kampuni za ndani, kukuza sekta ya bima na kuhamasisha matumizi ya bima katika kukabiliana na majanga nchini.

(3) Kutoza kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha asilimia sifuri (0) kwenye bidhaa za nguo zinazotengenezwa kwa kutumia pamba inayolimwa nchini kwa kipindi cha mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kuleta unafuu kwa wakulima wa pamba na viwanda vinavyotengeneza nguo nchini hasa katika kipindi hiki cha mvutano wa kibiashara baina ya mataifa makubwa hapa duniani.

(4) Kutoza kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha asilimia 0 kwenye mbolea inayozalishwa ndani ya nchi kwa kipindi cha miaka mitatu. Lengo la hatua hii ni kuleta unafuu kwa wakulima na walaji hasa katika kipindi hiki ambacho dunia imeingia kwenye mdororo wa kiuchumi.

(5) Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye mafuta ya kula yanayozalishwa ndani ya nchi kwa kutumia

mbegu zinazozalishwa nchini kwa muda wa mwaka mmoja. Hapo awali, msamaha huu ulitolewa kwa kipindi cha mwaka mmoja kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2024 na ukomo wake ni tarehe 30 Juni 2025. Lengo la hatua hii ni kuendelea kuleta unafuu wa bei ya mafuta ya kula nchini.

(6) Kufuta Msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani unaotolewa kwenye ununuaji na uingizaji wa *gaming supply*. Hatua hii inalenga kuleta usawa katika utozaji wa kodi kwa kuwa michezo mingine kama vile mpira wa miguu iwapo katika wigo wa utozaji wa kodi ya ongezeko la thamani. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 322,022.5.

(7) Kuweka sharti la msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye matairi ya trekta yanayotumika kwenye shughuli za kilimo yanayotambulika kwa *HS Code* 4011.70.00; *dam liners* zinazotambulika kwa *Heading* 39.20; *forks (HS Code* 8201.90.00); reki *(HS Code* 8201.30.00); na shoka *(HS Code* 8201.40.00) ambazo hutolewa baada ya kupata ridhaa ya Waziri mwenye dhamana ya masuala ya kilimo. Lengo la hatua hii ni kuleta unafuu kwenye sekta ya kilimo na kuhakikisha msamaha unatumika kwa malengo yaliyokuwa yamekusudiwa.

(8) Kufuta msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye lami zinazotambulika kwa *HS Code* 2713.20.00 na 2715.00.00. Lengo la hatua hii ni kuendana na azma ya Serikali ya kupunguza misamaha isiyo na tija ili kulinda mapato ya Serikali na kupunguza matumizi yanayohusiana na utozaji wa misamaha ya kodi *(tax expenditure)*. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 85,606.2.

(9) Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye magazeti yanayozalishwa nchini pekee. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za magazeti hayo na hivyo kuwezesha upatikanaji wa taarifa muhimu. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 1,274.4.

(10) Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye gesi asilia inayouzwa kwenda kwenye vituo vya kushindilia gesi *(Compressed Natural Gas Stations)* kwa ajili ya matumizi ya magari. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu kwa wawekezaji, kuvutia uwekezaji wa vituo vya kusambazia gesi asilia iliyosindikwa kwenye magari na kupunguza utegemezi wa mafuta na uzalishaji wa hewa ya ukaa.

(11) Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye matanki na mitungi ya gesi ya kupikia zinazotambulika kwa *HS Code* 7311.00.10 pamoja na mitambo ya kuondoa hewa ukaa yenye *HS Code* 8417.80.00 inayotumika katika uzalishaji wa mkaa mbadala. Hatua hii inalenga kupunguza gharama za upatikanaji wa bidhaa hizi ili kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini. Hatua hii inatarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 1,917.8.

(12) Kufanya marekebisho kwenye kipengele cha 15(8) cha Sehemu ya kwanza ya Jedwali la Misamaha ya Kodi ya ongezeko la thamani kwa kufuta neno *Liquified Petroleum and Natural gases* na kuweka neno *Liquified Petroleum Gas*. Lengo la hatua hii ni kuweka ufafanuzi na kutatua changamoto zilizokuwa zinajitokeza katika utozaji wa msamaha huo.

(13) Kufanya marekebisho kwenye kipengele cha 15(9) cha Sehemu ya kwanza ya Jedwali la Misamaha ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kufuta neno *Compressed Petroleum and Natural gases* na kuweka neno *Compressed Natural Gas for Motor vehicles* ili kuweka ufafanuzi na kutatua changamoto zilizopo katika utozaji wa msamaha husika.

Mheshimiwa Spika, kufanya marekebisho kwenye kipengele cha 15 cha Sehemu ya Pili ya Jedwali la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148, kwa kufuta msamaha kwenye vifaa visivyo vya gesi asilia iliyoshindiliwa kama vile *natural gas pipes, transportation and distribution pipes, natural gas metering equipment, gas receiving units, flare gas system, condensate tanks and leading facility, system piping and pipe rack* na

*condensate stabilizer* na badala yake kujumuisha katika kipengele katika msamaha wa *CNG*.

Mheshimiwa Spika, kufanya marekebisho kwenye kipengele cha 15(10) cha Sehemu ya kwanza ya Jedwali la Misamaha ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kufuta neno *compressed or liquified gas cylinders for petroleum and natural gases for cooking* na kuweka neno *liquified petroleum gas cylinders for cooking.* Hatua hii inalenga kuweka ufafanuzi kuhusu utofauti baina ya mitungi ya kuhifadhi gesi asilia iliyoshindiliwa na mitungi ya kupikia ya *liquified petroleum gas* ili kuendana na ajenda ya Kimataifa mahususi ya matumizi ya nishati safi.

Mheshimiwa Spika, kujumuisha masoko mtandao *(online market place platform)* na huduma za masoko za kimtandao *(network marketing platform)* kwenye wigo wa tafsiri ya neno wakala wa huduma za kimtandao *(online intermediation services)*. Lengo la hatua hii kutanua wigo wa kodi kwa kuweka ufafanuzi utakaopelekea kutatua changamoto zilizopo katika utozaji na usimamizi wa kodi ambapo tafsiri iliyopo sasa haijumuishi huduma hiyo. Lengo hili linatarajia kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 116,073.4.

Mheshimiwa Spika, kujumuisha *non-resident online payment services platform* zinazotumia miundombinu ya watoa huduma wengine kwenye wigo wa wakala wa fedha *(online intermediation payment platform)* na zinazotoa huduma hapa nchini kutokea nje ya nchi. Lengo la hatua hii ni kuongeza wigo wa mapato.

Mheshimiwa Spika, kutoza kiwango cha punguzo la kodi ya ongezeko la thamani cha 16% badala ya 18% kwenye ununuzi wa bidhaa pale ambapo malipo yake yanafanyika kwa njia ya mtandao (*B2C*) na mlaji atathibitisha kuwa ankara ya malipo iliyotolewa ina kiwango sahihi cha muamala uliofanyika. Hatua hii inalenga kuhamasisha matumizi ya mifumo kwenye ufanyaji wa malipo, kupunguza matumizi ya fedha taslimu na kurahisisha usimamizi wa kodi kwa kuwezesha upatikanaji wa taarifa za

miamala ya manunuzi. Hatua hii itapunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 32,312.

Mheshimiwa Spika, kuanzisha utaratibu wa uwakala wa ukusanyaji wa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* kwenye malipo yanayofanywa kwenda kwa wauzaji waliosajiliwa kukusanya kodi hiyo. Kupitia taasisi na taratibu zitakazowekwa na taasisi, mlipakodi, sekta zifuatazo zitakuwa zimewekwa kwenye orodha ya kodi la ongezeko la thamani na kuainishwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kodi ya Mapato, Sura ya 332; mapendekezo ninayoleta ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuweka unafuu wa kutoza kodi ya mapato kwa kundi la pikipiki ya miguu miwili, pikipiki ya miguu mitatu (bajaji) na magari ya kubeba mizigo yenye uzito usiozidi gramu 500 ikiwemo guta kwa kuweka utaratibu mpya wa kukadiria kodi ya mapato kwenye vyombo hivyo kama ambavyo nimeainisha kwenye jedwali Na.1. Ninapunguza na kuweka unafuu wa utozaji kodi ya mapato kwenye kundi la pikipiki ya miguu miwili, pikipiki ya miguu mitatu(bajaji) magari ya kubebea mizigo isiyozidi 500 (guta) na utaratibu huo tumeubainisha kwenye jedwali Na.1.

Mheshimiwa Spika, ambapo kwa sehemu ya kwanza namba moja kwenye idadi ya abiria tumeweka kama ambavyo tumebainisha na abiria wasiozidi watano kiwango cha 120,000 abiria wasiozidi watano hadi 15, kiwango cha 250,000. Daraja C kwenye magari ya mizigo kama ambavyo tumeonesha kwenye jedwali wasiozidi 500 hakuna, wasiozidi 500 hadi tani moja 250,000. Daraja D tumebainisha kwa upande wa pikipiki ya miguu miwili hakuna. Namba mbili, pikipiki ya miguu mitatu 120,000 kwa miwili 65,000.

Mheshimiwa Spika, kutoza kodi ya zuio kwa kiwango cha 10% kwenye faida ambayo haijagawanywa kwa wanahisa baada ya miezi sita. Lengo la hatua hii ikiwa ni kuongeza wigo wa

kodi wa mapato Serikalini. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 130,624.

Mheshimiwa Spika, kutoza kodi ya zuio kwa kiwango cha asilimia mbili kwenye malipo yanayotokana na ununuzi wa chumvi ghafi kwa wamiliki wa Leseni ya Uchimbaji Mdogo wa Madini *(Primary Mining Licence)* na Wachimbaji Wadogo wa Madini *(Artisanal Miners)*. Hatua hii inalenga kutatua changamoto zilizokuwa zinajitokeza katika ukusanyaji wa kodi katika sekta hiyo na kuweka utaratibu maalum wa utozaji wa kodi kwa wazalishaji hao.

Mheshimiwa Spika, kutoza kodi ya zuio kwa kiwango cha 10% kwenye malipo ya kamisheni inayotokana na matangazo ya michezo ya kubahatisha. Kodi hii itakuwa ni kodi ya mwisho *(final)*. Lengo la hatua hii ni kuendana na kanuni za usawa za utozaji kodi na kupanua wigo wa kodi. Hatua hii inatarajia kuongeza mapato ya Serikali kwa milioni 6,787.2.

Mheshimiwa Spika, kuongeza wigo wa kodi ya zuio kwenye malipo ya bima na bima mtawanyo *(insurance and re-insurance premium)* inayofanywa kwa kampuni za nje kutoka asilimia tano hadi 10%. Kiwango cha sasa hakijabadilishwa kwa takriban miaka 13 na hakiendani na hali ya uchumi iliyobadilika ndani ya miaka hiyo. Hatua hii inalenga kuongeza mapato ya Serikali kwa milioni 178,988.6.

Mheshimiwa Spika, kuongeza kiwango cha kodi ya zuio kwenye malipo ya huduma za kitaalamu za kiusimamizi zinazotolewa kwenye sekta ya uzinduzi *(extractive sector)* kutoka asilimia tano hadi 10%. Lengo la hatua hii ni kupunguza wigo wa kodi na kuendelea na mabadiliko ya hali ya uchumi duniani. Lengo la hatua hii inatarajia kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 7,429.7.

Mheshimiwa Spika, kupunguza ukomo wa hasara ya miaka ya nyuma iliyoruhusiwa kupunguziwa kodi wakati wa ukokotoaji wa kodi ya mapato kwa wafanyabiashara katika sekta ya madini,

petroli, mafuta na gesi na wanaojiendesha kwa hasara kutoka 70% hadi 60%.

Mheshimiwa Spika, kufuta msamaha wa kodi ya mapato unaotolewa kwa kipindi cha miaka 10 ya mwanzo kwa mwekezaji aliyesajiliwa katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi (*EPZ* na *SEZ*) pale bidhaa zilizozalishwa na huduma zinazotoka katika maeneo hayo zinapouzwa katika soko la ndani ya nchi. Marekebisho haya yanaenda sambamba na kufuta vipengele vinavyobainisha msamaha husika kwenye sheria zinazosimamia wawekezaji hao. Lengo la hatua hii ni kuendana na azma ya Serikali ya kupunguza misamaha ya kodi kwa lengo la kulinda mapato ya Serikali. Hatua hizi za kodi zinatarajiwa kuongeza jumla ya shilingi milioni 861,684.5.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ushuru wa bidhaa; kwa mujibu wa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa kifungu cha 124(2), kinaweka marekebisho kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha nchi kuwa na sera za kodi zilizostarabika na kuweka mazingira bora ya uwekezaji, Serikali ilianzisha utaratibu wa kurekebisha viwango vya ushuru wa bidhaa baada ya miaka mitatu. Ninapendekeza kufanya marekebisho kama ifuatavyo:-

(i) Kufuta ada ya leseni ya kiasi cha shilingi 300,000 inayotozwa kwa wazalishaji na waingizaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa. Hatua hii inalenga kuwapa unafuu wazalishaji na waingizaji wa bidhaa hizo hapa nchini.

(ii) Kupunguza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye *Un-denatured Ethyl Alcohol* yenye kilevi cha 80% na zaidi inayotoka nje kutoka shilingi 7,000 hadi 5,000 kwa lita na kutoka shilingi 5,000 hadi 4,000 kwa lita. Bidhaa hiyo inatambulika kwa *HS Code* 2207.10.00. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu katika ulipaji wa ushuru wa bidhaa wa awali kwa viwanda na kuendelea kulinda viwanda vya ndani.

(iii) Kupunguza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji vya kuongeza nguvu *(energy drinks)* vinavyozalishwa ndani ya nchi kutoka shilingi 561 kwa kila lita hadi shilingi 134.2 kwa lita. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu kwa wazalishaji wa ndani, kuongeza ushindani na kuchochea uwekezaji.

(iv) kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha Shilingi 50 kwa kilo ya *crisp* zinazozalishwa nchini na shilingi 100 kwa kilo ya *crisp* zinazozalishwa kutoka nje.

(v) kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia tano kwenye *ice cream* zinazozalishwa nchini kwa kutumia kakao au malighafi nyingine na 10% kwa zile zinazotumia malighafi kutoka nje ya nchi. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali.

(vi) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia tano kwa soseji na bidhaa zingine zinazofanana na hizo zinazozalishwa nchini na 10% kwa zile zinazoagizwa kutoka nje. Hatua hii inatarajia kuongeza mapato ya Serikali, kwa kiasi cha shilingi milioni 2,413.9.

(vii) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha 25% kwenye baruti zinazozalishwa nchini na zinazoagizwa kutoka nje ya nchi zinazotambulika kwa *HS Code* 3604.10.00. Lengo la hatua hili ni kupunguza athari za kimazingira ikiwemo uchafuzi wa hali ya hewa.

(viii) Kutoza ushuru kwa kiwango cha shilingi 22,000 kwa kila tani ya hewa ukaa inayozalishwa kwenye makaa ya mawe na gesi asilia. Lengo la hatua hii ni kudhibiti athari za kimazingira.

(ix) Kujumuisha watoa huduma za uhamishaji wa fedha na mifumo ya malipo ambao siyo taasisi za kifedha au watoa huduma za mawasiliano *(telecommunication operators)* kwenye wigo wa utozaji wa ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha 10%. Lengo la hatua hii ni

kuongeza wigo wa kodi na kuendana na kanuni za usawa za utozaji kodi. Hatua hii inatarajia kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 220,055.7.

(x) Kuweka msamaha wa ushuru wa bidha, hii nimetoka kuisoma. Hatua hizi za ushuru wa bidhaa kwa ujumla wake zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 1,069,436.8.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura 438; ninapendekeza kufanya marekebisho yafuatayo:-

(i) Kuweka sharti la mifumo au programu za kihasibu zinazotumika katika utoaji wa risiti za kielektroniki kuunganishwa na mifumo ya Mamlaka ya Mapato Tanzania ya usimamizi wa kodi. Lengo la hatua hii ni kuwezesha upatikanaji wa taarifa.

(ii) Kuweka sharti la maombi ya kuruhusiwa kutolipa kiasi cha kodi ambacho hakipo kwenye pingamizi au moja ya tatu ya kodi iliyokadiriwa kutegemeana na kiasi kitakachokuwa kikubwa, kuwasilishwa ndani ya siku 15 tangu tarehe ya kupokea maamuzi ya Kamishna Mkuu wa *TRA*. Hatua za usimamizi wa kodi kwa ujumla wake zinatarajia kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 430,055.54.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, ninapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290, kama ifuatavyo:-

(i) Kupunguza Tozo ya Ushuru wa Huduma *(Service Levy)* kutoka utaratibu wa sasa wa kutoza kiwango kisichozidi 0.3% ya pato ghafi kwenda kiwango mfuto cha 0.25% ya pato ghafi. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za ufanyaji biashara na uwekezaji nchini pamoja na kuendana na masharti ya Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuchukua hatua hizi za kupunguza ushuru wa aina hii na zingine zinazoendana na hii, miaka hadi miaka ili kuweza kutekeleza mpango huo wa MKUMBI.

(ii) Kupunguza kiwango cha Ushuru wa Hoteli (*Hotel levy)* kutoka 10% hadi asilimia mbili. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za ufanyaji biashara na uwekezaji hapa nchini. *(Makofi)*

(iii) Kufuta ada ya upakiaji *(loading)* na upakuaji *(offloading)* zinazotozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazohusiana na usafirishaji wa mizigo. Lengo la hatua hii ni kuwapunguzia gharama wananchi wetu wa Tanzania wanapojiletea shughuli za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Sheria ya Bima, Sura 394; ninapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Bima, Sura 394 na kuanzisha bima ya usafiri kwa wageni wanaoingia hapa nchini kwa kiwango cha dola za Marekani 44 kama ilivyo kwa upande wa Zanzibar. Bima hii ni kwa ajili ya dharura za kiafya zinazohusiana na safari kwa wageni wanapokuwa hapa nchini, kupotea kwa mizigo ya wageni, kugharamia wageni wanapoondoshwa kwa lazima au ikitokea hatari yenye kulazimu kwa uondoshwaji. Bima hii itakuwa na ukomo wa hadi siku 92 kwa mgeni ndani ya muda huo na haitahusisha raia wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na *SADC*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria ya Udhibiti wa Uingizwaji wa Bidhaa hapa Nchini, Sura 276; ninapendekeza kama ifuatavyo:-

(i) Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha 10% kwenye vifaa vya plastiki vinavyotumika majumbani vinavyoingizwa nchini vinavyotambulika kwa *HS Code* 39.24. Hatua hii itaongeza mapato kwa milioni 7,605.2.

(ii) Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha 10% kwenye vichwa vya trela vinavyoingizwa nchini vinavyotambulika kwa *HS Codes* 8701.21.90, 8701.22.90,

8701.23.90, 8701.24.90 na 8701.29.90. Hatua hii inatarajia kuongeza mapato ya Serikali kwa milioni 99,920.2.

(iii) Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha 10% kwenye hema za mbao, chuma na nyinginezo vinavyoingia nchini kwa utaratibu wa *HS Codes* 9406.10.90, 9406.20.90 na 9406.90.90. Hatua hii inalenga kuongeza fedha ya Serikali kwa kiasi cha milioni 4,735.3.

(iv) Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa viwango vya 10% kwenye nondo kama nilivyobainisha kwenye jedwali Na. 4.

(v) Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha asilimia tano kwenye misumari kama nilivyoelezea kwenye *HS Code* 7317.00.00. Hatua hizi zinalenga kuongeza mapato ya Serikali milioni 4,193.8.

(vi) Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha 10% kwenye samani zinazoingizwa hapa nchini kwenye *Heading* ya *HS Code* 94.03. Hatua hii inalenga kuongeza mapato.

(vii) Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha 15% kwenye mabati zinazotambulika kwa *HS Codes* kama nilivyobainisha kwenye jedwali hilo.

(viii) Kutoza tozo ya maendeleo kwenye viwanda kwa kiwango cha 10% kwenye *HS Codes* kama nilivyobainisha kwenye hilo jedwali namba 8 na orodha ya *HS Code* kama zinavyoonekana.

(ix) Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa viwango cha 10% shilingi 4500 kwa kila meta ya mraba kutegemeana na kiwango kilicho kikubwa kwenye marumaru vinavyotambulika kwa *HS Code* kama nilivyobainisha kwenye majedwali niliyoyabainisha.

Mheshimiwa Spika, hatua hii inalenga kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 49,663.2.

(x) Kuondoa klinka iliyokuwa inatambulika kwa *HS Code* 2523.10.00 kwenye wigo wa bidhaa zinazotozwa tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha 10%.

(xi) Kufuta sharti la kutotoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwenye bidhaa zinazozalishwa katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambazo zinakidhi vigezo vya uasili *(rules of origins)*. Lengo la hatua hiyo ni kulinda viwanda vya ndani, kuchochea ushindani na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hizi ni kuvutia uwekezaji ndani ya nchi, kuchochea mauzo nje ya nchi yetu na kulinda uzalishaji wa ndani ya nchi kwa bidhaa husika zinazozalishwa kwa wingi hapa nchini. Aidha, mapato yatakayopatikana na vyanzo husika yatatumika katika kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya msingi katika kongani za viwanda kwa lengo la kuvutia uwekezaji hapa nchini. Kwamba tutatoza kodi ya asilimia hizo ambazo tumesema ya maendeleo ya viwanda na fedha hizo tutaenda kuweka miundombinu kwenye kongani za viwanda ili tuweze kujenga viwanda vingi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria ya Bajeti, Sura Na. 439, Sheria ya Fedha ya Umma, Sura Na. 348 napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Bajeti Sura Na. 439 na Sheria ya Fedha za Umma, Sura Na. 348. Ili kuweka sharti la Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha kushirikishwa Wizara, Taasisi za Serikali, Wakala za Mamlaka za Serikali za Mitaa kabla ya kuanzisha tozo ama ada mpya wakati wa kuanzisha tozo ama wakati wa kufanya mabadiliko yoyote ya viwango vya ada ama tozo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii ni kuiwezesha Wizara ya Fedha kutekeleza majukumu yake ya usimamizi wa mapato ya Serikali ikiwemo kufanya tathmini ya athari za viwango vinavyopendekezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria ya Fedha za Umma, Sura Na. 388; ninapendekeza kuweka viwango tofauti kwa Wakala wa Serikali, Mashirika na Taasisi za Umma ya kuchangia kati ya 15% hadi 60% ya mapato ghafi katika Mfuko Mkuu wa Serikali kila mwezi badala ya utaratibu uliopo sasa wa kiwango cha mfuto cha 15% ya mapato ghafi kila robo mwaka. Ninapendekeza kurekebisha kifungu cha Sheria kwa kuweka sharti la maandalizi ya hesabu mjumuisho kwa kutumia hesabu za Taasisi za Umma zilizokaguliwa lengo la hatua hii ikiwa ni kurahisisha, kuimarisha uaminifu na utegemezi wa hesabu katika kufanya maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa usafirishaji bidhaa za nje Sura, Na. 199, ninapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Usafirishaji wa Bidhaa za kutoka nje ya nchi kwa kiwango cha 30% hadi 150 kwa kila kilo moja kutegemea na kiwango kilicho kikubwa kwenye vinia inayotambulika kwa *heading* 44.08. Lengo la hatua hii ni kulinda wazalishaji wa ndani watatoza 30% hadi shilingi 150 kwa zile zinazotoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usajili wa Utambuzi wa Watu, Sura Na. 36; ninapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Usajili na Utambuzi wa Watu, Sura Na. 36 ili kusamehe Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Wizara, Idara, Wakala na Taasisi za Serikali zinazowasilisha mapato yake yote Mfuko Mkuu wa Serikali kulipa ada ya matumizi ya taarifa za utambuzi *(NIDA)*.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Tume ya Mpango. Napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Tume ya Mipango, Sura Na. 127, kuweka masharti mbalimbali ya kufanya tathmini ya miradi ya uwekezaji wa umma katika miradi kabla ya kuidhinisha kama ilivyokuwa imebainishwa.

Mheshimiwa Spika, ninapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori, Sura Na. 283 kama ifuatavyo:-

(i) Mapato yatokanayo na ada kuwinda wanyama muhimu kama ilivyoainishwa katika kanuni za uwindaji

wa kitalii hususan shughuli za uwindaji kitalii katika Mapori ya Akiba yatagawanywa kama ambavyo nimeelekeza, nimebainisha katika mtiririko huo a, b, c na d;

(ii) Michango inayotolewa na Makampuni ya uwindaji ya kitalii zinazomiliki vitalu katika Mapori ya Akiba kama ambavyo nimebainisha katika mtiririko a, b, c na d;

(iii) Mapato yatokanayo na shughuli za utalii picha katika Mapori Tengefu yatagawanywa nayo kama ambavyo nimebainisha katika mtiririko huu wa orodha a, b, c na d;

(iv) Mapato yatokanayo na ada za kuwinda wanyama muhimu kama ilivyokuwa imebainishwa katika kanuni za uwindaji katika kuhusiana na shughuli za uwindaji wa kitalii katika Mapori Tengefu yatagawanywa na yenyewe kwa uwiano niliyoubainisha a, b, c na d na uwiano wake.

(v) Michango inayotolewa na Makampuni ya uwindaji ya kitalii vinayomiliki vitalu vya uwindaji katika Mapori ya Tengefu kwa ajili ya miradi ya maendeleo itagawiwa kama nimebainisha katika orodha a, b, c pamoja na d.

(vi) Kwa upande wa mapato yatokanayo na ada za uwindaji ya wanyama muhimu kama ilivyokuwa imeainishwa katika kanuni zake mgawanyo wake ni kama ambavyo nimebainisha katika ukurasa wa 116 pamoja na 117 hadi ukurasa wa 118.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria ya Uhifadhi wa Taifa. Marekebisho yaliyofanywa na Sheria ya Fedha ya mwaka 2024 kufuta kifungu kidogo cha 2(b), mgao wa 91% kwenda Mfuko Mkuu. Badala yake kuweka mgao wa 51% ya mapato yatokanayo na huduma zinazotolewa na Shirika la Hifadhi ya Taifa Tanzania kuwekwa kwenye Akaunti ya taasisi hizo ifikapo Benki Kuu ya Tanzania na matumizi yake yatafanyika kwa kuombwa

kibali kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwamba 40% ya mapato hayo yataingizwa Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria ya Msajili wa Hazina Mamlaka pamoja na majukumu, Sura Na. 370; ninapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 8(1)(f) cha Sheria ya Msajili wa Hazina ili kuweka viwango tofauti vya Wakala wa Serikali, Mashirika, Taasisi za Umma kuchangia katika 15% hadi 60% ya mapato ghafi ya Mfuko kama ambavyo nimeainisha katika pendekezo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande Sheria ya Alama za Bidhaa, Sura Na. 85; ninapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Alama za Bidhaa, Sura Na. 85 na kuongeza kifungu kinachoipa Tume ya Ushindani *(FCC)* nguvu ya kisheria ya kutekeleza jukumu lake la utunzaji wa alama za bidhaa. Aidha, ili kufanikisha utekelezaji wa jukumu hilo muhimu katika kudhibiti bidhaa bandia zinazozalishwa nchini na zinazoingizwa kutoka nje ya nchi, itatungwa kanuni mpya ya mwaka 2025 ambayo itabainisha viwango vya utozaji kama ambavyo nimebainisha katika Jedwali Na. 2. Ambalo limeelezea kwa kina viwango vyake na maelezo yake ya kina yametolewa katika ukurasa wa 123 pamoja na 124.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria ya Usimamizi wa Forodha wa jumuiya ya Afrika Mashariki napenda kufahamisha kwamba, Mkutano wa Jumuiya ya Bajeti ya Mashauriano ya Kibajeti ya Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(Pre-Budget Consultative Meeting of Ministers of Finance)* ulifanyika tarehe 20 Mei, 2025 jijini Arusha. Pamoja na masuala mengine ulitengeneza marekebisho ya kisera ikiwemo mabadiliko ya Viwango vya Ushuru wa Forodha vya Afrika Mashariki pamoja na kuweka mapendekezo ya kutekelezwa katika mwaka wa fedha ufuatao. Hatua ambazo zinazopendekezwa zinalenga kulinda viwango vya ndani, kuvutia uwekezaji na kupunguza gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo mapya ya mabadiliko ya viwango vya ushuru wa forodha ni kama ambavyo tumebainisha katika *HS Codes* ambazo tumeziorodhesha kwenye a, b, c, d, e, f,

g, h, i pamoja na zingine ambazo tumeziorodhesha kwenye ukurasa wa 132 hadi ukurasa wa 148 ambayo imeendelea hadi ukurasa wa 151.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria ya Utozaji wa Leseni za Biashara, Sura Na. 101, ninapendekeza kama ifuatavyo: Kufuta kifungu cha 3 kipengele kidogo cha (4) kinachozipa nguvu mamlaka za utoaji leseni za biashara kufunga biashara pale ambapo wafanyabiashara wamekiuka masharti.

Mheshimiwa Spika, ninarudia hili kufuta kifungu cha 3(4) kinachozipa nguvu mamlaka za utozaji wa leseni za biashara kufunga biashara pale ambapo wafanyabiashara wamekiuka masharti ya Sheria husika. Lengo la hatua hii ni kuwaondolea kero wafanyabiashara na kutekeleza maelekezo ya Serikali ya kutofunga biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuongeza kifungu cha 8(7) ambacho kinampa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya masuala ya biashara kuainisha shughuli za kibiashara ambazo hazipaswi kufanywa na wageni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninarudia kuongeza kifungu cha 8(7) ambacho kinampa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya biashara kuainisha shughuli za kibiashara ambazo hazipaswi kufanywa na wageni. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii ni kudhibiti uholela, utaratibu wa utekelezaji wa kifungu hiki utafanywa kwa kupitia Amri *(Order)* itakayotolewa na Waziri ambaye itakuwa na orodha ya shughuli za kibiashara ambazo hazipaswi kufanywa na wageni. Hatuna lengo la ubaguzi tuna lengo la mtu akitoka nje aongeze kitu cha msingi ambacho tunakitarajia tukipate kutoka kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uanzishwaji wa vyanzo vya mapato kwa ajili ya kudhibiti maambukizi ya UKIMWI na kugharamia Bima ya Afya kwa Wote. Mabadiliko ya kisera yanayoendelea duniani yamesababisha wadau muhimu wa maendeleo kupunguza

misaada iliyokuwa inatolewa kwa ajili ya huduma za afya ikiwemo kukabiliana na kudhibiti magonjwa mbalimbali hususan UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, hivyo, Serikali inapendekeza kuanzisha vyanzo mbadala vya mapato ili kupunguza nakisi ya kibajeti kwa kufanya marekebisho katika sheria mbalimbali. Aidha, ninapendekeza 70% ya mapato yatakayoongezeka ipelekwe kwenye Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI na 30% ipelekwe kwenye Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa Wote. Marekebisho hayo ni kama ifuatavyo:- *(Makofi)*

(i) Kufanya marekebisho Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura Na. 147 ili kuongeza ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji vya vilevi vinavyozalishwa na vinavyoingizwa kutoka nje ya nchi kama ifuatavyo:-

(a) Shilingi 20 kwa bia zinazotambulika kwa *Heading* 22.03;

(b) Shilingi 30 kwa mvinyo unaotambulika kwa *Heading* 22.04, 22.05 na 22.06;

(c) Shilingi 50 kwa *spirit* za vinywaji vingine vinavyotambulika kwa *Heading* 22.08;

(ii) Kufanya marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura Na. 147 ili kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye huduma za mawasiliano ya kielektroniki kutoka 17% hadi 17.5%;

(iii) Kufanya marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa na Mafuta, Sura Na. 220 ili kuongeza kiasi cha shilingi 10 kwa kila lita ya mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa;

(iv) Kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Madini, Sura Na. 123 ili kutoza kiwango cha asilimia 0.1 kwenye thamani ya soko ya madini;

(v) Kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura Na. 41 kuongeza kiwango cha kodi kwenye zawadi ya ushindi *(Winning tax)* kwenye michezo ya kubashiri matokeo *(Sports betting)* kutoka 10% hadi 15% kwenye michezo ya kasino ya ardhini pamoja na kutoka 12% hadi 15%;

(vi) Kutoza magari ya mashine zinazoingizwa kutoka nje ya nchi kama ifuatavyo nimebainisha. Shilingi 50,000 kwa magari makubwa shilingi 0 - 100 kwa 100,000 kwa magari yenye ukubwa wa injini (CC) kuanzia 1001-1500; shilingi 150,000 kwa magari yenye ukubwa wa injini (CC) kuanzia 1500 - 2500; shilingi 200,000 kwa magari yenye ukubwa wa injini (CC) kuanzia 2501 na zaidi; shilingi 250,000 kwa *Excavators, Bulldozers, Fork Lifts* na zenye *Heading* 84.29 na 84.27;

(vii) Kutoza shilingi 500 kwa kila tiketi inayotolewa na mtoa huduma wa usafirishaji kwa njia ya treni;

(viii) Kutoza shilingi 1000 kwa kila tiketi inayotolewa kwa mtoa huduma usafirishaji kwa njia ya anga.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi kwa pamoja zinatarajia kuongeza mapato ya Serikali kwa shilingi milioni 586,404.9 na zitakwenda kwenye Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote pamoja na Mfuko wa kugharamia masuala ya UKIMWI kama nilivyobainisha kwenye zile asilimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maboresho ya ada na tozo mbalimbali za taasisi za Serikali pamoja na utekelezaji wake. Ninapendekeza kufanya maboresho ya kurekebisha, kuanzisha, kufuta na kupunguza tozo mbalimbali kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa kuboresha Mfumo wa udhibiti wa Biashara *(Blueprint for Regulatory Reforms* na ku-*improve Business Environment)*. Marekebisho hayo nimeyabainisha kama ambavyo yako kwa upande wa Sekta ya Mifugo, Sekta ya Uvuvi, Sekta ya Utalii, Sekta ya Baraza la Sanaa la Taifa, Shirika la Viwango *TBS,* Wakala wa

Vipimo, Usimamizi wa Afya Mahali pa Kazi, Marekebisho madogo madogo pamoja na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kuendelea kutengeneza mazingira bora ya ufanyaji wa biashara na kuvutia uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, marekebisho madogo katika baadhi ya Sheria za Kodi na Sheria nyingine mbalimbali. Ninapendekeza kufanya marekebisho madogo madogo ya kodi pamoja na nyingine ziwe sanjari na azma ya kurahisisha utekelezaji wake kama ambavyo nimesema kwenye Sheria ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, Sura ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Utakumbuka kuwa tarehe 11 Machi, 2025, niliwasilisha Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 mbele ya Kamati ya Bunge lako zima. Ukomo wa bajeti ya Serikali katika mwaka 2025/2026 uliyopendekezwa ulikuwa shilingi bilioni 57,040.3. Baada ya kuwasilisha mapendekezo hayo ya ukomo, Serikali iliendelea kufanya tathmini ya athari zinazoweza kujitokeza kutokana na mabadiliko ya kisera ya Washirika wa Maendeleo. Tathmini hiyo iliyofanyika kwa vyanzo vyote vya mapato ya ndani na nje ilionesha kuwa kutakuwa na upungufu wa mapato kwa takribani shilingi bilioni 550.

Mheshimiwa Spika, hivyo, inapendekezwa kupunguza kiasi cha shilingi bilioni 550 kwenye makadirio ya awali ya shilingi bilioni 57,040.3 hadi shilingi bilioni 56,490.3. Fedha hizo zilizopunguzwa kwenye baadhi ya miradi ya maendeleo inayotegemea fedha kutoka nje kadhalika Sekta ya Afya na Elimu ambazo zilikuwa zinategemea baadhi ya fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zimepunguzwa na zitaongezewa kutokana na badiliko hilo ili ziweze kupata fedha na kutekeleza shughuli zake kama ambavyo nimetoka kuelezea.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mabadiliko hayo, sera za bajeti, mikakati ya kukusanya mapato pamoja na azma ya Serikali ya kudhibiti matumizi, Sura ya Bajeti inaonesha kuwa jumla ya

shilingi trilioni 56.49 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika katika mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii inatarajiwa kugharamia mapato ya ndani shilingi trilioni 40.47, misaada shilingi trilioni 1.07, mikopo shilingi trilioni 14.95. Kati ya mapato ya ndani yanayotarajiwa, mapato ya kodi ni shilingi trilioni 32.31, mapato yasiyo ya kodi shilingi trilioni 6.48, na mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa shilingi trilioni 1.68. Aidha, mikopo ikijumuisha trilioni 6.27 kutoka vyanzo vya ndani na shilingi trilioni 8.68 kutoka vyanzo vya nje.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya matumizi ya Serikali ya shilingi trilioni 56.49 kwa mwaka wa fedha 2025/2026., yanajumuisha stahiki za watumishi, michango ya pensheni shilingi trilioni 9.17; ununuzi wa bidhaa na huduma shilingi trilioni 5.58; malipo ya riba na mikopo shilingi trilioni 6.49; ruzuku kwa taasisi za Serikali, mashirika ya umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa shilingi trilioni 22.17. Aidha, Serikali inatarajia kutumia shilingi trilioni 7.72 kugharamia malipo ya deni la ndani na nje. Mfumo wa bajeti unaopendekezwa ni kama unavyooenekana sasa kwenye Jedwali Na.3.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutumia fursa hii kuwashukuru washirika wote wa maendeleo walioahidi kuchangia bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2025/2026 ili kufanikisha malengo hayo. Baadhi ya Taasisi na Washirika wa Maendeleo walioahidi ni pamoja na; Benki ya Dunia; Shirika la Fedha la Kimataifa; Benki ya Maendeleo ya Afrika; Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Kiuchumi; Benki ya Uwekezaji ya Ulaya; Mfuko wa Abu Dhabi; Mfuko wa Kuwait; Mfuko wa Kimataifa wa Kusaidia Mapambano Dhidi ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria; Mfuko wa *OPEC;* Mfuko wa Maendeleo ya Kimataifa *(OFID);* Mfuko wa Mazingira Duniani *(GEF);* Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi *(GCF);* Mfuko wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi; Mfuko wa *GRMF;* Umoja wa Mataifa na mashirika yote chini yake; Umoja wa Ulaya; *International Fund for Agricultural Development;* Umoja wa Shirika la Chanjo Ulimwenguni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee pia nizishukuru nchi wahisani walioahidi kuchangia katika utekelezaji wa bajeti hii ikiwemo Australia, Austria, Canada, China, Denmark, Finland, India, Indonesia, Ireland, Italia, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Norway, Oman, Poland, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uhispania, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswisi. Aidha, ninapendekeza kutambua mchango wa moja kwa moja wa ushirikiano kutoka kwa Asasi Zisizo za Serikali ambazo tumekuwa tukishirikiananazo na sekta binafsi, asasi za kiraia na mashirika yasiyo ya kiserikali na taasisi za kidini katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kimaendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuhitimisha nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa weledi wake katika kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais kuongoza Taifa letu. Hakika mchango wake ni mkubwa sana katika ujenzi wa Taifa na hautasahaulika. Hivyo, tutaendelea kumtumia busara zake, hekima zake, taaluma yake na uwezo wake katika kuendeleza ustawi na maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumtakia maisha mema na afya njema baada ya kustaafu, ninaomba nimuage kwa neno kutoka katika Biblia Takatifu, Kitabu cha Hesabu 6:24-26 "Bwana akubariki na kukulinda; Bwana akuangazie nuru ya uso wake na kukufadhili; Bwana akuinulie uso wake na kukupa amani." Amina! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Jimbo la Ruangwa kwa kuendelea kusimamia shughuli za Serikali bila kuchoka na kwa maelekezo mazuri kwetu Wizara ya Fedha na Wizara nyingine za kisekta katika utekelezaji wa majukumu yetu. Kadhalika, ninampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati, Mbunge wa Jimbo la Bukombe, kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu katika utekelezaji wa majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kukushukuru na kukupongeza wewe mwenyewe Dkt. Tulia Ackson Mwansasu, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mbunge wa Jimbo la Mbeya na sasa Uloye na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani. Hakika umetuheshimisha katika nyanja zote. Ninapenda kukudokeza kuwa, Watanzania, Bunge hili na dunia nzima wanajivunia. Aidha, niwapongeze pia Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika na Mbunge wa Jimbo la Ilala pamoja na Wenyeviti wa Bunge, kwa kazi nzuri walizozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza Mheshimiwa Profesa Ibrahim Hamis Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania; Dkt. Mustapher Mohamed Siyani, Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania; Profesa Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama na Mheshimiwa Eva Kiaki Nkya, Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, kwa kazi nzuri wanazozifanya Mhimili wa Mahakama na Sheria umeheshimisha nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie pia fursa hii kwa dhati kuwashukuru na kuwapongeza Wakuu wote wa vyombo vyote vya ulinzi na usalama ambao nimeelezea kazi yao kwa kirefu. Kila tukilala wao huwa hawalali. Niwatambue kwa majina, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Jenerali Jacob John Mkunda; Inspekta Jenerali wa Polisi, Camillus Wambura; Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa; Ndugu Suleiman Abubakar Mombo; Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, Jeremiah Katungu; Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji, Ndugu yangu John William Masunga; Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dkt. Anna Peter Makakala; Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Ndugu Crispin Chalamila; na Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya, Ndugu Aretas James Lyimo. Wote kazi yao wanayofanya ni ya kutukuka sana kama ambavyo nimetoka kutoa maelezo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru pia Mawaziri wenzangu Waheshimiwa Wabunge wote kwa kazi kubwa ambayo wamefanya. Ninawatakia kila la kheri Waheshimiwa Wabunge wote na kwa kazi kubwa waliyoifanya, hakika Watanzania

wasipate shida kuwarudisha tena ili mje kuwawakilisha vyema hapa mtakaporudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini ambaye ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti pamoja na Makamu Mwenyekiti Ndugu yangu Twaha Mpembenwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nimshukuru na kumpongeza Katibu Mkuu Kiongozi Balozi Moses Kusiluka kwa kazi nzuri anayofanya ambayo kwa kweli ameendelea kutusaidia katika majukumu yetu. Ninamshukuru *CPA* Charles Edward Kichere, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa kazi ya kizalendo na nzuri ambayo ameendelea kuifanya ya kufuatilia rasilimali za nchi yetu na kuhakikisha kwamba zianaleta manufaa yaliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee niruhusu nimshukuru Ndugu yangu Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, kaka yangu. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Mbunge wa Jimbo la Ubungo. Kaka yangu huyu ni Mwalimu mwema tumefanya kazi vizuri sana na mafanikio ambayo unayaona ya Wizara hizi, yeye ni Mwalimu na tumefanya kazi nzuri, tunawaomba wananchi wa Ubungo wamrudishe tena Bungeni. Unamwacha Profesa uende kwa nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Naibu Waziri Nyongo pamoja na pamoja na timu nzima ya Wizara ya Mipango na Uwekezaji ikiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Tausi Kida, pamoja na Katibu Mkuu wa Tume Fred Matola Msemwa na timu yote ambayo tumefanya nayo kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kipekee kutoa shukrani na kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Hamad Chande, Naibu Waziri wa viwango vya Wizara ya Fedha na Mbunge wa Jimbo la Kojani kwa kunisaidia kazi, hata niwapo kwenye vikao vya kimataifa huwa kama vile nipo tu kwa jinsi ambavyo Naibu Waziri

anafanya kazi vizuri. Wananchi wa Kojani wasisite kumrudisha tena Naibu Waziri wa viwango vya Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakika ninaendelea kumpongeza Mwalimu wangu, Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Dkt. Natu El-Maamry Mwamba, kwa kazi nzuri anayoifanya, akisaidiwa na wasaidizi wake Naibu Makatibu Wakuu akiwemo Ndugu Amina Shaaban, Ndugu Jenifa Omolo pamoja na Ndugu Elijah Mwandumbya na timu ya Wataalam wote wa Wizara ya Fedha ambao wamefanya kazi nzuri hasa kutuvusha katika vipindi hivi ambavyo dunia nzima ilikuwa inapita kwenye misukosuko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kumpongeza Gavana wa Benki Kuu, Emmanuel Mpawe Tutuba, ambaye amefanya kazi nzuri ya kusimamia uchumi, sera za kifedha na hata tukaweza kuvuka katika vipindi vya msukosuko. Nimpongeze pia Kamishna Yusuph Mwenda, ambaye amefanya kazi nzuri kwenye upande wa Mamlaka ya Mapato, maendeleo yote ni kodi yetu na ninawataka Watanzania na ninatoa rai kwamba tuendelee kuwapa ushirikiano Mamlaka ya Mapato katika kutekeleza jukumu la kodi. Kodi ni za maendeleo, kodi siyo za *TRA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii pia kumpongeza Dkt. Amina Msengwa, Mtakwimu Mkuu wa Serikali kwa kazi kubwa anayofanya ya kusaidia katika majukumu ya takwimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiwa ninaelekea kumaliza nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada alizofanya katika kuboresha sekta ya michezo. Jitihada hizo zimewezesha nchi yetu kuwa miongoni mwa nchi wenyeji wa Mashindano ya *CHAN* na *AFCON* 2027. Kufanyika kwa mashindano hayo kutasaidia kwa kiasi kikubwa kuendeleza na kukuza sekta ya michezo na utalii hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapongeza kwa dhati Simba kwa kutinga hatua ya fainali ya Kombe la Shirikisho Barani Afrika kwa

mara nyingine tangu Mwaka 1993. Simba inapokuwa ya kimataifa mimi huwa ni shabiki wake. Mafanikio haya ya Simba yanatokana na juhudi kubwa ya uwekezaji uliofanywa na Rais wa heshima wa timu hiyo Ndugu Mohamed Dewji. Hii siyo tu inatoa heshima kwa timu hiyo, bali pia inaitangaza nchi yetu katika ramani ya soka la kimataifa. Wakati wanacheza mashindano yale tulikuwa tunawaombea wapate tu kombe hata ambao siyo mashabiki kwa sababu hata wangeliweka chini ya uvungu wa ofisi yao bado lingekuwa Tanzania. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Simba wasibweteke kwa kuwa mafanikio kama hayo wanayojivunia leo, siyo mapya kwa Yanga. Mafanikio hayo wanayojivunia Simba siyo mapya kwa Yanga kwani walifika hatua kama hiyo mwaka juzi na walitolewa tu kwa uwiano wa goli la ugenini, hawakushindwa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumpongeza Ndugu yangu Ghalib Salim Mohamed *(GSM)*. Ndugu *GSM* ameleta chachu kubwa kwenye mafanikio ya Yanga. Niwashauri Wanayanga wanapoandaa ramani ya ujenzi wa uwanja mpya wasisahau kuweka sanamu kubwa ya *GSM*. Nitoe rai kwa vilabu vingine kuiga hatua hizo za Simba na Yanga kwa hatua hizo za mafanikio walizozifikia kwa manufaa ya soka la Tanzania. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza kipekee Mzee Said Salim Bakhresa kwa uwekezaji mkubwa katika tasnia ya michezo. Huyu ni wa mfano, uwekezaji wake umekuwa chachu ya maendeleo ya michezo nchini, hususan kupitia matangazo ya moja kwa moja (mubashara). Ni ukweli usiopingika kuwa maisha ya watu hayawezi kukamilika bila kuwa na furaha, hilo tumeliona kupitia Azam *TV* ambayo si tu imefanya kila mtu kuzungumzia mpira wa miguu, bali wanazungumzia na maisha mengine, wachezaji, wachezaji wa ngumi, mpira wa miguu pamoja na filamu. Licha ya kuwa kampuni hii ni binafsi, lakini kwa sasa imeshakuwa kama mali ya umma kutokana na umuhimu wake katika jamii. Kwa kweli Mzee Bakhresa aheshimiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niruhusu kipekee nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini kutumikia Taifa kwa nafasi ya Waziri wa Fedha tangu alipoingia madarakani. Huu ni uthibitisho na ni imani kubwa aliyonayo kwangu na nimeona fahari kufanya kazi chini ya kiongozi mwenye maono makubwa ya kuiletea nchi maendeleo. Mheshimiwa Rais, siyo tu amenipa fahari kufanya kazi chini yake bali ameiandika historia ya kipekee kwa Wanyiramba, Wasukuma na Wanyaturu wa Singida, kwa kuwa Mnyiramba wa kwanza kusaini kwenye Noti ya Nchi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hii ilikuwa ndoto yangu ya muda mrefu tena wasinipenipe ndoto! Hii ilikuwa ndoto ya muda mrefu tangu nipo kidato cha pili kufuatia mjadala tu ambao tulikuwa tunafanya, tukaiona sahihi ya marehemu Dkt. Gilman Rutihinda aliyekuwa Gavana wa Benki Kuu tukiwa kwenye *group discussion,* ambapo tulikuwa tunajadili sahihi ile ya Gavana wa Benki Kuu nikiwa na Ndugu zangu, ninawashukuru kwa sababu wao ndiyo walionitajia sahihi ya Gavana wa Benki Kuu akiwemo Sibomana ambaye alikuwa anatoka Wilaya moja na Gavana, Ndugu Robert Kitundu, Ndugu John Makuru, Ndugu Richard Marco, pamoja na Steven Nkenguye, wengine walionihakikishia kuwa inawezekana kwa mtu kusaini kwenye Noti ya nchi, ninamshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan ameikamilisha ndoto hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaamini nimeifanya kazi hii kwa uaminifu mkubwa na kazi hii nimeifanya kwa weledi wote, kazi hii nimeifanya kwa nguvu zangu zote, nikitekeleza ipasavyo miongozo ya Mheshimiwa Rais. Siwezi kuelezea zaidi vielelezo vya kila jambo lililofanyika kwenye kila Wizara ambavyo lisingeweza kufanyika bila fedha, hicho ni kielelezo. Upatikanaji wa fedha ili miradi ya maendeleo iweze kutekelezwa ya kila sekta hilo ndilo jukumu nililokuwa nimetumwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jukumu nililopewa la kuwa Waziri wa Fedha limenikumbusha nilipokuwa Kidato cha Tatu nikiwa Makamu Mwenyekiti wa Serikali ya Wanafunzi wa Shule ya Ilboru, mimi ndiyo nilikuwa ninakusanya ushuru. Nilikuwa nikikusanya

ushuru kwa wale wanaofanyia biashara shuleni, ninapeleka kwa Mwalimu wa malezi. Vilevile nikiwa Katibu Mkuu wa Serikali ya Shule ya Mazengo na Mwenyekiti wangu Ndugu Emil, ninajua yupo, mimi ndiyo nilikuwa ninakusanya ushuru wa wale wanaofanyia biashara pale ndani ya shule na malipo yake nilikuwa ninapata mandazi matatu kwa siku. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kazi hizo zilizifanya kwa uaminifu na fedha hizo nilikuwa ninawasilisha kila mwisho wa mwezi kwa Mwalimu wa malezi. Nimetambua hakika ukimtanguliza Mungu, uaminifu, weledi na bidii ni msingi wa ufanisi katika utumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa atakayeteuliwa kushika nafasi hii baada yangu na watumishi wote wa umma kujitahidi kujinyenyekeza, kumtanguliza Mungu katika majukumu yetu, tusimamie imara maslahi ya Taifa letu, haki za wananchi hasa wanyonge, tushinde vishawishi vya rushwa, tuzingatie sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza utumishi wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hakika sina la kusema, nina kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili ya Rais wetu, kama ilivyoelekezwa kwenye Quran Tukufu kwenye Sura Na. 14 Aya ya Saba, "Na alipotangaza Mola wenu Mlezi, Mkishashukuru nitakuzidishieni neema''. Itoshe tu kusema Mheshimiwa Rais ninashukuru sana na ninaendelea kukuombea afya njema ili kazi yako kubwa ambayo umefanya na hata tunapoenda kwenye uchaguzi kila Mtanzania akulipe kwa kukupigia kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Iramba Magharibi, wao ndiyo walionipa nafasi ya kuwa Mbunge wao, nimefanya kazi nao pamoja, ninaamini kwamba sijawaangusha na wataendelea kunichagua. Ninapenda kuwaahidi kuwa nitaendelea kushirikiana nao katika kuliletea maendeleo Jimbo letu la Iramba Magharibi. *Nsongeli zigizigi*, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa nitumie fursa hii kumshukuru mke wangu mpenzi na rafiki yangu Ndugu Neema Mwigulu Nchemba, ninadhani yupo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na watoto wetu Joshua, ninadhani yupo na yeye kaka yao huyo, Gracious, Isaac Mjumbe wa Baraza Kuu ninadhani na yeye yupo hapo, Bernice pamoja na *uncle* zangu Chris, Amani, Hope na dada zao wakubwa Nazareth, ninajua kaka zangu na dada zangu wapo hapa, maombi yao na na kunipa faraja kumeniwezesha kutekeleza vema majukumu ya kulitumikia Taifa na Watanzania katika nafasi niliyoaminiwa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapo awali, Mkutano huu ni wa mwisho kabla ya kuelekea kwenye Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani hapo Oktoba 2025, hivyo ninawaomba sana Watanzania wenzangu kutumia haki yao ya kikatiba ya kuchagua au kuchaguliwa katika ngazi hizo nilizozisema. Aidha, niviombe vyama vya siasa nchini kushiriki uchaguzi huo na kuwahimiza wananchi kutumia haki yao ya kikatiba kwa utulivu na amani kama ilivyo desturi ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ninasisitiza tena, Serikali chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi imedhamiria kwa dhati kuhakikisha maendeleo ya kiuchumi na huduma za kijamii zinawafikia Watanzania kwa gharama nafuu na kwa wakati. Sisi sote ni mashahidi kuwa Mheshimiwa Rais amefanya mageuzi makubwa ya kiuchumi kwa kukamilisha miradi mingi ya kimkakati katika sekta za uchukuzi, nishati, ujenzi, kilimo na huduma za jamii. Hii imeongeza ufanisi katika sekta za uzalishaji, fursa za ajira, kuimarisha kwa huduma kwa jamii pamoja na kuchochea ukuaji wa biashara na uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa mafanikio hayo, nina imani kuwa katika Uchaguzi huu Mkuu, CCM haitapoteza Jimbo lolote wala Kata na kura za Urais zitakwenda kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Mgombea Mwenza Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi. Hakika

yajayo yanafurahisha na Tanzania chini ya Mama itapata mafanikio makubwa zaidi kwa uchapakazi wake ambao tumeuona. "Kazi na Utu. Tunasonga Mbele". Mungu ibariki Afrika, Mungu ibariki Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA, MHESHIMIWA DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAPENDEKEZO YA SERIKALI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2025/26 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## I. UTANGULIZI

**1. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2025/26. Uwasilishaji wa bajeti hii umezingatia Ibara ya 137 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, ikisomwa pamoja na Kifungu cha 23(3) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni 124(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023.

**2. Mheshimiwa Spika**, sambamba na hotuba hii, vipo vitabu vinne (Na. I, II, III na IV) vinavyoelezea kwa kina takwimu za Bajeti ya Serikali. **Kitabu cha Kwanza** kinahusu makadirio ya mapato yatakayowezesha utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2025/26; **Kitabu cha Pili** kinahusu makadirio ya matumizi ya kawaida kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala wa Serikali; **Kitabu cha Tatu** ni makadirio ya matumizi ya kawaida kwa Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na **Kitabu cha Nne** kina makadirio ya matumizi ya maendeleo kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Ofisi za Wakuu wa Mikoa pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**3. Mheshimiwa Spika**, upo pia Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2025, Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2025 pamoja na Taarifa ya Vihatarishi vya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2025/26 ambayo ni sehemu ya bajeti hii.

**4. Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki vikao vya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hadi tunapoelekea kuhitimisha muda wa uwakilishi wa wananchi kwa awamu hii.

**5. Mheshimiwa Spika**, kwa moyo wa simanzi na huzuni kubwa niruhusu nitoe pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waheshimiwa Wabunge pamoja na watanzania kwa ujumla kwa kuondokewa na wapendwa wetu. Mtakumbuka kuwa, tumewapoteza viongozi mbalimbali wa kitaifa, wabunge wenzetu, watu wengine mashuhuri pamoja na wananchi wenzetu.

**6. Mheshimiwa Spika**, Taifa lilipata pigo la kuondokewa na Hayati Cleopa David Msuya, Makamu wa Kwanza wa Rais, Waziri Mkuu mstaafu na aliyewahi kuhudumu kama Waziri wa Fedha. Hayati Msuya atakumbukwa daima kwa uadilifu na mchango wake mkubwa kwa Taifa. Aidha, Bunge lako tukufu lilipata pigo la kuondokewa na Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani - Kanda ya Afrika. Tutaendelea kumkumbuka na kumuenzi kwa uzalendo na bidii yake katika utumishi kwa nchi yetu.

**7. Mheshimiwa Spika**, Taifa pia liliondokewa na viongozi wengine wakiwemo: Mheshimiwa John Tendwa aliyewahi kuwa Msajili wa Vyama vya Siasa ambaye atakumbukwa kwa kujenga misingi imara kwa vyama vya siasa nchini; Mheshimiwa Jaji Fredrick Mwita Werema aliyewahi kuwa Jaji wa Mahakama Kuu Divisheni ya Biashara na Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Mheshimiwa Profesa Philemon Mikol Sarungi, Daktari Bingwa wa Mifupa aliyewahi kuwa Mbunge, Mkuu wa Mkoa na Waziri katika Wizara mbalimbali; mwanadiplomasia mkongwe Mheshimiwa Balozi Juma Volter Mwapachu aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na mwakilishi wa kudumu wa Tanzania katika Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO); pamoja na viongozi wengine wote waliotangulia mbele ya haki.

**8. Mheshimiwa Spika**, wapo watanzania wenzetu waliofikwa na majanga mbalimbali yaliyosababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali na miundombinu ikiwemo kuporomoka kwa jengo la ghorofa Kariakoo Jijini Dar es Salaam, ajali za barabarani, maradhi na mabadiliko ya tabianchi. Tunawaombea majeruhi wote uponyaji wa haraka ili waweze kurejea katika shughuli zao. Aidha, nitoe pole kwa watanzania wote waliopoteza ndugu, jamaa, marafiki na mali zao kutokana na maafa hayo. **BWANA alitoa, na BWANA ametwaa; Jina la BWANA lihimidiwe…..*Inna Lillah Wa Inna illayh Rajiun!*.** Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina!!!

**9. Mheshimiwa Spika**, naomba kutumia fursa hii kuungana na familia ya wakristu kutoa pole kwa waumini na viongozi wa Kanisa Katoliki kwa kuondokewa na kiongozi mkuu wa kanisa hilo Baba Mtakatifu, Papa Francis. Niwasihi waumini wa Kanisa Katoliki na watu wote kuendelea kuyaenzi mazuri yote yaliyotekelezwa na Papa Francis na tuendelee kumuombea kwa Mwenyezi Mungu aipokee roho yake na kuilaza mahali pema peponi, Amina. Aidha, nipende kumpongeza Papa Leo XIV kwa kuchaguliwa kuliongoza Kanisa hilo. Namtakia kheri na fanaka katika utekelezaji wa majukumu yake.

**10. Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee, nitumie fursa hii kuwaomba wananchi waungane nami kumpongeza Mheshimiwa Profesa Mohamed Yakub Janabi, Mkurugenzi wa Hospitali yetu ya Taifa Muhimbili na Mshauri wa Rais – Afya kwa kutuheshimisha tena na kushinda kwa kishindo Uchaguzi wa Ukurugenzi wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Kanda ya Afrika. Ushindi huu ni alama nyingine ya kazi nzuri anayoifanya pamoja na kutambuliwa kwa mchango wa nchi yetu Barani Afrika. Kwa ushindi huu wa Profesa Janabi, **Hakika naiona Afrika yenye watu wenye afya njema, na wanaozingatia ulaji wenye afya!**

## II. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI

**11. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali chini ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26. Katika utekelezaji wa mpango

huu, Serikali imefanya makubwa yanayoonekana katika sekta mbalimbali za uchumi wetu. Ufanisi huu umedhihirisha kuwa **MAMA** ni kiongozi bora, mchapakazi, mwaminifu, mbunifu, muadilifu, mzalendo na mwenye nia na maono makubwa ya kuleta ustawi wa Taifa na maendeleo ya watanzania. Shabaha na Malengo ya Bajeti

**12.** **Mheshimiwa Spika**, katika bajeti ya mwaka 2024/25, Serikali ililenga kufikia malengo na shabaha za uchumi na bajeti ambapo, mwaka 2024 Pato halisi la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 5.5 ikilinganishwa na lengo la asilimia 5.4. Aidha, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Mei 2025, wastani wa mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.1 ikiwa ni ndani ya lengo la wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0 katika muda wa kati. Vilevile, bajeti ilikuwa na malengo ya kisera ya kuongeza uwezo wetu wa kuzalisha hapa nchini, hususan kwa bidhaa zinazoagizwa kutoka nchi za nje na zinazouzwa nje ya nchi ili kuongeza ajira na kuboresha mgawanyo wa vipato kwa watanzania. Kutokana na utekelezaji wa sera hizo, nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa ilipungua kufikia dola za Marekani milioni 5,157.2 mwaka 2024 kutoka dola za Marekani milioni 6,032.3 mwaka 2023.

**Mwenendo wa Mapato**

**13.** **Mheshimiwa Spika**, katika bajeti ya mwaka 2024/25, Serikali ilipanga kukusanya jumla ya shilingi trilioni 50.29 kutoka katika vyanzo vya ndani na nje. Hadi Mei 2025, kiasi cha shilingi trilioni 45.07 kimekusanywa, sawa na asilimia 89.6 ya lengo la mwaka. Mchanganuo wa mapato yaliyokusanywa katika kipindi hicho ikilinganishwa na lengo la mwaka ni kama ifuatavyo:

(i) Mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), yalikuwa shilingi trilioni 26.86, sawa na asilimia 91.3 ya lengo;

(ii) Mapato yasiyo ya kodi yanayokusanywa na Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali, yalifikia shilingi trilioni 2.97, sawa na asilimia 77.4 ya lengo;

(iii) Mapato yanayokusanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa yalifikia shilingi trilioni 1.26, sawa na asilimia 93.2 ya lengo;

(iv) Misaada na mikopo nafuu kutoka nje ya nchi iliyopokelewa ilikuwa shilingi trilioni 5.32, sawa na asilimia 87.5 ya lengo;

(v) Mikopo ya ndani ikijumuisha mikopo ya kulipia dhamana za Serikali zilizoiva ilifikia shilingi trilioni 6.23, sawa na asilimia 94.1 ya lengo; na

(vi) Mikopo ya masharti ya kibiashara ya nje ya nchi ilifikia shilingi trilioni 2.43, sawa na asilimia 81.3 ya lengo.

**14. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Awamu ya Sita imefanya mageuzi makubwa ambayo yameongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani. Ifahamike kuwa, kuimarika kwa makusanyo ya mapato ya ndani ni msingi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, utoaji wa huduma bora kwa wananchi na ustawi wa Taifa kwa ujumla.

**15. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita, mapato ya ndani yaliongezeka kutoka shilingi trilioni 20.59 mwaka 2020/21, sawa na wastani wa shilingi trilioni 1.72 kwa mwezi hadi shilingi trilioni 29.83 mwaka 2023/24, sawa na wastani wa shilingi trilioni 2.49 kwa mwezi. Aidha, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Mei 2025, mapato ya ndani yamezidi kuongezeka kufikia wastani wa shilingi trilioni 2.83 kwa mwezi. Vilevile, uwiano wa mapato ya ndani kwa Pato la Taifa umeongezeka kufikia asilimia 15.0 mwaka 2023/24 kutoka asilimia 13.7 mwaka 2020/21. Mwenendo huu chanya unadhihirisha mageuzi makubwa kwenye ukusanyaji wa mapato. Mafanikio hayo yametokana na:

(i) Utekelezaji wa sera madhubuti za bajeti na uimarishaji wa mifumo ya kiutendaji;

(ii) Matumizi sahihi ya mifumo ya kisasa ya TEHAMA iliyounganishwa (intergrated information systems);

(iii) Kuimarisha uhusiano kati ya TRA na walipakodi kupitia elimu ya mlipakodi, kampeni za uhamasishaji, na kuboresha huduma kwa wateja;

(iv) Uboreshaji wa masoko ya madini, ambayo yameongeza mapato kutoka sekta ya madini kupitia tozo na ada mbalimbali; na

(v) Ufuatiliaji wa karibu wa mashirika ya umma, kuhakikisha kwamba yanaongeza tija, yanachangia gawio kwa Serikali, na hayatumii vibaya rasilimali.

**16. Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla, mafanikio haya ya Serikali ya Awamu ya Sita katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ni matokeo ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Rais hususan katika usimamizi madhubuti wa uchumi pamoja na jitihada za watumishi wa umma, taasisi za fedha, sekta binafsi, na wananchi kwa ujumla. Kipekee, napenda kutoa pongezi na shukrani za dhati kwa taasisi zinazohusika katika ukusanyaji wa mapato ya ndani. Nianze kwa kuipongeza Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa usimamizi mzuri katika ukusanyaji wa mapato. Hakika TRA imefanya maboresho makubwa katika utendaji wake ambayo yamesaidia kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato ya ndani. **Kodi yetu, Maendeleo yetu!**

**17. Mheshimiwa Spika**, naomba pia kuipongeza Wizara ya Madini kwa kusimamia ipasavyo sekta ya madini ambayo imekuwa chanzo muhimu cha mapato, pamoja na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa usimamizi madhubuti wa mapato yanayokusanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ni dhahiri kuwa jitihada zao zimechangia kwa kiasi kikubwa mafanikio tunayoyaona leo katika eneo la mapato ya ndani.

**18. Mheshimiwa Spika**, nitoe rai kwa taasisi nyingine za Serikali zenye dhamana ya kukusanya mapato ziige mfano wa wizara na taasisi hizi kwa kuongeza jitihada za ukusanyaji wa mapato ili tuondokane na utegemezi wa bajeti. Aidha, Serikali itaendelea kuchukua hatua za kuboresha sera, mifumo, na mbinu za ukusanyaji mapato ili kufikia azma ya kujitegemea. Niwahakikishie

kuwa, Serikali haitamvumilia mtu yeyote atakayekwamisha azma hii.

**19. Mheshimiwa Spika**, naomba kusisitiza kuwa, sisi viongozi tuwe mstari wa mbele katika kulipa kodi, kuwahamasisha wananchi kulipa kodi stahiki kwa hiyari pamoja na kuhakikisha hatutumii mamlaka na madaraka yetu kusaidia ukwepaji kodi. Ikumbukwe hata Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alisema "***Kila mtanzania anapaswa kuelewa kwamba maendeleo hayawezi kupatikana kwa kutegemea misaada, ni lazima tulipe kodi***".

**20. Mheshimiwa Spika**, katika bajeti ya mwaka 2024/25, Serikali iliweka utaratibu wa kuingia mikataba ya utendaji (performance agreements) na wazalishaji wote tunaowapatia vivutio vya misamaha ya kodi ili kuweza kutathmini tija ya vivutio tunavyowapatia. Hadi Mei 2025, Serikali imefanikiwa kusaini mikataba 169 na wawekezaji mbalimbali. Hii itatusaidia kuondoa uwezekano wa kulea utovu wa tija (inefficiency) kwa wale wanaopata vivutio na kuhakikisha kuwa wanakua na kuhitimu kutoka katika mahitaji ya kulindwa. Tunapenda wanufaika wote wajue kuwa ulinzi wa kisera wanaopewa siyo wa maisha na hivyo, watumie fursa hiyo kuongeza ufanisi na kujenga uwezo wa kusimama wenyewe.

**Mwenendo wa Matumizi**

**21. Mheshimiwa Spika**, makadirio ya matumizi yaliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka 2024/25 ni shilingi trilioni 50.29 ambapo shilingi trilioni 33.75 ni matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 16.54 ni matumizi ya maendeleo. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Mei 2025, ridhaa ya matumizi iliyotolewa ilikuwa shilingi trilioni 42.90, sawa na asilimia 85.3 ya lengo la mwaka.

**22. Mheshimiwa Spika**, kati ya kiasi hicho, ridhaa ya matumizi ya shilingi trilioni 30.63, sawa na asilimia 90.8 ya lengo la mwaka ilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, ridhaa ya matumizi ya shilingi trilioni 15.74, sawa na asilimia 95.1 ya lengo la mwaka ilitolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Ridhaa ya matumizi ya maendeleo inajumuisha kiasi cha shilingi trilioni 3.47 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ambacho kilipelekwa moja kwa moja kwenye utekelezaji wa miradi (D-Fund).

**23. Mheshimiwa Spika**, baadhi ya maeneo yaliyopelekewa fedha katika kipindi cha Julai 2024 hadi Mei 2025 ni pamoja na: ugharamiaji wa deni la Serikali shilingi trilioni 11.16; ugharamiaji wa mishahara ya watumishi wa umma shilingi trilioni 10.27; na maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 shilingi bilioni 741.5. Aidha, kwa kutambua mchango wa wakandarasi, wazabuni na watoa huduma katika kujenga Taifa, Serikali imeendelea kulipa madeni yaliyohakikiwa ambapo kiasi cha shilingi trilioni 1.01 kimelipwa. Ulipaji wa madeni haya umesaidia kulinda mitaji na kuchochea shughuli za kiuchumi nchini.

**24. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kugharamia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikijumuisha: Ujenzi wa barabara, madaraja, na viwanja vya ndege ambapo shilingi trilioni 1.58 zilitolewa; ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya reli ikiwemo mradi wa ujenzi wa Reli ya Kiwango cha Kimataifa (SGR) shilingi trilioni 1.68; utekelezaji wa mradi wa Kufua Umeme katika Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP) MW 2,115 na mradi wa kusambaza umeme vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) shilingi bilioni 574.8; na ujenzi na ukarabati wa viwanja vya mpira kwa ajili ya maandalizi ya AFCON 2027 shilingi bilioni 179.8.

**25. Mheshimiwa Spika**, Serikali pia imeendelea kuboresha huduma za jamii kwa kugharamia: mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu na vyuo vya kati ambapo shilingi bilioni 636.0 zimetolewa; Programu ya Elimumsingi na Sekondari bila Ada shilingi bilioni 444.7; miradi ya maji mijini na vijijini shilingi bilioni 378.7; ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kwa ajili ya hospitali za mikoa, kanda na rufaa shilingi bilioni 414.7; ujenzi na ukarabati wa hospitali za wilaya, mikoa, kanda na rufaa shilingi bilioni 47.2; na ujenzi wa vituo vya afya na zahanati shilingi bilioni 7.3.

**Mwenendo na Uhimilivu wa Deni la Serikali**

**26. Mheshimiwa Spika**, hadi Aprili 2025, deni la Serikali lilikuwa shilingi trilioni 107.70. Kati ya kiasi hicho, deni la nje ni shilingi trilioni 72.94 na deni la ndani ni shilingi trilioni 34.76. Tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Oktoba 2024 imeonesha kuwa deni ni himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu. Katika tathmini hiyo, viashiria vinaonesha kuwa kwa mwaka 2024/25: thamani ya sasa ya deni la Serikali kwa Pato la Taifa ni asilimia 40.3 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55; thamani ya sasa ya deni la nje kwa Pato la Taifa ni asilimia 23.6 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 40; na thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 123.8 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 180.

**27. Mheshimiwa Spika**, Machi 2025, kampuni ya Moody's Investors Service ilifanya zoezi la mapitio ya kwanza ya tathmini ya nchi kukopesheka katika masoko ya fedha ya kimataifa kwa mwaka 2025. Baada ya kukamilika kwa zoezi hilo, kampuni hiyo ilichapisha matokeo ambayo yameendelea kuiweka Tanzania katika daraja la B1 kama ilivyokuwa kwa matokeo ya mwisho ya mwaka 2024. Aidha, kampuni nyingine kubwa ya Fitch Ratings inaendelea na mapitio ya kwanza kwa mwaka 2025 na inatarajia kuchapisha matokeo hivi karibuni. Kampuni hiyo ilichapisha matokeo ya mapitio ya mwisho Desemba 2024, ambapo iliiweka Tanzania katika daraja la B+.

**28. Mheshimiwa Spika**, matokeo ya tathmini ya nchi kukopesheka katika masoko ya mitaji ya kimataifa yanaendelea kuipa taswira chanya nchi yetu katika medani za kimataifa. Matokeo hayo ni bora kuliko nchi nyingine za ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Pamoja na mambo mengine, matokeo hayo yamechangiwa na jitihada za Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji kwa sekta binafsi, kukuza uchumi, kusimamia kwa makini deni la Serikali na kuimarisha ushirikiano wa kimataifa.

**29. Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ili kuhakikisha deni linaendelea kuwa himilivu ikiwemo:

Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi wa mikopo katika ugharamiaji wa bajeti; kuelekeza fedha za mikopo katika miradi inayokuza mapato ya ndani na mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi; na kuendelea kuwahimiza Maafisa Masuuli kuzingatia maandalizi ya msingi ya miradi kabla ya kuingia mikataba kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo iliyopo ili kuepuka ongezeko la gharama za mradi unaokopewa fedha.

## III. MAELEZO YA JUMLA

**30. Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa bajeti hii ni ya mwisho kabla ya kuelekea kwenye Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2025, sina budi kubainisha masuala muhimu ili wananchi watakapokuwa wameshika kalamu zao za maamuzi wasisite kuweka alama ya vema kwa mgombea urais na mgombea mwenza, wagombea wa nafasi za ubunge, uwakilishi na udiwani kupitia **Chama Cha Mapinduzi**.

**31. Mheshimiwa Spika**, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa mgombea wa Chama Cha Mapinduzi katika nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye Uchaguzi Mkuu utakaofanyika Oktoba, 2025. Aidha, niwapongeze wajumbe wa Halmashauri Kuu na Mkutano Mkuu wa CCM kwa kumchagua kiongozi huyu makini kupeperusha bendera ya Chama katika uchaguzi mkuu. Ni ukweli usiopingika kuwa kuchaguliwa kwake kugombea nafasi hiyo kumetokana na juhudi za kusimamia na kutekeleza kikamilifu Ilani ya CCM ya Uchaguzi ya Mwaka 2020 ili kuwaletea wananchi maendeleo. Ni dhahiri kuwa chombo madhubuti bila nahodha imara na hodari hakiwezi kumudu mawimbi. **Hakika Tanzania ya MAMA inameremeta!**

**32. Mheshimiwa Spika**, katika hatua nyingine, Chama Cha Mapinduzi kilimteua Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kuwa mgombea mwenza wa nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa tiketi ya CCM. Watanzania wanamfahamu Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa misimamo yake thabiti isiyoyumba kwenye masuala ya msingi na yenye

maslahi mapana kwa Taifa. Ni dhahiri kuwa misimamo hiyo inaenda sambamba na falsafa ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kutokutetereka wala kuyumba kwenye masuala yenye maslahi mapana kwa Taifa letu.

**33. Mheshimiwa Spika**, nimpongeze pia Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kuwa mgombea wa CCM katika nafasi ya Urais wa Zanzibar kwenye Uchaguzi Mkuu utakaofanyika Oktoba, 2025. Hivyo, niwasihi wananchi wa Zanzibar kumchagua tena Dkt. Hussein Ali Mwinyi kuwa Rais ili aweze kuendeleza mazuri yote aliyoanzisha.

**34. Mheshimiwa Spika**, uteuzi huu umeleta matumaini mapya kwa watanzania kwa kuwa uchaguzi mkuu utakwenda kuwapa watanzania viongozi wanaokidhi matarajio yao. **Tunamfahamu Dkt. Samia Suluhu Hassan! Tunamfahamu Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi! Tunamfahamu Dkt. Hussein Ali Mwinyi!, HATUBAHATISHI; Hakika kwa safu hii, Oktoba 2025 ushindi ni mapemaaaaaa!!**

**35. Mheshimiwa Spika**, kwa safu hiyo, tuna uhakika kuwa Serikali tutakayoichagua itasimamia uhuru wa Taifa letu, italinda utaifa na Muungano wetu, itaendelea kupambana na wahujumu uchumi, wala rushwa, mafisadi, wakwepa kodi na wazembe katika ofisi za umma. Huu ndio umekuwa msimamo na maelekezo ya Mheshimiwa Rais kwa wasaidizi wake wote.

**36. Mheshimiwa Spika**, Chama Cha Mapinduzi kimewaletea watanzania safu hii ya wagombea kwa sababu bado kuna kazi ya kufanya. Tumemaliza baadhi ya miradi ya kimkakati, lakini bado tuna kazi ya kuendelea na miradi ya kimkakati kwenye vipengele vilivyosalia. Tumemaliza suala la upatikanaji wa huduma za afya, tunakwenda kwenye ubora wa huduma za afya; tumemaliza upatikanaji wa elimu, sasa tunakwenda kwenye ubora wa elimu anayopewa mtoto wa kitanzania; tumemaliza kufikisha umeme kila kijiji sasa tunakwenda kwenye ngazi ya kitongoji na kaya.

**37. Mheshimiwa Spika**, tunakwenda kwenye upatikanaji wa maji kwenye kila kaya; na tunakwenda kwenye ubora wa miundombinu ya barabara mijini na vijijini. Aidha, tunakwenda kwenye *modernization* ya shughuli za uzalishaji, (kilimo bora, mbegu bora, ufugaji wa kisasa na uvuvi wa kisasa), tunakwenda kwenye kuongeza thamani ya mazao ndani ya nchi, kuongeza ujenzi na upanuzi wa viwanda, na kuweka mazingira bora ya uwekezaji na kufanya biashara.

**38. Mheshimiwa Spika**, katika hatua nyingine, kama watanzania, tuna kila sababu ya kujivunia umoja wetu, utaifa wetu, Muungano wetu na hatua kubwa za kimaendeleo tulizozipiga tangu nchi yetu imepata uhuru mwaka 1961. Tumevishinda vita vya ukabila, tumevishinda vita vya udini na tunasonga mbele na umoja wetu, utaifa wetu na muungano wetu. Pongezi nyingi kwa watanzania wote kwa ushindi huu, kwa uzalendo wetu na uhodari wa kuipenda Tanzania. Tangu kuasisiwa kwake, Tanzania imekuwa Taifa kimbilio la wengi kuanzia majirani na mataifa ya mbali kwa ujumla.

**39. Mheshimwa Spika**, historia hii njema katu haiwezi kutengwa na kazi nzuri iliyofanywa na Chama chenye vinasaba vya ukombozi, **Chama Cha Mapinduzi (CCM),** kilichorithi harakati za ukombozi tangu kuundwa kwake kwa muungano wa vyama vya TANU na ASP. Chama Cha Mapinduzi kimeendelea kuwa Chama cha kipekee Tanzania, Afrika na duniani kote kwa mchango wake katika historia ya ukombozi hapa nchini na kusini mwa Afrika.

**40. Mheshimiwa Spika**, Chama Cha Mapinduzi ndio kimeongoza vita dhidi ya maadui wakuu watatu - UJINGA, MARADHI na UMASIKINI. Ni dhahiri kuwa nchi yetu imepiga hatua kubwa sana katika kukabiliana na maadui hao tangu Rais wa awamu ya kwanza Baba wa Taifa Mwl. Julius Kambarage Nyerere alipotangaza vita hivyo. Wakati tunapata uhuru asilimia kubwa ya watanzania walikuwa hawajui kusoma na kuandika. Tulianza na idadi ndogo sana ya shule za msingi, sekondari, vyuo na idadi ndogo ya wanafunzi. Kwa mfano mwaka 1961 tulikuwa na shule za msingi 3,270, walimu 9,885 na wanafunzi 486,470 tu, sekondari shule 41 tu, walimu 764 tu na wanafunzi 11,832 tu, vyuo vya ualimu

8 tu, walimu 164 tu, na wanafunzi 1,723 tu, chuo kikuu kimoja tu, wahadhiri 6 tu na wanafunzi 14 tu.

**41. Mheshimiwa Spika**, kwa takwimu za mwaka 2024 nchi yetu sasa imefikisha shule za msingi 20,533 kutoka shule 3,270, walimu 229,840 kutoka walimu 9,885 na wanafunzi 11,391,185 kutoka wanafunzi 486,470 tu, sekondari shule 6,269 kutoka shule 41 tu, walimu 128,686 kutoka walimu 764 tu, na wanafunzi 3,314,198 kutoka wanafunzi 11,832 tu, vyuo vya ualimu 65 kutoka 8 tu, walimu 1,633 kutoka walimu 164 tu na wanafunzi 16,002 kutoka wanafunzi 1,723 tu, vyuo vikuu 79 kutoka chuo kikuu kimoja, wahadhiri 8,625 kutoka wahadhiri 6 na wanafunzi 334,854 kutoka wanafunzi 14. Hayo yote ya kumpiga vita adui **UJINGA** yamefanyika chini ya CCM. **Mheshimiwa Spika**, **CCM NA IHESHIMIWE!**

**42. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa kumpiga vita adui **MARADHI**, hatua kubwa imefikiwa katika nyanja zote ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya afya, wataalamu wa afya wa ngazi zote, upatikanaji wa vifaa tiba dawa na vitendanishi. Wakati tunapata uhuru, tulikuwa na madaktari watano (5) tu, ambapo kwa sasa madaktari bingwa pekee ni zaidi ya 2,469.

**43. Mheshimiwa Spika**, wakati tunapata uhuru, huduma za afya kwa nchi nzima zilikuwa duni sana, sasa tuko hatua za kuwa na Bima ya Afya kwa wote, tukiwa tumefanikiwa kupunguza vifo vya watoto na vifo vya mama wajawazito na kuimarisha huduma za kibingwa hapa nchini. Mafanikio hayo ni harakati na jitihada za kumpiga vita adui **MARADHI** na hayo yote yamefikiwa chini ya uongozi wa **Chama Cha Mapinduzi**, **Mheshimiwa Spika**, **CCM NA IHESHIMIWE!**

**44. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa kumpiga vita adui **UMASIKINI**, Taifa limepiga hatua kubwa, ambapo takwimu rasmi zinaonesha kuwa kati ya mwaka 1991 na 2018, umasikini umepungua. Mathalani katika kipindi hicho cha marejeo, asilimia ya watu waliokuwa wakiishi katika umasikini wa hali ya juu (umasikini wa chakula) ilipungua kwa kiasi kikubwa kutoka asilimia

21.6 hadi asilimia 8.0, huku kiwango cha umasikini wa mahitaji ya msingi kikishuka kutoka asilimia 38.6 hadi asilimia 26.4.

**45. Mheshimiwa Spika**, katika hatua nyingine, Serikali ya Awamu ya Sita imeonesha uhimilivu mkubwa wa kukabiliana na misukosuko ya kiuchumi, ya ndani na nje ya nchi iliyosababishwa na majanga ya asili yanayohusiana na mabadiliko ya tabianchi na yale ya kibinadamu yanayohusisha mizozo na migogoro ya kimataifa na mabadiliko ya kisera.

**46. Mheshimiwa Spika**, utakumbuka kuwa msukosuko wa kiuchumi ulioikumba dunia kwa muda mrefu kutokana na mzozo wa Ulaya Mashariki umesababisha kupanda kwa gharama za maisha na madhara mengineyo ikiwemo kupanda kwa gharama za usafirishaji na uzalishaji. Hali hii ilisababisha nchi nyingi kuingia kwenye madeni makubwa. Hata hivyo, Serikali ilichukua hatua za haraka na madhubuti za kukabiliana na madhara yote yaliyojitokeza.

**47. Mheshimiwa Spika**, baadhi ya hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kutoa ruzuku kwa kaya maskini ambapo shilingi bilioni 9,615 zimetumika, kuendelea na mpango wa elimu bila ada ambapo shilingi trilioni 1.3 zimetumika, shilingi trilioni 2.7 kwa mikopo ya elimu ya juu na kulipa nusu ya bei ya mbolea ili kupunguza gharama ambapo kiasi cha shilingi bilioni 708.6 kilitumika katika kipindi cha miaka mitatu (2021/22 – 2023/24). Katika programu hii ya ruzuku, Serikali imekuwa ikimlipia mkulima wa Tanzania nusu ya gharama kwa bei ya kila mfuko. Sio kila nchi ilifanya jambo hili, hii inaonesha ni kiasi gani Serikali ya CCM inavyowajali wananchi.

**48. Mheshimiwa Spika**, katika hatua nyingine Serikali ilitoa shilingi bilioni 100 kila mwezi katika kipindi cha kuanzia Juni hadi Desemba, 2022 kufidia bei za mafuta (petroli, dizeli na mafuta ya taa) ili kufanya nishati hizo muhimu kuwa na bei inayohimilika kwa kila mtanzania na kuwezesha kupatikana kila wakati na kila kona ya nchi. Hatua hii iliwezesha watanzania waendelee kumudu gharama za uzalishaji na usafirishaji.

**49. Mheshimiwa Spika**, hali hii imeifanya Tanzania kuwa na uimara katika mfumuko wa bei, ukuaji wa uchumi na viashiria vingine vya uchumi jumla. Aidha, Serikali ilichukua hatua za kupunguza na kufuta kodi kwenye baadhi ya bidhaa muhimu kama vile mafuta ya kula ili kumfanya mtanzania kumudu gharama za maisha. Sio kila nchi ilifanya jambo hili, hii inaonesha ni kiasi gani Serikali ya CCM inavyowajali wananchi.

**50. Mheshimiwa Spika**, maeneo mengine ambayo yalijitokeza na kuleta taharuki katika mataifa mengi ni pamoja na kuadimika kwa fedha za kigeni katika nchi nyingi za Afrika. Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania, imetekeleza vyema Sera ya Fedha na hivyo kuimarisha viwango vya kubadilisha fedha za kigeni kuwa himilivu.

**51. Mheshimiwa Spika**, hivi karibuni tumeshuhudia mabadiliko ya sera za nje hususan katika mataifa makubwa zikiwemo nchi wabia wa maendeleo wa Tanzania. Sera hizo zinajumuisha kufuta na kupunguza misaada kupitia taasisi ama mashirika ya kimataifa ya nchi hizo ambayo kwa sehemu kubwa ilikuwa ikielekezwa kwa mashirika yasiyo ya serikali hapa nchini. Kufuatia hali hiyo, Serikali imefanya tathmini ya kina kubaini sekta zitakazoathirika na imeanza kuchukua hatua stahiki. Maeneo yalioguswa ni sekta ya afya na maeneo mengine ambapo hadi sasa Serikali imetoa zaidi ya shilingi bilioni 82 kuziba pengo lililotokana na mabadiliko hayo.

**52. Mheshimiwa Spika**, katika muda wa kati, Serikali itatenga bajeti itakayolenga kuziba pengo la fedha zilizokuwa zinatarajiwa kupatikana kutoka kwa wabia hao. Katika hatua za muda mrefu, Serikali inapanga kuwekeza kwenye viwanda vinavyozalisha bidhaa hizo zilizokuwa zinaingizwa kutoka nje kwa fedha za msaada. Aidha, Serikali imeandaa mkakati wa kuongeza uzalishaji wa bidhaa ndani ya nchi na kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje (import substitution) pamoja na mkakati wa kuongeza mauzo nje ya nchi (export promotion) ili kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni na kuimarisha thamani ya shilingi ya Tanzania.

**53. Mheshimiwa Spika**, tunao uwezo wa kushirikiana na sekta binafsi kuzalisha dawa za malaria, kifua kikuu na magonjwa mengineyo ndani ya nchi. Naomba niwahakikishie watanzania, hakuna maisha ya mtanzania yatapotea au kuwa mashakani kwa kupungua kwa fedha za msaada. Hizi ni baadhi tu ya hatua zinazoonesha Serikali ya CCM inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni Serikali inayowajali watanzania na kila siku inashughulikia upatikanaji wa majawabu ya masuala yanayowahusu wananchi wake. Watanzania wana imani na CCM na Rais wetu, tuendelee na ujenzi wa Taifa, kazi tuliyopewa tunaiweza.

**54. Mheshimiwa Spika**, nitoe rai kwa watanzania wote tunaoipenda nchi yetu, tusiruhusu misingi na nguzo za Taifa letu zitikiswe na tusiingie kwenye mtego wa adui. Sote ni mashahidi kuwa mataifa yaliyowahi kuingia kwenye mfarakano kwa kiasi kikubwa ulisababishwa na mizaha mizaha na kutokuheshimu misingi ya kitaifa, maneno ya rejareja yasiyo na ushahidi ya mtu mmoja mmoja, yasiyo na ushahidi kwa baadhi ya taasisi zisizo za serikali na yasiyo na ushahidi kwa baadhi ya vyombo vya habari.

**55. Mheshimiwa Spika**, wakati mwingine uhalifu wa mtu mmoja mmoja au vikundi hujitokeza na kuwa tishio kwenye maisha ya kila siku ya wananchi. Ikumbukwe, katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tatu walijitokeza wahalifu ambao walikuwa wanateka magari ya mizigo na mabasi ya abiria katika maeneo mbalimbali nchini. Hata hivyo, **vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vilisimama imara na kukomesha uhalifu huo.** Aidha, katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Nne ulitokea uhalifu wenye sura ya ugaidi uliohusisha urushwaji wa mabomu kwenye nyumba za ibada, mikusanyiko ya watu na mashambulizi ya mtu mmoja mmoja wakiwemo watu wenye ulemavu wa ngozi. Tumesahau hili? **Vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vilisimama imara na kukomesha uhalifu huo.**

**56. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano, ulitokea uhalifu wa watoto kutekwa na kuuwawa, mtu mmoja mmoja kupigwa risasi kwenye makazi yake au katika utekelezaji wa majukumu yake. Mtakumbuka, waliuwawa

wenyeviti wa vijiji, vitongoji na mitaa wanaotokana na CCM na tulishuhudia pia miili iliyokuwa kwenye magunia na mifuko ikiwa imetupwa baharini. Na haya tumesahau? **Vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vilisimama imara na kukomesha uhalifu huo.**

**57. Mheshimiwa Spika**, hata sasa vimejitokeza viashiria vya uhalifu kama huo ambavyo havipiganwi kwa kupeleka vikosi na kampeni au kusema tunapigana vipi? Tukiendelea kunyoosheana vidole na kunyooshea vidole vyombo vyetu vya ulinzi na usalama tutaacha adui aendelee na uhalifu. Vita vya aina hii vinapiganwa kwa intelijensia, hivyo niwasihi watanzania wenzangu tuviache vyombo vya ulinzi na usalama vifanye kazi yake na tuendelee kufanya kazi kwa maendeleo ya Taifa letu.

**58. Mheshimiwa Spika**, wakati mwingine uchochezi wa adui huwa ni kwa lengo la kuzifikia rasilimali nyingi au za kipekee zinazopatikana katika Taifa husika. Tunayo mifano yote ikiwemo ya mataifa yaliyokuwa na migogoro iliyochochewa na waliotamani kupora rasilimali hizo na pindi zilipoisha, migogoro nayo iliisha huku mataifa hayo yakiachwa masikini. Tumeshuhudia uchochezi katika mataifa mengine ukijipenyeza nyakati za uchaguzi kupitia wananchi kuchukiana wao kwa wao au wao na Serikali zao. **Sote tuwe macho!!!**

**59. Mheshimiwa Spika**, hatuna Taifa lingine zaidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wala hatuna mbadala wa amani, usalama, utulivu na Muungano wetu. Tutambue kuwa, kinacholengwa ni rasilimali zetu na sifa ya kipekee ya kuwa kisiwa cha amani ambayo Tanzania imeendelea kuwa nayo. Watanzania tuilinde amani yetu, ikituponyoka ni ngumu sana kuirejesha.

**60. Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuhakikisha kuwa mipaka yote ya nchi yetu inakuwa salama, pamoja na kuwepo kwa umoja, amani, mshikamano na utulivu. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) limeendelea kutoa mchango kwa kushiriki katika operesheni mbalimbali za ulinzi wa amani kupitia misheni za Umoja wa Mataifa na jumuiya za kikanda. Ushiriki huo umeimarisha diplomasia ya ulinzi, ushirikiano

na kuiletea sifa nchi yetu. Ninavipongeza vyombo vyetu vya ulinzi na usalama chini ya Amiri Jeshi Mkuu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada kubwa zinazoendelea kuchukuliwa ili kuhakikisha hali ya ulinzi, usalama, amani na utulivu inaendelea kuimarika.

## IV. MAFANIKIO YA SERIKALI

**61**. **Mheshimiwa Spika**, kama unavyofahamu, bajeti ya mwaka 2025/26 inakamilisha kipindi cha kwanza cha Awamu ya Sita ya Utawala wa **MAMA YETU MPENDWA** Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sote ni mashahidi kuwa tangu ashike hatamu ya uongozi mwaka 2021, amesimama kidete kuhakikisha shughuli za maendeleo zinasonga mbele. Hakika ni mengi yamefanyika katika kipindi cha uongozi wake. ***KAZI NA UTU, TUNASONGA MBELE!!***

### Utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati

**62. Mheshimiwa Spika**, wakati Serikali ya Awamu ya Sita inapokea uongozi, utekelezaji wa mradi wa kielelezo wa Ujenzi wa Mradi wa Julius Nyerere Hydro Power Project (JNHPP) MW 2,115 ulikuwa unaendelea ambapo hadi sasa umefikia asilimia 99.93 na tayari umeanza kuzalisha umeme. Kwa upande mwingine, utekelezaji wa ujenzi wa Daraja la Kigongo – Busisi lenye urefu wa kilomita 3 na barabara unganishi yenye urefu wa kilomita 1.66 kwa kiwango cha lami ujenzi ulikuwa unaendelea na sasa umekamilika kwa asilimia 100.0 na unatarajiwa kuzinduliwa tarehe 19 Juni, 2025.

**63. Mheshimiwa Spika**, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alipokea mradi wa reli ya kisasa (SGR) ukiwa umetekelezwa kwa asilimia 83.55 kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro (Lot 1) na asilimia 57.57 kwa kipande cha Morogoro hadi Makutupora (Lot 2) ambapo vipande hivyo vimekamilika na mabehewa yamenunuliwa na treni imeanza kutoa huduma ya usafiri wa abiria. Tangu kuanza kwa safari za treni kupitia reli ya SGR hadi Machi 2025, TRC imesafirisha jumla ya abiria 2,054,828 na kuwezesha kukusanya mapato ya jumla ya shilingi bilioni 60.25.

**64. Mheshimiwa Spika**, sisi sote tumeshuhudia usafiri kwa kutumia reli ya SGR umepunguza muda wa safari kutoka saa tisa (9) hadi saa tatu (3) kwa safari kati ya Dar es Salaam na Dodoma. Vilevile, utekelezaji wa kipande cha tano cha kutoka Mwanza – Isaka (km 341) umefikia asilimia 63.16. Kwa upande mwingine, Serikali imefanya majaribio ya treni ya mizigo ya SGR tarehe 01 Juni 2025.

**65. Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa kuwa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alianza ujenzi wa reli Lot 3 (Makutupora – Tabora, km 368) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 14.53; Lot 4 (Tabora – Isaka, km 165) asilimia 6.65; Lot 6 (Tabora - Kigoma) na Lot 7 (Uvinza - Musongati) ambazo hazikuwepo wakati Mheshimiwa Rais akipokea kijiti. Dhamira ya Serikali ni kujenga reli ya SGR katika maeneo mbalimbali ya nchi. Katika kutekeleza lengo hili, Serikali inaendelea kutafuta fedha kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo ikiwa ni pamoja na wawekezaji kwa utaratibu wa ubia baina ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP).

**66. Mheshimiwa Spika**, Upatikanaji wa rasilimali fedha utawezesha ujenzi wa reli ya SGR kwa maeneo yaliyobaki yanayojumuisha reli ya SGR ya kutoka Kaliua - Mpanda - Karema (km 321); Mtwara - Mbamba Bay na matawi (Spurs) ya Liganga na Mchuchuma (km 1,000); Tanga – Arusha - Musoma (km 1,028); Reli ya Jiji la Dar es Salaam (km 166); na Reli ya Jiji la Dodoma (km 107). Kwa upande wa Reli ya TAZARA, Serikali za Tanzania, Zambia na China zilisaini Hati ya Makubaliano (MoU) ya kuboresha uendeshaji wa TAZARA.

**Miundombinu Wezeshi**

**Uchukuzi**

**67. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2024/25, Serikali imeendelea kuwekeza katika bandari zetu nchini ili ziweze kutoa huduma kwa tija na ufanisi na kwa lengo la kuchochea shughuli za maendeleo nchini, hususan katika sekta za kilimo, madini, uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma. Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imepata mafanikio mbalimbali kupitia

uwekezaji uliofanywa kwenye bandari, hususan Bandari ya Dar es Salaam.

**68. Mheshimiwa Spika**, mafanikio hayo ni pamoja na: kuongezeka kwa mapato ya kodi ya forodha ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Februari 2025 jumla ya shilingi trilioni 8.26 zimekusanywa, sawa na ongezeko la shilingi trilioni 1.18 ikilinganishwa na shilingi trilioni 7.08 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24; na kupungua kwa gharama za uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam kutoka shilingi bilioni 975.0 hadi shilingi bilioni 685.2 katika kipindi hicho. Hii imewezesha kuwa na fedha za ziada za kuanza utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kuendeleza bandari ikiwa ni pamoja na Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Matenki ya Kupokea Mafuta kwa Pamoja (Tank Farm) katika Bandari ya Dar es Salaam.

**69. Mheshimiwa Spika**, mafanikio mengine ni ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege vya Songwe (Mbeya), Mtwara, Songea, Iringa, Geita, Msalato, Kigoma, Tabora, Sumbawanga, Shinyanga, na Musoma. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni kuendelea kuliimarisha Shirika la Ndege Tanzania - ATCL kwa kununua ndege saba (7) ambapo ndege sita (6) ni za abiria na ndege moja (1) ni ya mizigo hivyo Shirika kuwa na jumla ya ndege 16 kutoka ndege tisa (9) zilizokuwepo mwaka 2020/21.

**Ujenzi**

**70. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha miundombinu ya ujenzi, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: kuongezeka kwa mtandao wa barabara zinazounganisha wilaya, mikoa na nchi jirani zinazosimamiwa na TANROADS kutoka kilometa 36,361.95 mwaka 2021 hadi kilometa 37,435.04 Aprili 2025; kukamilika kwa ujenzi wa madaraja makubwa ikiwemo Daraja la Tanzanite (Dar es Salaam), Wami (Pwani), Ruhuhu (Ruvuma), Mpwapwa (Dodoma), Msingi (Singida) na Kigongo – Busisi (Mwanza/Geita) na kuendelea na ujenzi wa madaraja makubwa ambayo ni pamoja na Lower Mpiji, Simiyu na Pangani; kukamilika kwa mradi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT), Awamu ya

Pili (II); na kuendelea na ujenzi wa Awamu ya Tatu (III), ya Nne (IV) na ya Tano (V).

**71. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa barabara za mijini na vijijini zinazosimamiwa na TARURA, Serikali ya Awamu ya Sita imeongeza bajeti kwa zaidi ya mara sita (6). Hii imewezesha kufungua barabara nyingi mijini na vijijini. Aidha, ujenzi, ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya barabara kupitia TARURA umefanyika kwa kiwango kikubwa ambapo ujenzi wa barabara za changarawe umeongezeka kutoka kilomita 24,493 mwaka 2020 hadi kilomita 44,372.21 Aprili 2025, sawa na ongezeko la asilimia 81.16.

**72. Mheshimiwa Spika**, urefu wa barabara za vijijini na mijini zilizojengwa kwa kiwango cha lami umeongezeka kutoka kilomita 2,025 hadi kilomita 3,467.30, sawa na ongezeko la asilimia 71.22. Aidha, mtandao wa barabara umeongezeka kutoka kilometa 108,946.18 mwaka 2020 hadi kilometa 144,429.77 mwaka 2025, sawa na ongezeko la asilimia 32.57.

**Nishati**

**73. Mheshimiwa Spika**, Serikali imefanya maboresho makubwa katika sekta ya nishati na hivyo kuwezesha upatikanaji wa nishati ya uhakika na kwa gharama nafuu. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: kukamilika kwa asilimia 99.93 ya ujenzi wa mradi wa uzalishaji umeme katika Bwawa la Julius Nyerere lenye uwezo wa kuzalisha umeme wa megawati 2,115; kukamilisha usambazaji wa umeme katika vijiji vyote 12,318 vya Tanzania Bara; kuendelea na ujenzi wa mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP); na kukamilika kwa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 kutoka Singida hadi Arusha, kV 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma na kV 132 kutoka Tabora hadi Urambo.

**74. Mheshimiwa Spika**, mafanikio mengine ni: Kuendelea na maandalizi ya kutekeleza mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia kuwa kimiminika (Liquefied Natural Gas – LNG) na kutekeleza shughuli za utafiti na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vya kimkakati vya Songo Songo Magharibi, Mnazi Bay

Kaskazini, Eyasi - Wembere na 4/1B na 4/1C; pamoja na kusambaza gesi asilia katika taasisi, viwandani, majumbani na kuimarisha matumizi ya *Compressed Natural Gas* (CNG) katika vyombo vya moto. Aidha, Serikali imekamilisha kuunganisha mikoa yote kwenye Grid ya Taifa.

**75. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji na matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini ambapo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni *Champion* wa jambo hili la kihistoria. Serikali iliandaa na inatekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 – 2034) kwa lengo la kuhakikisha kuwa asilimia 80 ya watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034. Hatua hii itapunguza utegemezi wa kuni na mkaa, ambao husababisha uharibifu wa misitu na athari za kiafya kutokana na moshi unaotokana na nishati hizo. Huu ni mpango muhimu sana kwa ustawi wa jamii na maendeleo endelevu. Maisha ya mjini sasa yanahamia kila kijiji.

**Huduma za Jamii**

**Afya**

**76. Mheshimiwa Spika**, sekta ya afya imeendelea kupata mafanikio mbalimbali kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanyika ikiwemo: Uboreshaji wa miundombinu ya kutolea huduma za afya ambapo vituo vya kutolea huduma za afya nchini vimeongezeka kutoka vituo 8,458 mwaka 2020 hadi 9,826 mwaka 2024; kukamilika kwa awamu ya kwanza ya ujenzi na kuanza kutoa huduma kwa hospitali mpya za rufaa katika mikoa ya Songwe, Geita, Simiyu na Katavi; ujenzi wa hospitali mpya za halmashauri 129 ikiwa ni ongezeko la asilimia 31.63 ya lengo la kujenga hospitali 98; na uboreshaji wa huduma za dharura ambapo idadi ya hospitali zenye majengo ya kutolea huduma za dharura zimeongezeka kutoka hospitali saba (7) mwaka 2020 hadi hospitali 116 mwaka 2024.

**77. Mheshimiwa Spika**, kati ya mwaka 2020 hadi 2024, mafanikio mengine yaliyopatikana ni: Kuongezeka kwa majengo ya ICU kutoka 14 hadi 73; idadi ya magari ya kubeba wagonjwa

imeongezeka kutoka magari 540 hadi magari 1,267; kuimarika kwa huduma za afya ya mama na mtoto ambapo vituo vya afya vinavyotoa huduma za dharura za uzazi vimeongezeka kutoka vituo 340 hadi vituo 523; kuimarika kwa upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba, na vitendanishi ambapo upatikanaji wa dawa umeongezeka kutoka asilimia 73 hadi asilimia 86; kuongeza mitambo ya uchunguzi wa magonjwa kama vile MRI kutoka nne (4) hadi 13 , CT-Scans kutoka 12 hadi 45, Digital X Rays kutoka 73 hadi 491; na ununuzi wa PET Scan kwa ajili ya uchunguzi na matibabu ya saratani.

**78. Mheshimiwa Spika**, kwa sasa kuna vituo vya afya katika kila tarafa na baadhi ya kata za kimkakati kulingana na jiografia na wingi wa wananchi. Aidha, MAMA amejenga hospitali za kanda, rufaa, mikoa na wilaya ambazo hazikuwepo pamoja na kuboresha miundombinu na kuweka vifaa tiba vya kisasa kwenye hospitali zilizopo kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kupata huduma kwa urahisi katika maeneo yao.

**79. Mheshimiwa Spika**, Serikali imetunga Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote namba 13 ya mwaka 2023 na inaendelea kuweka mazingira wezeshi ya utekelezaji wa sheria hiyo. Jambo hili ni kubwa na linakwenda kuwapa uhakika wa matibabu watanzania wote hususan wale wenye kipato cha chini.

**Elimu**

**80. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kutekeleza vipaumbele vya sekta ya elimu kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya shule za msingi na shule za sekondari ikiwemo shule 26 za wasichana za kidato cha tano na sita katika mikoa 26 nchini. Aidha, Serikali pia imeendelea kuongeza vyumba vya madarasa ya elimu ya msingi kutoka 128,425 mwaka 2020 hadi madarasa 155,330 mwaka 2024 na vyumba vya madarasa ya elimu ya sekondari kutoka 46,928 mwaka 2020 hadi 81,052 mwaka 2024.

**81. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kutekeleza mpango wa elimu bila ada kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha sita kwa

kuongeza fedha za kugharamia mpango huo kutoka shilingi bilioni 312.1 mwaka 2020 hadi shilingi trilioni 1.3 mwaka 2024. Maboresho hayo yamechangia ongezeko la wanafunzi kutoka 14,940,925 mwaka 2020 hadi 16,155,281 mwaka 2024.

**82.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali imekamilisha ujenzi wa vyuo 29 vya mafunzo ya ufundi stadi ambavyo vimeanza kutoa mafunzo, kuendelea na ujenzi wa vyuo 65 na kukarabati vyuo 29 vya elimu ya mafunzo ya ufundi stadi. Jitihada hizo zimewezesha ongezeko la udahili wa wanafunzi katika vyuo vya elimu ya ufundi kutoka wanafunzi 344,815 mwaka 2020 hadi 440,000 mwaka 2024. Aidha, katika kuhakikisha watoto kutoka familia zenye kipato cha chini wanapata fursa sawa ya elimu, Serikali inayoongozwa na *MAMA YETU* msikivu na mwenye kujali ilianza kutoa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vya kati kwa kozi za kipaumbele.

**83.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali pia imeendelea kuongeza bajeti ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na vyuo vya kati kutoka shilingi bilioni 464.0 mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni 787.4 mwaka 2024/25 na hivyo kuongeza idadi ya wanufaika wa mikopo hiyo kutoka wanafunzi 145,000 mwaka 2020/21 hadi wanafunzi 245,799 mwaka 2024/25. Aidha, Serikali iliongeza kiwango cha posho (*boom)* hadi shilingi 10,000 kwa siku kwa wanafunzi.

**84.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Awamu ya Sita imefanya mabadiliko ya mfumo wa elimu na mitaala ambapo sasa elimu ya msingi itakuwa mpaka kidato cha nne na kuweka msisitizo kwenye elimu ya amali. Mabadiliko kama haya kwa mara ya mwisho yalifanyika mwaka 1977 ambapo mfumo wa elimu ya msingi ulibadilishwa na kuanzishwa kwa mpango wa UPE.

**Maji**

**85.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali ya awamu ya sita imekwamua miradi iliyokuwa imekwama kwa muda mrefu, kama Mradi wa Maji Same - Mwanga Korogwe ulioanza kujengwa mwaka 2014 na kukamilika Machi, 2025 takribani miaka 11. Mradi huo una uwezo wa kuhudumia wananchi wapatao 456,000. Aidha, Mradi

wa Maji wa Bunda ulioanza kujengwa mwaka 2012 na kukamilika mwaka 2022, takribani miaka 10 na kuhudumia wananchi wapatao 227,450.

**86. Mheshimiwa Spika**, kadhalika, mradi wa ujenzi wa tekeo la maji kwa ajili ya Mji wa Kigoma ulianza kujengwa mwaka 2015 na kukamilika mwaka 2022 takriban miaka 7 na una uwezo wa kuhudumia wananchi wapatao 215,000. Vilevile, Mradi wa Maji Mugango - Kiabakari hadi Butiama ulioanza kujengwa mwaka 2020 na kukamilika mwaka 2025 takribani miaka mitano (5) na una uwezo wa kuhudumia wananchi zaidi ya 100,000.

**87. Mheshimiwa Spika**, Serikali imefanikisha ununuzi wa seti 25 za mitambo ya uchimbaji wa visima na kuwezesha uchimbaji wa visima 1,221 na seti tano (5) za mitambo na kuwezesha ujenzi wa mabwawa 16 nchini. Aidha, Serikali imeandaa na kuanza kutumia mifumo ya takwimu na usimamizi wa ankara za maji. Mifumo hiyo imeboresha ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na huduma za maji na usafi wa mazingira hivyo kuimarisha uendelevu wa huduma hizo. Vilevile, Serikali imekamilisha Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 Toleo la Mwaka 2025 ambayo utekelezaji wake utaongeza kasi na ufanisi katika upatikanaji wa huduma za maji nchini.

**88. Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla, utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji umeboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama ambapo kwa upande wa vijijini huduma hiyo imeongezeka kutoka wastani wa asilimia 70.1 mwaka 2020 hadi asilimia 83.0 mwaka 2024 na kwa maeneo ya mijini kutoka wastani wa asilimia 84.0 hadi wastani wa asilimia 91.6 katika kipindi hicho.

**Sekta za Uzalishaji**

**Kilimo**

**89. Mheshimiwa Spika**, mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya kilimo (mazao) ni pamoja na kuongezeka kwa: ukuaji wa sekta kutoka asilimia 2.7 mwaka 2022 hadi asilimia 4.0 mwaka 2024;

uzalishaji wa mazao ya chakula kutoka tani 17,148,290 mwaka 2021/22 hadi tani 22,803,316 mwaka 2023/24 na hivyo, kuongeza utoshelevu wa chakula nchini kufikia asilimia 128; na uzalishaji wa mbolea kutoka tani 32,239 mwaka 2020/21 hadi tani 158,628 mwaka 2024/25.

**90.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali imekamilisha ujenzi wa maghala 46 na vihenge 20 vya kuhifadhia nafaka na hivyo, kuongeza uwezo wa kuhifadhi mazao kutoka tani 200,000 hadi tani 700,000. Aidha, Serikali itaendelea na utekelezaji wa kuanzisha vituo 1,000 vya zana za kilimo "Mechanization program" na kununua matrekta elfu 10 inayolenga kuwezesha upatikanaji wa matrekta kwa wakulima kupitia vituo vya upatikanaji wa zana za kilimo kwa njia ya ruzuku. Vilevile, mtandao wa umwagiliaji umeongezeka kutoka hekta 560,000 mwaka 2021/22 hadi hekta 960,000 mwaka 2024/25, sawa na asilimia 80 ya lengo la hekta 1.2 na miradi 780 yenye zaidi ya hekta 500,000 inaendelea kutekelezwa.

**Uvuvi**

**91**. **Mheshimiwa Spika**, mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya uvuvi ni pamoja na: ujenzi wa bandari ya uvuvi Kilwa Masoko ambao umefikia asilimia 81.9; kuongezeka kwa mauzo ya mazao ya uvuvi nje ya nchi kutoka tani 167,256.16 hadi tani 199,387.26; na ununuzi wa boti za kisasa za uvuvi 219 zenye thamani ya shilingi bilioni 19.7. Boti hizo zimegawanywa ukanda wa Pwani 144, Ziwa Victoria 55, Tanganyika 14, Nyasa nne (4) na Rukwa mbili (2). Aidha, jumla ya vizimba 248 vimetolewa kwa wanufaika wa ufugaji wa samaki katika Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika ambapo wanufaika wa moja kwa moja ni 1,213 wanatokana na vyama vya ushirika 17, vikundi 31 na watu binafsi.

**Mifugo**

**92.** **Mheshimiwa Spika**, mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya mifugo ni pamoja na kuongezeka: Viwanda vya kuchakata nyama inayouzwa nje ya nchi kutoka viwanda vitatu (3) hadi saba (7); nyama inayouzwa nje ya nchi kutoka tani 1,669 hadi tani 14,701; na maeneo ya malisho kutoka hekta 2,788,901.17 mwaka

2020/21 hadi hekta 3,489,701.13 mwaka 2024/25. Aidha, Serikali ilinunua na kusambaza mitamba 1,630 katika mashamba matano (5) ya Serikali ya kuzalisha mifugo pamoja na ujenzi wa mabwawa 19 yenye thamani ya shilingi bilioni 10.69 kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa maji kwa mifugo.

**93. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha, kuendeleza ushirika na hatimaye kuinua sekta ya kilimo, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya uzinduzi wa Benki ya Ushirika Tanzania tarehe 27 Aprili 2025. Benki hii imeanza na mtaji wa shilingi bilioni 58 ambapo ushiriki wa wananchi katika kutumia huduma zinazotolewa na benki hiyo unatarajiwa kuongeza mitaji katika sekta za uzalishaji, kuongeza fursa za ajira na kuchochea shughuli za kiuchumi nchini. Kwa upande mwingine, ili kuboresha huduma za ugani, Serikali ilinunua na kusambaza pikipiki 7,944 kwa maafisa ugani wa mifugo na mazao katika halmashauri 184.

**Viwanda, Biashara na Uwekezaji**

**94. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuchukua hatua mahsusi za kuimarisha na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kufanya maboresho ya sheria 12 ili kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji na kuleta unafuu kwa wawekezaji wa sekta binafsi. Aidha, Serikali imefuta au kupunguza tozo, ada na faini zipatazo 383 zilizobainishwa kuwa kero katika ufanyaji wa biashara. Sambamba na hilo, Serikali imeanza maandalizi ya Mpango wa Pili wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji nchini unaolenga kuvutia uwekezaji wa nje na ndani, kuongeza fursa za ajira, kurasimisha sekta isiyo rasmi, uboreshaji wa miundombinu wezeshi, upatikanaji wa soko la kimataifa kwa bidhaa za ndani na kukuza ushindani na ubora.

**95. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuhamasisha ujenzi na upanuzi wa viwanda vya kuongeza thamani mazao ya kilimo pamoja na vile vinavyozalisha bidhaa zinazohitajika kwa wingi na zinazotumia malighafi zinazopatikana nchini kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wake, kuzalisha ajira na kukuza mauzo ya

nje ya nchi. Kupitia jitihada hizo, viwanda vipya vimejengwa na vingine vimefanyiwa upanuzi na kuwezesha utoshelevu wa baadhi ya bidhaa kwa mfano marumaru, vioo, mabati, *clinker* na saruji.

**96. Mheshimiwa Spika**, Serikali pia inaendelea na utekelezaji wa mikakati ya kupunguza uagizaji wa bidhaa ambazo uzalishaji wake wa ndani bado hautoshelezi, kwa kuanzisha miradi mipya ya viwanda vya mbolea na viwanda vya sukari ili kuondokana na uagizaji kutoka nje. Mapendekezo ya hatua za kikodi nitakazowasilisha yamezingatia jitihada za kulinda viwanda vyetu, kuvutia upanuzi wa viwanda na ujenzi wa viwanda vipya.

**Madini**

**97. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita, mchango wa sekta ya madini katika Pato la Taifa umeendelea kuimarika na kukua kutoka asilimia 6.8 mwaka 2020 na kufikia asilimia 10.1 mwaka 2024. Aidha, kasi ya ukuaji wa sekta ya madini imeongezeka kutoka asilimia 7.3 mwaka 2020 na kufikia asilimia 8.3 mwaka 2024. Katika kipindi hicho, Serikali imeendelea kuboresha sheria, kanuni na miundombinu mbalimbali ikiwemo nishati na maji migodini hali ambayo imeweka mazingira wezeshi ya uwekezaji na kuongeza ufanisi wa kazi katika shughuli za madini.

**98. Mheshimiwa Spika**, mafanikio mengine yaliyopatikana ni: kuongeza ukusanyaji wa maduhuli kutoka shilingi bilioni 587.3 mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni 875.6 kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025; kudhibiti utoroshwaji wa madini; kuhamasisha uwekezaji kwenye shughuli za madini; kurejesha minada ya madini ya vito; na ununuzi wa mitambo 10 ya uchorongaji miamba kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

**99. Mheshimiwa Spika**, Serikali imewezesha upatikanaji wa dhahabu kwa ajili ya Hazina ya Taifa ya fedha za kigeni (Foreign Reserves), ambapo hadi Mei 2025 Benki Kuu imenunua takribani tani 4.8 za dhahabu iliyozalishwa na kuchakatwa hapa nchini. Hii

inatoa taswira nzuri ya kuongezeka kwa uwezo wetu katika kuongeza thamani kwenye mazao ya maliasili zetu.

**Maliasili na Utalii**

**100. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Awamu ya Sita, Serikali imeendelea kuimarisha sekta ya maliasili na utalii kwa kuendeleza na kukuza vivutio mbalimbali vya utalii ikiwemo kuanzishwa kwa programu maalum za kuitangaza Tanzania kimataifa kama vile filamu ya Tanzania – *The Royal Tour* pamoja na filamu ya *Amazing Tanzania*. Katokana na jitihada hizo, idadi ya watalii imeongezeka kutoka watalii 1,183,416 mwaka 2020 hadi watalii 5,360,247 mwaka 2024. Aidha, mapato yatokanayo na watalii wa nje ya nchi yameongezeka kutoka dola za Marekani milioni 715.0 mwaka 2020 hadi dola za Marekani bilioni 3.9 mwaka 2024.

**101. Mheshimiwa Spika**, mafanikio haya yameiwezesha Tanzania kutambulika kimataifa ambapo imeshika nafasi ya tisa (9) duniani na nafasi ya tatu (3) barani Afrika mwaka 2024 kwa ongezeko la mapato yatokanayo na shughuli za utalii, ikilinganishwa na kipindi cha kabla ya janga la UVIKO-19. Aidha, Tanzania imetambulika kuwa eneo linalovutia zaidi kiutalii barani Afrika (Africa's Leading Destination) kwa mwaka 2024 na Hifadhi ya Taifa Serengeti imeendelea kuwa mshindi wa tuzo ya hifadhi bora duniani kwa mara ya tano (5) mfululizo kutoka mwaka 2019 hadi mwaka 2024.

**Utawala Bora**

**102. Mheshimiwa Spika**, katika kuendeleza dhana ya utawala bora, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameboresha utekelezaji wa majukumu ya Serikali kwa kuzingatia falsafa ya 4Rs (Reconciliation, Resilience, Reform and Rebuild). Falsafa hiyo inalenga kulileta Taifa pamoja, kujenga hali ya kuvumiliana, kuwa na makubaliano ya pamoja na kulijenga upya Taifa letu ili kuendelea kudumisha amani iliyopo. Tukumbuke kuwa hata Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alisisitiza umuhimu wa kuilinda amani kwa kusema "***Tusipoilinda amani, tutajuta tukiwa hatuna uwezo wa kuirejesha***".

**103. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha haki inapatikana kwa wakati, uwazi na kwa usawa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alianzisha Tume ya Haki Jinai kwa lengo la kufanya mapitio ya mfumo mzima wa haki jinai nchini. Tume hiyo ilitoa mapendekezo ya kukabiliana na changamoto mbalimbali zilizobainika zikiwemo matumizi mabaya ya mamlaka, ucheleweshwaji wa haki na ukosefu wa miundombinu rafiki. Katika kutekeleza mapendekezo hayo, Serikali imeunganisha mifumo ya TEHAMA kati ya Mahakama, Polisi na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka pamoja na kuongeza Ofisi za Mashtaka kwenye ngazi ya wilaya.

**104. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (Samia Legal Aid Campaign) kwa kutoa elimu na msaada wa kisheria kwa wananchi wenye uhitaji. Utekelezaji wa Kampeni hiyo umesaidia kuimarisha upatikanaji wa haki kwa wananchi na kuongeza uelewa kuhusu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Aidha, Serikali imefanya urekebu wa sheria kuu 446 kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa haki kwa wananchi katika masuala mbalimbali.

**Muungano**

**105. Mheshimiwa Spika**, kama tunavyofahamu Aprili 2025, Muungano wetu umetimiza miaka 61. Kwa dhati kabisa, naomba nitumie fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuendelea kutuongoza vema katika kuulinda na kuuenzi Muungano wetu wa kipekee. Kwa nafasi hii pia, nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa utendaji wake mahiri ambapo pamoja na masuala mengine, Ofisi yake inaratibu na kusimamia masuala ya Muungano.

**106. Mheshimiwa Spika**, Muungano wetu ni tunu adhimu ambayo imetusaidia kuendelea kufikia shabaha na malengo mbalimbali

kama nchi na kwa kila upande wa Muungano. Kwa vipindi tofauti tangu kuasisiwa kwa Muungano, Serikali zetu zimeendelea kushirikiana kutatua na kukwamua changamoto na hoja mbalimbali za Muungano zilizopo na zinazojitokeza. Hivyo, nitoe rai kwa watanzania wenzangu kuendelea kuenzi tunu ya Muungano wetu kwa kuendeleza upendo na mshikamano uliopo.

**Diplomasia ya Uchumi**

**107. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuimarisha ushirikiano na uhusiano baina ya nchi yetu na mataifa mengine, jumuiya za kikanda na mashirika ya kimataifa. Hii imewezesha: Upatikanaji wa fursa za ajira; kupatikana kwa misaada na mikopo yenye masharti nafuu; kuimarika kwa mtangamano wa kikanda unaozingatia maslahi ya pande zote; kuongezeka kwa wawekezaji na watalii; upatikanaji wa fursa mpya za masoko ya bidhaa na huduma nje ya nchi; na kuongezeka kwa fursa za ufadhili wa masomo kwa watanzania nje ya nchi. Mafanikio haya yanadhihirisha dhamira ya dhati ya Serikali katika kuleta maendeleo ya kweli kwa watanzania kupitia diplomasia ya uchumi na ushirikiano wa kimataifa.

**Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi**

**108. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Awamu ya Sita inaendelea kuchukua hatua madhubuti kwa ajili ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Miongoni mwa hatua hizo ni utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 – 2032) ambao unalenga kutatua changamoto za mazingira nchini. Aidha, Serikali imeanzisha Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni ili kuimarisha usimamizi na kunufaika zaidi na biashara ya kaboni nchini.

**109. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha nchi inakuwa na uhimilivu wa kiuchumi dhidi ya mabadiliko ya tabianchi, Serikali inatekeleza programu mbalimbali za uhifadhi wa mazingira ambazo pamoja na masuala mengine zinahusisha maboresho ya sheria, kanuni na taratibu mbalimbali. Kwa upande mwingine, Serikali imeendelea kunufaika na programu mbalimbali za

uhifadhi wa mazingira kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ikiwemo Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kupitia dirisha la *Resilience and Sustainability Facility (RSF)*.

**Uendelezaji wa Makao Makuu Dodoma**

**110. Mheshimiwa Spika**, Serikali imefanikiwa kuyaenzi maono ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ya kuifanya Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi. Maono hayo yalianza kutekelezwa na awamu zilizopita za uongozi ambapo katika Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli maono hayo yalitekelezwa kwa kasi zaidi. Kasi hiyo inaendelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita na mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa Ikulu ya Chamwino na miundombinu yake pamoja na jengo la Makao Makuu ya Mahakama ya Tanzania (Judiciary Square).

**111. Mheshimiwa Spika**, Serikali pia inaendelea na ujenzi wa: majengo 34 ya ofisi za Serikali na miundombinu yake katika Mji wa Serikali – Mtumba pamoja na makao makuu ya taasisi mbalimbali za Serikali; Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato; na barabara za mzunguko wa nje (outer ring road) na mzunguko wa ndani (inner ring road). Ukamilishwaji wa majengo hayo na miundombinu jijini Dodoma unategemewa kuwawezesha wananchi kupata huduma kwa urahisi na kupendezesha Jiji na hivyo kuwa moja ya vivutio vya utalii. ***LANGA IDODOMA KUNOJILE!***

**Sekta ya Fedha**

**112. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa huduma jumuishi za fedha nchini ikiwemo kujenga na kuanza kutumika kwa Mfumo wa Malipo ya Papo kwa Papo (Tanzania Instant Payment System - TIPS). Aidha, katika kuhakikisha bei ni rafiki kwa wananchi, Benki Kuu ya Tanzania ilitoa mwongozo wa kupunguza gharama ya kutuma fedha baina ya benki kutoka gharama ya zaidi ya shilingi 10,000 kwa muamala hadi gharama isiyozidi shilingi 2,000.

**113. Mheshimiwa Spika**, kadhalika, Benki Kuu imetoa mwongozo kwa watoa huduma za fedha kuhusu kushusha gharama za miamala kutoka benki kwenda mitandao ya simu na kutoka mitandao ya simu kwenda benki kutoka gharama ya zaidi ya shilingi 12,000 hadi gharama isiyozidi shilingi 5,000. Mwongozo huu una lengo la kulinda maslahi ya watumiaji na kuhakikisha unafuu wa gharama kwa wananchi, na utaanza kutumika kuanzia tarehe 01 Julai 2025.

**114. Mheshimiwa Spika**, pamoja na jitihada hizo Serikali itaendelea kushirikiana na watoa huduma wote wa sekta ya fedha katika kufanya mageuzi ya kupunguza matumizi ya fedha taslimu katika uchumi. Aidha, Serikali imepanga kuzindua Mkakati wa Kukuza Matumizi ya Huduma za Fedha na Malipo kwa Njia za Kidijitali kwa kipindi cha miaka mitatu. Mkakati huo unalenga kufanya maboresho ya sera, sheria na miongozo inayohusu malipo ya kidijitali. Hivyo, nitoe rai kwa watoa huduma za fedha kuendelea kupunguza gharama za miamala ya kidijitali ili kuwezesha wananchi kufanya malipo kwa njia za kidijitali na kwa gharama nafuu.

**115. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuweka mazingira wezeshi katika kuhakikisha sekta binafsi inapata mikopo kwa wakati na kwa gharama nafuu. Mikopo kwa sekta binafsi imeongezeka kutoka shilingi bilioni 20,308.3 mwaka 2020 hadi shilingi bilioni 36,097.4 mwaka 2024. Ongezeko hilo lilichangiwa na: Utekelezaji thabiti wa sera za fedha na bajeti; kuendelea kutoa elimu ya masuala ya fedha nchini; na kuimarika kwa mazingira wezeshi ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini. Aidha, kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi kumesaidia kuongeza mitaji kwa wawekezaji na hivyo kuchochea shughuli mbalimbali za kiuchumi.

**116. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuimarisha ukwasi wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) ambapo mtaji wa benki hiyo umekua kutoka shilingi bilioni 76.72 mwaka 2020 hadi shilingi bilioni 507.06 mwaka 2024. Hii imewezesha utoaji wa mikopo ya moja kwa moja yenye thamani ya shilingi bilioni 712.58 na kuwanufaisha wakulima wadogo, wa kati na wakubwa 361,809.

Aidha, TADB ilifanikisha utoaji wa mikopo ya shilingi bilioni 318.85 kupitia Mfuko wa Dhamana wa Wakulima Wadogo (SCGS) na kuwanufaisha wakulima 572,303; biashara ndogo na za kati za kilimo, (SMEs) 505; vyama vya msingi (AMCOS) na vikundi vya wakulima 529.

**Maslahi ya Watumishi wa Umma na Wastaafu**

**117. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuboresha maslahi ya watumishi wa umma na wastaafu ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020. Katika kipindi hicho, mafanikio makubwa yamepatikana ikiwemo kupandisha vyeo watumishi wa umma wapatao 476,470 ambapo jumla ya shilingi bilioni 689.9 zimetumika. Hali hii imeongeza ari ya kufanya kazi kwa watumishi pamoja na utoaji wa huduma bora kwa wananchi. Aidha, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021/22 hadi Mei 2025, Serikali imelipa madai ya malimbikizo ya mishahara jumla ya shilingi bilioni 318.37 kwa watumishi na wastaafu 187,152.

**118. Mheshimiwa Spika**, mwaka 2022/23, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliongeza kima cha chini cha mshahara kutoka shilingi 300,000 hadi shilingi 370,000, sawa na ongezeko la asilimia 23.3, kwa lengo la kuongeza motisha na kuwezesha watumishi wa umma kumudu gharama za maisha. Aidha, kwa kutambua mchango wa watumishi wa umma katika ujenzi wa Taifa letu na kwa kuwa ni MAMA mwenye upendo na anayejali, tarehe 1 Mei, 2025 katika maadhimisho ya siku ya wafanyakazi duniani, Mheshimiwa Rais, ameongeza tena kima cha chini cha mshahara kutoka shilingi 370,000 hadi shilingi 500,000, sawa na ongezeko la asilimia 35.1. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa bajeti hii imezingatia nyongeza hiyo. Hivyo, tutarajie kuyaona maokoto haya kwenye mishahara yetu kuanzia Julai 2025.

**119. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Awamu ya Sita inatambua umuhimu na mchango mkubwa wa wastaafu katika ujenzi wa Taifa hili. Kwa kuzingatia hilo, katika mwaka 2025/26, Serikali itaongeza kima cha chini cha pensheni ya kila mwezi kwa wastaafu wanaolipwa na HAZINA kutoka shilingi 100,125.9 hadi

shilingi 250,125.9, sawa na ongezeko la asilimia 149.8 na utekelezaji wake utaanza katika pensheni ya Julai 2025.

**120. Mheshimiwa Spika**, napenda kuwahakikishia watanzania kuwa Serikali inaendelea kusimamia mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kuhakikisha inabaki kuwa himilivu na kulipa mafao ya wastaafu wote kwa wakati. Katika kutekeleza azma hiyo, kutoka mwaka 2021 hadi Mei 2025, Serikali imelipa madeni yenye thamani ya shilingi trilioni 2.67. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 2.18 ni madeni ya PSSSF ya waliokuwa wafanyakazi kabla ya mwaka 1999 (Pre99), shilingi bilioni 433.71 ni madeni ya NSSF ya muda mrefu na shilingi bilioni 63.52 ni madeni ya Kampuni ya Pension Property Limited (PPL).

**121. Mheshimiwa Spika**, sambamba na hilo, Serikali imeandaa utaratibu wa kumaliza deni lote la Pre-99 ndani ya miaka mitatu. Kwa mwaka 2025/26, kupitia hatifungani isiyokuwa ya fedha taslimu (non-cash bond), Serikali imetenga shilingi bilioni 630 kwa ajili ya deni la Pre-99 na shilingi bilioni 180 kwa ajili ya kumaliza deni la Mfuko wa NHIF. Jitihada hizo za kuboresha maslahi ya wafanyakazi na wastaafu zimedhihirisha kuwa **MAMA** anaweza.

**Uzalishaji wa Ajira**

**122**. **Mheshimiwa Spika**, kupitia utekelezaji wa sera, mikakati, mipango na programu mbalimbali, Serikali imeboresha mazingira wezeshi ya uwekezaji na ufanyaji biashara. Aidha, maboresho hayo yamechochea shughuli za kiuchumi na kuzalisha fursa za ajira kwa sekta rasmi na sekta isiyo rasmi nchini. Kutokana na jitihada hizo, katika kipindi cha Novemba 2020 hadi Februari, 2025 jumla ya ajira 8,084,204 zimezalishwa katika sekta hizo. Hivyo, kiwango cha ajira kilichozalishwa kimevuka lengo la Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020 la kuzalisha ajira milioni nane (8) katika kipindi hicho. **Kidumu Chama Cha Mapinduzi!!!**

**Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi**

**123. Mheshimiwa Spika**, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba mikataba minne (4) ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na

Sekta Binafsi (PPP) yenye mtaji wa jumla ya shilingi bilioni 681.53 imesainiwa katika mwaka 2024/25 kwa ajili ya kutoa huduma ya usafiri wa mabasi katika Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) kwa Awamu ya Kwanza (Kimara – Kivukoni na matawi yake ya Gerezani na Morocco) na Awamu ya Pili (Mbagala – Kivukoni na matawi yake ya Mbagala – Morocco kupitia Chang'ombe na Mbagala – Gerezani). Miradi hii imeandaliwa ili kuongeza ufanisi katika uendeshaji na utoaji huduma kwenye mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka, pamoja na kupunguza mzigo wa bajeti kwa Serikali. Aidha, Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa Sekta Binafsi kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya PPP kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma za jamii.

**124. Mheshimiwa Spika**, ifahamike kuwa haya niliyoyaeleza hivi punde ni baadhi tu ya mafanikio yaliyopatikana katika sekta mbalimbali chini ya uongozi wa Jemedari wetu. Mafanikio ya kina ni kama yalivyoelezwa na waheshimiwa mawaziri wa kisekta wakati wakiwasilisha bajeti zao. Hivyo, nitoe rai kwa waheshimiwa wabunge kuyanadi mafanikio hayo kwa wananchi tunapoelekea Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2025.

## V. BAJETI YA MWAKA 2025/26

**125. Mheshimiwa Spika**, bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/26 imeandaliwa kwa kuzingatia: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26); Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020; Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 2050; Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; pamoja na nyaraka, miongozo na makubaliano mengine ya kikanda na kimataifa ambayo Tanzania imeridhia.

**126. Mheshimiwa Spika**, bajeti ya Serikali ya mwaka 2025/26 ni ya tano na mwisho katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26) wenye dhima ya Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu. Aidha, dhima kuu ya Bajeti ya Mwaka 2025/26 kama ilivyokubaliwa na

nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni ***"Mageuzi Jumuishi ya Uchumi kupitia Uimarishaji wa Ukusanyaji Mapato ya Ndani, Uwekezaji wa Kimkakati wenye Kuzalisha Fursa za Ajira na Uboreshaji wa Hali ya Maisha ya Wananchi".***

**Shabaha za Uchumi Jumla**

**127**. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia mwenendo wa viashiria mbalimbali vya uchumi jumla na utekelezaji wa bajeti ya Serikali, shabaha na malengo ya uchumi jumla kwa mwaka 2025/26 ni kama ifuatavyo:

(i) Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 6.0 mwaka 2025 kutoka ukuaji wa asilimia 5.5 mwaka 2024;

(ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0 katika muda wa kati;

(iii) Mapato ya ndani kufikia asilimia 16.7 ya Pato la Taifa mwaka 2025/26 ikilinganishwa na asilimia 15.8 mwaka 2024/25;

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.3 ya Pato la Taifa mwaka 2025/26 kutoka asilimia 12.8 mwaka 2024/25;

(v) Nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa asilimia 3.0 ya Pato la Taifa mwaka 2025/26 kutoka asilimia 3.4 mwaka 2024/25; na

(vi) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

## Misingi ya Bajeti

**128. Mheshimiwa Spika**, uandaaji wa shabaha na malengo ya uchumi jumla kwa mwaka 2025/26 umezingatia misingi (*assumptions*) inayojumuisha: Kuongeza ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uwekezaji na biashara; kuendelea kuhimili athari za majanga ya asili na yasiyo ya asili ikiwemo ukame, vita, magonjwa ya mlipuko na mafuriko; uchumi imara wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya fedha na bidhaa; kuendelea kuimarika kwa upatikanaji na usalama wa chakula nchini; na uwepo wa amani, usalama, umoja na utulivu wa ndani na nchi jirani.

## Maeneo ya Vipaumbele kwa Mwaka 2025/26

**129. Mheshimiwa Spika**, bajeti hii inaendeleza na kukamilisha utekelezaji wa miradi, programu za maendeleo na afua zinazochangia maeneo makuu ya vipaumbele vya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambavyo ni: Kuchochea uchumi shindani na shirikishi; kuimarisha uzalishaji wa bidhaa viwandani na utoaji huduma; kukuza uwekezaji na biashara; na kuchochea maendeleo ya watu na kuendeleza rasilimali watu ili kuhakikisha ufikiwaji wa malengo ya Dira 2025.

**130. Mheshimiwa Spika**, baadhi ya maeneo mahsusi yatakayopewa kipaumbele katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2025/26 ni pamoja na kuendelea: Kutekeleza na kukamilisha miradi ya kielelezo na ile ya kimkakati; kuimarisha sekta za uzalishaji zenye matokeo chanya katika kukuza uchumi; kuimarisha rasilimali watu hususan katika sekta za huduma za jamii; na kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji nchini ili kuvutia ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli mbalimbali za kiuchumi.

**131. Mheshimiwa Spika**, maeneo mengine mahsusi ya vipaumbele ni pamoja na ugharamiaji wa: Deni la Serikali; mishahara na stahiki za watumishi wa umma; pamoja na ujenzi na ukarabati wa viwanja vya michezo kwa ajili ya maandalizi ya michuano ya AFCON 2027. Aidha, nipende kuwafahamisha

watanzania kuwa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 tutaugharamia kwa fedha zetu za ndani.

**132. Mheshimiwa Spika**, miradi mahsusi ya maendeleo katika maeneo ya vipaumbele itakayotekelezwa na Serikali katika bajeti ya mwaka 2025/26 imeainishwa kwa kina katika hotuba iliyowasilishwa leo asubuhi na Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji alipokuwa akiwasilisha taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26.

**133. Mheshimiwa Spika,** katika hotuba yake pia aliambatisha taarifa ya tathmini ya baadhi ya miradi iliyofanyiwa tathmini ya athari za mabadiliko ya tabia nchi.Tathmini hii ilifanyika kwa lengo la kujiridhisha na uzingatiaji wa masuala ya mazingira katika utekelezaji wa miradi. Nitumie fursa hii kulihakikishia Bunge lako tukufu kuwa Serikali imejipanga na itahakikisha upatikanaji wa fedha ili kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wakati.

**134. Mheshimiwa Spika**, maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ni ushahidi wa dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Chama Cha Mapinduzi katika kuendeleza mafanikio yaliyopatikana kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 hususan katika kuboresha ustawi wa maisha ya wananchi. Hivyo, ninawasihi na kuwaomba wananchi waendelee kukiamini Chama Cha Mapinduzi na kukichagua kwa kishindo katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 2025. **Hakika mwaka 2025 watanzania tunaenda na MAMA!!!**

**Mikakati ya Kuongeza Mapato**

**135. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2025/26, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha ukusanyaji wa mapato ikiwemo:

(i) Kuendelea kuhamasisha umma kuhusu kutoa na kudai risiti za malipo za kielektroniki za EFD;

(ii) Kuboresha utaratibu wa ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vinavyosimamiwa na mamlaka za udhibiti;

(iii) Kuendelea kuboresha Mfumo wa TAUSI ili kuhakikisha vyanzo vyote vya mapato vya Mamlaka za Serikali za Mitaa vinajumuishwa katika mfumo huo;

(iv) Kuongeza ufanisi wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya mashirika, taasisi za umma na wakala za Serikali ili kuhakikisha gawio na michango stahiki inawasilishwa kwa wakati;

(v) Kuendelea kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (MKUMBI); na

(vi) Kuendelea kuhamasisha matumizi ya njia za kidijitali katika kufanya malipo wakati wa ununuzi wa bidhaa na huduma.

**Mikakati ya Usimamizi wa Matumizi**

**136. Mheshimiwa Spika**, mwaka 2025/26 mikakati ya usimamizi wa matumizi itajumuisha:

(i) Kuendelea kusimamia na kuimarisha matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA katika utekelezaji wa shughuli za Serikali ikijumuisha mifumo ya usimamizi wa rasilimali watu, malipo serikalini, ununuzi na usimamizi wa mali za Serikali;

(ii) Kuimarisha uwajibikaji na udhibiti katika matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo ili kuziba mianya ya ubadhirifu kwa lengo la kupata thamani ya fedha katika matumizi ya Serikali; na

(iii) Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini katika utekelezaji wa miradi ili kuhakikisha inatekelezwa kwa ufanisi na

kuokoa gharama za ziada zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji.

## VI. MABORESHO YA MFUMO WA KODI, ADA, TOZO NA HATUA NYINGINE ZA MAPATO

**137. Mheshimiwa Spika,** sasa naomba kuwasilisha kwako mapendekezo ya kufanya maboresho ya mfumo wa kodi, ikiwemo baadhi ya viwango vya kodi, tozo na ada zinazotozwa chini ya sheria mbalimbali pamoja na kuboresha taratibu za ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya Serikali. Maboresho haya yamezingatia migogoro na vita vya kibiashara baina ya mataifa yaliyoendelea, kutokana na nchi ya Marekani kutangaza mabadiliko mbalimbali ya kisera kwa lengo la kuinua uchumi wake. Aidha, yanalenga pia kutafuta vyanzo vipya vya mapato, kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya ndani ya nchi na kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali (*Domestic Revenue Mobilization and Improvements in Tax Administration)*.

**138. Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea na dhamira ya kuwa na mfumo wa kodi ambao ni tulivu na wa kutabirika unaolenga kuchochea shughuli mbalimbali za uzalishaji mali ndani ya nchi kwa kuweka mkazo katika sekta za kimkakati kama vile viwanda, madini, kilimo, ufugaji na uvuvi, nishati, uchukuzi na usafirishaji, na sekta za kijamii za elimu na afya ili kuendelea kuboresha na kukuza uchumi jumla, kuongeza ajira na hatimaye kupunguza ukali wa maisha ya wananchi ("*Macro economic objectives for economic growth*").

**139. Mheshimiwa Spika,** mapendekezo ya kurekebisha mfumo wa kodi kwa mwaka 2025/26 yanatarajiwa kuiongezea Serikali jumla ya shilingi milioni 4,260,023.77 Marekebisho yanayopendekezwa yanahusu Sheria zifuatazo:

1. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148;

2. Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332;

3. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147;

4. Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438;
5. Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, SURA 290;
6. Sheria ya Bima, SURA 394;
7. Sheria ya Kudhibiti Uingizwaji wa Bidhaa Nchini, SURA 276;
8. Sheria ya Bajeti, SURA 439;
9. Sheria ya Fedha za Umma, SURA 348;
10. Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje ya Nchi, SURA 196;
11. Sheria ya Usajili na Utambuzi wa Watu, SURA 36;
12. Sheria ya Tume ya Mipango, SURA 127;
13. Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori, SURA 283;
14. Sheria ya Hifadhi za Taifa, SURA 282;
15. Sheria ya Msajili wa Hazina (Mamlaka na Majukumu), SURA 370;
16. Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, SURA 284;
17. Sheria ya Madini, SURA 123;
18. Sheria ya Alama za Bidhaa, SURA 85;
19. Sheria ya Tume ya Ushindani, SURA 285;
20. Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC);

21. Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi ya Mwaka 2024;

22. Kanuni za Sheria ya Usalama Barabarani za mwaka 2024;

23. Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004;

24. Sheria ya Utoaji wa Leseni za Biashara, SURA 101;

25. Uanzishaji wa Vyanzo vya Mapato kwa Ajili ya Kudhibiti Maambukizi ya Ukimwi na Kugharamia Bima ya Afya kwa Wote;

26. Maboresho ya Ada na Tozo mbalimbali za Taasisi za Serikali pamoja na Utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Kufanya Biashara (Blueprint);

27. Marekebisho madogo madogo katika baadhi ya Sheria za Kodi na Sheria nyingine mbalimbali; na

28. Tarehe ya kuanza kutekeleza hatua mpya za kodi.

**1. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148**

**140. Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148 kama ifuatavyo:

i. Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye viuatilifu vinavyotambulika kwa HS Codes 3808.61.00, 3808.62.00 na 3808.69.00. Lengo la hatua hii ni kuwapa unafuu wakulima ya kupata dawa za kuua wadudu mashambani na hivyo kuongeza uzalishaji wa mazao nchini. Hatua hii pia inalenga kuendana na kanuni za usawa za utozaji kodi kwa kuwa viuatilifu vya aina nyingine vimesamehewa kodi hii;

ii. Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye miamala ya ununuzi wa bima mtawanyo (reinsurance) inayofanywa baina ya kampuni za bima na zile za bima mtawanyo. Lengo la hatua hii ni kuongeza ushindani wa kampuni za ndani, kukuza Sekta ya Bima na kuhamasisha matumizi ya bima katika kukabiliana na majanga nchini;

iii. Kutoza kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha asilimia 0 kwenye bidhaa za nguo zinazotengenezwa kwa kutumia pamba inayolimwa nchini kwa kipindi cha mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kuleta unafuu kwa wakulima wa pamba na viwanda vinavyotengeneza nguo nchini hasa katika kipindi hiki cha mvutano wa kibiashara baina ya mataifa yaliyoendelea kutokana na nchi ya Marekani kutangaza mabadiliko mbalimbali ya kisera kwa lengo la kuinua uchumi wake;

iv. Kutoza kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha asilimia 0 kwenye mbolea inayozalishwa ndani ya nchi kwa kipindi cha miaka mitatu. Lengo la hatua hii ni kuleta unafuu kwa wakulima na walaji hasa katika kipindi hiki ambacho dunia imetoka kwenye mdororo wa kiuchumi duniani;

v. Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye mafuta ya kula yanayozalishwa ndani ya nchi kwa kutumia mbegu zinazozalishwa nchini kwa muda wa mwaka mmoja. Hapo awali, msamaha huu ulitolewa kwa kipindi cha mwaka mmoja kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2024 na ukomo wake ni tarehe 30 Juni 2025. Lengo la hatua hii ni kuendelea kuleta unafuu wa bei ya mafuta ya kula nchini;

vi. Kufuta Msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani unaotolewa kwenye ununuaji na uingizaji wa *gaming supply*. Hatua hii inalenga kuleta usawa katika utozaji wa kodi kwa kuwa michezo mingine kama vile mpira wa miguu ipo katika wigo wa utozaji wa kodi ya

ongezeko la thamani. Hatua hii inatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 322,022.5;

vii. Kuweka sharti la msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye matairi ya trekta yanayotumika kwenye shughuli za kilimo yanayotambulika kwa HS Code 4011.70.00; *dam liners* zinazotambulika kwa *Heading* 39.20; *forks* (HS Code 8201.90.00); reki (HS Code 8201.30.00); na shoka (HS Code 8201.40.00) kutolewa baada ya kupata ridhaa ya Waziri mwenye dhamana ya masuala ya kilimo. Lengo la hatua hii ni kuleta unafuu kwenye sekta ya kilimo na kuhakikisha msamaha unatumika kwa malengo yaliyokusudiwa;

viii. Kufuta msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye lami (bitumen) zinazotambulika kwa HS Code 2713.20.00 na 2715.00.00. Lengo la hatua hii ni kuendana na azma ya Serikali ya kupunguza misamaha isiyo na tija ili kulinda mapato ya Serikali na kupunguza matumizi yanayohusiana na utoaji wa misamaha ya kodi (tax expenditure). Hatua hii inatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 85,606.2**;

ix. Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye magazeti yanayozalishwa nchini pekee. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za magazeti hayo na hivyo kuwezesha upatikanaji wa taarifa muhimu. Hatua hii inatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 1,274.4;

x. Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye gesi asilia inayouzwa kwenda kwenye vituo vya kushindilia gesi (Compressed Natural Gas Stations) kwa ajili ya matumizi ya magari. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu kwa wawekezaji, kuvutia uwekezaji wa vituo vya kusambazia gesi asilia iliyosindikwa kwenye magari

na kupunguza utegemezi wa mafuta na uzalishaji wa hewa ya ukaa;

xi. Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye matanki na mitungi ya gesi ya kupikia zinazotambulika kwa HS Code 7311.00.10 pamoja na mitambo ya kuondoa hewa ukaa yenye HS Code 8417.80.00 inayotumika katika uzalishaji wa mikaa mbadala. Hatua hii inalenga kupunguza gharama za upatikanaji wa bidhaa hizi ili kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini. Hatua hii inatarajiwa **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 1,917.8;**

xii. Kufanya marekebisho kwenye kipengele cha 15 (8) cha Sehemu ya kwanza ya Jedwali la Misamaha ya Kodi ya ongezeko la thamani kwa kufuta neno *Liquified Petroleum and Natural gases* na kuweka neno *Liquified Petroleum Gas*. Lengo la hatua hii ni kuweka ufafanuzi na kutatua changamoto zilizopo katika utoaji wa msamaha husika na hivyo kufikia malengo yaliyokusudiwa. Aidha, tathmini iliyofanyika imebaini kuwa kutokana na ukuaji wa teknolojia, neno *Liquified Petroleum and Natural gases* halitumiki katika sekta ya nishati;

xiii. Kufanya marekebisho kwenye kipengele cha 15 (9) cha Sehemu ya kwanza ya Jedwali la Misamaha ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kufuta neno *Compressed Petroleum and Natural gases* na kuweka neno *Compressed Natural Gas for Motor vehicles* ili kuweka ufafanuzi na kutatua changamoto zilizopo katika utoaji wa msamaha husika na hivyo kufikia malengo yaliyokusudiwa. Tathmini iliyofanyika imebaini kuwa, kutokana na ukuaji wa teknolojia, neno "*Compressed Petroleum*" halitumiki katika sekta ya mafuta. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni** 132,436.3;

xiv. Kufanya marekebisho kwenye kipengele cha 15 cha Sehemu ya Pili ya Jedwali la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148, kwa kufuta msamaha kwenye vifaa visivyo vya gesi asilia iliyoshindiliwa (CNG) kama vile *natural gas pipes, transportation and distribution pipes, natural gas metering equipment, gas receiving units, flare gas system, condensate tanks and leading facility, system piping and pipe rack* na *condensate stabilizer* na badala yake kujumuisha katika kipengele husika msamaha wa CNG *Compressor* na CNG *metering equipment* ambavyo ni vifaa muhimu vinavyotumika katika vituo vya kujaza na kupima gesi asilia iliyoshindiliwa (CNG). Lengo la hatua hii ni kuhakikisha msamaha unawanufaisha wawekezaji wa vituo vya CNG na hivyo kuendana na ajenda ya Kimataifa kuhusu matumizi ya nishati safi;

xv. Kufanya marekebisho kwenye kipengele cha 15 (10) cha Sehemu ya kwanza ya Jedwali la Misamaha ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kufuta neno *Compressed or Liquified gas cylinders for petroleum and natural gases for cooking* na kuweka neno *Liquified Petroleum Gas cylinders for cooking.* Hatua hii inalenga kuweka ufafanuzi kuhusu utofauti baina ya mitungi ya kuhifadhia gesi asilia iliyoshindiliwa (CNG) na mitungi ya gesi ya kupikia ya *Liquified Petroleum Gas* (LPG) ili kuendana na ajenda ya Kimataifa kuhusu matumizi ya nishati safi. Aidha, tathmini iliyofanyika imebaini kuwa, kutokana na ukuaji wa teknolojia, hakuna mitungi ya kuhifadhia gesi asilia iliyoshindiliwa kwa ajili ya kutumika kama nishati ya kupikia;

xvi. Kujumuisha masoko mtandao (online marketplace platform) na huduma za masoko za kimtandao (network marketing platform) kwenye wigo wa tafsiri ya neno wakala wa huduma za kimtandao (online intermediation services). Lengo la hatua hii kutanua wigo wa kodi kwa kuweka ufafanuzi utakaopelekea kutatua changamoto zilizopo katika utozaji na

usimamizi wa kodi ambapo tafsiri iliyopo sasa haijumuishi huduma hizo katika utozaji kodi. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni** 116,073.4;

xvii. Kujumuisha *Non-resident online payment services platform* zinazotumia miundombinu ya watoa huduma wengine kwenye wigo wa wakala wa fedha (online intermediation payment platform) na zinazotoa huduma hapa nchini kutokea nje. Lengo la hatua hii ni kuongeza wigo wa kodi;

xviii. Kutoza kiwango cha punguzo la kodi ya ongezeko la thamani cha asilimia 16 badala ya asilimia 18 kwenye ununuzi wa bidhaa pale ambapo malipo yake yatafanyika kwa njia ya mtandao (B2C) na mlaji atathibitisha kuwa ankara ya malipo iliyotolewa ina kiwango sahihi cha muamala uliofanyika. Hatua hii inalenga kuhamasisha matumizi ya mifumo kwenye ufanyaji wa malipo, kupunguza matumizi ya fedha taslimu na kurahisisha usimamizi wa kodi kwa kuwezesha upatikanaji wa taarifa za miamala ya manunuzi. Hatua hii inatarajia **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 32,312.57;** na

xix. Kuanzisha utaratibu wa uwakala wa ukusanyaji wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwenye malipo yanayofanywa kwenda kwa muuzaji aliyesajiliwa kukusanya kodi hiyo. Kupitia utaratibu huo, Taasisi/Mlipakodi/Sekta zifuatazo zitakuwa wakala na watapaswa kukusanya asilimia 3 ya kodi la ongezeko la thamani na kuiwasilisha TRA: Wizara yenye dhamana ya masuala ya fedha; Taasisi za Serikali zinazokusanya mapato na kutumia bila kuwasilisha Mfuko Mkuu wa Serikali; pamoja na walipakodi waliosajiliwa kukusanya VAT kama itakavyobainishwa kwenye Kanuni za Uwakala wa Kukusanya VAT. Lengo la hatua hii ni kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato yanayotokana na kodi ya ongezeko la thamani. Hatua

hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 210,646.7.** Hatua hizi za Kodi ya ongezeko la thamani kwa ujumla wake zinatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 833,829.13.**

**2. Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332**

**141**. **Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332 kama ifuatavyo:

i. Kuweka unafuu wa kutoza kodi ya mapato kwa kundi la pikipiki ya miguu miwili, pikipiki ya miguu mitatu (Bajaji) na magari ya kubeba mizigo yenye uzito usiozidi Kilogramu 500 ikiwemo *Guta* kwa kuweka utaratibu mpya wa kukadiria kodi ya mapato kwenye vyombo hivyo kama ilivyoanishwa kwenye **Jedwali Na 1.** Maboresho ya viwango vya kodi elekezi yanalenga kuweka unafuu wa kodi kwa kundi husika na hivyo kurahisisha utekelezaji wa sheria;

***Jedwali Na. 1.*** Utaratibu wa kukadiria kodi ya mapato unaopendekezwa kwa wasafirishaji wa Abiria na Mizigo kwa kutumia viwango elekezi vya kodi kwa kila Chombo

**a) Daraja A: Magari ya Abiria**

| Utaratibu wa Sasa | | | Utaratibu Unaopendekezwa | |
|---|---|---|---|---|
| **SN** | **Idadi ya Abiria** | **Kiwango** | **Idadi ya Abiria** | **Kiwango** |
| 1. | Hakuna | Hakuna | Abiria wasiozidi 5 | 120,000 |
| 2. | Abiria wasiozidi 15 | 250,000 | Abiria 5 hadi 15 | 250,000 |

**b) Daraja C: Magari ya Mizigo**

| Utaratibu wa Sasa | Utaratibu Unaopendekezwa |
|---|---|

| SN | Uwezo wa Gari (Tani) | Kiwango | Uwezo wa Gari (Tani) | Kiwango |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Hakuna | Hakuna | Uzito usiozidi Kg 500 | 120,000 |
| 2. | Uzito usiozidi tani 1 | 250,000 | Uzito Kg 500 na usiozidi tani 1 | 250,000 |

### c) Daraja D: Magari Binafsi ya Kukodisha

| Utaratibu wa Sasa | | | Utaratibu Unaopendekezwa | |
|---|---|---|---|---|
| **SN** | **Aina ya Chombo** | **Kiwango** | **Aina ya Chombo** | **Kiwango** |
| 1. | Pikipiki ya Miguu miwili | 65,000 | Pikipiki ya Miguu miwili | Hakuna |
| 2. | Pikipiki ya Miguu Mitatu | 120,000 | Pikipiki ya Miguu Mitatu | Hakuna |

ii. Kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 12 cha Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332 ili kujumuisha faida ambayo haijagawanywa kwa wanahisa (retained earnings) kwenye tafsiri ya neno mtaji (equity). Lengo la hatua hii ni kuchochea uingizaji wa mitaji katika shughuli za uchumi;

iii. Kutoza kodi ya zuio kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye faida ambayo haijagawanywa kwa wanahisa baada ya miezi sita. Lengo la hatua hiyo ni kuongeza wigo wa kodi na mapato ya Serikali. Hatua hii inatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 130,624;

iv. Kutoza kodi ya mapato kwa kiwango cha asilimia 3.5 kwenye mapato yanayotokana na uuzaji wa mazao ya misitu. Kiwango cha kodi husika kitalipwa kwa awamu moja (Single Installment Tax) kwa kila thamani ya mzigo. Lengo la hatua hii ni kuendelea kurasimisha sekta ya misitu, kuhakikisha uvunaji endelevu wa mazao hayo na kuongeza wigo wa kodi. Hatua hii inatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 111,567.5;**

v. Kutoza kodi ya zuio kwa kiwango cha asilimia 2 kwenye malipo yanayotokana na ununuzi wa chumvi ghafi kwa wamiliki wa Leseni ya Uchimbaji Mdogo wa Madini (Primary Mining Licence) au Wachimbaji Wadogo wa Madini (Artisanal Miners). Hatua hii inalenga kutatua changamoto zilizopo kwenye ukusanyaji kodi katika sekta hiyo kwa kuweka utaratibu maalum wa utozaji kodi kwa wazalishaji hao. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 4,151.3;**

vi. Kutoza kodi ya zuio kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye malipo ya kamisheni inayotokana na matangazo ya michezo ya kubahatisha. Kodi hii itakuwa ni kodi ya mwisho (final). Lengo la hatua hii ni kuendana na kanuni za usawa za utozaji kodi na kupanua wigo wa kodi. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 6,787.2;**

vii. Kuongeza kiwango cha kodi ya zuio kwenye malipo ya bima na bima mtawanyo (insurance and re-insurance premium) yanayofanywa kwa kampuni za nje (non-resident) kutoka asilimia 5 hadi asilimia 10. Kiwango cha sasa hakijabadilishwa kwa takriban miaka 13 na hakiendani na hali ya uchumi iliyobadilika ndani ya miaka hiyo. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 178,988.6;

viii. Kuongeza kiwango cha kodi ya zuio kwenye malipo ya huduma za kitaalamu na kiusimamizi zinazotolewa kwenye sekta ya uziduaji (extractive sector) kutoka asilimia 5 hadi asilimia 10. Lengo la hatua hii ni kupanua wigo wa kodi na kuendana na mabadiliko ya hali ya uchumi duniani kwa kuwa kiwango cha sasa hakijabadilishwa kwa muda mrefu. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 7,427.7;**

ix. Kuongeza kiwango cha kodi ya mapato mbadala (Alternative Minimum Tax) inayolipwa na Makampuni yanayotengeneza hasara kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo kutoka asilimia 0.5 hadi asilimia 1. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali na kudhibiti uepaji wa kodi. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 222,583.8;

x. Kupunguza ukomo wa hasara ya miaka ya nyuma inayoruhusiwa kupunguzwa wakati wa ukokotoaji wa kodi ya mapato kwa wafanyabiashara katika sekta ya madini, petroli, mafuta na gesi wanaojiendesha kwa hasara kutoka asilimia 70 hadi asilimia 60. Lengo la hatua hii ni kuiwezesha Serikali kukusanya mapato mapema kutoka kwenye sekta husika. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 123,610; na

xi. Kufuta msamaha wa kodi ya mapato unaotolewa kwa kipindi cha miaka 10 ya mwanzo kwa wawekezaji waliosajiliwa katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi (EPZ na SEZ) pale bidhaa zilizozalishwa na huduma zinazotoka katika maeneo hayo zinapouzwa katika soko la ndani ya nchi. Marekebisho haya yanaenda sambamba na kufuta vipengele vinavyobainisha msamaha husika kwenye sheria zinazosimamia wawekezaji hao. Lengo la hatua hii ni kuendana na azma ya Serikali ya kupunguza misamaha ya kodi kwa lengo la kulinda mapato ya Serikali na kupunguza matumizi yanayohusiana na utoaji wa misamaha ya kodi (tax expenditure). Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 75,944.4.**

Hatua hizi za kodi ya mapato kwa ujumla wake zinatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 861,684.5.**

**3. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147**

**142. Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa kifungu cha 124(2), marekebisho ya viwango maalum vya ushuru wa bidhaa (specific duty rates) kwa bidhaa zote zisizo za petroli yanaweza kufanyika kila mwaka ili kuviwianisha na mfumuko wa bei na viashiria vingine vya uchumi jumla.

**143. Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha nchi kuwa na sera za kodi zinazotabirika na kuweka mazingira bora ya uwekezaji, Serikali ilianzisha utaratibu wa kurekebisha viwango vya ushuru wa bidhaa kila baada ya miaka mitatu (3) kuanzia mwaka wa fedha 2023/24. Aidha, napendekeza pia kufanya marekebisho kwa bidhaa nyingine kama ifuatavyo: -

i. Kufuta ada ya leseni ya kiasi cha shilingi 300,000 inayotozwa kwa wazalishaji na waingizaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa. Hatua hii inalenga kuwapa unafuu wazalishaji na waingizaji wa bidhaa hizo nchini hivyo kuendana na azma ya Serikali ya kupunguza gharama za ufanyaji biashara na kuvutia uwekezaji. Hatua hii inatarajiwa **kupunguza** mapato ya Serikali kwa shilingi milioni 1,517.1;

ii. Kupunguza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye *Un-denatured Ethyl Alcohol* yenye kilevi cha asilimia 80 au zaidi inayotoka nje ya nchi kutoka shilingi 7,000 hadi shilingi 5,000 kwa kila lita na kutoka shilingi 5,000 hadi shilingi 4,000 kwa kila lita ya *Un-denatured Ethyl Alcohol* yenye kilevi cha asilimia 80 au zaidi inayozalishwa ndani ya nchi. Bidhaa hiyo inatambulika kwa HS Code 2207.10.00. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu katika ulipaji wa ushuru wa bidhaa wa awali kwa viwanda na kuendelea kulinda viwanda vya ndani. Hatua hii inatarajia **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 38.4;**

iii. Kupunguza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji vya kuongeza nguvu (energy drinks) vinavyozalishwa ndani ya nchi kutoka shilingi 561 kwa kila lita hadi shilingi 134.2 kwa kila lita. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu kwa wazalishaji wa ndani, kuongeza ushindani na kuchochea uwekezaji

nchini. Hatua hii inatarajia **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 170.2;**

iv. Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha Shilingi 50 kwa kilo ya *crisps* zinazozalishwa nchini, na shilingi 100 kwa kilo ya *crisps* zinazoingizwa kutoka nje ya nchi. Bidhaa hizo zinatambulika kwa HS Codes 1905.90.90, 2005.20.00 na 2008.99.00. Lengo la hatua hii ni kupunguza athari za kiafya ikiwemo ongezeko la uzito (obesity) zinazotokana na matumizi ya bidhaa hizo pamoja na kuongeza mapato ya Serikali. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 6,475;**

v. Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 5 kwenye aisikrimu (ice cream) zinazotengezwa nchini kwa kutumia kakao au malighafi nyingine, na asilimia 10 kwa zile zinazoingizwa kutoka nje ya nchi. Bidhaa hizo zinatambulika kwa HS Code 2105.00.00. Lengo la hatua hii ni kupunguza athari za kiafya zinazotokana na matumizi ya bidhaa hizi, kuongeza mapato ya Serikali, na kulinda wazalishaji wa ndani. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 119,465.5;

vi. Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 5 kwa soseji na bidhaa zingine zinazofanana na hizo zinazozalishwa nchini, na asilimia 10 kwa zile zinazoingizwa kutoka nje ya nchi. Bidhaa hizo zinatambulika kwa HS Code 1601.00.00. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali, kuvutia uwekezaji nchini na kulinda wazalishaji wa ndani. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 2,413.9;**

vii. Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye sabuni zinazoingizwa kutoka nje ya nchi zinazotambulika kwa HS Codes 3401.11.00, 3401.19.00, 3402.50.00 na 3402.90.00. Lengo la hatua hii ni kulinda wazalishaji wa ndani na kuongeza ajira. Hatua hii inatarajia

**kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 143,395.8;**

viii. Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha shilingi 400 kwa kila kilo ya viberiti vinavyoingizwa nchini vinavyotambulika kwa *Heading* 36.05. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani vinavyozalisha viberiti na kuchochea uwekezaji ndani ya nchi. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 6,399.8;**

ix. Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye vito bandia (imitation jewellery) vinavyotengenezwa au vinavyoingizwa kutoka nje ya nchi vinavyotambulika kwa Heading 71.17. Lengo la hatua hii ni kuongeza wigo wa kodi na mapato ya Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 5,676.6**;

x. Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha shilingi 500 kwa kila kilo ya siagi/majarini (margarine) inayoingizwa nchini inayotambulika kwa *Heading* 15.17. Lengo la hatua hii ni kulinda wazalishaji wa ndani wa siagi ya karanga (peanut butter) kwa kuwa bidhaa hiyo hutumika kama mbadala wa majarini. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 38,442.6;

xi. Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 20 kwenye vifaa vya jikoni vilivyotumika (used tableware, kitchenware and other related products) vinavyoingizwa nchini. Vifaa hivyo vinavyotengenezwa kwa kutumia malighafi kama plastiki, mbao, chuma, shaba na aluminium vinatambulika kwa HS Codes zifuatavyo: HS Codes 3924.10.00; 3924.90.00; *Heading* 44.19; HS Codes 7323.91.00, 7323.92.00, 7323.93.00, 7323.94.00 na 7323.99.00; HS Code 7418.10.00; HS Codes 7615.10.10 na 7615.10.90; na vile vinavyotengenezwa kwa malighafi nyingine vinavyotambulika kwa *Heading* 82.15. Lengo la hatua hii ni

kuongeza wigo wa kodi na kupunguza madhara ya kiafya na athari za kimazingira zinazotokana na matumizi ya bidhaa ya aina hizo. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 9,042.5;

xii. Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 25 kwenye baruti (fireworks) zinazozalishwa nchini na zinazoingizwa kutoka nje ya nchi zinazotambulika kwa HS Code 3604.10.00. Lengo la hatua hili ni kupunguza athari za kimazingira ikiwemo uchafuzi wa hali ya hewa zinazotokana na matumizi ya baruti hizo wakati wa sherehe mbalimbali. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 8,375.3;**

xiii. Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 30 kwenye vifaa vya sigara za kielektroniki (parts of electronic cigarettes) vinavyotambulika kwa HS Code 8543.90.00 na vimiminika vya sigara za kielektroniki (Electronic Cigarettes consumable liquids) vinavyotambulika kwa HS Code *2404.12.00*. Lengo la hatua hii ni kupunguza athari zinazotokana na matumizi ya bidhaa hizo na kuongeza wigo wa kodi. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 3,322.2;

xiv. Kutoza ushuru kwa kiwango cha shilingi 22,000 (takriban dola za Marekani 8) kwa kila tani ya hewa ukaa inayozalishwa kwenye makaa ya mawe na gesi asilia. Lengo la hatua hii ni kudhibiti athari za kimazingira zinazotokana na matumizi ya nishati hizi pamoja na kuongeza mapato ya Serikali. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni** 374,159;

xv. Kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye malipo ya kutazama vipindi maalum vya televisheni (pay per view) kutoka asilimia 5 hadi asilimia 10. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato kwa kiasi cha shilingi milioni 113,376.8;

xvi. Kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye samani (furniture) zinazoingizwa nchini zinazotambulika kwa *Heading* 94.03 kutoka asilimia 20 kwenda asilimia 30. Lengo la hatua hii ni kulinda watengenezaji wa samani nchini na kuvutia uwekezaji nchini ili kuendelea kukuza sekta zinazofungamana na uzalishaji husika. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 5,814**;

xvii. Kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye gesi asilia kutoka shilingi 0.45 kwa kila futi za ujazo (cubic feet) hadi shilingi 0.55 kwa kila futi za ujazo. Lengo la hatua hii ni kulinda thamani ya fedha kwa kuwa kiwango cha sasa hakijabadilishwa kwa takriban miaka 8 na hakiendani na hali ya uchumi katika kipindi hicho. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni** 14,927.8;

xviii. Kujumuisha watoa huduma za uhamishaji wa fedha (money transfer) na mifumo ya malipo ambao siyo Taasisi za Kifedha au watoa huduma za mawasiliano (telecommunication operators) kwenye wigo wa utozaji wa ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 10. Lengo la hatua hii ni kuongeza wigo wa kodi na kuendana na kanuni za usawa za utozaji kodi. Hatua hii inatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni** 220,055.7;

xix. Kujumuisha wazalishaji wa mvinyo unaotambulika kwa *Heading* 22.05 kwenye wigo wa watumiaji wa *ethanol* wanaotumia utaratibu wa kujirejeshea (offset) ushuru wa bidhaa uliolipwa wakati wa ununuzi wa malighafi hiyo inayotumika kwenye uzalishaji. Lengo la hatua hii ni kuendana na kanuni za usawa za utozaji kodi kwa kuwa wazalishaji wengine wa mvinyo unaotambulika kwa *Heading* 22.08 na 22.04 wanatumia utaratibu huo; na

xx. Kuweka msamaha wa ushuru wa bidhaa kwenye *Un-denatured Ethyl Alcohol* inayotumika kwa matumizi mengine yasiyohusu uzalishaji wa vilevi mathalani uzalishaji wa ladha za vyakula (Food Flavors) kama vile cocoa, vanila, na

kahawa. Bidhaa hiyo inatambulika kwa HS Code 2207.10.00. Msamaha husika utatolewa baada ya kupata ridhaa ya Waziri mwenye dhamana ya masuala husika ili kuhakikisha msamaha unatumika kama ilivyokusudiwa na si vinginevyo. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za uzalishaji, kuongeza ushindani wa viwanda hivyo, pamoja na kuongeza fedha za kigeni kwa kuwa bidhaa husika kwa kiasi kikubwa zinauzwa nje ya nchi. Hatua hii inatarajia **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 180.**

Hatua hizi za ushuru wa bidhaa kwa ujumla wake zinatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 1,069,436.8.**

**4. Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438**

**144. Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438 kama ifuatavyo:-

i. Kuweka sharti la mifumo au programu za kihasibu zinazotumika katika utoaji wa risiti za kielektroniki kuunganishwa na mifumo ya Mamlaka ya Mapato Tanzania ya usimamizi wa kodi. Lengo la hatua hii ni kuwezesha upatikanaji wa taarifa, kupunguza gharama za uwajibikaji na kurahisisha usimamizi wa kodi; na

ii. Kuweka sharti la maombi ya kuruhusiwa kutolipa kiasi cha kodi ambacho hakipo kwenye pingamizi au moja ya tatu ya kodi iliyokadiriwa kutegemeana na kiasi kitakachokuwa kikubwa, kuwasilishwa ndani ya siku kumi na tano tangu tarehe ya kupokea maamuzi ya Kamishna Mkuu wa TRA (tax decision). Lengo la hatua hii ni kumpa mlipakodi muda wa kutosha wa kufanya maombi husika na hivyo kutimiza haki yake ya kuwasilisha pingamizi la kodi (tax objection).

Hatua za Usimamizi wa Kodi kwa ujumla wake zinatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 430,055.54.**

**5. Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, SURA 290.**

**145. Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, SURA 290, kama ifuatavyo:

i. Kupunguza tozo ya ushuru wa huduma (service levy) kutoka utaratibu wa sasa wa kutoza kiwango kisichozidi asilimia 0.3 ya pato ghafi kwenda kiwango mfuto cha asilimia 0.25 ya pato ghafi. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za ufanyaji biashara na uwekezaji nchini pamoja na kuendana na masharti ya Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI). Aidha kiwango pendekezwa kinalenga pia kuondoa changamoto ya utozaji kiwango tofauti wa tozo husika katika Halmashauri. Hatua hii inatarajia **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 95,412;

ii. Kupunguza kiwango cha ada ya ushuru wa hoteli (hotel levy) kutoka asilimia 10 hadi asilimia 2. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za ufanyaji biashara na uwekezaji nchini. Hatua hii inatarajiwa **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 9,779.3; na

iii. Kufuta ada za upakiaji (loading) na upakuaji (offloading) zinazotozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazohusiana na usafirishaji wa mizigo. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za ufanyaji biashara na uwekezaji nchini ili kuendana na masharti ya Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara nchini (MKUMBI).

Hatua hizi kwa ujumla wake zinatarajiwa **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 105,191.3.**

**6. Sheria ya Bima, SURA 394**

**146**. **Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Bima, SURA 394 ili kuanzisha bima ya usafiri kwa wageni wanaoingia hapa nchini kwa kiwango cha dola za Marekani 44 kama ilivyo kwa upande wa Zanzibar. Bima hii ni kwa ajili ya dharura za kiafya zinazohusiana na safari kwa wageni wanapokuwa hapa nchini, kupotea kwa mizigo ya wageni, kugharamia wageni wanapoondoshwa kwa lazima au ikitokea hatari yenye kulazimu uondoshwaji. Bima hii itakuwa na ukomo wa hadi siku 92 kwa mgeni ndani ya muda huo na haitahusisha raia wa EAC na SADC. Utaratibu huu utakuwa wa ubia kati ya sekta binafsi na Serikali ikiwakilishwa na Shirika la Bima la Taifa, ambapo mgawanyo wa mapato utabainishwa ili kuweka ufanisi katika uendeshaji wake.

**7. Sheria ya Kudhibiti Uingizwaji wa Bidhaa Nchini, SURA 276**

**147**. **Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kudhibiti Uingizwaji wa Bidhaa Nchini, Sura 276 kwa baadhi ya bidhaa zinazoingizwa nchini kama ifuatavyo:

i. Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye vifaa vya plastiki vinavyotumika majumbani (kitchenware, tableware and other household articles of plastics) vinavyoingizwa nchini vinavyotambulika kwa *Heading* 39.24. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shillingi **milioni 7,605.2;**

ii. Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye vichwa vya trela vinavyoingizwa nchini vinavyotambulika kwa HS Codes 8701.21.90, 8701.22.90, 8701.23.90, 8701.24.90 na 8701.29.90. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shillingi **milioni 99,920.2;**

iii. Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye hema za mbao, chuma na nyinginezo (prefabricated building) vinavyoingizwa nchini na

kutambulika kwa HS Codes 9406.10.90, 9406.20.90, na 9406.90.90. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shillingi **milioni 4,735.3;**

iv. Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye nondo (bars and rods) zinazotambulika kwa HS Codes 7214.10.00; 7214.20.00; 7214.30.00; 7214.91.00; 7214.99.00; 7213.10.00; 7213.20.00; na 7213.99.00. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shillingi **milioni 34,604.2;**

v. Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha asilimia 5 kwenye misumari (nails) inayoingizwa nchini inayotambulika kwa HS Code 7317.00.00. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shillingi **milioni 4,193.8;**

vi. Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye samani (furnitures) zinazoingizwa nchini zinazotambulika kwa *Heading* 94.03. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shillingi **milioni 4,880.7;**

vii. Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha asilimia 15 kwenye mabati (flat rolled products) zinazotambulika kwa HS Codes 7209.16.00; 7209.17.00; 7209.18.00; 7209.25.00; 7209.26.00; 7209.27.00; 7209.28.00; 7209.90.00; 7210.30.00; 7209.41.00; 7210.49.00; 7210.61.00; 7210.69.00; 7210.70.00; 7210.90.00; 7210.23.00; 7211.90.00; 7212.20.00; 7210.30.00; 7212.40.00; 7212.50.00; 7212.60.00; 7225.50.00; 7225.91.00; 7225.92.00; 7225.99.00; 7226.92.00; na 7226.99.00. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shillingi **milioni 67,303.9.**

viii. Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye vioo vinavyotambulika kwa *HS Codes* 7003.12.00; 7003.19.00; 7003.20.00; 7003.30.00; 7004.20.00; 7004.90.00; 7005.10.00; 7004.21.00; 7005.29.00; 7005.30.00; 7004.00.00; 7007.11.00; 7007.19.00; 7007.21.00; 7007.29.00;

7008.00.00; 7009.91.00; na 7009.92.00. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shillingi **milioni 4,726.9;**

ix. Kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha asilimia 10 au shilingi 4500 kwa kila mita ya mraba kutegemeana na kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye marumaru (ceramic tiles) vinavyotambulika kwa HS Code 6907.21.00; 6907.22.00; 6907.23.00; 6907.30.00; na 6907.40.00. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shillingi **milioni 49,663.2;**

x. Kuondoa klinka inayotambulika kwa HS Code 2523.10.00 kwenye wigo wa bidhaa zinazotozwa tozo ya maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha asilimia 10. Hatua hii inalenga kupunguza gharama kwa viwanda (non-integrated industries) vinavyoagiza bidhaa hiyo kutoka nje ya nchi kwa ajili ya uzalishaji wa saruji nchini; na

xi. Kufuta sharti la kutotoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwenye bidhaa zinazozalishwa katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC Partners States) ambazo zinakidhi vigezo vya uasili (Rules of Origins). Lengo la hatua hiyo ni kulinda viwanda vya ndani, kuchochea ushindani na kuongeza mapato ya Serikali.

Lengo la hatua hizi ni kuvutia uwekezaji nchini, kuchochea mauzo nje ya nchi na kulinda uzalishaji wa ndani kwa kuwa bidhaa husika zinazalishwa kwa wingi nchini. Aidha, mapato yatakayotokana na vyanzo husika yatatumika katika kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya msingi katika kongani za viwanda kwa lengo la kuvutia uwekezaji nchini. Hatua hizi kwa pamoja zinatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shillingi **milioni 277,603.4.**

**8. Sheria ya Bajeti, SURA 439 na Sheria ya Fedha za Umma, SURA 348**

**148**. **Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Bajeti, SURA 439 na Sheria ya Fedha za Umma,

SURA 348 ili kuweka sharti la Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kushirikishwa na Wizara, Taasisi za Serikali, Wakala au Mamlaka za Serikali kabla ya kuanzisha tozo au ada mpya, wakati wa kuanza kutoza au wakati wa kufanya mabadiliko yoyote ya viwango vya ada na tozo mbalimbali. Lengo la hatua hii ni kuiwezesha Wizara ya Fedha kutekeleza majukumu yake ya usimamizi wa mapato ya Serikali ikiwemo kufanya tathmini ya athari za viwango vinavyopendekezwa, kutafuta mbadala wa makadirio ya mapato yaliyokusudiwa hususan pale ambapo viwango vinapungua na kuratibu utoaji wa taarifa za kuishauri Serikali au Mamlaka za juu kuhusu mwenendo wa viwango vinavyotozwa nchini. Hatua hii inatokana na utozaji wa baadhi ya ada na tozo kuanzishwa bila kuwa na ridhaa ya Wizara ya Fedha na hivyo kuleta mwingiliano wa utozaji na vyanzo ambavyo baadhi tayari vinatozwa na Serikali Kuu.

**9. Sheria ya Fedha za Umma, SURA 348**

**149**. **Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 12(3) cha Sheria ya Fedha za Umma, SURA 348 kama ifuatavyo:

i. Kuweka viwango tofauti kwa Wakala wa Serikali, Mashirika na Taasisi za Umma ya kuchangia kati ya asilimia 15 hadi asilimia 60 ya mapato ghafi katika Mfuko Mkuu wa Serikali kila mwezi badala ya utaratibu uliopo sasa wa kiwango mfuto cha asilimia 15 ya mapato ghafi kila robo mwaka; na

ii. Kurekebisha kifungu cha 30 cha Sheria ya Fedha za Umma, SURA 348 kama ifuatavyo:

   a) Kuweka sharti la maandalizi ya hesabu za majumuisho kwa kutumia hesabu za taasisi za umma zilizokaguliwa. Lengo la hatua hii ni kuimarisha uaminifu na utegemezi wa hesabu katika kufanya maamuzi ya Serikali;

   b) Kupunguza muda unaotumiwa na Maafisa Masuuli kuandaa hesabu kutoka miezi

mitatu baada ya kuisha mwaka wa fedha hadi miezi miwili; na

c) Kuweka bayana sharti kwa Maafisa Masuuli kuandaa hesabu kwa kutumia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu (International Public Sector Accounting Standards - IPSAS) katika sekta ya umma na ridhaa ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kutumia Viwango vya Kimataifa vya Kihasibu (International Financial Reporting Standards – IFRS) iwapo kuna ulazima wa kutumia viwango hivyo.

**10. Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje ya Nchi, SURA 196**

**150**. **Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje ya Nchi, SURA 196 ili kutoza tozo ya usafirishaji wa bidhaa kwenda nje ya nchi kwa kiwango cha asilimia 30 au shilingi 150 kwa kila kilo moja kutegemeana na kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye vinia inayotambulika kwa Heading 44.08. Lengo la hatua hii ni kulinda wazalishaji wa ndani wa bidhaa za mbao. Hatua hii inatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni **82,722.6**.

**11. Sheria ya Usajili na Utambuzi wa Watu, SURA 36**

**151**. **Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Usajili na Utambuzi wa Watu, SURA 36 ili kusamehe Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Wizara, Idara, Wakala na Taasisi za Serikali zinazowasilisha mapato yake yote Mfuko Mkuu wa Serikali kulipa ada ya matumizi ya taarifa za utambuzi zilizo chini ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA). Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za kiutendaji na kuhimiza matumizi ya taarifa husika.

**12. Sheria ya Tume ya Mipango, SURA 127**

**152**. **Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Tume ya Mipango, SURA 127 ili kuweka masharti mbalimbali ya kufanya tathmini ya miradi ya uwekezaji wa umma

katika miradi kabla ya kuidhinisha kama itakavyobainishwa kwenye kanuni. Lengo la hatua hii ni kuweka uwazi katika ufanyaji wa tathmini hizo na kuwezesha kuweka mikakati itakayosaidia katika kuhimili athari za miradi hiyo.

**13. Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori, SURA 283**

**153. Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori, SURA 283 kama ifuatavyo:-

i. Mapato yatokanayo na ada za kuwinda wanyama muhimu kama ilivyoainishwa katika kanuni za uwindaji wa kitalii kuhusiana na shughuli za uwindaji wa kitalii katika Mapori ya Akiba yatagawanywa kama ifuatavyo:

   a. Asilimia 0 itapelekwa Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori (WMA);

   b. Asilimia 6.25 itapelekwa katika Halmashauri za wilaya husika;

   c. Asilimia 0 itapelekwa kwenye Halmashauri za vijiji vinavyopakana na kitalu cha uwindaji husika; na

   d. Asilimia 93.75 itapelekwa Mfuko Mkuu wa Serikali (Consolidated Fund).

ii. Michango inayotolewa na kampuni za uwindaji wa kitalii zinazomiliki vitalu katika Mapori ya Akiba kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya jamii yatagawanywa kama ifuatavyo:

   a. Asilimia 0 itapelekwa Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori (WMA);

   b. Asilimia 0 itapelekwa katika Halmashauri za wilaya husika;

c. Asilimia 100 itapelekwa kwa halmashauri za vijiji vinavyopakana na kitalu cha uwindaji husika; na

d. Asilimia 0 itapelekwa Mfuko Mkuu wa Serikali (Consolidated Fund).

iii. Mapato yatokanayo na shughuli za utalii wa picha katika Mapori Tengefu yatagawanywa kama ifuatavyo:

a. Asilimia 0 itapelekwa Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori (WMA);

b. Asilimia 15 itapelekwa katika halmashauri za wilaya husika;

c. Asilimia 15 itapelekwa kwa halmashauri za vijiji vinavyopakana na eneo ambapo shughuli za utalii wa picha zinafanyika; na

d. Asilimia 70 itapelekwa Mfuko Mkuu wa Serikali (Consolidated Fund).

iv. Mapato yatokanayo na ada za kuwinda wanyama muhimu kama ilivyoainishwa katika kanuni za uwindaji wa kitalii kuhusiana na shughuli za uwindaji wa kitalii katika Mapori Tengefu yatagawanywa kama ifuatavyo:

a. Asilimia 0 itapelekwa Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori (WMA);

b. Asilimia 18.75 itapelekwa katika halmashauri za wilaya husika;

c. Asilimia 0 itapelekwa kwa halmashauri za vijiji vinavyopakana na kitalu cha uwindaji husika; na

d. Asilimia 81.25 itapelekwa Mfuko Mkuu wa Serikali (Consolidated Fund).

v. Michango inayotolewa na kampuni za uwindaji wa kitalii zinazomiliki vitalu vya uwindaji wa kitalii katika Mapori ya Tengefu kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya jamii itagawiwa kama ifuatavyo:

a. Asilimia 0 itapelekwa Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori (WMA);

b. Asilimia 0 itapelekwa katika halmashauri za wilaya husika;

c. Asilimia 100 itapelekwa kwa halmashauri za vijiji vinavyopakana na kitalu cha uwindaji husika; na

d. Asilimia 0 itapelekwa Mfuko Mkuu wa Serikali (Consolidated Fund).

vi. Mapato yatokanayo na shughuli za utalii wa picha katika Maeneo ya Wazi kitagawiwa kama ifuatavyo:

a. Asilimia 0 itapelekwa Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori (WMA);

b. Asilimia 15 itapelekwa katika halmashauri za wilaya husika;

c. Asilimia 60 itapelekwa kwa halmashauri za vijiji vinavyopakana na eneo ambapo shughuli za utalii wa picha zinafanyika; na

d. Asilimia 25 itapelekwa Mfuko Mkuu wa Serikali (Consolidated Fund).

vii. Mapato yatokanayo na ada za uwindaji wa wanyama muhimu kama ilivyoainishwa katika kanuni za uwindanji wa kitalii kuhusiana na shughuli za uwindaji wa kitalii katika Maeneo ya Wazi yatagawiwa kama ifuatavyo:

a. Asilimia 0 itapelekwa Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori (WMA);

   b. Asilimia 18.75 itapelekwa katika halmashauri za wilaya husika;

   c. Asilimia 0 itapelekwa kwa halmashauri za vijiji vinavyopakana na kitalu cha uwindaji husika; na

   d. Asilimia 81.25 itapelekwa Mfuko Mkuu wa Serikali (Consolidated Fund).

viii. Michango inayotolewa na kampuni za uwindaji wa kitalii zinazomiliki vitalu katika Maeneo ya Wazi kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya jamii kitagawiwa kama ifuatavyo:

   a. Asilimia 0 itapelekwa Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori (WMA);

   b. Asilimia 0 itapelekwa katika halmashauri za wilaya husika;

   c. Asilimia 100 itapelekwa kwa halmashauri za vijiji vinavyopakana na kitalu cha uwindaji husika; na

   d. Asilimia 0 itapelekwa Mfuko Mkuu wa Serikali (Consolidated Fund).

ix. Mapato yatokanayo na shughuli za utalii wa picha katika Maeneo ya Jumuiya za hifadhi za Wanyamapori yatagawiwa kama ifuatavyo:

   a. Asilimia 65 itapelekwa Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori (WMA);

   b. Asilimia 10 itapelekwa katika halmashauri za wilaya husika;

   c. Asilimia 0 itapelekwa kwa halmashauri za vijiji vinavyounda WMA; na

d. Asilimia 25 itapelekwa Mfuko Mkuu wa Serikali (Consolidated Fund).

x. Mapato yatokanayo na ada ya pango kwa ajili ya shughuli za utalii wa picha katika Maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori kitagawiwa kama ifuatavyo:

e. Asilimia 85 itapelekwa Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori (WMA);

f. Asilimia 5 itapelekwa katika halmashauri za wilaya husika;

g. Asilimia 0 itapelekwa kwa halmashauri za vijiji vinavyounda WMA; na

h. Asilimia 10 itapelekwa Mfuko Mkuu wa Serikali.

xi. Kiasi cha mapato kinachotokana na ada za wanyama kufuatia shughuli za uwindaji wa kujikimu wa wenyeji katika Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya wanyamapori kitagawiwa kama ifuatavyo:

a. Asilimia 50 itapelekwa Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori (WMA);

b. Asilimia 35 itapelekwa katika halmashauri za wilaya husika;

c. Asilimia 0 itapelekwa kwa halmashauri za vijiji vinavyounda WMA; na

d. Asilimia 15 itapelekwa Mfuko Mkuu wa Serikali (Consolidated Fund).

Mgao wa Mapato kwa Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori (WMA), Halmashauri za Vijiji na Halmashauri za Wilaya utapelekwa kwenye akaunti ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) ambayo itazigawa kwa wahusika kwa mujibu wa kanuni

husika zilizotengenezwa chini ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, SURA 283.

**14. Sheria ya Hifadhi za Taifa, SURA 282**

**154**. **Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 9 cha Sheria ya Hifadhi za Taifa, SURA 282 kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Fedha ya mwaka 2024 ili kufuta kifungu kidogo cha 2(b) cha mgao wa asilimia 91 kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali na badala yake kuweka mgao wa asilimia 51 ya mapato yatokanayo na huduma zinazotolewa na Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania kuwekwa kwenye Akaunti ya taasisi hiyo iliyopo Benki Kuu ya Tanzania, na matumizi yake yatafanyika kwa kuomba kibali kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali na kwamba asilimia 40 ya mapato hayo yataingizwa Mfuko Mkuu wa Serikali.

**15. Sheria ya Msajili wa Hazina (Mamlaka na Majukumu), Sura 370**

**155**. **Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 8(1)(f) cha Sheria ya Msajili wa Hazina (Mamlaka na Majukumu), SURA 370 ili kuweka viwango tofauti kwa Wakala wa Serikali, Mashirika na Taasisi za Umma ya kuchangia kati ya asilimia 15 hadi asilimia 60 ya mapato ghafi katika Mfuko Mkuu wa Serikali kila mwezi badala ya utaratibu uliopo sasa wa kiwango mfuto cha asilimia 15 ya mapato ghafi kila robo mwaka. Aidha, Taasisi husika zitaanza kuchangia viwango vipya mara baada ya Msajili wa Hazina kukamilisha uchambuzi kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na kutoa mwongozo. Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina inaendelea na tathmini ya utendaji kazi ikiwemo uwezo wa kimapato wa Wakala wa Serikali, Mashirika na Taasisi za Umma.

**16. Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, SURA 284**

**156**. **Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 12 cha Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, Sura 284 kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Fedha ya mwaka 2024 ili kufuta Kifungu kidogo cha (b) cha mgao

wa asilimia 91 kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali na badala yake kuweka mgao wa asilimia 51 ya mapato yatokanayo na huduma zinazotolewa na Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania kuwekwa kwenye Akaunti ya taasisi hiyo iliyopo Benki Kuu ya Tanzania, na matumizi yake yatafanyika kwa kuomba kibali kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali na kwamba asilimia 40 ya mapato hayo yataingizwa Mfuko Mkuu wa Serikali.

**17. Sheria ya Madini, SURA 123**

**157**. **Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 59 cha Sheria ya Madini, SURA 123 ili kuweka sharti la makampuni yenye mikataba na Serikali, kutenga dhahabu kiwango kisichopungua asilimia 20 ya uzalishaji kwa ajili ya uyeyushaji, uchenjuaji, usafishaji, na biashara nchini kama ilivyo kwa Makampuni mengine ambayo hayana mikataba na Serikali. Sharti hilo litekelezwe kwa kukamilisha majadiliano na Serikali na kufanya marekebisho ya mikataba husika ndani ya siku thelathini baada ya kupitishwa kwa Sheria ya Fedha

**18. Sheria ya Alama za Bidhaa, SURA 85**

**158**. **Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Alama za Bidhaa, SURA 85 kwa kuongeza kifungu kinachoipa Tume ya Ushindani (FCC) nguvu ya kisheria ya kutekeleza jukumu la utunzaji wa alama za biashara (recordation). Aidha, ili kufanikisha utekelezaji wa jukumu hilo muhimu katika kudhibiti bidhaa bandia zinazozalishwa nchini na zinazoingizwa kutoka nje ya nchi, itatungwa kanuni mpya (The Merchandise Marks (Recordation) Regulations, 2025 ambayo itabainisha viwango vya utozaji kama ilivyobainishwa kwenye Jedwali Na. 2.

***Jedwali Na. 2***. Viwango vya Ada ya Utunzaji wa Alama za Biashara (Recordation).

| Na. | Ada ya Maombi ya Utunzaji Alama za Biashara | Kiwango (Sh) |
|---|---|---|
| 1 | Maombi ya kutunza alama ya bidhaa | 200,000.00 |

| | | |
|---|---|---|
| 2 | Maombi ya kubadili umiliki wa alama | 150,000.00 |
| 3 | Maombi ya kubadili jina la alama | 100,000.00 |
| 4 | Maombi ya kuhuisha alama ya bidhaa | 50,000.00 |
| 5 | Maombi ya kutafuta taarifa ya alama ya bidhaa | 3,000.00 |
| 6 | Maombi ya nakala ya taarifa ya alama ya bidhaa | 3,000.00 |

**19. Sheria ya Tume ya Ushindani, SURA 285**

**159**. ***Mheshimiwa Spika,*** napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Tume ya Ushindani ya mwaka 2003 kama ifuatavyo:

i. Kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 78(1)(a) kwa kubainisha kuwa, mapato ya Tume ya Ushindani (FCC) yanapaswa kujumuisha asilimia 2.5 ya ada zinazotokana na leseni ya biashara badala ya utaratibu wa sasa uliopo ambapo mapato yanapaswa kuwa si zaidi ya asilimia 2.5; na

ii. Kuongeza kifungu kinachobainisha kuwa asilimia moja ya mapato ghafi ya Mamlaka za Udhibiti zilizotajwa kwenye Kifungu cha 78(1)(c) cha Sheria ikiwemo EWURA, LATRA, TCRA na TCAA yatawasilishwa kwa Tume ya Ushindani. Hatua hii inalenga kutatua changamoto zilizopo sasa ambapo sheria imebainisha vyanzo vya mapato na Taasisi zinazopaswa kuwasilisha sehemu ya mapato yake Tume ya Ushindani (FCC) bila kuweka viwango husika.

**20.** Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC)

**160**. ***Mheshimiwa Spika,*** napendekeza kufuta Kanuni za Usimamizi wa Mazingira za mwaka 2024 (The Environmental Management Fees and Charges Amendment Regulations, 2024 GN. No. 588) na

kurejesha kanuni za awali za usimamizi wa mazingira za mwaka 2021 (The Environmental Management Fees and Charges Amendment Regulations, GN No. 387). Lengo la hatua hii ni kuruhusu mchakato wa utungwaji wa kanuni mpya utakaoshirikisha wadau wote muhimu wa Serikali na sekta binafsi na unaozingatia masharti ya Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI). Hatua hii pia inalenga kupata kanuni bora zinazotekelezeka.

## 21. Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi ya Mwaka 2024

**161**. ***Mheshimiwa Spika,*** napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi ya Mwaka 2024 kama ifuatavyo:

i. Kujumuisha kipengele kinachobainisha msamaha wa Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 75 kwenye bidhaa za mtaji zisizo za asili zinazoingizwa na wawekezaji waliosajiliwa chini ya Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi. Lengo la hatua hii ni kuendelea kuweka unafuu kwa wawekezaji nchini na kuhakikisha bidhaa mtaji zisizo za asili zinapatikana kwa bei nafuu;

ii. Kujumuisha kipengele kinachobainisha bidhaa ambazo hazikidhi kupata msamaha (negative list) kama ilivyokuwa katika Sheria ya Uwekezaji iliyofutwa. Bidhaa hizo ni pamoja na sukari, vinywaji, mabati, viyoyozi, saruji, mabati, PVC, mabomba (HDPE Pipes) na *cutleries*. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani, ajira na mapato ya Serikali; na

iii. Kuipa hadhi ya uwekezaji wa kimkakati (strategic investment) miradi ya sekta ya madini ambayo Mikataba ya Msingi (Framework Agreements) imesainiwa baina ya Serikali na Wawekezaji wa sekta ya madini nchini. Lengo la hatua hii ni kuvutia

uwekezaji kwenye sekta ya madini na kuongeza mchango wa sekta kwenye ukuaji wa Pato la Taifa.

**22. Kanuni za Sheria ya Usalama Barabarani za mwaka 2024**

**162**. ***Mheshimiwa Spika,*** napendekeza kufanya marekebisho kwenye Kanuni za Sheria ya Usalama Barabarani za mwaka 2024 kama ifuatavyo:

i. Kupunguza ada ya usajili wa pikipiki za biashara kutoka shilingi 340,000 hadi shilingi 170,000 kwa miaka mitatu. Ada husika italipwa wakati wa usajili wa awali pekee;

ii. Kufuta kodi ya mapato kwa mwaka inayolipwa kwa utaratibu wa presumptive tax na kuanzisha ulipaji wa mara moja wa ada na presumptive tax kwa kiasi cha shilingi 120,000 badala ya shilingi 290,000. Ada na kodi hii italipwa wakati wa usajili; na

iii. Kupunguza ada ya leseni ya uendeshaji wa pikipiki, bajaji na guta kutoka shilingi 70,000 hadi shilingi 30,000.

**22. Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004**

**163. Mheshimiwa *Spika,*** napenda kukufahamisha kwamba, mkutano wa Mashauriano ya Kibajeti wa Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC Pre-Budget Consultative Meeting of Ministers of Finance) uliofanyika tarehe 20 Mei 2025 jijini Arusha, pamoja na masuala mengine ulipendekeza hatua mbalimbali za kisera ikiwemo mabadiliko ya Viwango vya Pamoja vya Ushuru wa Forodha vya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC Common External Tariff) zinazopendekezwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2025/26;

**164. *Mheshimiwa Spika,*** hatua zinazopendekezwa zinalenga kulinda viwanda vya ndani ya nchi, kuvutia uwekezaji, kupunguza

gharama za uzalishaji wa bidhaa nchini ili kuleta ushindani, kulinda walaji, kuongeza ajira, kuchochea ukuaji wa sekta mbalimbali za kiuchumi pamoja na kuongeza mapato ya Serikali.

**165.** ***Mheshimiwa Spika,*** mapendekezo ya Mawaziri wa Fedha ya kufanya mabadiliko kwenye Viwango vya Pamoja vya Ushuru wa Forodha yanahusisha hatua mpya na zinazoendelea ambazo zimekuwa zikitekelezwa katika mwaka wa fedha 2024/25. Hatua hizo ni kama zifuatazo:

i. Mapendekezo ya hatua mpya za mabadiliko ya Viwango vya Ushuru wa Forodha ni kama ifuatavyo:-

   a. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 25 au dola za Marekani 350 kwa kila tani moja ya ujazo (metric ton) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya ushuru wa asilimia 25 au dola za Marekani 200 kwa kila tani moja ya ujazo (metric ton) kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa za mabati zinazotambulika kwa HS Codes 7210.49.00; 7210.61.00; 7210.69.00; 7210.70.00; na 7210.90.00. Hatua hii inalenga kulinda viwanda vya ndani, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

   b. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 35 au dola za Marekani 350 kwa kila tani moja ya ujazo (metric ton) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa za mabati zinazotambulika kwa HS Codes 7212.40.00; na 7212.50.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

   c. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 25 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye karatasi zinazotambulika kwa HS Code 4804.51.00 kwa lengo la kulinda viwanda vinavyozalisha karatasi hizo hapa nchini;

d. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 35 au dola za Marekani 300 kwa kila tani moja ya ujazo (Metric ton) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye mafuta ya kula yaliyochakatwa kwa kiwango cha mwisho (refined edible oils) yanayotambulika kwa HS Codes 1507.90.00; 1508.90.00; 15.09; 15.10; 1511.90.30; 1511.90.90; 1512.19.00; 1512.29.00; 1513.19.00; 1513.29.00; 19.00; 1514.99.00; 1515.19.00; 29.00; 1515.50.00; 1515.60.00 na 1515.90.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani na kuhamasisha uchakataji wa mbegu zinazozalishwa ndani ya nchi na mafuta ghafi yaliyoingizwa nchini ili kuongeza thamani ya bidhaa (value addition), kukuza ajira, pamoja na kuongeza mapato ya Serikali;

e. Kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye mabasi ya abiria yanayotumia mafuta ya petroli, dizeli na gesi yanayotambulika kwa HS Codes 8702.10.99; 8702.20.99 na 8702.90.99 yanayoingizwa nchini kwa ajili ya mradi wa mabasi yaendayo haraka. Hatua hii inalenga kupunguza gharama za uingizaji wa mabasi hayo ili kurahisisha huduma ya usafiri kwa wananchi;

f. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa ya mbao ikiwemo *medium density fibreboard* (MDF) zinazotambulika kwa *Heading* 44.11 kwa lengo la kulinda wazalishaji wa ndani;

g. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye vinia na mbao laini (veneered panels and plywood) zinazotambulika kwa *Heading* 44.12 kwa lengo la kulinda wazalishaji wa ndani;

h. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye

mawe yanayotumika kama mapambo katika ujenzi (monumental or building stone) yanayotambulika kwa *Heading* 68.02 kwa lengo la kuhamasisha matumizi ya mawe yanayopatikana nchini;

i. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 35 au dola za Marekani 3.0 kwa kila mita moja ya mraba (square meter) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 35 pekee kwa mwaka mmoja kwenye marumaru zinazotambulika kwa HS Codes 6907.21.00; 6907.22.00; 6907.23.00; 6907.30.00; na 6907.40.00. Hatua hii inalenga kulinda viwanda vya ndani vinavyozalisha marumaru, pamoja na kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo kutoka nje;

j. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 35 au dola za Marekani 250 kwa kila tani moja ya ujazo (metric ton) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya ushuru wa asilimia 35 pekee kwa mwaka mmoja kwenye nondo zinazotambulika kwa *Heading* 72.14. Hatua hii inalenga kulinda viwanda vya ndani, kuvutia uwekezaji, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

k. Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwenye midoli au mwanasesere (toys) zinazotambulika kwa HS Code 9503.00.00 kwa lengo la kuongeza mapato ya Serikali;

l. Kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye karatasi zinazotambulika kwa HS Code 4811.90.00 zinazotumiwa na wazalishaji wa lebo, karatasi za kutolea risiti za kielektroniki pamoja na mbao laini (plywood). Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwenye viwanda vinavyotumia malighafi hii; na

m. Kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kwa kiwango cha asilimia 0 na asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi zinazotambulika kwa HS Codes 2713.20.00; 5603.14.00; 2710.19.59; 3920.10.10 na 6802.99.00 zinazotumiwa na wazalishaji wa *waterproofing membranes*. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu wa Ushuru wa Forodha kwenye viwanda vinavyotumia malighafi hizi.

**i. Mapendekezo ya kuendelea na utekelezaji wa Viwango vya Ushuru wa Forodha vya mwaka 2024/25 ni kama ifuatavyo:-**

a. Kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye mashine za kielektroniki zinazotumika kukusanya mapato ya Serikali (Cash registers, Electronic Fiscal Device (EFD) Machines and Point of Sale (POS) machines) zinazotambulika kwa HS Codes 8470.50.00 na 8470.90.00. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha matumizi ya vifaa hivi katika kuhasibu mapato ya Serikali;

b. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye unga wa kakao unaoingizwa kutoka nje unaotambulika kwa HS Code 1805.00.00. Hatua hii inalenga kuhamasisha kilimo cha zao la kakao, uongezaji wa thamani wa zao hilo nchini pamoja na kuongeza mapato ya Serikali;

c. Kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya kuhifadhia kahawa vinavyotambulika kwa HS Codes 7310.21.00; 6305.10.00; 4819.20.90; na 5407.44.00 vinavyotumiwa na viwanda vya kusaga kahawa nchini. Hatua hii inalenga kuongeza thamani zao la kahawa na kuweka unafuu wa gharama kwenye viwanda vinavyosaga kahawa hapa nchini;

d. Kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya mbegu

vinavyotambulika kwa HS Codes 6305.10.00; 4819.40.00; 7310.29.90; 6305.33.00; 6305.20.00; 6304.91.90 na 7607.19.90. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu kwa wazalishaji wa mbegu hapa nchini;

e. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 10 au dola za Marekani 125 kwa kila tani moja ya ujazo (Metric ton) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya ushuru wa asilimia 10 pekee kwenye bidhaa za chuma kwa mwaka mmoja. Bidhaa hizi zinatambulika kwa HS Codes 7209.16.00; 7209.17.00; 7209.18.00; 7209.25.00; 7209.26.00; 7209.27.00; 7209.28.00; 7209.90.00; 7211.23.00; 7211.90.00; 7225.50.0 na 7226.92.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani vinavyozalisha bidhaa hizo, kuhamasisha uwekezaji, kuongeza mapato ya Serikali pamoja na kukuza ajira nchini;

f. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 25 au dola za Marekani 250 kwa kila tani moja ya ujazo (metric ton) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya kiwango cha asilimia 25 au dola za Marekani 200 kwa kila tani moja ya ujazo (metric ton) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye bidhaa za chuma zinazotambulika kwa HS Codes 7213.10.00; 7213.20.00; 7213.99.00; 7306.30.00; 7306.50.00; 7306.61.00; 7306.69.00; na 7306.90.00 kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha nondo hapa nchini, kuhamasisha uwekezaji, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

g. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye fito za plastiki zijulikanazo kama *PVC Profiles* zinazotambulika kwa HS Codes 3916.10.00; 3916.20.00; na 3916.90.00 zinazotumika kutengenezea fremu za milango na madirisha. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali;

h. Kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye ngano inayotambulika kwa HS

Codes 1001.99.10 na 1001.99.90 kwa lengo la la kupunguza gharama kwa viwanda vinavyozalisha unga wa ngano nchini;

i. Kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi ya kutengeneza sabuni ijulikanayo kama *RBD palm stearin* inayotambulika kwa HS Code 1511.90.40 kwa viwanda vinavyotengeneza sabuni kwa lengo la kuweka unafuu kwa wazalishaji wa sabuni nchini;

j. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 25 au dola za Marekani 1.35 kwa kila kilo moja ya viberiti (safety match) vinavyotambuliwa kwenye HS Code 3605.00.00 kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 25 pekee kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha viberiti nchini dhidi ya bidhaa zenye ruzuku kutoka nje na hivyo kuwa na ushindani sawa katika soko;

k. Kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 60 badala ya asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye maji ya kunywa (mineral and aerated waters) yanayotambulika kwa HS Code 2201.10.00. Hatua hii inalenga kulinda viwanda vinavyozalisha maji ya kunywa nchini;

l. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 0 kwenye *Gypsum Powder* inayotambulika kwa HS Code 2520.20.00 kwa mwaka mmoja kwa lengo la kulinda wazalishaji wa *Gypsum Powder* nchini;

m. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 35 badala ya asilimia 35 au dola za Marekani 0.40 kwa kilo moja kutegemea kiwango kipi kikubwa kwa mwaka mmoja kwenye mitumba inayotambulika kwa HS Codes 6309.00.10; 6309.00.20; na 6309.00.90 inayoingia kutoka nje ya nchi. Hatua hii inalenga kuweka unafuu kwa watumiaji wa bidhaa hii hapa nchini;

n. Kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwenye malighafi, vipuri na mashine vinavyotumika katika kutengeneza

viatu vya ngozi na nguo. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha ukuaji wa sekta ya nguo na ngozi nchini;

o. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 25 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye matairi mapya ya pikipiki (new pneumatic tyres of rubber) yanayotambulika kwa HS Code 4011.40.00. Lengo la hatua ni kuhamasisha uzalishaji wa matairi hayo nchini kwa kuwa kuna malighafi za kutosha;

p. Kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye mikebe ya chuma (Iron or steel cans) inayotumika katika sekta ya maziwa ambayo inatambulika kwa HS Codes 7310.10.00 na 7310.29.90. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu kwenye mikebe inayotumika kuhifadhia maziwa ili kulinda walaji pamoja na kuhamasisha uzalishaji wa maziwa nchini;

q. Kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 10 au asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza sabuni (Organic surface-active agents) zinazotambulika kwa HS Codes 3402.31.00; 3402.39.00; 3402.49.00. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu kwa wazalishaji wa sabuni za unga na za maji nchini;

r. Kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 10 au asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kuchakata ngozi zinazotambulika kwa HS Codes 3208.20.10; 3208.20.20; 3208.90.20 na 3210.00.10. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu kwa wachakataji wa ngozi nchini;

s. Kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 10 au asilimia 25 mwaka mmoja kwenye malighafi zinazotumika kuzalisha mbolea zinazotambulika kwa HS Codes 2710.99.00, 2528.00.00 na 3505.20.00 kwa lengo la kuweka unafuu kwa wazalishaji wa mbolea nchini;

t. Kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya chai iliyochakatwa vinavyotambulika kwa HS Codes 4819.20.90; na 5407.44.00. Hatua hii inalenga kuweka unafuu kwa wachakataji wa chai (tea blenders) nchini;

u. Kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwa waunganishaji wa pikipiki za matairi matatu bila kujumuisha fremu ili ziweze kutengenezwa na kuunganishwa hapa nchini (CKD for three-wheel motorcycles excluding chassis and its components) zinazotambulika kwa HS Code 8704.21.90. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu kwa waunganishaji wa pikipiki hizo nchini ili kurahisisha usafirishaji wa mizigo;

v. Kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 10 au asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza mabomba ya plastiki (glass reinforced plastic pipes) zinazotambulika kwa HS Codes 3920.61.10, 7019.19.00, 7019.11.00, 6006.90.00, 7019.12.00, 3920.10.10, 4016.93.00, na 3907.91.00. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu kwa watengenezaji wa mabomba hayo nchini ili kupunguza gharama za uzalishaji na kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya maji;

w. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 10 au dola za Marekani 125 kwa kila tani moja (Metric ton) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye mabati yanayotambulika kwa HS Code 7212.20.00 kwa mwaka mmoja badala ya ushuru wa asilimia 10 pekee. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani, kuhamasisha uwekezaji, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

x. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye taulo za watoto (baby diapers) zinazotambulika kwa HS Code 9619.00.90. Lengo la

hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa hii nchini, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

y. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 25 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye nyuzi za pamba (cotton yarn) zinazotambulika kwa *Headings* 52.05, 52.06 na 52.07 isipokuwa nyuzi za pamba zinazotambulika kwa HS Code 5205.23.00. Lengo la hatua ni kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa hiyo na kuongeza thamani ya zao la pamba (value addition) nchini;

z. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwenye bidhaa za mbogamboga na matunda zinazotambulika kwa HS Codes 0604.20.00; 0604.90.00; 0808.10.00; na 0808.30.00 kwa mwaka mmoja. Hatua hii inalenga kulinda wazalishaji wa bidhaa za mbogamboga na matunda hapa nchini;

aa. Kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kutoka asilimia 25 au asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye karatasi zinazotambulika kwa HS Codes 4804.39.00; 4805.11.00; 4805.19.00; 4805.24.00; na 4805.25.00; zinazotumika kama malighafi ya kutengeneza vifungashio aina ya maboksi (corrugated boxes). Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu kwa wazalishaji wa vifungashio hivyo hapa nchini ili wananchi waweze kuvipata kwa urahisi na kwa bei nafuu;

bb. Kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kutoka asilimia 35 hadi asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza sabuni (toilet soap) zinazotambulika kwa HS Code 3401.20.10. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu kwa wazalishaji wa sabuni nchini, kuhamasisha uwekezaji, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

cc. Kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 25 au asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza nyaya za umeme (electrical cables)

zinazotambulika kwa HS Codes 7312.10.00; 7217.20.00; 7408.19.00; 7409.11.00; 7605.21.00; 2710.19.56; 3815.90.00; 5402.19.00; 5903.90.00; 7907.00.00; na 2712.10.00. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu kwa watengenezaji wa nyaya hizo pamoja na kuvutia uwekezaji nchini;

dd. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 25 badala ya asilimia 10 kwenye kamba zinazotengenezwa kwa nyuzi zenye asili ya plastiki (Twine of other synthetic fibers) zinazotambulika kwa HS Code 5607.50.00 kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa mbadala hapa nchini pamoja na kuongeza ajira;

ee. Kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye kadi janja (smart cards) zinazotambulika kwa HS Code 8523.52.00 zitakazoingizwa nchini na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA). Hatua hii inalenga kupunguza gharama za uingizaji wa kadi hizo ili kurahisisha upatikanaji wa vitambulisho vya Taifa kwa wananchi;

ff. Kupunguza ushuru wa forodha kutoka kiwango cha asilimia 50 hadi asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye vitenge vinavyotambulika kwa HS Codes 5208.51.10; 5208.52.10; 5209.51.10; 5210.51.10; 51.10; 5212.15.10; 5212.25.10; 5513.41.10; na 5514.41.10. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu kwenye uagizaji wa vitenge ili kulinda walaji;

gg. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 25 au dola za Marekani 0.25 kwa kila mita moja kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 25 pekee kwa mwaka mmoja kwenye vitambaa vya pamba (cotton grey fabric) vinavyotambulika kwa HS Codes 5208.11.00; 5208.12.00; 5208.13.00; 5208.19.00; 5209.11.00; 5209.12.00; 5208.19.00; 5210.11.00; 5210.19.00; 5211.11.00; 5211.12.00; 5211.19.00; na 5212.21.00. Lengo la hatua hii ni kuchochea uzalishaji wa vitambaa hivyo kwa kutumia pamba inayozalishwa hapa nchini, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

hh. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 25 badala ya asilimia 10 kwenye karatasi za kutolea risiti za kielektroniki zinazotambulika kwa HS Code 4811.90.00 kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani vinavyozalisha bidhaa hii;

ii. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 35 au dola za Marekani 350 kwa kila tani moja ya ujazo (Metric ton) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 35 pekee kwa mwaka mmoja kwenye misumari inayotambulika kwa HS Code 7317.00.00. Hatua hii inalenga kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa hizo nchini, kuhamasisha uwekezaji wa bidhaa za chuma, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

jj. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 35 badala ya kiwango cha asilimia 100 au dola za Marekani 460 kwa kila tani moja ya ujazo kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwa mwaka mmoja kwenye sukari ya matumizi ya kawaida (consumption sugar) inayotambulika kwa HS Code 1701.14.90 inayoagizwa kutoka nje ya nchi kwa vibali maalum kutoka Bodi ya Sukari Tanzania kwa lengo la kuziba pengo (gap) la uzalishaji wa sukari hapa nchini;

kk. Kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kutoka asilimia 35, asilimia 25 au asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kuzalisha bidhaa mtaji (capital goods) zinazotumika viwandani zinazotambulika kwa *Headings* 73.07; 83.11; 85.44; 68.06; 74.19; 72.08; 73.12; 73.15; 73.18; 84.82; 84.83; 72.22; 73.04; 84.81; 84.84; 73.25; 40.10; na 76.06. Hatua hii inalenga kuweka unafuu kwa wazalishaji wa bidhaa mtaji hapa nchini ili bidhaa hizo ziweze kupatikana kwa unafuu kwa viwanda vya ndani pamoja na kuchochea uwekezaji wa kuzalisha bidhaa hizo hapa nchini;

ll. Kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 35, asilimia 25 au asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza rejeta (radiators) za vyombo vya moto zinazotambulika kwa HS Codes 7409.11.00; 7409.19.00; 7410.11.00;

7410.12.00; 7409.21.00; 8001.10.00; 3810.90.00. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu pamoja na kuchochea uwekezaji katika uzalishaji wa rejeta hapa nchini;

mm. Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 10 au asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza *wiring harnesses* za vyombo vya moto zinazotambulika kwa HS Codes 8538.90.00; 4016.99.00; 8205.59.00; 8536.10.00; 8536.69.00; 8536.90.00; 8547.20.00; 3926.90.90; 3917.32.00; na 8544.30.00. Hatua hii inalenga kuweka unafuu kwa wazalishaji pamoja na kuchochea uwekezaji katika uzalishaji wa *wiring harnesses* nchini ili kuendana na masharti ya Kanuni ya Uunganishaji wa Bidhaa za Jumuiya ya Afrika Mashariki;

nn. Kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye betri za umeme (lithium-ion electric accumulators) zinazotambulika kwa HS Code 8507.60.00 zinazotumiwa na wazalishaji au waunganishaji wa magari na pikipiki nchini. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu pamoja na kuchochea uwekezaji katika uzalishaji au uunganishaji wa magari na pikipiki hapa nchini ili kuwezesha upatikanaji wa bidhaa ya mwisho kwa bei nafuu;

oo. Kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kwa kiwango cha asilimia 0 badala ya asilimia 25 au asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vinavyotumiwa na wazalishaji wa maziwa kwa joto la juu yanayodumu kwa muda mrefu (UHT Milk), *yoghurt* na maziwa ya unga vinavyotambulika kwa HS Codes 3923.50.90; 4819.20.90; 4819.30.00; 4819.50.00; 4821.90.00; na 7607.19.90. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu kwa wazalishaji wa maziwa hapa nchini, kuongeza ajira pamoja na kuhamasisha uwekezaji kwenye sekta ya maziwa nchini;

pp. Kuweka unafuu wa ushuru wa forodha kwa utaratibu wa *duty remission* kwa kiwango cha asilimia 0 kwa mwaka mmoja

kwenye malighafi zinazotumiwa na wazalishaji wa *optical fiber cables* zinazotambulika kwa HS Codes 3215.19.00; 3403.99.00; 3506.91.00; 3818.00.00; 3907.99.00; 3916.90.00; 3917.39.00; 3919.90.90; 3920.69.90; 3920.99.90; 3921.14.90; 3921.90.90; 5402.11.00; 5404.90.00; 7019.90.90;8536.90.00; 8544.49.00. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu kwa wazalishaji wa *optical fiber cables* hapa nchini ili kurahisisha upatikanaji wa mawasiliano kwa gharama nafuu, kuongeza ajira pamoja na kuhamasisha uwekezaji kwenye sekta ya mawasiliano;

qq. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 35 badala ya asilimia 10 kwenye vioo vya kawaida na vioo vigumu (float and toughened glasses) vinavyotambulika kwa HS Codes 7005.10.00; 7005.21.00; 7005.29.00; 7005.30.00; 7007.19.00; 7007.29.00 na 7008.00.00 kwa mwaka mmoja. Hatua hii inalenga kulinda wazalishaji wa vioo nchini, kuongeza ajira na mapato ya Serikali;

rr. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 10 au dola za Marekani 300 kwa kila tani moja ya ujazo (metric ton) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 10 pekee kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa za mabati zinazotambulika kwa HS Code 7212.60.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

ss. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 25 au dola za Marekani 300 kwa kila tani moja ya ujazo (metric ton) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya kiwango cha asilimia 10 pekee kwenye bidhaa za chuma zinazotambulika kwa HS Codes 7225.91.00; 7225.92.00; na 7225.99.00 kwa mwaka mmoja. Hatua hii inalenga kulinda viwanda vinavyozalisha mabati hapa nchini, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

tt. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 35 au dola za Marekani 500 kwa kila tani moja ya ujazo (metric ton) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya kiwango cha asilimia 35 kwenye mabati yanayotambulika kwa HS Codes 7210.30.00 na 7210.41.00 kwa mwaka mmoja. Hatua hii inalenga

kulinda viwanda vinavyozalisha mabati hayo ndani ya nchi, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali;

uu. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 50 badala ya kiwango cha asilimia 35 kwenye chumvi (table salt) inayotambulika kwa HS Code 2501.00.90 kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kulinda wazalishaji wa chumvi nchini;

vv. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 10 au dola za Marekani 300 kwa kila tani moja (Metric ton) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye bidhaa za chuma zinazotambulika kwa HS Code 7226.99.00 kwa mwaka mmoja badala ya ushuru wa asilimia 10 pekee. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani, kuongeza ajira, kuvutia uwekezaji, kuongeza mapato ya Serikali pamoja na kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo kutoka nje;

ww. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 10 kwa mwaka mmoja badala ya asilimia 0 kwenye mafuta ghafi ya soya, karanga, nazi, mnyonyo, haradali n.k yanayotambulika kwa HS Codes 1507.10.00; 1508.10.00; 1513.11.00; 1513.21.00; 1514.11.00; 1514.91.00; na 1515.11.00. Lengo la hatua hii ni kuoanisha viwango vya mafuta ghafi haya vifanane na viwango vya mafuta ghafi ya alizeti, pamba, mahindi na mafuta ghafi mengineyo ambayo viwango vyake ni asilimia 10. Aidha, hatua hii pia inalenga kulinda na kuhamasisha uzalishaji wa mbegu za mafuta ya kula nchini, kuongeza ajira pamoja na kulinda fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mafuta hayo nje ya nchi; na

xx. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 25 au dola za Marekani 300 kwa kila tani moja ya ujazo (metric ton) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya ushuru wa asilimia 25 au dola za Marekani 200 kwa kila tani moja ya ujazo (metric ton) kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa za mabati zinazotambulika kwa HS Code 7212.30.00. Hatua hii inalenga kulinda viwanda vya ndani, kuongeza ajira pamoja na mapato ya Serikali.

**166.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na hatua nilizobainisha hapo juu, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kuanzisha Kanuni za Uunganishaji na Uzalishaji wa Bidhaa za Jumuiya ya Afrika Mashariki, 2025 (The EAC Assembling and Manufacturing of Products Regulations, 2025) ambazo utekelezaji wake utaanza Julai 2026. Kanuni hizi zinalenga kuweka mwongozo wa uanzishaji na usimamizi wa skimu (scheme) za uunganishaji na uzalishaji wa bidhaa ndani ya nchi wanachama ili kuongeza matumizi ya bidhaa zinazozalishwa ndani ya Jumuiya.

**167.** ***Mheshimiwa Spika,*** napendekeza kuendelea kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 25 badala ya asilimia 0 kwenye sukari ya matumizi ya kawaida (consumption sugar) inayotambulika kwa HS Code 1701.14.90 kwa ajili ya kuziba pengo (gap) la uzalishaji wa sukari na kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 0 kwenye sukari kwa matumizi ya viwandani inayotambulika kwa HS Code 1701.99.10 zitakazoagizwa kutoka nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kwa vibali maalum kutoka Bodi ya Sukari Tanzania. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani vinavyozalisha sukari.

Hatua hizi kwa ujumla wake zinatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 223,478.2.**

**24. Sheria ya Utoaji wa Leseni za Biashara, SURA 101**

**168**. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuiwezesha nchi kuwa na sera bora za biashara na kuweka mazingira mazuri ya ufanyaji biashara baina ya wazawa na wageni, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Utoaji wa Leseni za Biashara, SURA 101 kama ifuatavyo:

i. Kufuta kifungu cha 3(4) kinachozipa nguvu mamlaka za utoaji wa leseni za biashara kufunga biashara pale ambapo wafanyabiashara wamekiuka masharti ya Sheria husika. Lengo la hatua hii ni kuwaondolea kero wafanyabiashara na pia kutekeleza maelekezo ya Serikali ya kutofunga biashara; na

ii. Kuongeza kifungu cha 8(7) ambacho kinampa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya biashara

kuainisha shughuli za kibiashara ambazo hazipaswi kufanywa na wageni. Utaratibu wa utekelezaji wa kifungu hiki utafanywa kupitia Amri (Order) itakayotolewa na Waziri ambayo itakua na orodha ya shughuli za kibiashara ambazo hazipaswi kufanywa na wageni.

**25. Uanzishaji wa Vyanzo vya Mapato kwa Ajili ya Kudhibiti Maambukizi ya Ukimwi na Kugharamia Bima ya Afya kwa Wote**

**169**. ***Mheshimiwa Spika,*** mabadiliko ya kisera yanayoendelea duniani yamesababisha wadau muhimu wa maendeleo kupunguza misaada iliyokuwa inatolewa kwa ajili ya huduma za afya ikiwemo kukabiliana na kudhibiti magonjwa mbalimbali hususan UKIMWI. Hivyo, Serikali inapendekeza kuanzisha vyanzo mbadala vya mapato ili kupunguza nakisi ya kibajeti iliyotokana na kupungua kwa misaada hiyo kwa kufanya marekebisho katika sheria mbalimbali. Aidha, inapendekezwa asilimia 70 ya mapato yatakayoongezeka ipelekwe kwenye Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI (ATF) na asilimia 30 ipelekwe kwenye Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa Wote. Marekebisho hayo ni kama ifuatavyo:

i. Kufanya marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147 ili kuongeza ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji vya kilevi vinavyozalishwa na vinavyoingizwa kutoka nje ya nchi kama ifuatavyo: shilingi 20 kwa lita kwa bia zinazotambulika kwa *Heading* 22.03; shilingi 30 kwa lita kwa mvinyo unaotambulika kwa *Heading* 22.04, 22.05, na 22.06; shilingi 50 kwa lita kwa pombe kali na vinywaji vingine vinavyotambulika kwa *Heading* 22.08;

ii. Kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147 ili kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye huduma za mawasiliano ya kielektroniki kutoka asilimia 17 hadi asilimia 17.5;

iii. Kufanya marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, SURA 220 ili kutoza kiasi cha

shilingi 10 kwa kila lita ya mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa**;**

iv. Kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Madini, SURA 123 ili kutoza kiwango cha asilimia 0.1 kwenye thamani ya soko ya madini;

v. Kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, SURA 41 ili kuongeza kiwango cha kodi kwenye zawadi ya ushindi (Winning tax) kwenye michezo ya kubashiri matokeo (sports betting) kutoka asilimia 10 hadi asilimia 15; na kwenye michezo ya kasino ya ardhini (land-based casino) kutoka asilimia 12 hadi asilimia 15**;**

vi. Kutoza magari na mashine (heavy machines) zinazoingizwa kutoka nje ya nchi kama ifuatavyo: Shilingi 50,000 kwa magari yenye ukubwa wa injini (CC) kati ya 0 -1000; Shilingi 100,000 kwa magari yenye ukubwa wa injini (CC) kuanzia 1001-1500; Shilingi 150,000 kwa magari yenye ukubwa wa injini (CC) kuanzia 1501-2500; Shilingi 200,000 kwa magari yenye ukubwa wa injini (CC) kuanzia 2501 na zaidi; Shilingi 250,000 kwa mashine (*Excavators, Bulldozers, Fork Lifts*) zenye *Heading* 84.29 na 84.27**;**

vii. Kutoza shilingi 500 kwa kila tiketi inayotolewa na mtoa huduma za usafirishaji kwa njia ya treni; na

viii. Kutoza shilingi 1000 kwa kila tiketi inayotolewa na mtoa huduma za usafirishaji kwa njia ya anga.

Hatua hizi kwa pamoja zinatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa shilingi **milioni 586,404.9.**

**26. Maboresho ya Ada na Tozo mbalimbali za Taasisi za Serikali pamoja na Utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Kufanya Biashara (Blueprint)**

**170**. ***Mheshimiwa Spika,*** napendekeza kufanya maboresho ya kurekebisha, kuanzisha, kufuta au kupunguza ada na tozo mbalimbali zinazotozwa na Wizara, Idara na Taasisi zinazojitegemea ili kuleta usimamizi bora wa sekta mbalimbali na kuboresha mazingira ya biashara nchini. Hatua hizi ni moja ya sehemu ya mwendelezo wa utekelezaji wa Mpango wa kuboresha Mfumo wa udhibiti wa Biashara (Blueprint for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment). Marekebisho hayo ni kama ifuatavyo:

**i. Wizara ya Mifugo na Uvuvi a) Sekta ya Mifugo**

Kufanya marekebisho kwenye ada ya kibali cha kusafirisha mifugo katika minada ya mpakani kutoka shilingi 31,000 hadi shilingi 30,000 kwa kila ng'ombe; na shilingi 7,000 hadi shilingi 6,500 kwa kila mbuzi na kondoo. Lengo la hatua hii ni kuleta unafuu kwa wafugaji.

**b) Sekta ya Uvuvi**

Kufanya marekebisho ya tozo mbalimbali kwenye Sekta ya Uvuvi kama ilivyoainishwa kwenye *Kiambatisho Namba 7*. Aidha, napendekeza kupunguza ada ya uingizaji wa samaki aina ya *fin fish* kutoka dola za Marekani 2.5 hadi shilingi 1,300 kwa kila kilo moja ya samaki hao. Utozaji huo hautahusisha samaki aina ya Tilapia. Lengo la hatua hiyo ni kuchochea uingizwaji wa samaki kwa ajili ya matumizi ya chakula pamoja na kuongeza malighafi katika viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi nchini.

**ii. Wizara ya Maliasili na Utalii**

Kuunganisha huduma za malazi zilizothibitishwa kwenye kundi A (*Approved A)* na Kundi B (*Approved B)* na kutambulika kama Huduma za Malazi zilizothibitishwa (Approved Accomodation Facilities). Hatua hii inaenda sambamba na

kupunguza ada ya leseni kwa kundi hili kutoka dola za Marekani 800 hadi shilingi 766,500. Lengo la hatua hiyo ni kuwa na uwiano sawa wa ada za leseni kwa kuwa ada hiyo kwa sasa ni kubwa ikilinganishwa na makundi mengine ya huduma husika.

**iii. Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA)**

Kufanya maboresho ya tozo na ada kwenye huduma zinazotolewa na Baraza la Sanaa la Taifa kama ilivyoainishwa kwenye *Kiambatisho Namba 8.*

**iv. Shirika la Viwango Tanzania (TBS).**

Kufanya marekebisho ya tozo na ada mbalimbali kwenye ukaguzi wa viwango vya ubora wa bidhaa, kama ilivyoainishwa kwenye *Kiambatisho Namba 10.*

**v. Wakala wa Vipimo (WMA)**

Kufanya Maboresho ya ada na tozo mbalimbali zinazotozwa na Wakala wa Vipimo kama zilivyoainishwa kwenye *kiambatisho Namba 9.*

**vi. Wakala wa Usimamizi wa Afya Mahali pa Kazi** Kuweka sharti la riba kwenye faini kutozidi kiwango cha asilimia 100 ya faini ya awali badala ya utaratibu wa sasa wa kutoza riba kwa kiwango cha asilimia 5 ya faini kwa kila siku ambayo inapelekea deni hilo kuendelea kuongezeka.

**27. Marekebisho madogo madogo katika baadhi ya Sheria za Kodi na Sheria nyingine mbalimbali.**

**171**. ***Mheshimiwa Spika,*** napendekeza kufanya marekebisho mengine madogo madogo yasiyo ya kisera katika sheria mbalimbali za kodi pamoja na sheria nyingine ili ziwe sanjari na azma ya kurahisisha utekelezaji wake. Marekebisho hayo yataainishwa katika Muswada wa **Sheria ya Fedha ya mwaka 2025** na Matangazo ya Serikali *(Government Notices)*.

### 28. Tarehe ya Kuanza Kutekeleza Hatua Mpya za Kodi

**172. *Mheshimiwa Spika,*** hatua hizi za kikodi zinazopendekezwa zitaanza kutekelezwa tarehe 1 Julai, 2025, isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo. Aidha, Marekebisho hayo yataainishwa katika Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2025 na Matangazo ya Serikali (Government Notices).

**173. Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa kuwa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliunda Tume ya Rais ya Maboresho ya Mfumo wa Kodi nchini kwa lengo la kufanya tathmini ya kina ya mfumo mzima wa kodi ili kuongeza ufanisi wa ukusanyaji mapato. Tume inaendelea na tathmini kutokana na maoni yaliyopokelewa kutoka kwa wadau mbalimbali. Baada ya kukamilika kwa tathmini hiyo, Tume inatarajiwa kuwasilisha taarifa yenye mapendekezo kuhusu mfumo bora zaidi wa usimamizi wa kodi unaozingatia misingi ya utozaji kodi inayotambulika kimataifa. Aidha, mfumo huo utaweka mazingira bora ya biashara na uwekezaji, urasimishaji wa uchumi, kupanua wigo wa kodi, na kupunguza kero za walipa kodi kwa kadri inavyowezekana.

## VII. SURA YA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2025/26

### Mfumo wa Bajeti ya Serikali

**174. Mheshimiwa Spika,** utakumbuka kuwa tarehe 11 Machi 2025, niliwasilisha Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/26 mbele ya Kamati ya Bunge zima. Ukomo wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/26 uliopendekezwa ulikuwa shilingi bilioni 57,040.3. Baada ya kuwasilisha mapendekezo hayo ya ukomo, Serikali iliendelea kufanya tathmini ya athari zinazoweza kujitokeza kutokana na mabadiliko ya sera za Washirika wa Maendeleo. Tathmini hiyo ilifanyika kwa vyanzo vyote vya mapato ya ndani na nje ambayo ilionesha kupungua kwa mapato kwa takribani shilingi bilioni 550. Hivyo, inapendekezwa kupunguza kiasi cha shilingi bilioni 550 kwenye makadirio ya awali ya shilingi bilioni 57,040.3 hadi shilingi bilioni

56,490.3. Fedha hizo zitapunguzwa kwenye baadhi ya miradi ya maendeleo inayotegemea fedha za nje.

**175. Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia mabadiliko hayo, sera za bajeti, mikakati ya kukusanya mapato pamoja na azma ya Serikali ya kudhibiti matumizi, Sura ya Bajeti inaonesha kuwa jumla ya shilingi trilioni 56.49 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika katika mwaka 2025/26. Bajeti hii inatarajiwa kugharamiwa na mapato ya ndani ya shilingi trilioni 40.47, misaada shilingi trilioni 1.07 na mikopo ya shilingi trilioni 14.95. Kati ya mapato ya ndani yanayotarajiwa, mapato ya kodi ni shilingi trilioni 32.31, mapato yasiyo ya kodi shilingi trilioni 6.48, na mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa shilingi trilioni 1.68. Aidha, mikopo inajumuisha shilingi trilioni 6.27 kutoka vyanzo vya ndani na shilingi trilioni 8.68 kutoka vyanzo vya nje.

**176. Mheshimiwa Spika**, makadirio ya matumizi ya Serikali ya shilingi trilioni 56.49 kwa mwaka 2025/26 yanajumuisha: Stahiki za watumishi na michango ya pensheni (Serikali Kuu) shilingi trilioni 9.17; ununuzi wa bidhaa na huduma shilingi trilioni 5.58; malipo ya riba za mikopo shilingi trilioni 6.49; na ruzuku (subsidies & transfers) kwa taasisi za Serikali, mashirika ya umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa shilingi trilioni 22.17. Aidha, Serikali inatarajia kutumia shilingi trilioni 7.72 kugharamia malipo ya mtaji kwa deni la ndani na nje. Mfumo wa bajeti unaopendekezwa kwa mwaka 2025/26 umeainishwa katika ***Jedwali Na. 03.***

**177. Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Washirika wetu wa Maendeleo walioahidi kuchangia bajeti ya mwaka 2025/26 ili kufanikisha malengo ya maendeleo ya kitaifa. Washirika wa Maendeleo walioahidi kuchangia ni taasisi na mashirika ya kimataifa ikiwemo: Benki ya Dunia; Shirika la Fedha la Kimataifa; Benki ya Maendeleo ya Afrika; Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi katika Afrika; Benki ya Uwekezaji ya Ulaya; Mfuko wa Abu Dhabi; Mfuko wa Kuwait; Mfuko wa Kimataifa wa Kusaidia Mapambano Dhidi ya Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria (Global Fund); Mfuko wa OPEC kwa Maendeleo ya Kimataifa (OFID); Mfuko wa Mazingira Duniani (GEF); Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (GCF); Mfuko wa Kuhimili Mabadiliko ya

Tabianchi (Adaptation Fund); Mfuko wa GRMF; Umoja wa Mataifa na mashirika yote chini yake; Umoja wa Ulaya; International Fund for Agricultural Development (IFAD); pamoja na Shirika la Chanjo Ulimwenguni (GAVI).

**178. Mheshimiwa Spika**, kipekee pia nizishukuru nchi wahisani walioahidi kuchangia utekelezaji wa bajeti hii ambazo ni Australia, Austria, Canada, China, Denmark, Finland, India, Indonesia, Ireland, Italia, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Norway, Oman, Poland, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uhispania, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswisi. Aidha, napenda kutambua mchango pamoja na ushirikiano kutoka kwa asasi zisizo za serikali wakiwemo sekta binafsi, asasi za kiraia, mashirika yasiyo ya serikali na taasisi za kidini katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo hapa nchini.

**Jedwali Na.03: Mapendekezo ya Mfumo wa Bajeti kwa Mwaka 2025/26**

*Shilingi milioni*

| | |
|---|---|
| **Mapato** | **41,536,016** |
| **Mapato ya kodi** | **32,306,123** |
| Kodi za mapato | 11,491,400 |
| o/w Kodi ya Ajira (P.A.Y.E) | 5,888,445 |
| Kodi itokanayo na orodha ya malipo ya mishahara (Skills Develeopment Levy) | 420,934 |
| Kodi ya majengo/mali | 188,960 |
| Kodi za bidhaa na huduma | 13,762,949 |
| o/w Kodi ya Ongezeko la Thamani | 9,132,076 |
| Ushuru wa bidhaa | 4,412,479 |
| Kodi za biashara za kimataifa | 6,395,239 |

| | |
|---|---|
| Kodi nyingine | 46,641 |
| **Misaada/Michango** | **1,069,884** |
| Kutoka kwa nchi wahisani | 355,712 |
| Kutoka kwa mashirika ya kimataifa | 714,172 |
| | |
| **Mapato mengine** | **8,160,009** |
| o/w Mamlaka za Serikali za Mitaa | 1,680,507 |
| | |
| **Matumizi** | **46,453,030** |
| **Mishahara na stahiki za watumishi** | **9,172,019** |
| o/w Mishahara kwa watumishi wa Serikali Kuu | 7,052,355 |
| Michango ya hifadhi za jamii | 2,119,664 |
| **Gharama za bidhaa na huduma** | **5,576,148** |
| o/w Malipo ya madeni ya watumishi, wazabuni na wakandarasi | |
| **Malipo ya riba** | **6,493,715** |
| Malipo ya riba nje | 2,796,427 |
| Malipo ya riba ndani kwa taasisi zisizo Serikali Kuu | 3,697,288 |
| Malipo kwa taasisi ambazo ni Serikali Kuu | - |
| **Ruzuku kwenye taasisi za uwekezaji** | **112,560** |
| Kwa mashirikia ya umma | 111,510 |

| | |
|---|---|
| Kwa sekta nyingine | 1,050 |
| o/w Mishahara ya watumishi | |
| **Ruzuku na michango** | **22,052,853** |
| Kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa | 9,431,497 |
| o/w Mishahara ya watumishi | 5,583,591 |
| Ununuzi wa samani na uwekezaji | 2,310,011 |
| Kwa taasisi za umma | 13,104,642 |
| o/w Mishahara ya watumishi | 2,158,513 |
| Ununuzi wa samani na uwekezaji | 6,829,210 |
| **Mafao na misaada ya kijamii** | **1,001,950** |
| Mafao ya hifadhi za jamii | 992,638 |
| Misaada ya huduma za jamii | 9,163 |
| Mafao na viinua mgongo | 149 |
| **Gharama nyingine** | **2,043,785** |
| | |
| **Salio la Mapato na Matumizi** | **(4,917,014)** |
| | |
| **Uwekezaji katika mali zisizo za kifedha** | **2,321,959** |
| Gharama za majengo, miundombinu, magari, mashine n.k | 2,029,710 |
| | |

| | |
|---|---|
| Mali zisizozalishwa/mali za asili | 76 |
| | |
| **Nakisi ya Bajeti bila Misaada** | **(8,308,858)** |
| | |
| **Nakisi ya bajeti ikijumuisha misaada** | **(7,238,973)** |
| | |
| **Ugharamiaji wa nakisi ya bajeti** | (7,238,973) |
| **Mikopo halisi** | **7,238,973** |
| **Mikopo ya ndani** | **2,952,630** |
| Mikopo ya ndani | 6,278,186 |
| Malipo ya mikopo ya ndani | (3,325,557) |
| | |
| **Mikopo ya nje** | **4,286,343** |
| Mikopo ya nje | 8,676,050 |
| Malipo ya mikopo ya nje | (4,389,707) |
| | |
| **Jumla ya Bajeti** | **56,490,252** |
| **Nakisi ya bajeti/Pato la Taifa** | **3.0%** |

***Chanzo**: Wizara ya Fedha*

**Vihatarishi vya Utekelezaji wa Bajeti**

**179. Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2025/26 unaweza kuathiriwa na vihatarishi vinavyoweza kujitokeza na hivyo kusababisha kutofikiwa kwa shabaha na malengo ya bajeti.

Vihatarishi hivyo ni pamoja na: mabadiliko ya bei za bidhaa muhimu; kuongezeka kwa riba za mikopo; kushuka kwa thamani ya shilingi; madeni sanjari; mabadiliko ya tabianchi na majanga ya asili; migogoro ya kisiasa, mahusiano ya kidiplomasia na mabadiliko ya sera za Washirika wa Maendeleo pamoja na udukuzi na shambulio la mifumo ya kielektroniki.

**180. Mheshimiwa Spika**, endapo vihatarishi hivyo vitatokea vinaweza kusababisha: Kutofikiwa kwa lengo la ukusanyaji wa mapato; kasi ndogo ya utekelezaji wa miradi; kuongezeka kwa gharama za bidhaa, malighafi, huduma na utekelezaji wa miradi; kuongezeka kwa gharama za kuhudumia deni la Serikali; na kuongezeka kwa gharama za mikopo ya kibiashara katika masoko ya fedha. Aidha, athari nyingine ni pamoja na: Kupungua kwa misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo; kuongezeka kwa nakisi ya bajeti; kupungua kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo; uharibifu wa miundombinu; na kuongezeka kwa madai na madeni ya wazabuni na watoa huduma.

**181. Mheshimiwa Spika**, ili kukabiliana na athari za vihatarishi katika utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka 2025/26, Serikali itaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kuendelea: Kutekeleza na kusimamia sera za fedha na bajeti; kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kuimarisha Upatikanaji wa Fedha za Kigeni; kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 – 2034); kuimarisha usalama katika mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa fedha za umma na shughuli za Serikali; kutekeleza Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022-2032); na kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana, Sura 134. *Maelezo ya kina kuhusu vihatarishi vya bajeti yapo katika Taarifa ya Vihatarishi vya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2025/26 iliyoambatishwa.*

## VIII. HITIMISHO

**182. Mheshimiwa Spika**, nikiwa naelekea kuhitimisha hotuba yangu, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, kwa weledi wake katika kuendelea kumsaidia na kumshauri Mheshimiwa Rais kuongoza Taifa letu. Hakika mchango wake mkubwa katika ujenzi wa Taifa hautasahaulika. Hivyo, tutaendelea kutumia busara, hekima, taaluma na uzoefu wake katika kuendeleza ustawi wa maendeleo ya Taifa letu. Nitumie fursa hii kumtakia maisha mema na afya njema baada ya kustaafu. Naomba nimuage kwa neno kutoka katika Biblia Takatifu, Kitabu cha **Hesabu 6:24-26 *"BWANA akubariki na kukulinda; BWANA akuangazie nuru ya uso wake na kukufadhili; BWANA akuinulie uso wake na kukupa amani" Amina!***

**183. Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii pia kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Jimbo la Ruangwa kwa kuendelea kusimamia shughuli za Serikali bila kuchoka na kwa maelekezo mazuri kwangu katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku. Kadhalika, nimpongeze na kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waziri wa Nishati na Mbunge wa Jimbo la Bukombe, kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu katika utekelezaji wa majukumu yake.

**184. Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani. Hakika Mheshimiwa Spika umetuheshimisha katika nyanja za kitaifa na kimataifa. Napenda kukudokeza kuwa, Watanzania, Bunge hili na duniani kote tunajivunia uongozi wako mahiri. Aidha, niwapongeze pia Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika na Mbunge wa Jimbo la Ilala pamoja na wenyeviti wa vikao vya Bunge kwa kuongoza vizuri majadiliano kwa muda wote wa Bunge hili.

**185. Mheshimiwa Spika**, niwapongeze Mheshimiwa Prof. Ibrahim Hamis Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Mustapher Mohamed Siyani, Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania; Prof. Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama; na Mheshimiwa Eva

Kiaki Nkya, Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, kwa kazi nzuri ya kuongoza Mhimili wa Mahakama.

**186. Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru kwa dhati kabisa wakuu wote wa vyombo vya ulinzi na usalama kwa uzalendo na utumishi wao uliotukuka. Naomba niwatambue kwa majina: Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Jenerali Jacob John Mkunda; Inspekta Jenerali wa Polisi, Camillus Mongoso Wambura; Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa, Bw. Suleiman Abubakar Mombo; Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, Jeremiah Yoramu Katungu; Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Bw. John William Masunga; Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dkt. Anna Peter Makakala; Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Bw. Crispin Francis Chalamila; na Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Bw. Aretas James Lyimo.

**187. Mheshimiwa Spika**, nawashukuru mawaziri wenzangu na waheshimiwa wabunge wote kwa ushirikiano walionipa wakati wa kutekeleza majukumu yangu kama mbunge mwenzao na Waziri katika wizara hii. Niwatakie kila la kheri waheshimiwa wabunge wote watakaotangaza nia ya kugombea tena ubunge katika uchaguzi mkuu ujao. Nina matumaini makubwa kuwa, wananchi hawatasahau kazi kubwa na nzuri mliyoifanya. **Mwenyezi Mungu atufanikishe sote – Amin**!!!

**188. Mheshimiwa Spika**, napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini kwa maoni na ushauri wakati wa maandalizi na utekelezaji wa Bajeti ya Serikali. Aidha, niwashukuru wenyeviti na wajumbe wa kamati za kisekta kwa mchango na maoni wakati wa maandalizi ya bajeti za sekta wanazosimamia.

**189. Mheshimiwa Spika**, kipekee nimshukuru na kumpongeza Katibu Mkuu Kiongozi Balozi Dkt. Moses Mpogole Kusiluka kwa kazi nzuri anayofanya ya uratibu na usimamizi wa utekelezaji wa shughuli za Serikali. Aidha, nimshukuru CPA Charles Edward

Kichere, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya ya kukagua hesabu za taasisi mbalimbali za Serikali.

**190. Mheshimiwa Spika**, kipekee nimshukuru ndugu yangu Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Mbunge wa Jimbo la Ubungo, pamoja na Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Mbunge wa Jimbo la Maswa Mashariki pamoja na watumishi wote wa Wizara na taasisi zake wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Tausi Mbaga Kida na Katibu Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Mipango Dkt. Fred Matola Msemwa, kwa ushirikiano wanaonipatia katika utekelezaji wa majukumu yangu. Sote ni mashahidi wa kazi nzuri iliyotekelezwa na Wizara hii kupitia mafanikio yaliyopatikana katika uandaaji na usimamizi wa utekelezaji wa mpango wa Taifa wa maendeleo na maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050.

**191. Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha na Mbunge wa Jimbo la Kojani kwa kunisaidia katika utekelezaji wa majukumu yangu. **Hakika ni Naibu Waziri wa Viwango**. Aidha, nimshukuru na kumpongeza kwa dhati mwalimu wangu Dkt. Natu El-Maamry Mwamba, kwa kuweka historia ya kuwa mwanamke wa kwanza kushika wadhifa wa kuwa Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali. Hakuna atakayepinga kuwa ameitendea haki nafasi hiyo kwa kutunza vyema **chungu cha Hazina**. Vilevile, natambua mchango mkubwa wa Naibu Makatibu Wakuu Bi. Amina Kh. Shaaban, Bi. Jenifa C. Omolo na Bw. Elijah G. Mwandumbya kwa ushauri na usimamizi makini wa majukumu ya Wizara. Kadhalika, natambua kazi nzuri inayofanywa na Viongozi na Watumishi wa Wizara ya Fedha na taasisi zake katika maandalizi na usimamizi wa utekelezaji wa bajeti ya Serikali.

**192. Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii pia kumshukuru Ndugu Emmanuel Mpawe Tutuba, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, kwa kusimamia sekta ya fedha kwa ustadi mkubwa. Aidha, nimshukuru Ndugu Yusuph Juma Mwenda, Kamishna Mkuu wa

Mamlaka ya Mapato Tanzania, kwa jitihada kubwa anazofanya za kuongeza ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Nimshukuru pia Dkt. Amina Suleiman Msengwa, Mtakwimu Mkuu wa Serikali, kwa kuendelea kusimamia vema uzalishaji na usambazaji wa takwimu rasmi.

**193. Mheshimiwa Spika**, napenda pia kutoa shukrani kwa: Viongozi na Watendaji wa Wizara; Idara Zinazojitegemea; Wakala na Taasisi za Serikali; Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na wadau mbalimbali. Kushiriki kwao kwa namna moja au nyingine kumefanikisha maandalizi ya bajeti hii.

**194. Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake za kuboresha sekta ya michezo nchini. Jitihada hizo zimewezesha nchi yetu kuwa miongoni mwa nchi wenyeji wa mashindano ya CHAN 2024 na AFCON 2027. Kufanyika kwa mashindano hayo kutasaidia kwa kiasi kikubwa kuendeleza na kukuza sekta ya michezo na utalii nchini. Hivyo, nitoe rai kwa sekta binafsi kuchangamkia fursa hiyo adhimu kwa kuwa ujio wa wageni wakati wa michuano hiyo utahitaji huduma mbalimbali kama malazi, chakula na usafiri.

**195. Mheshimiwa Spika**, niipongeze kwa dhati timu ya Simba kwa kutinga fainali ya kombe la Shirikisho Barani Afrika kwa mara nyingine tangu mwaka 1993. Mafanikio haya ya Simba yanatokana na juhudi kubwa ya uwekezaji inayofanywa na Rais wa heshima wa Timu hiyo Ndugu Mohamed Dewji. Hii si tu inatoa heshima kwa Timu hiyo, bali pia inaitangaza nchi yetu katika ramani ya soka la kimataifa. Kusema kweli, Simba ya mwaka huu imepambana sana hasa ukizingatia kuwa Kocha bado anaijenga timu anayoitaka. Hivyo, nitoe pongezi kwa menejimenti ya timu pamoja na mashabiki wa Simba ambao wanaendelea kuwa mashabiki bora kabisa wakiongozwa na meneja wangu mimi (Striker), maarufu kama Semaji la CAF.

**196. Mheshimiwa Spika**, hata hivyo, Simba wasibweteke kwa kuwa mafanikio ambayo wanajivunia leo sio mapya kwa Yanga kwani walifika hatua kama hiyo mwaka juzi ambayo kwa kiasi

kikubwa ilichangiwa na uwekezaji uliofanywa na Ghalib Salim Mohamed (GSM). Ndugu GSM ameleta chachu kubwa kwenye mafanikio ya Yanga. Niwashauri yanga wanapoandaa ramani ya ujenzi wa uwanja mpya wasisahau kuweka SANAMU KUBWA YA GSM. Aidha, nitoe rai kwa vilabu vingine kuiga hatua hizo za Simba na Yanga kwa manufaa ya soka la Tanzania.

**197. Mheshimiwa Spika**, nimpongeze pia Mzee Said Salim Bakhresa kwa uwekezaji mkubwa katika tasnia ya michezo ambao umekuwa chachu ya maendeleo ya michezo nchini, hususan kupitia matangazo ya moja kwa moja (mubashara). Ni ukweli usiopingika kuwa, maisha ya watu hayawezi kukamilika kama hayana furaha, hilo tumeliona kupitia Azam TV ambayo si tu wamefanya kila mtu kuzungumzia mpira wa miguu wa nchi hii, lakini pia wameinua maisha ya wachezaji hasa wa ngumi, mpira wa miguu pamoja na wacheza filamu kupitia tamthilia mbalimbali za kitanzania. Licha ya kuwa kampuni hii ni ya binafsi, lakini sasa imekuwa kama mali ya umma kutokana na umuhimu wake katika jamii yetu ya Tanzania. Mzee Bakhresa aheshimiwe.

**198. Mheshimiwa Spika**, niruhusu kipekee nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini kutumikia Taifa kwa nafasi ya Waziri wa Fedha tangu alipoingia madarakani. Huu ni uthibitisho wa imani kubwa aliyonayo kwangu na ni fahari kufanya kazi chini ya kiongozi mwenye maono makubwa ya kuiletea nchi yetu maendeleo. Mheshimiwa Rais sio tu amenipa fahari kufanya kazi chini yake bali ameiandika historia ya kipekee kwa wanyiramba, wasukuma na wanyaturu wa Singida kuwa mnyiramba wa kwanza kusaini kwenye NOTI ya nchi.

**199. Mheshimiwa Spika**, hii ilikuwa ndoto yangu tangu kidato cha pili kufuatia mjadala uliobainisha sahihi ya marehemu Dkt. Gilman Rutihinda aliyekuwa Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania. Shukrani kwa marafiki zangu wa *group discussion* (Robert Kitundu, Sibomana Willium, John Makuru, Richard Marco, Steven Nkenguye) na wengine walionihakikishia kuwa inawezekana mtu kusaini kwenye NOTI ya nchi.

**200. Mheshimiwa Spika**, naamini kazi hii nimeifanya kwa uaminifu mkubwa, kazi hii nimeifanya kwa weledi wangu wote, kazi hii nimeifanya kwa nguvu zangu zote nikitekeleza ipasavyo miongozo ya Mheshimiwa Rais. Siwezi kuelezea zaidi ya vielelezo vya kila jambo lililofanyika kwenye kila wizara ambalo lisingeweza kufanyika bila fedha. Upatikanaji wa fedha ili miradi ya maendeleo kwenye kila sekta iweze kutekelezwa ndio jukumu nililopewa.

**201. Mheshimiwa Spika**, jukumu nililopewa la kuwa Waziri wa Fedha limenikumbusha nilipokuwa kidato cha tatu nikiwa Makamu Mwenyekiti wa Serikali ya Wanafunzi Ilboru, mimi ndio nilikuwa nakusanya ushuru wa shule kwa wafanyabiashara waliokuwa wanafanya biashara ndani ya eneo la shule na kuwasilisha makusanyo mwisho wa mwezi kwa mwalimu wa nidhamu na Elimu ya Kujitegemea - EK. Kadhalika, nilipokuwa kidato cha tano nikiwa Katibu Mkuu wa Serikali ya Wanafunzi Mazengo, mimi ndio nilikuwa nakusanya ushuru wa shule kwa wafanyabiashara waliokuwa wanafanya biashara ndani ya eneo la shule na kuwasilisha makusanyo mwisho wa mwezi kwa mwalimu wa nidhamu.

**202**. **Mheshimiwa Spika, HAKIKA**, **KUMTANGULIZA MUNGU, UAMINIFU, WELEDI NA BIDII** ni msingi wa ufanisi katika kutoa utumishi uliotukuka. Nitoe rai kwa atakaeteuliwa kushika nafasi hii baada yangu na watumishi wote wa umma tujitahidi kujinyenyekeza na kumtanguliza Mungu katika majukumu yetu, tusimamie maslahi ya Taifa na haki za wananchi wanyonge, tushinde vishawishi vya rushwa, tuzingatie sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza utumishi wa umma.

**203. Mheshimiwa Spika**, kwa hakika nina kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kama ilivyoelekezwa katika Qur'an Tukufu kwenye Sura ya 14 Aya ya 7, *"Na alipotangaza Mola wenu Mlezi: Mkishukuru nitakuzidishieni (neema)…...".* Itoshe tu kusema namshukuru sana Mheshimiwa Rais, naendelea kumuombea afya njema yeye na familia yake ili kazi kubwa aliyoianza ya kuwaletea maendeleo makubwa wananchi wa Tanzania iweze kukamilika.

**204. Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Iramba Magharibi walionipa nafasi ya kuwa Mbunge wao na kufanya kazi nao pamoja, ninaamini kwamba sikuwaangusha. Napenda kuwaahidi kuwa nitaendelea kushirikiana nao katika kuliletea maendeleo Jimbo la Iramba Magharibi. ***NSONGELI ZIGIZIGI! ASANTENI SANA!!!***

**205. Mheshimiwa Spika**, kipekee kabisa nitumie fursa hii kumshukuru mke wangu na rafiki yangu kipenzi Bi. Neema Mwigulu Nchemba pamoja na watoto wetu Joshua, Gracious, Isaac na Bernice kwa maombi yao na kunipa faraja inayoniwezesha kutekeleza vyema majukumu ya kuwatumikia watanzania.

**206. Mheshimiwa Spika**, kama nilivyosema hapo awali, mkutano huu ni wa mwisho kabla ya kuelekea kwenye Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani hapo Oktoba 2025. Hivyo, niwaombe sana watanzania wenzangu kutumia haki yao ya kikatiba ya kuchagua au kuchaguliwa katika ngazi hizo tatu nilizoziainisha. Aidha, niviombe vyama vya siasa nchini kushiriki uchaguzi huo na kuwahimiza wananchi kutumia haki hii kwa amani na utulivu kama ilivyo desturi yetu.

**207. Mheshimiwa Spika**, nisisitize tena, Serikali chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi imedhamiria kwa dhati kuhakikisha maendeleo ya kiuchumi na huduma za kijamii zinawafikia wananchi kwa gharama nafuu na kwa wakati. Sisi sote ni mashahidi kuwa Mheshimiwa Rais amefanya mageuzi makubwa ya kiuchumi kwa kukamilisha miradi mingi ya maendeleo katika sekta za uchukuzi, nishati, ujenzi, kilimo na huduma za jamii. Hii imeongeza ufanisi katika sekta za uzalishaji, fursa za ajira, kuimarika kwa huduma za jamii, pamoja na kuchochea ukuaji wa biashara na uwekezaji.

**208. Mheshimiwa Spika**, kwa mafanikio hayo, nina imani kuwa katika uchaguzi huu CCM haitapoteza JIMBO lolote wala KATA yoyote, tunaenda kushinda kwa kishindo kikubwa. **Hakika yajayo yanafurahisha** na Tanzania chini ya **MAMA** itapata mafanikio

makubwa zaidi kupitia uchapaji kazi wake na dhamira thabiti ya kuwaletea watanzania maendeleo endelevu. ***KAZI NA UTU, TUNASONGA MBELE!!***

**Mungu ibariki Afrika, Mungu ibariki Tanzania.**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. Mheshimiwa Waziri ameshawasilisha Bajeti ya Serikali nasi tumeisikia. Kama ilivyo ada utaratibu wetu utaendelea lakini ninampongeza maana amesimama kwa muda mrefu sana. Kwa hiyo, hongera sana Mheshimiwa Waziri kwa usomaji mzuri wa bajeti. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia, ninamshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu kwa kuungana nasi mpaka mwisho akiwa anasikiliza, kwa hiyo tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Sasa, Mheshimiwa Waziri kwanza ile nakala ngumu na nakala tepe kuna maeneo ambayo zile aya zinatofautiana, wataalam wakarekebishe hii nakala tepe ili ifanane na nakala ngumu kwa sababu ile itakuwa rahisi zaidi kurekebisha kuliko hii nakala ngumu. Kwa hiyo, irekebishwe na ile ili ziwe zinaendana. Ninadhani sehemu ambazo zimeanza kutofautiana ni aya ya 138 kuendelea mbele. Zimetofautiana zile aya, kwa hiyo zikarekebishwe kwenye ile nakala tepe. *(Makofi)*

Halafu lingine Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu Mheshimiwa Waziri alisema kitabu chake alichowasilisha kiingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge, kwa hiyo maeneo yale ambayo yamesomwa takwimu tofauti na kile kilichoandikwa kwenye kitabu, taarifa yake hii aliyoisoma kwenye Taarifa Rasmi za Bunge zitasoma yale ambayo yameandikwa kwenye kitabu hiki. Kwa

sababu wakati wa kufuatilia kuna maeneo ambayo yalikuwa yanasomwa kama mamia wakati yanapaswa yasomwe maelfu, na kuna maeneo ambayo yalipaswa kusomwa milioni yakasomwa kama elfu. Kwa hiyo, ile kidogo ikaleta mkanganyiko. *(Makofi)*

Sasa hiyo ili kuifanyia marekebisho kwa sababu ni maeneo mengi kidogo, kwa hivyo hayo yatarekebishwa yote kwa pamoja ili taarifa aliyoisoma Mheshimiwa Waziri pamoja na hii ambayo imeingia kwenye Taarifa Rasmi za Bunge ziweze kufanana. Kwa hivyo, sitasoma ni maeneo gani yanayohitaji marekebisho lakini yote yatarekebishwa kwa agizo hili ambalo nimelitoa sasa.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, sasa nilete tangazo kwenu la wageni walioko Bungeni ambao wameungana nasi katika kusikiliza ambacho Mheshimiwa Waziri amekuja kutusomea hapa kwa niaba ya Serikali nzima na sasa niwatambulishe kwenu.

Tutaanza na wageni waliokaa Jukwaa la Spika. Kwanza ni Mheshimiwa Fredrick Tluway Sumaye ambaye ni Waziri Mkuu Mstaafu na Mheshimiwa Anne Semamba Makinda, ambaye pia ni Spika wa Bunge Mstaafu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia Dkt. Frank George Haule Hawassi ambaye ni mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi na Katibu wa *NEC*, Uchumi na Fedha wa Chama Cha Mapinduzi; Ndugu Salum Reja, Katibu wa Sekretarieti ya Chama cha Mapinduzi; karibu sana. Yupo Ndugu John Chacha Milumbe, ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Wazazi Chama Cha Mapinduzi; karibu sana. *(Makofi)*

Wapo pia Mheshimiwa Rosemary Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma; na Ndugu Fadhili Chibago, Naibu Meya Jiji la Dodoma; karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Balozi Dkt. Moses Mpogole Kusiluka, Katibu Mkuu Kiongozi; Jenerali Jacob John Mkunda ambaye ni Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi; karibu sana, Inspekta Jenerali Camillus

Wambura, Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania; Ndugu Fadhili Saga ambaye ni Naibu Mkurugenzi Mkuu Idara ya Usalama wa Taifa, akimwakilisha Mkurugenzi Mkuu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Jeremiah Yoramu Katungu, ambaye ni Kamishna Jenerali Jeshi la Magereza; Ndugu John William Masunga ambaye ni Kamishna Jenerali Jeshi la Zimamoto na Uokoaji; na Dkt. Anna Peter Makakala ambaye ni Kamishna Jenerali wa Uhamiaji. Karibuni sana. Ahsante sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Yupo Ndugu Crispin Francis Chalamila ambaye ni Mkurugenzi Mkuu Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU); na Ndugu Aretas James Lyimo ambaye ni Kamishna Jenerali Mamlaka ya Dawa za Kulevya. Karibuni sana. *(Makofi)*

Viongozi wetu kutoka Vyombo vya Ulinzi na Usalama tunawashukuru sana kwa kazi nzuri na tunaungana na maneno aliyosema Mheshimiwa Waziri. Ahsanteni sana kwa kazi nzuri na tunaamini hizi changamoto ambazo tunazipitia sasa mtazifanyia kazi kama ambavyo mmekuwa mkifanya miaka yote. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia wapo Dkt. Natu Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha; Ndugu Emmanuel Tutuba ambaye ni Gavana wa Benki Kuu; Ndugu Yusuph Mwenda, Kamishna Mkuu Mamlaka ya Mapato Tanzania; Ndugu Nehemiah Mchechu, Msajili wa Hazina; Jaji Mstaafu Sivangilwa Sikalakwa Mwangesi, ambaye ni Kamishna Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; na Ndugu James Kaji ambaye ni Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Vitambulisho ya Taifa *(NIDA)*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo vile vile Askofu Dkt. Magnus Mhiche ambaye ni Makamu Askofu Mkuu wa Makanisa ya *Tanzania Assemblies of God*; Dkt. Mafelle Ihoyelo, Mwakilishi wa Sheikh Mkuu wa Tanzania; na Sheikh Mustafa Rajabu, ambaye ni Sheikh wa Mkoa wa Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Balozi Dkt. Asha Rose Migiro ambaye ni Mjumbe Tume ya Taifa ya Mipango; karibu sana, ahsante sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Kuna Ndugu Omari Issa, Mjumbe Tume ya Taifa ya Mipango; Ndugu Theobald Sabi, Afisa Mtendaji Mkuu Benki ya *NBC* na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mabenki Tanzania; Dkt. James Andilile, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *(EWURA)*. Karibu sana. Haya ahsanteni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, malizia utambulisho, malizia utambulisho.

**SPIKA:** Ahsanteni sana. Yupo Mheshimiwa Haroon Pirmohamed, Mbunge Mstaafu wa Mbarali. Haya ahsanteni sana, ahsanteni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Wapo pia Ndugu Zelia Njeza ambaye ni Rais wa Chama cha Wakaguzi wa Ndani Tanzania; Ndugu Seif Hassan, Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Wakaguzi wa Ndani Nchini; Ndugu Godlisten Mollel ambaye ni Mkurugenzi Kampuni ya Mesera Dar es Salaam; na Ndugu Alfredy Mapunda, Mkurugenzi Mkuu Kampuni ya *SICPA* Tanzania. Karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Rodrick Benjamin, Mzee wa Kanisa Kiongozi *TAG ICC*; na Ndugu Francis Mdoe, Mzee wa Kanisa *TAG ICC*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Sasa huyu alishatambulishwa na Mumewe, lakini inabidi nimtambulishe kwa sababu amekaa Jukwaa la Spika. Yupo Ndugu Neema Nchemba, Mke wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Karibu sana, karibu sana. Haya ahsante sana, ahsante sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Wageni waliokaa Jukwaa la Kulia kwa Spika, hawa ni Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu. Tutaanza na Dkt. Jim Yonaz ambaye ni Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, na Uratibu; Ndugu Mululi Mahendeka, Katibu Mkuu Ikulu; Ndugu

Juma Mkomi, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Ndugu Adolf Ndunguru, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, TAMISEMI; na Mhandisi Cyprian Luhemeja, Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Mary Maganga, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu; Dkt. Faraji Mnyepe, Katibu Mkuu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; Ndugu Ally Gugu, Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; Ndugu Eliakim Maswi, Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria; Balozi Dkt. Samwel Shelukindo, Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje, anayeshughulikia masuala ya nje; na Balozi Stephen Mbundi, Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje anayeshughulikia masuala ya Afrika Mashariki. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia Ndugu Gerald Mweli, Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo; Profesa Riziki Shemdoe, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Mhandisi Anthony Sanga, Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Profesa Godius Kahyarara, Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi; Balozi Mhandisi Aisha Amour, Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi; na Dkt. Hashil Abdallah, Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo vile vile Profesa Carolyne Nombo ambaye ni Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sanyansi, na Teknolojia; Dkt. John Jingu, Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake, na Makundi Maalum; Mhandisi Mwajuma Waziri, Katibu Mkuu Wizara ya Maji; Ndugu Gerson Msigwa, Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; na Ndugu Mohammed Abdulla, Katibu Mkuu Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo Profesa Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama. Karibu sana. Ahsanteni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Wapo Ndugu Kaspar Mmuya, Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma; Ndugu Jenifa Omolo, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya

Fedha, Huduma za Hazina; na Ndugu Elijah Mwandumbya, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Usimamizi wa Uchumi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia Mabalozi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa na Washirika wa Maendeleo amba oni Mheshimiwa Ahamada Elbadaui Mohamed Fakih, ambaye ni Balozi wa *Comoro* na Mkuu wa Mabalozi nchi; Mheshimiwa Jesper Kammersgaard ambaye ni Balozi wa *Denmark* Nchini Tanzania; Mheshimiwa Endrew Zumbe Kumwenda, Balozi wa Malawi Nchini Tanzania; Mheshimiwa Jean Pierre Massala, Balozi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo Nchini Tanzania; na Mheshimiwa Leontine Nzeymana, ambaye ni Balozi wa Burundi Nchini Tanzania. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Jenerali Patrick Nyumvuha, ambaye ni Balozi wa Rawanda Nchini Tanzania; Ndugu Maksym Nemyria, ambaye ni Kaimu Balozi Jamhuri ya *Ukraine* Nchini Tanzania; Ndugu Sylivester Ernest, Mwakilishi wa Balozi wa Uingereza Nchini Tanzania; Ndugu Priva Clemence, Mwakilishi wa Balozi wa Norway Nchini Tanzania; Ndugu Richard Shaba, Mwakilishi wa Balozi wa Ujerumani Nchini Tanzania; na Ndugu Mark Schand ambaye ni Mwakilishi kutoka Umoja wa Mataifa, *(United Nations)*. Karibu sana. *(Makofi)*

Wapo pia Ndugu Suzan Namando, Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa, *(United Nations);* Ndugu Evance Siangicha, Mchumi Ofisi ya Mratibu wa Umoja wa Mataifa; Ndugu Duncan Ouma, Mkuu wa Misheni, Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AFDB)*; Ndugu Chelaus Rutta ambaye ni Mwakilishi Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF);* Ndugu Sebastian Acevedo Mejia ambaye ni Mwakilishi Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF)*; na Ndugu Aghassi Mkrtchyan ambaye ni Kiongozi wa Programu ya Uchumi anayesimamia Nchi ya Tanzania, Zambia, Zimbabwe na Malawi kutoka Benki ya Dunia. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia Ndugu John George, Afisa Mawasiliano Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Watoto *(UNICEF)* Dodoma; na Ndugu Zena

Amury, Mtaalam wa Sera za Kijamii, Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Watoto *(UNICEF)* Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki. Nao ni Mheshimiwa Dkt. Ngwaru Maghembe; na Mheshimiwa Machano Ali Machano, Mheshimiwa Nadra Mohamed. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, familia ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, aliwatambulisha baadhi ya walioko hapo, nami nitawasoma. Yupo Ndugu Joshua Mwigulu Nchemba, mtoto wa Mheshimiwa Waziri; Ndugu Gracious Mwigulu Nchemba, mtoto wa Mheshimiwa Waziri; Ndugu Isaac Mwigulu Nchemba na Ndugu Bernice Mwigulu Nchemba, watoto wa Mheshimiwa Waziri. Ndugu Jugulu Madelu, kaka wa Mheshimiwa Waziri. Ndugu Sam Madelu, mdogo wa Mheshimiwa Waziri. Ndugu Shabani Madelu, mtoto wa Mheshimiwa Waziri; Ndugu Musa Wilson, ndugu wa Mheshimiwa Waziri; Ndugu Chris Gerald, Ndugu Nazareth Jonas, Ndugu Hope Teretio na Ndugu Aman Said. Hawa ni watoto wa Mheshimiwa Waziri, anaowalea. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Juvenile Leonard, Ndugu Emil Ngaponda, Dkt. Kelvin Njunwa na Ndugu Baraka Munisi. Hawa ni marafiki wa Mheshimiwa Waziri. Ndugu Daniel Ngure, shemeji wa Mheshimiwa Waziri; na Ndugu Iq-Lima Issa, rafiki wa Mheshimiwa Waziri. Karibuni sana.

Yupo Ndugu Christine Mbonya, Mjumbe Kamati ya Ushauri, Bodi ya Wakaguzi wa Ndani Nchini. Karibu. *(Makofi)*

Inabidi ninywe maji kidogo. *(Makofi)*

Menejimenti ya Ofisi ya Bunge; Ndugu Triphonia Mng'ong'o, Mjumbe; *CPA* Layson Mwanjisi, Mjumbe; *CPA* Paul Msisi, Mjumbe; Ndugu Pius Mboya, Mjumbe; Ndugu Daniel Eliufoo, Mjumbe; Ndugu Deogratias Egidio, Mjumbe; Ndugu Aziza Waziri Kheir, Mjumbe; Ndugu Hawa Rajabu, Mjumbe; Ndugu Lily Mraba, Mjumbe; Ndugu Peter Magati, Mjumbe; Ndugu Hanifa

Masaninga, Mjumbe; Ndugu Zuhura Mtatifikolo, Mjumbe; na Ndugu Frank Mbilinyi, Mjumbe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia, Washarika 45 wa Kanisa la *TAG ICC* kutoka Mkoani Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Sasa tunaanza wageni waliokaa jukwaa la kushoto kwa Spika:-

Yupo Dkt. Zarau Wendeline Kibwe, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji, Benki ya Dunia, anayesimamia Kundi la Kwanza la Nchi za Kanda ya Afrika; Dkt. Fred Msemwa, Katibu Mtendaji Tume ya Taifa ya Mipango; Mheshimiwa Mohamed Ahmed, Naibu Msajili Vyama vya Siasa. Karibu sana. *(Makofi)*

Sijajua! Ameitwa Mheshimiwa, lakini nafikiri ndio *title* yake pengine! Sawa. *(Makofi)*

Ndugu Juma Rahis, Kaimu Mkurugenzi Tume Huru ya Uchaguzi *(INEC)*; Dkt. Jabiri Bakari, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA);* Ndugu Abdul Mombokaleo, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania *(TAA);* Ndugu Salim Msangi, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Usafiri wa Anga; Ndugu Charles Itembe, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje *(EPZA);* na Ndugu Masanja Kadogosa, Mkurugenzi Mkuu Shirika la Reli Tanzania *(TRC)*. *(Makofi)*

Vilevile yupo Ndugu Mussa Kuji, Kamishna wa Uhifadhi Shirika la Hifadhi la Taifa *(TANAPA);* na Profesa Dosantos Silayo, Kamishna wa Uhifadhi Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania *(TFS)*. *(Makofi)*

Tunao, Ndugu Abdul-Razak Badru, Kamishna wa Uhifadhi Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro *(NCAA);* Ndugu Mlage Kabange, Kaimu Kamishna wa Uhifadhi Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyama Pori Tanzania *(TAWA);* Ndugu Kaimu Mkeyenge, Mkurugenzi Mtendaji Shirika la Bima la Taifa *(NIC);* na Ndugu Masha Mshomba, Mkurugenzi Mkuu Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF)*. *(Makofi)*

Wengine ni Dkt. Rhimo Nyansaho, Mkurugenzi Mkuu Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma *(PSSSF);* Ndugu Mwanahiba Mzee, Mkurugenzi Mkuu Mfuko wa Pembejeo za Kilimo; na Mhandisi Victor Seif, Mtendaji Mkuu Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini *(TARURA)*. *(Makofi)*

Yupo *CPA* Elihuruma Lema, Mkurugenzi wa Fedha na Utawala Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu; Dkt Catherine Joakim, Mtendaji Mkuu Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS;* Ndugu Ephraim Mafuru, ambaye ni Mkurugenzi Mkuu Bodi ya Utalii Tanzania; Ndugu Stephen Mokare, Mkurugenzi wa Milki na Miradi Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha; na Ndugu Athuman Kwikima, Mkurugenzi Huduma za Mamlaka, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini *(LATRA)*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Godfrey Nyaisa, Mkurugenzi Mtendaji Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni *(BRELA);* Ndugu Fredrick Nshekanabo, Afisa Mkuu wa Fedha Benki ya *CRDB;* Ndugu Chabu Mishwaro, Meneja Kanda ya Kati Benki ya *CRDB;* Ndugu Suzan Shuma, Mkurugenzi wa Biashara Serikalini, Benki ya *CRDB;* na Ndugu Grace Adam, Meneja Tawi la Bunge Benki ya *CRDB*. *(Makofi)*

Mwakilishi wa Afisa Mtendaji na Mtendaji Mkuu wa Benki ya *TCB,*; Ndugu Ruth Zaipuna, Afisa Mtendaji Mkuu Benki ya *NMB;* Ndugu Filbert Mponzi, Afisa Mkuu wa Fedha Benki ya *NMB*; Ndugu Vicky Bishubo, Afisa Mkuu wa Biashara Serikalini, Benki ya *NMB;* Ndugu Grace Matemu, Meneja Tawi la Bunge, Benki ya *NMB;* Ndugu Mirage Msuya, Mkuu wa Matawi ya *NBC,* Kanda ya Kati; na Ndugu Theresia Umbela, Meneja, Tawi la Bunge, Benki ya *NBC*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, punguzeni kelele kidogo ili na mimi nipunguze sauti kwa sababu, ninyi mnanifanya niongee kwa sauti sana, nyie mnasababisha. Kwa hiyo, tulieni kidogo, ili Spika wenu awe salama. *(Kicheko/Makofi)*

Tunaendelea, Ndugu Silvest Uisso Arumasi, Mkurugenzi Mtendaji Benki ya AKIBA; Ndugu Esther Maruma, Mkurugenzi

Mtendaji *BOA* Benki; Ndugu Nandi Mwiyombella, Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano *BOA* Benki; Ndugu Joseph Mnembuka, Meneja Tawi la Dodoma, *BOA* Benki; Ndugu Esther Mang'enya, Afisa Mtendaji Mkuu Benki ya Azania; Ndugu Endael Mziray, Mkurugenzi wa Sheria, Benki ya Azania; Ndugu Liberia Assey, Meneja Tawi la Dodoma Benki ya Azania; Ndugu Manzi, Afisa Mtendaji Mkuu Benki ya *STANBIC*. *(Makofi)*

Samahani, jina kumbe linaendelea! Huyu ni Ndugu Manzi Rwegasira. Ni Afisa Mtendaji Mkuu, Benki ya *STANBIC*. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Joan Mbise, Meneja Tawi la Dodoma Benki ya *STANBIC;* Ndugu Jacob Mbwele, Afisa Mtendaji Mkuu wa Fedha Benki ya *Equity*; Ndugu Adolphina William, Kaimu Afisa Mtendaji Benki ya Maendeleo ya Kilimo *(TADB);* Ndugu Gbenga Makinde, Mkurugenzi Mtendaji Benki ya *UBA;* Ndugu Ravneet Chowdhury, Afisa Mtendaji Mkuu Benki ya *DTB;* Ndugu Alex Mziray, Kaimu Mkurugenzi Mkuu Benki ya *NCBA;* Ndugu Lilian Mbassy, Mkurugenzi Mkuu Benki ya Uwekezaji Tanzania *(TIB);* na Ndugu Angelina Ngalula, Mwenyekiti Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania *(TPSF)*. *(Makofi)*

Wapo Ndugu Janice Kaisa, Mkurugenzi Mkuu *SIMUSOLAR;* Ndugu Obeid Laizer, Mkurugenzi Mtendaji Benki ya *ABSA;* Ndugu Imani John, Mkurugenzi Mtendaji Benki ya *Access;* Ndugu Michelle Kilpin, Mkurugenzi Mtendaji Kampuni ya Bia Tanzania *(TBL);* Ndugu Obinna Anyalebechi, Mkurugenzi Mtendaji *Serengeti Breweries*; Ndugu Peter Nalitolela, Afisa Mtendaji Mkuu Soko la Hisa Dar es Salaam *(DSE);* na Ndugu Godfrey Malauri, Mwenyekiti wa Madalali, Soko la Hisa Tanzania. *(Makofi)*

Ndugu Godfrey, eeeh! Naona ana vyeo viwili, ama vimerudia! Haya, ameandikwa mara mbili. Sawa.

Yupo, Profesa Hozen Mayaya, Mkuu wa Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini *(IRDB);* Profesa Yohana Msanjila, Mkuu wa Chuo cha *St. John's*; Dkt. Mashala Yusuph, Mkuu wa Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo; Dkt. Victoria Lihiru, Mhadhiri Chuo Kikuu Huria; Ndugu Elvanus Kapira, Mkuu wa Chuo cha Madini; na Dkt.

Siriel Shaidi Mchembe, Mhadhiri wa Chuo cha Usimamizi wa Fedha *(IFM)* na Mlezi Vyuo Vikuu. *(Makofi)*

Wapo Wakili Onesmo Olengurumwa, Mratibu Kitaifa Mtandao wa Mashirika ya Haki za Binadamu Tanzania *(THRDC)* na Ndugu John Kalage, Mkurugenzi Haki Elimu. *(Makofi)*

Yupo Mheshimiwa Muttamwega Bhatti Mgaywa, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji Taasisi ya Masuala ya Elimu Tanzania *(TASEC)* na Mbunge Mstaafu wa Mwibara (1995 - 2010). Karibu sana.

Wapo Ndugu Raymond Kanegene, Mratibu Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu *(LHRC)* Dodoma; na Ndugu Warda Habib Shayo, Mkurugenzi Taasisi ya Wanawake Kuamka Tanzania *(WOWAP)*. *(Makofi)*

Wapo Ndugu Maiko Salali, Mkurugenzi Taasisi ya Watu Wenye Ulemavu; Ndugu Regina Mengi, Mkurugenzi Mtendaji *IPP Media;* Ndugu Patrick Kahemele, Afisa Mtendaji Mkuu *AZAM Media;* Ndugu Aisha Dachi, Mkurugenzi Mtendaji Kampuni ya Magazeti ya Serikali *(TSN);* Ndugu Deodatus Balile, Mwenyekiti Jukwaa la Wahariri Tanzania *(TEF);* Ndugu Josephat Mwenge Mwanzi, Meneja Programu Baraza la Habari Tanzania *(MCT);* Ndugu Rosalynn Mndolwa Mworia, Mkurugenzi Mtendaji Mwananchi Communication *Limited;* na Ndugu Steve Diallo, Mkurugenzi *Sahara Media group*. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Benjamin Majura, Naibu Mkaguzi Mkuu Hesabu za Serikali za Mitaa; Ndugu Salhina Mkumba, Naibu Mkaguzi Mkuu Hesabu za Serikali za Umma; Ndugu Wendy Massoy, Naibu Mkaguzi Mkuu Hesabu za Serikali Kuu; na Ndugu Alhaji Saad Kusilawe, Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi *Organization* wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Wapo ndugu Adam Ngalawa, Katibu Mwandamizi Ofisi ya Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi; Ndugu Leah Mbeke, Mkuu wa Kitengo cha Ufuatiliaji Ilani na Sera za Kijamii za Chama Cha Mapinduzi; na Ndugu Aboubakary Liongo, Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Wapo Mheshimiwa Irene Musokwa, Jaji wa Mahakama Kuu; Mheshimiwa Jabir Shekimweri, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma; na Mheshimiwa Mayeka Mayeka, Mkuu wa Wilaya ya Kongwa. Karibuni *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine ambao wamekaa jukwaa la vioo, ambao ni watendaji kutoka Wizara ya Fedha na Taasisi zake. Wote wasimame kwa pamoja, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nirejee tangazo ambalo nililitangaza mapema leo kuhusu kesho mdahalo ambao ni wa muhimu sana sisi wote kuhudhuria. Mdahalo huo, wataanza wawasilishaji saa nne kamili. Kwa hiyo, pamoja na kwamba, Bunge tutaahirisha mpaka Jumatatu, lakini Waheshimiwa Wabunge ni muhimu kuwepo kwenye huo mdahalo kwa sababu, siku ya kesho inatumika, kwa ajili ya kutafakari hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na pia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Kwa hiyo ni vizuri tukatumia muda huo kusoma zaidi kuhusu haya na wataalam watakuwepo, kwa ajili ya kutueleza na mambo hayo kwa upana zaidi; itatusaidia michango yetu ya wiki ijayo hapa Bungeni.

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu nyote, niwakaribishe wageni wote ambao mmeweza kutenga muda wenu kuja kuungana na sisi. Tunawashukuru sana kwa kuja, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Pia Waheshimiwa Wabunge wamewapigia makofi kuashiria kwamba, wamefurahi mmekuja na mje tena siku nyingine. Tunawakaribisha sana. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge, naahirisha Shughuli za Bunge mpaka Jumatatu, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.01 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 16 Juni, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*